**BUNGE LA TANZANIA**

__________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

__________

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Arobaini na Tisa – Tarehe 10 Juni, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawaomba tukae.

Waheshimiwa tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Arobaini na Tisa, katika siku hii muhimu sana katika kalenda ya Bunge ya mwaka 2021. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango Kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Ruvuma.

Na. 405

**Mgao wa Dawa Kituo cha Afya Msindo-Namtumbo**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Kituo cha Afya Msindo kilichopo Wilayani Namtumbo kinapata mgao mdogo wa dawa usiokidhi mahitaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mgao wa dawa katika Kituo cha Afya Msindo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Msindo kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kilipandishwa hadhi kutoka Zahanati na kuwa Kituo cha Afya tarehe 26 Machi, 2014. Kituo hiki kimekuwa kikipokea mgao wa dawa kama Zahanati badala ya Kituo cha Afya kwa kuwa Halmashauri haikuwasilisha maombi husika kadri ya utaratibu. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto hiyo ikiwemo kutumia fedha za makusanyo

zinazotokana na uchangiaji wa huduma za afya kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Wastani wa upatikanaji wa dawa muhimu katika kituo hiki ni asilimia 87.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kuwasilisha rasmi maombi ya mgao wa fedha za dawa za Kituo cha Afya Msindo kupitia ruzuku ya Serikali Kuu ili mgao huo urekebishwe na kukiwezesha kituo hicho kupatiwa mgao wa dawa wenye hadhi ya Kituo cha Afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, lakini asilimia zinatotajwa hapa za mgao wa dawa unaokwenda katika Kituo cha Afya hiki si sawa na uhalisia uliopo kwenye eneo la tukio.

Mimi nimuombe sasa Naibu Waziri baada ya Bunge hili aje katika kituo hicho cha afya ajionee uhalisia wa mgao huo wa dawa kwa sababu wananchi bado wanahangaika. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, katika kituo hicho cha afya wananchi wamejitolea kujenga jengo la upasuaji kwa gharama zao wao wenyewe na kwamba wamekwama katika masuala ya vifaa vya madukani; bati, boriti, nondo, rangi na mambo mengine yanayohusiana na vifaa vya dukani. Kwa misingi hiyo, je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia katika kituo hiki cha afya ili kuweza kuwawezesha wananchi hawa waweze kupata Kituo cha Afya na nguvu zao zisipotee bure? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jibu lake lilikuwa ni kwamba hamjaomba bado kama Halmashauri ili kiwe Kituo cha Afya. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya nyongeza tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetangulia kujibu katika swali la msingi kwamba Serikali imeweka utaratibu uko wazi kwamba zahanati inapopandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya maombi ya Halmashauri husika yanapelekwa kwa Katibu Mkuu Afya ili kupata mgao wa dawa kwa ngazi ya kituo cha afya na si zahanati kama ilivyokuwa mwanzo.

Kwa hiyo, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani kwa kazi kubwa anayofanya kufuatilia huduma za afya katika kituo hiki cha afya, lakini nimhakikishie kwamba tumeshaelekeza Halmashauri ilete maombi hayo na tutahakikisha sasa mgao wa dawa unaendana na kituo cha afya ili wananchi wasipate changamoto ya upungufu wa baadhi ya dawa.

Mheshimiwa Spika, pili nipongeze sana wananchi wa Namtumbo na katika eneo hili la Msindo kwa kuchangia maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Afya na kuanza ujenzi wa jengo la mama na mtoto, lakini pia jengo la upasuaji. Nimhakikishie kwamba tutahakikisha na sisi kama Serikali tunakwenda kufanya tathmini na kutafuta fedha kuunga mkono nguvu za wananchi ili Kituo cha Afya kiweze kufanya kazi vizuri zaidi, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, tunaenda swali linalofuata la Mbunge wa Mbulu Mjini, Mheshimiwa Zacharia Issaay.

Na. 406

**Hitaji la Walimu wa Sayansi Mji wa Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je lini Serikali itaajiri walimu wa masomo ya sayansi katika Shule za Sekondari za Halmashauri ya Mji Mbulu ili wanafunzi wapate ujuzi wa masuala ya sayansi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay , Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2019/2020 Serikali imeajiri na kuwapanga walimu 17 wa sayansi na hisabati na mafundi sanifu wa maabara wawili katika Halmashauri ya Mji Mbulu kati ya walimu 10,418 wa Sekondari na mafundi sanifu maabara 397 walioajriwa katika kipindi hicho.

Aidha, Serikali inaendelea kuratibu zoezi la kuajiri walimu 6,949 kwa nafasi za ajira zilizotangazwa mwezi Mei, 2021 ambao watapangwa kwenye shule mbalimbali zikiwemo na shule za Halmashauri ya Mji Mbulu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana; pamoja na majibu mazuri ya Serikali, majibu ambayo yanaeleza ni walimu kumi tu wa sayansi walioajiriwa kwa muda wa miaka mitano hali inayopelekea wanafunzi wengi wa Jimbo la Mbulu Mji na maeneo mengine nchini kushindwa kufanya mazoezi ya sayansi, na kwa kuwa tatizo hili limewagharimu wananchi kwa muda mrefu kwa ajili ya kuwachangia walimu wa kujitolea katika shule za Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

Nini kauli ya Serikali ya kutusaidia walau tatizo hili linapungua katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu pamoja na maeneo mengine nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa tupo kwenye mchakato wa ajira na majibu ya awali nilipofuatilia Wizarani walikuwa wamesema tuna walimu wengi wa sayansi na tatizo hili limewagharimu wanafunzi hao wasifanye vizuri.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa nafasi pekee ya kuondoa walau kiasi kikubwa cha upungufu wa walimu kwa shule za sekondari katika Jimbo la Mbulu Mji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza alikuwa nataka kujua kauli ya Serikali ya kupunguza tatizo la walimu wa sayansi hususan katika eneo lake lakini na maeneo mengine nchini; ni kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba Serikali itaendelea kuajiri walimu na tutaendelea kuangalia kada mbalimbali hususan kada za walimu wa sayansi pamoja na wataalam na mafundi sanifu wa maabara ili tuweze kuwasaidia.

Kwa hiyo, miongoni mwa vigezo ambavyo tumevizingatia sana ukiacha vile vigezo vya awali ambavyo tulivitaja ikiwemo watu kukaa muda mrefu ambao hawajapata ajira, lakini miongoni mwa vigezo ambavyo tunavitumia sasa hivi ni pamoja na ku-*consider* walimu wa sayansi katika ajira hizi ambazo tutazitoa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimtoe wasiwasi tu kwamba Serikali tutaendelea kuwapanga katika maeneo

yote ikiwemo katika eneo lako la Mbulu Mji. Kwa hiyo, hilo niahidi kwa Wabunge wote kwamba tutazingatia Majimbo yote katika kipindi hiki kuwaletea walimu wa sayansi lakini hatutawaacha na walimu wa *arts* ambao wamesoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba alitaka tu kujua ni namna gani tunawasaidia kuwatoa. Jukumu kubwa ni kwamba Serikali itaendelea kuajiri kulingana na upatikanaji wa fedha na kadri tutakavyoajiri ndivyo ambavyo tutaendelea kuwapanga, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika walimu hawa wa sayansi kipaumbele ni kwa walimu wa hesabu jamani, hakuna sayansi bila hesabu, walimu wa hesabu ni wachache mno. Mheshimiwa Hawa Mchafu nilikuona. *(Makofi)*

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hali iliyopo Halmashauri ya Mji wa Mbulu ya ukosefu wa walimu wa sayansi inafanana kabisa na hali ya Halmashauri zote za Mkoa wa Pwani kuwa na uhaba wa walimu wa sayansi.

Je, ni lini sasa Serikali itatupatia walimu hawa wa sayansi ili kuweza kukidhi mahitaji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuwa swali hili linajirudia, sasa Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Ummy Mwalimu inatakiwa kauli yako sasa hapo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde kwa majibu mazuri, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Hawa Mchafu kutaka kujua ni lini Serikali itapeleka walimu wa sayansi katika shule za sekondari za Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, tunakiri tunayo changamoto ya uhaba wa walimu wa sayansi na uchambuzi ambao tumeufanya ndani ya miezi mitatu kuna shule takribani 1,000 za sekondari wanafunzi wetu hawajawahi kukutana na mwalimu wa *physics face to face,* lakini tuna shule takribani 400 watoto wetu wa sekondari hawajawahi kumuona mwalimu wa hesabu akiingia darasani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo hili tumeliona na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kutupa kibali cha kuajiri walimu katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge tunakamilisha uchambuzi wa maombi ya walimu ambao wameomba nafasi hizi za ajira tulizozitoa na kipaumbele kama tulivyosema ni kutatua changamoto hii ya walimu wa sayansi hususan pia katika masomo ya hesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongeze, sambamba na kuendelea kuomba kibali cha ajira kutoka kwa wenzetu Ofisi ya Rais - Utumishi tumeona ipo fursa ya kutumia maendeleo ya *Information Communication and Technology (ICT)* ili pia kuwawezesha wanafunzi wetu kupata masomo au walimu wa sayansi na hesabu kupitia mtandao.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tumeliona, tutaweka walimu wazuri watarekodi mada zote muhimu halafu wanafunzi wetu watakuwa pia wanaweza kusoma masomo ya sayansi kwa kutumia njia ya mtandano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu ya nyongeza, tuendelee Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu.

Na. 407

**Ranchi/Shamba la Kuzalisha Mifugo Nangaramo**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, wananchi wa Jimbo la Nanyumbu watanufaika vipi na Shamba la Uzalishaji Mifugo Nangaramo?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali kwa swali hilo, Mheshimiwa Abdallah Ulega - Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Nangaramo ni miongoni mwa mashamba matano ya kuzalisha mitamba chotara wa maziwa na nyama kwa lengo la kusambaza kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, faida zinazopatikana kwa wananchi wanaozunguka Shamba la Nangaramo ni pamoja na wananchi kupata elimu kupitia mikutano ya ujirani mwema kuhusu fursa za upatikanaji wa mitamba ya maziwa na nyama kwa lengo la kuwahamasisha kufuga ili kuboresha lishe ya familia, kutoa ajira na mbolea kwa uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, mbili, kutoa mafunzo ya ufugaji bora kwa shule za msingi na sekondari. Aidha, wanafunzi kutoka katika Shule ya Sekondari Mkangaula wamenufaika na mafunzo hayo walipokuwa kwenye mafunzo maalum; na tatu, uongozi wa shamba hushiriki shughuli mbalimbali za kijamii kama vile ujenzi wa shule na utoaji wa ajira za muda mfupi na mrefu kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya swali la nyongeza

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, shamba hili la Nangaramo lilianzishwa mwaka 1986 wakati Wilaya ya Nanyumbu ikiwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Ukubwa wa shamba hili ni hekta 5,633; hivi ninavyozungumza kuna ng'ombe 300 tu; vijiji vinavyozunguka shamba hili vina uhaba mkubwa wa mahali pa kulima; vijiji vya Kata ya Kamundi, Mkolamwana, Kamundi na Chekereni vina shida kubwa ya mahali pa kulima hata Kata ya Nangomba, Vijiji vya Nangomba na Mji Mwema vina shida kubwa ya mahali pa kulima.

Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri; je, haoni wakati muafaka umefika maeneo haya ambayo hayatumiki kwa shughuli za mifugo wakaruhusiwa wananchi wanaozunguka vijiji hivi wakalima mazao ya muda mfupi, pale ambapo mtakapokuwa tayari basi mnaweza mkayachukua maeneo yenu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mwaka 2018 kulikuwa na mgogoro mkubwa kati ya wanakijiji cha Mkolomwana na shamba hili, hali iliyopelekea kijana mmoja kupoteza maisha Bwana Ahmad Swalehe na vijana 36 kupelekwa mahakamani. Kwa kuwa kesi ile imekwisha na vijana wale wameachiwa huru kutokuwa na hatia katika mgogoro huu; nini hatma ya kijana huyu marehemu ambaye amepoteza maisha yake kwenye mgogoro huu, je, Serikali ipo tayari kumlipa fidia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili; la kwanza linasema mnakalia hekta 5,000 na ng'ombe hamna kama yale ya ranchi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya Mhata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namuelewa Mheshimiwa Mhata na juu ya jambo la mahitaji ya wananchi wa kata na vijiji alivyovitaja vinavyozunguka shamba letu la Nangaramo. Naomba nichukue jambo hili kwa niaba ya Wizara, tutakutana na Mheshimiwa Mhata na tuweze kukubaliana kwenda katika eneo hili la Nangaramo na kuhakikisha tunakwenda kufanya tathmini ya kuona hiki anachokisema na kuzungumza na wananchi na pale itakapoonekana inafaa tunaweza tukaona namna ya kuweza kuwasaidia wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hili linalohusu marehemu huyu; jambo hili ni kubwa, naomba nilichukue, atueleze vyema na sisi tutafanya mashauriano ya kuona namna iliyo bora ya kuweza kulimaliza suala hili, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; Wilaya ya Maswa nayo ina ranchi kubwa takribani ekari 12,000 Ranchi ya Shishiu pale Maswa na Mheshimiwa Waziri analifahamu hilo.

Je, wana mpango gani wa kuwagawia wananchi wa Maswa watumie ranchi hiyo kwa ajili ya matumizi ya ufugaji maana hatuoni Serikali inafanya juhudi gani katika ranchi hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya lingine huko Maswa chaka hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, aah Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa majibu yake mazuri kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mawazo ya wananchi kuona kwamba maeneo ya Wizara ya Mifugo

ambayo ni pamoja na ranchi na eneo ambalo analizungumza Mheshimiwa Nyongo lenyewe sio ranchi Ni *holding ground*, kwamba linapokuwa hivyo basi wananchi wapewe au wafanye shughuli zinginezo. Tunakubaliana kwamba tunafanya tathmini ya maeneo yote tuliyonayo ili tuone ni kwa namna gani yanaweza yakatumiwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa eneo la Shishiu, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa wameleta andiko na mpango wao kuonesha ni kwa namna gani wanataka kutumia hilo eneo. Wameeleza wanataka eneo dogo, sisi tumewarudishia tukawaambia leteni mpango wa kutumia eneo lote la Shishiu kwa ujumla wake halafu tutaona ni kwa namna gani sasa mnakwenda kulitumia halafu tuweze kuwapa nafasi ya kulitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe tu Waheshimiwa Wabunge na wananchi maeneo ya Wizara ya Mifugo ambayo yapo wazi, tunataka tuyatumie kikamilifu kwa kuwashirikisha wananchi wenyewe, lakini sekta binafsi ili iweze kuwekeza vizuri kwenye hayo maeneo na yaweze kutumika kwa tija zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu ya kutia moyo sana hayo, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante; kwa kuwa katika swali la msingi majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ilikuwa kwamba lengo la Shamba la Nangaramo ni kusambaza mitamba, lakini katika maeneo mengi yenye mashamba haya mitamba hiyo imekuwa ndama wake wanauzwa kwa shilingi 1,500,000 na hivyo wananchi kushindwa kumudu gharama za kununua ndama.

Je, Serikali haioni haja ya kuondoa kabisa hayo mashamba na kwa vile lile lengo la msingi la kusambaza mitamba halijafanikiwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu, Mheshimiwa Waziri yaani ndama shilingi milioni moja na nusu, ndio swali lipo tu hapo yaani. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; kuhusiana na bei ya mitamba, hiyo ni biashara; na ndama au ng'ombe wanaouziwa wananchi bei yake inajumlisha gharama za kumtunza yule ng'ombe pamoja na gharama zingine zote.

Mheshimiwa Spika, sasa huwezi kumnunua ng'ombe ambaye Mheshimiwa Mbunge anamuita ni ndama, *actually* ni ng'ombe kwa sababu huyo ng'ombe anaponunuliwa kwetu anakuwa yupo tayari kubeba mimba ili aweze kuzaa. Sasa sio ndama kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amemuita na pengine tutaangalia utaratibu ambao unapelekea mpaka kufikia gharama za namna hiyo, tuone kama tunaweza taratibu za gharama zikapungua tuweze kuwauzia kwa bei ambayo ni *reasonable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitangaze tu kwamba kwa Shamba la Nangaramo tayari tumewauzia wananchi walio karibu na shamba hilo mitamba 14 wameweza kununua na shamba letu kwa sababu linazalisha sio mitamba mingi sana, inatafutwa na wana *order* kubwa mpaka sasa hivi wanasubiria. Sasa suala la bei tutaliangalia tuone ni kwa namna gani inaweza kupungua ili wananchi waweze kununua mitamba mingi zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunashukuru kwa majibu hayo, mtakumbuka alikuwa anazungumzia habari ya hekta 5,000 umeuza mitamba 14, *you can imagine size* ya *area* na... eeh, lakini pia shilingi milioni moja na nusu huyu ndama watani zangu kule Songea kwa Waziri wa Maliasili milioni moja na nusu unapata mke eti, sasa huku unanunua ndama tu kweli hii bei kwa kweli; Waheshimiwa nafikiri tutakubaliana inabidi iangaliwe kwa kina Msongozi kule. *(Kicheko)*

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala.

Na. 408

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Ujenzi wa Barabara ya Kilwa**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi wa Mbagala Kokoto hadi Kongowe wanaopisha ujenzi wa barabara ya Kilwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara Ujenzi na Uchukuzi ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara kwa lengo la kushughulikia tatizo sugu la msongamano wa magari, hususan katika barabara kuu za Jiji la Dar es Salaam ikiwemo barabara ya Kilwa kuanzia Mbagala Rangitatu mpaka Kongowe yenye urefu wa kilometa 3.8. Utekelezaji wa mpango huu unahusisha upanuzi wa barabara kutoka njia mbili kuwa njia nne pamoja na ujenzi wa Daraja la Mzinga.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha ujenzi huo unafanyika bila vikwazo, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha hatua za awali za kupitia jedwali la fidia na kuhakiki mali za wananchi wanaostahili kulipwa fidia. Aidha, zoezi hili liliwahusisha pia viongozi wa Serikali za Mitaa husika ili kuhakikisha wananchi wote wanaostahili kulipwa fidia wanalipwa stahili zao kwa mujibu wa sheria zilizopo. Hivyo wananchi wa Mbagala eneo la

Kokoto hadi Kongowe wanaombwa kuwa wavumilivu wakati zoezi la kuhakiki taarifa za fidia linaendelea. Mara uhakiki utakapokamilika wahusika wote watalipwa fidia kulingana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa kuhakiki mali za wananchi pamoja na majedwali haya ya fidia ulianza toka mwaka 2018, je, wananchi wa Kokoto hadi Kongowe wanataka kujua wavumilie mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni nini hatma ya wananchi wa Mbagala Rangitatu eneo la Charambe hadi kule Mbande ambao wamewekewa mawe ya hifadhi ya barabara toka mwaka 2010 na bila kupewa maelezo yoyote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge wa Mbagala ambaye ni Meya Mstaafu wa Manispaa ya Temeke kilio chako kimesikika Mheshimiwa Mbunge na ndio maana Mheshimiwa Rais alitembelea katika eneo lako na ametoa maelekezo. Kiongozi Mkuu wa nchi akitembelea nchi hayo ni maelekezo sisi ni watekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika ni kwamba ni fidia imefanyika, mkandarasi yupo pale *site* ataleta taarifa, watu wa *TANROADS* Mkoa wa Dar es salaam watapitia taarifa hiyo, tutafanya *joint verification* kwa maana ya Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Fedha na *Valuer* wa Serikali baada ya hapo

wananchi wale watalipwa fidia. Maelekezo ni kwamba ujenzi hautaanza mpaka tuondoe vikwazo vya kulalamikiwa na wananchi baada ya kulipwa haki zao. Kwa hiyo, naomba wavute subira katika jambo hilo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Mbunge anauliza habari ya mawe ambayo imewekwa pale katika *road reserve* ya Mbande kwenda Msongola mpaka Mvuti. Ni kweli kwamba wananchi baadhi walilipwa wakati huo, lakini tumekubaliana kwamba tukianza upanuzi wa barabara hiyo, yule mwananchi ambaye anafikiwa kwa wakati huo atakuwa analipwa fidia yake, hayo ndio majibu ya Serikali, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

Na. 409

**Serikali Kufungua Ofisi Ndogo ya Hazina Zanzibar**

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Ofisi Ndogo ya Hazina Zanzibar kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Muungano ili kurahisisha huduma kwa wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wanaoishi Zanzibar?

**SPIKA:** Majawabu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Masauni, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jang'ombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za malipo ya mafao ya wastaafu wanaolipwa na Wizara ya Fedha na Mipango

hufanyika kupitia Ofisi za Hazina Makao Makuu, Dodoma. Aidha, Ofisi za Hazina Ndogo zilizopo katika Mikoa ya Tanzania Bara hutumika kwa ajili ya kukusanya hoja za wastaafu na kuziwasilisha Hazina Makao Makuu, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa wastaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaoishi Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Muungano wa Tanzania mara zote imekuwa ikifanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kupokea hoja za madai ya wastaafu hao na kuziwasilisha Hazina Makao Makuu, Dodoma kwa ajili ya taratibu za malipo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Muungano wa Tanzania itaimarisha ushirikiano na Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuwahudumia wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wanaoishi Zanzibar kama ambavyo hushirikiana na Ofisi za Hazina Ndogo zilizopo Tanzania Bara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante; humu mna jibu hakuna jawabu, kwa sababu nilichoomba kwamba ni lini Serikali itafungua Ofisi ya Hazina Ndogo lakini jibu lililokuwemo humu wamesema watafanya mashirikiano na Wizara ya Fedha ya Zanzibar kitu ambacho hakiwezekani kwamba taarifa za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zikawepo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hawa wazee taarifa zao zipo Wizara ya Fedha ya Muungano, wanapokuwa na matatizo wanakwenda Dar es Salaam na wanachukua muda mwingi hadi wengine wanasamehe mafao yao. *(Makofi)*

Sasa nataka jawabu Serikali ina mpango gani wa kuwa na ofisi kama ilivyokuwa ofisi nyingine? Mpango wa kuwa na ofisi, hilo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, hawa wazee wanaokuja mpaka wakakata tamaa wakarudi wakasamehe mafao yao Serikali itachukua hatua gani?

**SPIKA:** Majibu ya maswali Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa *Engineer* Masauni, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Omar Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza hatujapokea malalamiko ambayo yanaonesha kuna usumbufu wa malipo ya wastaafu kupitia utaratibu ambao tunao sasa hivi wa kushirikiana kati ya Wizara za Fedha za pande mbili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kama ana malalamiko mahususi ambayo pengine hayajatufikia sisi, basi ayawasilishe tutayashughulikia haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na lini tutajenga ofisi, masuala ya ujenzi wa ofisi ni masuala ambayo yanahitaji bajeti na uwezo wa kifedha na maandalizi. Kwa hiyo, kutoa kauli hasa ni lini kwa sasa hivi inaweza ikawa sio rahisi sana hata hivyo Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba kwa sababu ofisi hizi ndogo zilizopo mikoani kwa upande wa Tanzania Bara ambazo zimejengwa huwa zinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Umma na Kanuni zake ambayo pamoja na mambo mengine, zinahudumia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Idara za Serikali ya Muungano ambazo kwa upande wa Zanzibar Ofisi za Tawala za Miko ana hizi Idara za Serikali shughuli zake zinafanywa na Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hiyo, shughuli zile hazijakwama kwa upande wa Zanzibar kwa sababu zinasimamiwa na Wizara ya Fedha ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo sio masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi ambazo tayari zimeshajengwa majengo huko kama *BOT* na *TRA* zina Ofisi

Zanzibar, kwa hiyo, masuala mengine ya ujenzi wa miundombinu ni masuala ambayo hayaendi kwa wakati mmoja, yanakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *concern* yake Serikali tunaitambua na pale ambapo hali itaruhusu basi tutakamilisha utaratibu huu ambao amependekeza.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge...

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** *Hallow.*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Amar.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuomba Mwongozo kwa Kanuni ya 76.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu...

**SPIKA:** Sio kila mtu anayo hebu isome.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Kanuni ya 76...

**SPIKA:** Inahusiana na kuomba mwongozo, *okay.*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Ndio.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuna tukio ambalo lilitokea ndani ya Bunge la kuhusiana na mavazi. Jambo hili limeonesha matumaini na kama unavyoona Bunge lako limependeza, nipende kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge akinamama kwa kuitikia hili, lakini pia niwapongeze

sana kina mama kwa kikao cha juzi, walitiwa moyo sana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwaaminisha mambo makubwa mazuri ndani ya jamii, wajiamini kama vile *tea bag. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninawaomba hao Wabunge akina mama watusaidie sasa kwenye maeneo yetu huko kwenye Majimbo kuhakikisha kwamba tunakuwa na dawati la akina baba la kusikiliza kero zao wanavyonyanyaswa na wake zao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala hili ni la msingi kwa sababu sasa hivi kuna dawati la kina mama ambao wanasikilizwa, lakini pia kina baba wapo ambao wananyanyasika hawana pa kupeleka malalamiko yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako suala hili liende likafanyike bila kuathiri desturi za makabila mfano Wasukuma kumtanguliza mama kwenda shambani sio tatizo na sio unyanyasaji, lakini pia kwa Wakurya mwanamama kukaa wiki moja bila kuomba fimbo ya kupigwa si tatizo.

Kwa hiyo, ninaomba mwongozo wako, kama utaniruhusu kwa hili ambalo limefanyika kwenye mavazi ninaweza nikatoa akina mama mfano wachache tu wamevaa vizuri sana kama kuna uwezekano uniruhusu nitoe zawadi kwa Waheshimiwa Wabunge akina mama wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale unachokoza nyuki, akina mama ni jeshi kubwa. Juzi tu hapa walituacha peke yetu humu ndani tulitetereka, tukabaki wapweke kwa sababu tuliwa-*miss* sana. Japo nimejaribu tutengeneza njama hivi tupitishe sheria moja ya haraka haraka hivi nisiwatajie sheria yenyewe ilikuwa inahusu nini, tukaogopa kwamba tukishamaliza hapa Wabunge

wanaume itaishia dawatini kwa Mheshimiwa Rais kule itakwama. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini kwa kweli tunawapongeza kwa mkutano wa juzi wa wanawake ambao ulihutubiwa na Mheshimiwa Rais, ulikuwa mkutano mkubwa na wa aina yake uliofanyika hapa Dodoma. Ama kweli wanawake wa Dodoma wanaweza, waliuandaa vizuri sana na Mikoa mingine sasa muige ile *mark* ambayo imefanywa na Dodoma. *(Makofi)*

Nikubaliane na Mheshimiwa katika baadhi ya mambo na baadhi amechapia utani kidogo, kwa kweli panahitajika dawati la wanaume mahali. Kweli kabisa tukienda na mwendo huu tukadhania wanaume wapo *okay,* wanaume wana hali ngumu sana ila wamelelewa katika msingi ambao hawasemi, wanagumia tu mmh, mmh. Sasa hawa nao wasaidiwe jamani na ni wakina mama ninyi muwapiganie maana ninyi wenyewe mna watoto wa kiume, si ndio jamani.

Tuangalie wapo wanaonyanyasika kweli kweli, la sivyo, lakini lile dawati nadhani ni la jinsia si ndio?  Sio la wanawake lile, si ni la jinsia? La pande zote mbili? Lakini ukienda pale unakuta mwanamke ndio yuko pale, sasa haki yako kweli! *(Kicheko)*

Basi imechukuliwa ngoja tutakuja kuiangalia kwa aina yake. Lakini tutamuomba Mheshimiwa Rais siku nyingine aite mkutano wa wanaume tu na sisi tu-*revenge,* ili wanawake waone wa kwetu utakaokuwa mkubwa zaidi ya wa kwao. Ahsante sana Waheshimiwa.  *(Makofi/Kicheko)*

Leo ni siku ya aina yake, tutakuwa na wageni wengi sana asubuhi hii na jioni ndio itakuwa maradufu ya hawa wa asubuhi. Lakini nianze kwa kuwataja; tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, ambao ni viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi zake.  Tunaye Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Emmanuel Tutuba; kama hawako pale lakini wako *around*. Nafikiri hawa watu wa Wizara ya Fedha nitawataja jioni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; ni wageni 50 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao ni walimu, wafanyakazi na wanafunzi wa *Wonder Kids Pre & Primary School* wakiongozwa na Meneja wa Shule Ndugu Shannel Nchimbi. *Wonder Kids*, karibuni sana, karibuni sana. Mheshimiwa Shangazi wanatoka wapi hao? Naam Shangazi. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, wanatoka Ruangwa hao.

**SPIKA:** Wanatoka Ruangwa, hongereni sana vijana wangu wa *Wonder Kids* kutoka Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanapendeza sana. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, hawa ndio wale walioshangilia goli la mita 45 la Bernard Morrison. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hongereni sana na karibuni sana, *Wonder Kids*. Wanatoka kule Ruangwa, jamani si mnaona elimu ya Tanzania? Mama Ndalichako anafanya kazi jamani. Mpaka Ruangwa mambo mazuri namna hii na Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa pamoja. Tunawashukuruni sana. Karibuni sana, *Wonder Kids*. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao ni wapiga kura wake; Ndugu Cedrick Msabi, Ndugu Jesca Protas na Ndugu Modesta Samwel, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Nyamoga ambao ni rafiki zake kutoka nchini Ujerumani, Ndugu Ricket Werner na Ndugu Ibrahim Sumbe, karibuni sana, karibuni sana, wale pale. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Daniel Awack ambao ni wana CCM kutoka Kata ya Kansay, Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha, wakiongozwa na Ndugu Nikola Matte, karibuni sana kutoka Arusha, mbarikiwe. *(Makofi)*

Wageni 27 wa Mheshimiwa Erick Shigongo ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Buchosa, Mkoa wa Mwanza, wakiongozwa na Mheshimiwa Idama Kibanzi. Madiwani kutoka Buchosa? Wale pale, karibuni sana, Waheshimiwa Madiwani. Karibuni sana mjifunze shughuli za Bunge na Mbunge wenu Erick Shigongo sijui hata kama mmeona anapokaa. Yupo pale amejaa tele na anafanya kazi nzuri sana, muendelee kushirikiana katika kuendeleza Buchosa na wale wa kutoka Visiwani basi karibuni.

Juzi, Mheshimiwa Shigongo aliongelea habari ya umeme unavyokuwa bei kubwa sana huko katika Visiwa vya Buchosa na mambo yamekaa sawasawa hongereni sana na karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi ambao ni wapiga kura wake kutoka Lushoto Mkoani Tanga, wakiongozwa na Ndugu Ahmadi Pangaleli, wale pale. Karibuni sana kutoka Lushoto, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga, ambao ni wachungaji kutoka Jimbo la Mbogwe, Geita wakiongozwa na Askofu Timotheo Lutobola, karibuni sana, ahsante sana. Baba Askofu Lutobola yupo wapi? Ahsante sana, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Janejelly Ntate ambao ni viongozi wa TUGHE kutoka Kibaha, Mkoani Pwani, wakiongozwa na Mwenyekiti wa TUGHE Taifa, Ndugu Archi Mntambo, karibuni sana TUGHE, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mchungahela ambaye ni mtoto wake wa kwanza kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Germin Mchungahela, karibu sana, karibu. *(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Santiel Kirumba ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Solwa, Mkoani Shinyanga wakiongozwa na Mheshimiwa Aidi Malekasi. Madiwani kutoka Solwa? Karibuni sana, karibuni sana, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Grace Tendega, ambaye ni Mkufunzi Mstaafu kutoka Chuo cha Ualimu Butimba, Ndugu Wilson Mwangomo, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Daniel Baran ambao ni Waheshimiwa Madiwani na walimu kutoka Jimboni Babati, Mkoani Manyara wakiongozwa na Mheshimiwa Michael Bimu, wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Venant Protas ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kutoka Jimboni Sengerema Ndugu Husna Omary, karibu, karibu Husna. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambao ni walimu kutoka Jimbo la Mbulu, Mjini Manyara, wakiongozwa na Mwalimu Timotheo Kasmiri na Mwalimu Messy Kessy, karibuni sana, wako kule juu kabisa. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni Ndugu Abbas Chikawe na Ndugu John Zebedayo; wale kule, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Benaya Kapinga ambaye ni rafiki yake kutoka Dar es Salaam, Ndugu Reuben Utouh, karibu sana, Reuben. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao ni viongozi wa Kanisa la *FCC* – Tanzania kutoka Jijini Mbeya, Ndugu Stephano Sikabenga, Ndugu Elly Mwamwezi na Ndugu Majaliwa Sikabenga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 16 ambao ni Wanajumuiya wa Baraza la Wazazi wa Chama cha Mapinduzi Tawi la Kimara ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, wakiongozwa na Ndugu John Ndomba, karibuni sana, karibuni sana, sana. *(Makofi)*

Wageni 69 wa Chuo cha Biblia Dodoma, *Tanzania Assemblies of God*, *Bible College,* wakiongozwa na Mwalimu

Frida Mwaipopo. *TAG*, karibuni sana, sana, karibuni sana, karibuni sana na muendelee kuliombea Taifa. *(Makofi)*

Wageni watatu kutoka Ofisi ya Uhamiaji Dodoma, wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, Ndugu Mrisho Kakozi, Ndugu Pius Charles na Ndugu Rose Mligo, karibuni sana, sana, sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Tunalo tangazo; kwanza kuna kipeperushi ambacho mtagawiwa natumaini mmekiona cha Mfuko wa Pembejeo, mkisome vizuri na muone namna mnavyoweza ku-*take advantage* ya huo Mfuko ikiwa ni pamoja na wapiga kura wenu.

Tunalo tangazo la punguzo maalum la kutembelea eneo la Hifadhi la Ngorongoro kuanzia tarehe 30 Juni baada ya kumaliza Bunge hadi tarehe 2 Julai. Waziri wa Maliasili na Utalii ameandaa punguzo maalum la kutembelea eneo la Hifadhi la Ngorongoro kuanzia tarehe 30 Juni hadi tarehe 2 Julai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri anawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote wenye nia ya kutembelea eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani. Gharama ni nafuu zinazojumuisha tozo ya kiingilio hifadhini, usafiri wa basi kutoka Dodoma hadi Karatu na kurudi, malazi ya siku mbili katika Hoteli ya Nyota Nne, usafiri wa magari ya utalii na chakula. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa mkajiandikishe mapokezi kwenye Jengo la Utawala pale Bungeni. Sasa bei kiasi gani ameficha kidogo, labda baadaye atatuambia. *(Makofi/Kicheko)*

Leo ni siku maalum kama nilivyowaambia, Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane, naomba tusikilizane.

Leo ni siku maalum na ina mambo mengi muhimu sana, muda sio mrefu nitamkaribisha hapa mbele, Waziri wa

Mipango, kufuatana na kanuni zetu, Waziri anayehusika na Mipango, halafu jioni saa 10.00 kamili nitamkaribisha hapa mbele Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, kabla sijafanya hivyo, kwa kawaida siku kama ya leo, huwa tunaweka mezani *Monetary Policy Statements* – Ripoti za kutoka Benki Kuu. *(Makofi)*

Sasa kwa leo bado hatujazipata, kwa hiyo, ningeomba niisisitize Serikali wajitahidi, watuletee haraka inavyowezekana kwa sababu ndio utamaduni wetu, ndio ada ya siku kama ya leo. Pamoja na hotuba zinazosomwa, lakini Wabunge lazima waangalie *Monetary Policy Statements*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi nafikiri umesikia hilo hebu jaribu kuli-*spearhead* hilo. Basi baada..., ndio Mheshimiwa Waziri wa Nchi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tumepokea maelekezo hayo, ni bahati mbaya tu kidogo kuna jambo halikuwa limekaa sawasawa, lakini baada ya muda sio mrefu zitakuwa ziko tayari na zitawekwa kwenye meza yako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

## HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2020 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**SPIKA:** Sasa namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Mipango ili atuwasilishie Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango sasa ni wakati wako, karibu sana Dkt. Mwigulu Nchemba. *(Makofi)*

Waheshimiwa makofi zaidi, ahsante sana. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

**SPIKA:** Sikupangiii muda, wewe soma hotuba yako utakavyoona inafaa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nilisisitize tangazo kuwa leo tarehe 10 saa 10.00 ni Bajeti ya Kimkakati. *(Makofi)*

Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/ 2022. Taarifa hizo ni msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 nitakayowasilisha katika Bunge lako Tukufu hivi leo alasiri.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe, Waheshimiwa Wabunge wote, Chama cha Mapinduzi na Watanzania wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitoe pole kwa Taifa kwa kuondokewa na viongozi wakuu, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali

ya Mapinduzi ya Zanzibar na Balozi Mhandisi John Kijazi aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangu kuapishwa kwake tumeshuhudia namna anavyoendelea kuliongoza Taifa letu kwa busara, hekima, ueledi na umahiri mkubwa na kuendeleza ushirikiano wa nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ujasiri na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuendelea kuwatumikia watanzania katika wadhifa wake wa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa, nitatekeleza majukumu haya kwa bidii, ueledi, uadilifu na uzalendo wa kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa

Mwaka 2021/2022 zimezingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa wadau katika hatua zote za uandaaji na maamuzi katika ngazi zote Serikalini. Ni vigumu kuwataja wadau wote waliotoa maoni na ushauri hadi kufikia hapa, lakini ni vyema nitambue mchango mkubwa wa Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako pamoja na Naibu Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha pia napenda kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri makini waliotupatia. Uandaaji wa Taarifa nilizowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu umenufaika kwa kiasi kikubwa na michango na ushauri na busara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya Mwaka 2020 imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na sekta mbalimbali kwa mwaka husika ikilinganishwa na mwaka 2019. Aidha, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 yamezingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka, 2020 na Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati analihutubia Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 22 Aprili, 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Mpango umezingatia sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda pamoja na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi mwaka 2020, tukianzia na uchumi wa dunia. Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF)* la Aprili, 2021 inaonesha kuwa mwaka 2020 dunia ilikuwa na mdororo wa uchumi kwa kupata ukuaji hasi wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na ukuaji na ukuaji chanya wa asilimia 2.8 wa mwaka 2019. Ukuaji hasi

ulisababishwa na kupungua kwa shughuli za kiuchumi duniani hususani biashara, usafirishaji na utalii kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO – 19.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchumi wa Afrika na Kikanda, mwaka 2020 nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji hasa wa uchumi wa wastani wa asilimia 1.9 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2019. Nchi zinazotegemea utalii kama chanzo kikubwa cha ukuaji wa uchumi ikiwemo Cape Verde, Mauritius na zile zinazotegemea mafuta kama Angola, Cameroon, Chad, Congo, Jamhuri ya Guinea, Gabon, Nigeria na Sudan ya Kusini zilipata athari kubwa kutokana na UVIKO – 19 na kuchangia ukuaji hasi wa nchi za Afrika na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa; licha ya mlipuko wa UVIKO – 19, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizokuwa na ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2020 uliokuwa chanya. Pato la Taifa la Tanzania lilikuwa kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 wa mwaka 2019. Sekta zilizochangia kwa kiwango kikubwa ukuaji wa juu wa mwaka 2020 ni pamoja na sekta ya ujenzi ambayo ilikuwa asilimia 9.1; habari na mawasiliano asilimia 8.4; uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 8.4; huduma zinazohusiana na utawala asilimia 7.8; shughuli za kitaalamu asilimia 7.3 ambazo zinajumuisha sayansi na ufundi, madini na mawe asilimia 6.7 na afya na huduma za jamii kwa asilimia 6.5.

Mheshimiwa Spika, wastani wa pato kwa mtu lilikadiriwa kufikia shilingi 2,653,790 sawa na dola za Kimarekani 1,151 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi za Kitanzania 2,573,324 sawa na dola za Marekani 1,118.9 kwa mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.1.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei; mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo ulikuwa kwa asilimia 3.3 kwa mwezi Mei, 2021. Hii imechangiwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, kushuka kwa bei za mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa

thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola za Kimarekani na sarafu zingine duniani na usimamizi madhubuti wa sera za kifedha na bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha ya kuongeza ukwasi ambayo imesaidia kupunguza baadhi ya viwango vya riba katika masoko ya fedha hususan riba za mikopo. Wastani wa riba za mikopo ya Benki Kuu katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2021 ulipungua hadi asilimia 16.58 na riba za mikopo ya kipindi cha mwaka mmoja zilifikia wastani wa asilimia 16.05. Aidha, wastani wa riba za amana ulikuwa asilimia 6.95 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2021 na riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja zilifikia wastani wa asilimia 8.77 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2021.

Mheshimiwa Spika, ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi inayoendana na mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi yaani *M3* uliongezeka na kufikia shilingi trilioni 31.0 Aprili, 2021 ikilinganishwa na shilingi trilioni 28.76 Aprili, 2020 sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Ongezeko hili ni matokeo ya usimamizi thabiti wa sera za kifedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 4.8 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa katika shughuli binafsi ambazo zilipata asilimia 35.8 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 15.7, uzalishaji viwandani asilimia 10.1 na kilimo asilimia 8.0.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukuzaji rasilimali; mwaka 2020 ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika ulifikia shilingi trilioni 59.2 kutoka shilingi trilioni 55.8 za mwaka 2019 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Aidha, ukuzaji wa rasilimali za kudumu kwa bei za miaka husika uliongezeka

kwa asilimia 7.8 kutoka shilingi trilioni 59.4 mwaka 2019 hadi shilingi trilioni 64.0 mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nje; katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2021 urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje uliimarika kufikia nakisi ya dola za Kimarekani bilioni 1.2 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani bilioni 1.4 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020. Kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa kulichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu na bidhaa za maua na mbogamboga sambamba na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta na vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili, 2021 thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma ilifikia dola za Kimarekani bilioni 8.5 na thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje zilifikia dola za Kimarekani bilioni 9.3 katika kipindi husika. Thamani ya mauzo ya bidhaa ilifikia dola za Kimarekani bilioni 6.4 na thamani za bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilifikia dola za Kimarekani bilioni 8.1; Mapato yatokanayo na huduma yalifikia dola za Kimarekani bilioni 2.2 Aprili, 2021 na malipo ya huduma yalifikia dola za Kimarekani bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa akiba ya fedha za kigeni; akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi Aprili, 2021 akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani bilioni 4.97 ambayo inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takribani miezi 5.8. Kiwango hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0 ambapo pia ni zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwenendo wa thamani ya shilingi; thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani imeendelea kuwa tulivu ambapo dola moja ya Kimarekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi

2,298.5 Aprili, 2021 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,291.3 Aprili, 2020. Utulivu wa shilingi umetokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika usimamizi wa sera za fedha pamoja na bajeti na kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma pamoja na uhamisho wa mali nje ya nchi pamoja na mwenendo chanya wa baadhi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa; hadi Aprili, 2021 deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 60.9. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 43.7 na deni la ndani ni shilingi trilioni 17.3. Deni hilo linatokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Taarifa ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba, 2020 inaonesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwa kuzingatia ukomo wa viashiria vyote vinavyokubalika kimataifa. Maelezo ya kina kuhusu hali ya uchumi kwa mwaka 2020 yapo katika kitabu cha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021; katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 Serikali ilikuwa inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kupitia Mipango ya Maendeleo ya mwaka mmoja mmoja. Dhima kuu ya Mpango wa Pili ilikuwa ni “Ujenzi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.”

Mheshimiwa Spika, Serikali ilijenga miundombinu ya msingi ili kuwezesha Wananchi kujiletea maendeleo na kuchochea uwekezaji katika viwanda. Katika kipindi hicho, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha:-

(i) Miundombinu ya Reli; kufikia asilimia 91 ya ujenzi wa Reli ya Kisasa katika kipande cha Dar es Salaam kwenda Morogoro kilometa 300 na asilimia 61 kwa kipande cha Morogoro kuja Makutupora na kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka kilometa 341 chenye thamani ya shilingi trilioni 3.07.

(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115: utekelezaji wake umeshafikia takribani asilimia 52.

(iii) Uboreshaji wa Shirika la Ndege la Tanzania; kununuliwa kwa ndege 11 za abiria na mizigo; kuboreshwa kwa karakana ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro; ununuzi wa jozi ya injini za akiba kwa ndege aina ya *Dash* 8 Q400; na kulipa bima za ndege *Boeing 787-8 Dreamliner* na *Dash 8 Q400*.

(iv) Kwa upande wa Miradi ya Umeme; kukamilika kwa baadhi ya miradi ikiwemo mradi wa njia ya kusafirishia umeme kV 220 kutoka Makambako hadi Songea; ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme pamoja na njia za kusafirishia umeme katika Mradi wa Njia ya Kusafirishia Umeme wa Msongo wa kV 220 Bulyanhulu, Geita; kukamilika kwa asilimia 80 ya utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo - MW 80; kukamilika kwa usanifu wa miradi ya Kakono MW 87 na Malagarasi MW 45; na kuunganishwa umeme kwa jumla ya vijiji 10,312 kati ya vijiji 12,317 sawa na asilimia 83.7 ya vijiji vyote hapa nchini.

(v) Kwa upande wa ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; mafanikio ni kuendelea kwa ujenzi wa viwanja vya ndege vya Geita asilimia 95, Songea asilimia 95 na Mtwara asilimia 55; kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato ambao utagharimu dola za Kimarekani takribani milioni 330, ambayo ni sawa na shilingi bilioni 759 na uzinduzi wa ujenzi wa upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85.

(vi) Upande wa uendelezaji wa bandari; Bandari ya Dar es Salaam tukianza nayo ni kuboreshwa kwa gati namba 1 – 5; kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari *(RoRo);* Bandari ya Mtwara; ni kukamilika kwa ujenzi wa gati jipya na kwa upande wa Bandari ya Tanga; mafanikio ni kukamilika kwa uongezaji wa kina cha lango la kuingia meli.

(vii) Kwa upande wa Bandari za Maziwa Makuu; mafanikio ni kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Nyamirembe, Magarine, Lushamba, Ntama na Mwigobero katika Ziwa Victoria na kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Sibwesa na Kabwe pamoja na kuendelea na ujenzi wa Bandari za Karema, Ujiji, Kibirizi na Lagosa katika Ziwa Tanganyika; na kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu. Tukianza na Ziwa Victoria na Tanganyika; mafanikio ni kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili za *New Butiama Hapa Kazi Tu* na *New Victoria Hapa Kazi Tu.* Mafanikio mengine ni kuendelea na ujenzi wa meli mpya za *MV Mwanza Hapa Kazi Tu* yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambao umefika asilimia 74 na kukamilika kwa ujenzi wa chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza chenye uwezo wa kubeba meli au chombo chenye uzito kuanzia tani moja hadi tani 4,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ziwa Nyasa; mafanikio ni kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja na kuanza kufanya kazi kwa meli mpya ya MV Mbeya II.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara na madaraja makubwa; Serikali imeendelea kujenga na kukarabati mtandao wa barabara nchini kwa lengo la kufungulia fursa za kiuchumi katika maeneo mbalimbali, kuongeza wigo wa utoaji huduma za msingi na ustawi wa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha ujenzi wa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilometa 3,537; barabara kuu na za mikoa kilometa 2,209 na barabara za halmashauri kilometa 1,328. Hivyo kufanya mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami kufikia kilometa 13,044.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni kukamilika na kuanza kutumika kwa daraja la juu la Kijazi yaani ni *Kijazi Interchange* na kukamilika kwa asilimia 87.38 ya upanuzi wa barabara sehemu ya Kimara – Kiluvya kilometa 19.2 na kuendelea na ujenzi wa daraja dogo la Busisi la Kigongo – Busisi lililoko Mwanza ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 27. Mafanikio mengine ni kuendelea na ujenzi wa Daraja jipya la Tanzanite hapo Dar es Salaam ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 77.19 na Daraja Jipya la Wami Mkoani Pwani ambao utekelezaji wake umeshafikia asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya; mafanikio ni ujenzi wa hospitali 99 za halmashauri ambapo hospitali 67 zimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje; kujengwa kwa hospitali 10 za rufaa za mikoa; kukamilika kwa ujenzi wa zahanati 1,198; na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabaati wa jengo la mionzi katika Hospitali ya Rufaa Dodoma. Mengine ni kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru ambayo ipo Dodoma ambayo imeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje; na mengine ni kununuliwa kwa mashine za kidijitali za mionzi, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu unaootesha vimelea ambayo ni *BACTEC 960 (Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT)* pamoja na *Blood Culture Machine* katika Hospitali ya Rufaa ya Kifua Kikuu ya Kibong'oto iliyopo Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni ununuzi wa mashine ya *Positron Emmission Tomography (PET Scan*) kwa ajili ya Hospitali ya *Ocean Road* na ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo upatikanaji wa aina 30 za dawa zenye kukidhi magonjwa ya msingi 30 ulifikia asilimia 86 na la mwisho ni upatikanaji wa aina 312 za dawa muhimu ambao mafanikio yake yamefikia asilimia 74.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu; mafanikio ni kuendelea kutekeleza sera ya Serikali ya kuongeza fursa za elimu bora kwa kila mtoto wa Kitanzania kwa kugharamia elimu msingi bila ada ambapo wastani wa shilingi bilioni 20.8

zinatolewa kila mwezi na mafanikio mengine ni kujengwa kwa miundombinu muhimu katika shule 3,904 ambapo shule za msingi ni 3,021 na sekondari 883. Mabweni yaliyojengwa ni 547, nyumba 101 za walimu, majengo ya utawala 25 na maktaba 43.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133 na kukarabatiwa kwa shule kongwe 84 kati ya 89. Mafanikio mengine ya Serikali ni kuongezeka kwa wigo wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu na kuendelea kugharamia chakula na malazi kwa wanachuo wote katika vyuo 35 vya mafunzo ya ualimu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji mijini na vijijini; kukamilika kwa miradi 1,845 ya maji mijini na vijijini hivyo kuwezesha huduma za maji kufikia asilimia 85 kwa wananchi waishio mijini na asilimia 72.3 vijijini hadi Machi, 2020. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na kukamilika ni miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa miradi ya maji katika mji wa Kigoma asilimia 90, Mwanza asilimia 76 na Arusha asilimia 62. Mafanikio mengine ni kukamilika na kuzinduliwa kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega. Aidha, katika eneo linalohudumiwa na *DAWASA* mikoa ya Dar es Salaam na Pwani utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande kilimo, mifugo na uvuvi. tukianza na kilimo; mafanikio ni kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji hivyo kuongezeka kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 katika mwaka 2020. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa skimu 17 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 8,536 kupitia *ASDP II* na skimu tano za Kigugu – Mvomero hekta 195, Msolwa Ujamaa hekta 40, Njage – Kilombero hekta 75, Mvumi – Kilosa hekta 249 na *Kilangali Seed Farm* – Kilosa hekta 400 na kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga – *Expanded Rice*

*Production Project (ERPP)*; kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kufikia tani 76,726 kwa mwaka 2020. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo, Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo; mafanikio ni kuimarishwa kwa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji kilichopo *Usa River,* Arusha kwa kununua kifaa *(chiller)* kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni na kujengwa kwa viwanda vipya vya kikemikali vya nyama vya *Tanchoice* ambacho kipo Pwani, *Elia Food Oversees Limited* ambacho kipo Arusha na *Beijing Company Limited* ambacho kipo Shinyanga. Mafanikio mengine ni kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Food and Beverage Company Limited* kilichopo Arusha na kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha chanjo cha *Hester Bioscience Africa Limited* ambacho kipo Pwani chenye uwezo wa kuzalisha chanjo aina 37 na mafanikio mengine ni kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho na kuendelea kwa ukamilishwaji wa ujenzi wa machinjio ya kisasa yaliyopo Vingunguti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, mafanikio ni kuongezeka kwa uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 kwa mwaka 2015/2016 hadi tani 497,567 kwa mwaka 2019/2020. Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya sangara kutoka tani 23,000.6 kwa mwaka 2015/2016 hadi tani 27,596.3 kwa mwaka 2019/2020. Mafanikio mengine yakiwa ni kuongezeka mauzo ya samaki pamoja na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.3 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 506.2 kwa mwaka 2019/2020 na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Kuu Uvuvi Mbegani na ununuzi wa meli nne za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini; mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanzishwa kwa kampuni mpya ya *Twiga Minerals Corporation* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania hisa asilimia 16 na Kampuni ya *Barrick* hisa asilimia

84, ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; kuanzishwa kwa Kampuni ya *Tembo Nickel Corporation* ambapo ni ubia kati ya Serikali ya Tanzania ambayo ina asilimia 16 na Kampuni ya *LZ Nickel Mining Limited* ambayo ina hisa asilimia 84 kwa ajili ya uchimbaji wa madini wa *Nickel* Kabanga. Na mafanikio mengine ikiwa ni kuanzishwa kwa kiwanda cha *Mwanza Precious Metals Refinery (MPMR)* kwa ajili ya kuchenjua dhahabu na mafanikio mengine yakiwa ni kujengwa kwa masoko 39 na vituo 50 vya kuuzia madini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana yanajenga msingi wa kuendelea kutekeleza mpango wa maendeleo kwa kasi zaidi hususan kwa kuzingatia kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema "Kazi Iendelee". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maono na miongozo yake inatoa dira na mwelekeo mpya wa Taifa katika kutumia vyema fursa mbalimbali za kikanda na kimataifa. Natoa rai kwa Watanzania wenzangu tuyaenzi mafanikio haya na tuendelee kufanya kazi kwa bidii ili kuliletea mafanikio zaidi Taifa letu tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022; malengo na shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2021/2022; katika kipindi cha mwaka 2021/2022, shabaha za uchumi jumla zilizozingatiwa katika mpango ni kama ifuatavyo:-

Mosi, kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la Taifa kufikia asilimia 5.6 mwaka 2021; kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 5.0 katika muda wa kati.

Tatu, mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2021/2022 na wastani wa asilimia 16.3 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2023/2024. Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya

Pato la Taifa kwa mwaka 2021/2022 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2020/2021; kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na la mwisho kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2021/2022; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Hivyo, miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2021/2022 inaakisi maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambayo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu, na kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kipaumbele inayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/ 2022 inajumuisha miradi ya kielelezo ambayo ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa *(Standard Gauge Railway);* mradi wa kufua umeme wa maji wa Mwalimu Julius Nyerere – MW 2,115; kuboresha Shirika la Ndege; mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga na mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika ulioko kule Lindi.

Mheshimiwa Spika, mingine ni miradi ya magadi soda ambayo ni ya Engaruka, makaa ya mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga, mradi wa kufua umeme wa maji ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) ulioko Njombe, ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu, bandari ya uvuvi Mbegani na ununuzi wa meli za uvuvi. Miradi mingine ni Kiwanda cha sukari Mkulazi, ufuatiliaji wa mafuta na gesi katika vitalu vya Eyasi Wembere mpaka kule Luono, Wilayani

Iramba na *Mnazi Bay* kule *North,* pamoja na Kanda Maalum za Kiuchumi, na kuongeza rasilimali watu yenye ujuzi adimu na wataalam wa ujuzi wa kati na wabobezi kwa maendeleo ya viwanda na ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi, msukumo utawekwa katika miradi inayolenga kuwa na utulivu wa uchumi na uendelezaji wa reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, nishati, bandari, viwanja vya ndege pamoja na utekelezaji wa mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Katika eneo hili, miradi ifuatayo itapewa uzito:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uendelezaji wa miundombinu; reli, katika mwaka wa fedha 2021/2022 shughuli zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na, ukarabati wa njia kuu ya reli katika maeneo ya Tabora - Kigoma, Tabora – Isaka, Mwanza – Kigoma na matengenezo ya njia ya reli ya Tanga – Arusha. Ukarabati wa karakana na majengo ya reli, pamoja na ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa na ukarabati wa mabehewa, ukarabati wa mfumo wa ishara na mawasiliano wa reli, pamoja na uwekaji alama za mipaka katika maeneo ya reli.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara; kipaumbele kitawekwa katika barabara za lami zinazofungua fursa za kiuchumi ambazo ni barabara za Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea pamoja na Lukuyufusi – Mkenda (kilometa 122.5), Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena, Tabora - Ipole - Koga – Mpanda, barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (kilometa 235), Manyoni - Itigi – Tabora, Handeni– Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (kilometa 460) pamoja na Dodoma – Mtera - Iringa (km 273.), Dodoma – Babati (kilometa 243), Mbeya – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (kilometa 528), Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (kilometa 389), barabara ya Mtwara – Newala - Masasi (kilometa 210), Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba *Bay* (kilometa 343.2), barabara

ya Nzega – Tabora (kilometa 289), barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (kilometa 234.8), Igawa – Songwe –Tunduma na mchepuo wa Mbeya (kilometa 273.5) na Makambako – Songea na mchepuo wa Songea (kilometa 295). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani kama ambavyo zimeoneshwa katika kitabu cha hotuba. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara za kupunguza msongamano za Jijini Dar es Salaam ambazo ni kilometa 138.5 pamoja na barabara za mikoa, kuboresha miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kwa awamu zote nne, ujenzi wa barabara za juu utaendelea Jijini Dar es Salaam, barabara za mzunguko katika Jiji la Dodoma ambayo ni Makao Makuu ya nchi na barabara za vijijini na mijini kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA).* Vilevile Serikali itaendelea na ujenzi wa madaraja makubwa yakiwemo madaraja ya *New Wami* lililoko Pwani, Kitengule (Kagera), Kirumi (Mara) na Mkenda kule Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa majini, Serikali itaendelea kuboresha usafiri wa majini kwa kujenga na kukarabati meli katika maziwa makuu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari za Maziwa Makuu. Kwa upande wa usafiri wanga, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa jengo la pili la abiria, kuboresha huduma katika viwanja vingine vya ndege, kuendelea kuboresha viwanja vya ndege ikiwa ni pamoja na kiwanja cha Kimataifa cha Songwe, Msalato, viwanja vya mikoa pamoja na kuanza ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Kigoma, Sumbawanga, Tabora pamoja na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika chuo chetu cha Taifa cha Usafirishaji.

Kwa upande wa nishati, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Kinyerezi *I Extension*

- MW 185, Rusumo – MW 80, Malagarasi MW 45 na Kikonge – MW 330 na mradi wa njia za kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi pamoja na mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka - *North – West Grid Extension* (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi) na mradi wa kusafirisha umeme wa kV 220 Geita – Nyakanazi na mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 400 Singida - Arusha – Namanga. Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini pamoja na miradi ya gesi asilia na mafuta ikijumuisha ujenzi wa bomba la mafuta safi kutoka Dar es Salaam hadi Ndola, Zambia na usambazaji wa gesi asilia kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapinduzi ya TEHAMA, Serikali itaendelea kuimarisha teknolojia ya habari na mawasiliano kwa kuendelea na upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi wa Mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi unaojumuisha mradi wa Tanzania ya kidigitali na kuimarisha matumizi ya Serikali mtandao katika utoaji huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma, miradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni uzalishaji viwandani; miradi itakayotekelezwa ni pamoja na, kiwanda cha mashine na vipuri *KMTC*, kuboresha Shirika la *Tanzania Automotive Technology Centre,* kiwanda cha kuunganisha matrekta ya *URSUS* kilichoko Kibaha na eneo la Kongano ya Viwanda – *TAMCO* na mradi wa mashamba na viwanda vya mazao ya mafuta. Aidha, Serikali itaendeleza maeneo maalumu ya uwekezaji *(SEZ/EPZ).*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo, maeneo yatakayopewa msukumo ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, kuongeza matumizi ya teknolojia na mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya

tabianchi, kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao na kuimarisha vituo vya utafiti wa mbegu bora, vyuo vya mafunzo na vituo vya mafunzo ya wakulima na huduma za ugani. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo zana, mbegu bora, mbolea na viuatilifu na kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao. Vilevile, Serikali itaendelea na kuhamasisha uzalishaji wa mazao yakiwemo mazao ya kimkakati ya mkonge, chikichi, tumbaku, pareto, korosho, kahawa na pamba na alizeti.

Mheshimiwa Spika, mifugo, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za ugani, tafiti, tiba na udhibiti wa magonjwa ya mifugo, kuboresha huduma za uhimilishaji mifugo, kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi miradi inayotarajiwa kutekelezwa inajumuisha kufufua Shirika la Uvuvi – *TAFICO*, kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasilimali za uvuvi na mazingira, kujenga na kuimarisha miundombinu ya mazao ya uvuvi ikiwa pamoja na kuratibu vituo vya ukuzaji viumbe vya maji na kuimarisha huduma za ugani pamoja na Taasisi ya wakala wa elimu ya mafunzo ya uvuvi *(FETA)* na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, vito vya thamani na gesi asilia, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo na kuanzisha mradi wa makaa ya mawe ya kupikia kupitia Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO* na kufanya tafiti za jiolojia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo na utafiti wa madini ya viwandani *(gypsum, iron, graphite, limestone, coal, radioactive, helium gas)* kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania – *GST*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma, mambo ambayo yanatarajiwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo; kwa upande wa maliasili, miradi inayotarajiwa kupewa kipaumbele ni pamoja na mradi wa kuendeleza maliasili na

kukuza utalii katika maeneo ya kipaumbele, mradi wa kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya wanyamapori tanzania, mradi wa kujenga uwezo wa taasisi na mafunzo ya misitu na ufugaji nyuki, mradi wa panda miti kibiashara, mradi wa kuwezesha mnyororo wa thamani ya mazao ya nyuki, mradi wa uendelezaji wa utalii wa mikutano na matukio, na programu ya misitu na uendelezaji wa mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu kwa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma na biashara, Serikali itawekeza na kuweka mkazo katika uendelezaji wa Kituo cha Biashara na Ugavi Kurasini ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa eneo hilo pamoja na kutafuta wawekezaji mahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za fedha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mpango kabambe wa maendeleo ya sekta ya fedha. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha na kuimarisha uendeshaji wa Benki ya Maendeleo - *TIB*, pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kilimo – *TADB,* pamoja na Soko la Mitaji na Dhamana, huduma za bima, huduma ndogo za fedha pamoja na huduma jumuishi za fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usimamizi wa Mashirika ya Umma, Serikali, Serikali itaimarisha usimamizi na uendeshaji wa Mashirika ya Umma ili kuyahakikishia kuwa yanazalisha na kutoa huduma kwa tija na kwa upande wa usimamizi wa uchumi jumla, Serikali itaendelea kuimarisha usimamzi wa viashira vya uchumi jumla ikijumuisha, kudhibiti mfumuko wa bei, utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti ili kuchochea ukuaji wa uchumi, kuimarisha uzalishaji na mauzo nje, mambo mengine yatakayofanyika ni kuongeza ajira, mapato ya fedha za kigeni, na kupunguza utegemezi wa kibajeti na hivyo kujiimarisha na kuimarisha ustawi wa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza uwekezaji na biashara, Serikali itaendelea kutekeleza mpango wa kuboresha biashara na uwekezaji *(blueprint)* ili kuvutia

uwekezaji wa sekta binafsi. Miradi mahsusi itayotekelezwa ni pamoja na mradi wa kuboresha mfumo wa kodi, mradi wa uendelezaji wa masoko ya bidhaa, kuendeleza na udhibiti wa ubora wa bidhaa na kukuza soko la biashara Tanzania – *TMX* kwa kujumuisha mazao ya chai, mkonge, kokoa, kahawa, mpunga, mahindi, mbao, pamba, pamoja na mazao ya mifugo na nyanya kwenye soko la bidhaa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuchochea maendeleo ya watu, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unaakisi maisha ya watu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha maisha ya watu kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu na mafunzo kwa ujumla, afya na ustawi wa jamii, kinga ya jamii, huduma za maji na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali itatekeleza miradi ifuatayo; kwa upande wa afya na ustawi wa jamii, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa za mikoa, kuboresha miundombinu katika hospitali za mikoa, kuimarisha upatikanaji wa damu salama, kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa hospitali za halmashauri, vituo vya afya pamoja na zahanati. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya maendeleo ya jamii pamoja na kuwezesha huduma za ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, mambo yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea na utoaji wa elimu msingi bila ada na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi pamoja na vyuo vya ualimu. Aidha, Serikali itaendelea na ukarabati wa vyuo vikuu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ardhi, mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi; katika kuendelea kupanga, kupima

na kuimarisha ardhi hapa nchini na vijijini, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya uimarishaji wa mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani, na uimarishaji wa miundombinu ya upimaji wa ramani na uboreshaji wa milki za ardhi na upangaji wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma ya majisafi na majitaka, Serikali itaendelea kuboresha huduma za maji mijini na vijijini kwa kutekeleza miradi ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa, ikiwa ni kujenga na kukarabati miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa, kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya Masasi – Nachingwea, Same – Mwanga – Korogwe, Ziwa Victoria – Igunga, Nzega na Tabora, Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na kuboresha huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hifadhi ya jamii. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuimarisha Programu ya Kusaidia Kaya Maskini na kuboresha huduma za hifadhi ya jamii kwa kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Jamii (2019/2020 - 2022/ 2023).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, Serikali itaendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kupitia utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali ikiwemo, kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kuwezesha taasisi za fedha zinazogharamia maendeleo ambazo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na Benki ya Maendeleo *(TIB)* kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuongeza mapato katika Halmashauri zetu, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuwezesha halmashauri kujitegemea kimapato ikijumuisha miradi ya masoko ya kimkakati, stendi, maegesho ya malori, viwanda ili kuongeza wigo wa utoaji huduma, na kuimarisha ukusanyaji wa mapato na hatimaye halmashauri zetu kuweza kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendeleza rasilimali watu, msukumo wa pekee utawekwa katika miradi na programu ambazo zinalenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasilimali watu hapa nchini. Miradi na programu hizo ni pamoja na ukuzaji ujuzi wa nguvukazi na kuimarisha upatikanaji wa takwimu za soko la ajira, kukuza ubunifu na kuwezesha uhawilishaji wa teknolojia kwa vijana na watu wenye ulemavu na kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango na umuhimu wa sekta binafsi katika ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa utaratibu wa Ubia kati ya sekta binafsi pamoja na sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa ikijumuisha kukarabati na kujenga majengo ya Ofisi za Balozi katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Oman na Ethiopia. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyumba tisa vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia, Kurasini - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa mpango wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 utaendelea kuzingatia umuhimu wa kuimarisha Muungano wetu. Miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa pamoja Tanzania Bara na Zanzibar ni pamoja na:-

(i) Kukarabati na kujenga Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Wete - Pemba na Kilimani – Dodoma na kukamilisha ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu – Zanzibar.

(ii) Kuongoa ardhi iliyoharibika na kuboresha kingo za mito katika maeneo ya Kaskazini A - Unguja na Kishapu - Shinyanga katika maeneo ya mradi kwa kutekeleza miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kupitia mfumo wa ikolojia.

(iii) Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo wa Jamii *(TASAF III).*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele yanapatikana katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Nne.

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa mpango; kwa mwaka 2021/2022, shilingi trilioni 13.33 zinakadiriwa kutumika ili kugharamia miradi ya maendeleo, kiasi hicho ni sawa na asilimia 37 ya Bajeti yote ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 6.18 ni matarajio ya mapato ya ndani na shilingi trilioni 4.19 ni mkopo wa ndani na nje yenye masharti ya kibiashara na shilingi trilioni 2.96 ni misaada na mikopo nafuu kutoka nje. Sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo itatumika kugharamia utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Aidha, miradi mingine ya maendeleo, itaendelea kugharamiwa kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma pamoja na sekta binafsi *(PPP)* pamoja na utaratibu wa Kampuni Maalum *(Special Purpose Vehicles).*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa kufanya yafuatayo; kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kupanuka kwa wigo wa walipakodi; kuimarisha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari ikiwemo kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA na kutoa elimu kwa umma. Pili ni kuendelea na kuimarisha sekta isiyo rasmi; kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na kuendelea kuijengea uwezo *TRA* kwa kuongeza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji ni moja ya nyenzo muhimu itakayowezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Katika mwaka 2020/2021 Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya ufuatiliaji wa tathmini wa miradi 248 katika sekta za Uchukuzi, Viwanda, Elimu, Afya, Ujenzi, Utawala Bora, Kilimo, Mifugo, Maji na Barabara inayotekelezwa Tanzania Bara na

Visiwani. Serikali itaendelea kutumia mbinu na viashiria vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ili kupima utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 na kuchukua hatua za kutatua changamoto zitakazobainika katika utekelezaji. Aidha, Serikali itaendelea kuzingatia miongozo mbalimbali ya ufuatiliaji wa tathmini ya mpango ikiwemo Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348. Vilevile Serikali itatoa Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Tathmini ya Miradi ya Maendeleo kwa ajili ya kuongoza uratibu na ufuatiliaji na tathmini ili kupata matokeo yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inazielekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, pamoja na Wakala za Serikali, Taasisi pamoja na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafsiri malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022 – 2025/2026 katika Mipango na Bajeti za Kisekta kwa mwaka 2021/2022. Aidha, Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa mpango kazi pamoja na kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo na kuwajengea uwezo watumishi katika tasnia ya ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kuandaa na kutoa miongozo mbalimbali ya ukusanyaji, uchambuzi na uchakataji wa takwimu za viashiria vitakavyosaidia katika ufuatiliaji, tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Spika, katika majumuisho kama nilivyoeleza hapo awali, Mpango huu ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya

Watu." Kama inavyofahamika, nchi yetu imefanikiwa kuingia katika kundi la nchi za hadhi ya uchumi wa kipato cha kati kupitia utekelezaji wa mipango iliyotangulia. Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2021/2022 unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana ya kuimarisha utulivu wa viashiria vya uchumi jumla na kasi ya ukuaji wa uchumi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na kuongeza uwekezaji wa viwanda vinavyotumia nguvukazi na malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini hususan mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, madini na gesi asilia, kuendeleza ujenzi wa miundombinu wezeshi na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali ikijumuisha sekta ya viwanda na kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasilimali watu hapa nchini, hususan katika kuwajengea vijana stadi za kazi ili waweze kujiajiri na kuongeza tija katika uzalishaji na kuchochea maendeleo ya watu kwa kuimarisha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji pamoja na umeme vijijini.

Hitimisho; kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za kidini, washirika wa maendeleo na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ushirikiano wao umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ninawaomba waendelee kushirikiana na Serikali katika kutekeleza Mpango ili kufikia malengo tuliyojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni (Mbunge), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa 2020 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022.

Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Emmanuel Mpawe Tutuba kwa kusimamia kikamilifu maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mtani wangu Mheshimiwa Silo Daniel Baran, kama nilivyotangulia kusema awali wametusaidia sana wakiwa wanawakilisha Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango *www.mof.go.tz*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU L. NCHEMBA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2020 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2021/22 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika,**naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Taarifa hizo ndiyo msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 nitakayowasilisha katika Bunge hili Tukufu leo alasiri.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine katika Bunge hili baada ya majadiliano ya bajeti za mafungu mbalimbali. Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muhimu katika kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena, nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Chama cha Mapinduzi na Watanzania wote kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi, Amina. Aidha, nitoe pole kwa Taifa kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Balozi Mhandisi John Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangu kuapishwa kwake tumeshuhudia namna anavyoendelea kuliongoza Taifa letu kwa busara, hekima, weledi na umahiri mkubwa na kuendeleza mashirikiano na nchi mbalimbali. Aidha, niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ujasiri na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi wake kikamilifu.

5. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mhe. Othman Masoud

Othman Sharif kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vilevile, natoa pongezi kwa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Mhe. Rais kuendelea kuwatumikia watanzania katika wadhifa wake wa Waziri Mkuu.

6. **Mheshimiwa Spika,** kipekee natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa nitatekeleza jukumu hili kwa bidii, weledi, uadilifu na uzalendo wa kiwango cha hali ya juu.

7. **Mheshimiwa Spika,** kama unavyofahamu, nchi yetu na dunia kwa ujumla inakabiliwa na athari za UVIKO-19. Athari hizo zimesababisha kushuka kwa shughuli za kiuchumi duniani, ikiwemo uzalishaji, biashara, sanaa na burudani, utalii na usafirishaji wa bidhaa. Katika kukabaliana na athari hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali, ikiwemo kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa biashara duniani ili kutumia fursa zitokanazo na athari za UVIKO-19 kwa manufaa mapana ya Taifa na kuendelea kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga na maambukizi kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa na ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya.

8. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa za Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 zimezingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa wadau katika hatua za uandaaji na maamuzi katika ngazi zote serikalini. Ni vigumu kuwataja wadau wote waliotoa maoni na ushauri hadi kufikia hapa, lakini ni vyema nitambue mchango mkubwa wa Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Sillo Daniel Baran (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri makini waliotupatia. Uandaaji wa taarifa nilizowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu umenufaika

kwa kiasi kikubwa na mchango, ushauri na busara za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

9. **Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla na sekta mbalimbali kwa mwaka husika, ikilinganishwa na mwaka 2019. Aidha, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 yamezingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia rasmi Bunge hili la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021. Aidha, Mpango umezingatia Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda na kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Vilevile, Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia misingi ya mipango ya awali iliyolenga kuimarisha na kukuza uchumi fungamanishi, jumuishi na shindani unaohimili utandawazi. Katika kutekeleza Mpango wa mwaka 2021/22, msukumo mkubwa utawekwa katika kuliwezesha Taifa letu kutumia kikamilifu fursa zilizopo ili kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

## MWENENDO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2020

### Uchumi wa Dunia

10. **Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili 2021 inaonesha kuwa, mwaka 2020, dunia ilikuwa na mdororo wa uchumi kwa kupata ukuaji hasi wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na ukuaji chanya wa asilimia 2.8 mwaka 2019. Ukuaji hasi ulisababishwa na kupungua kwa shughuli za kiuchumi duniani hususan, biashara, usafirishaji na utalii kutokana na mlipuko wa UVIKO-19. Hata hivyo, uchumi wa dunia unatarajiwa kuimarika na kufikia ukuaji wa asilimia

6.0 mwaka 2021 na asilimia 4.4 mwaka 2022. Hii inatokana na matarajio ya kurejea kwa shughuli za kiuchumi kutokana na kuendelea kusambazwa kwa chanjo ya UVIKO-19 na hatua za kuinua chumi zinazochukuliwa na nchi mbalimbali.

**Uchumi wa Afrika na Kikanda**

11. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2020, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji hasi wa uchumi wa wastani wa asilimia 1.9, ikilinganishwa na ukuaji chanya wa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2019. Mdororo wa uchumi katika baadhi ya nchi ulitokana na athari ya zuio la baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwa ni njia ya kukabiliana na mlipuko wa UVIKO-19. Aidha, zuio la baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii lilisababisha kushuka kwa mauzo ya bidhaa nje ya kanda na kupungua kwa shughuli za utalii. Ukuaji wa uchumi katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2021 na asilimia 4.0 mwaka 2022.

12. **Mheshimiwa Spika,** Nchi zinazotegemea utalii kama chanzo kikubwa cha ukuaji wa uchumi zikiwemo Carpe Verde na Mauritius na zile zinazotegemea mafuta (Angola, Cameroon, Chad, Congo, Jamhuri ya Guinea, Gabon, Nigeria na Sudan ya Kusini) zilipata athari kubwa kutokana na UVIKO-19 na kuchangia ukuaji hasi wa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa ujumla mwaka 2020, nchi 32 kati ya nchi 45 za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara zilikuwa na ukuaji hasi wa uchumi sawa na asilimia 71.1 ya nchi zote, nchi mbili zilikuwa na ukuaji wa asilimia sifuri (0) na nchi kumi na moja (11) ikiwemo Tanzania zilikuwa na ukuaji chanya wa uchumi.

**Uchumi wa Taifa**

**Pato la Taifa**

13. **Mheshimiwa Spika,** licha ya mlipuko wa UVIKO-19 ulioathiri uchumi wa nchi nyingi duniani, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizokuwa na ukuaji chanya wa uchumi

kwa mwaka 2020. Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Ukuaji chanya ulitokana na hatua ya Serikali ya kuruhusu shughuli za kiuchumi na kijamii kuendelea na wakati huohuo wananchi wakisisitizwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya. Aidha, kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi nchini kulichangiwa na athari za UVIKO-19 katika nchi washirika wa kibiashara pamoja na mafuriko yaliyosababisha uharibifu wa miundombinu ya usafirishaji na kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo.

14. **Mheshimiwa Spika,** athari za janga la UVIKO-19 zilijitokeza zaidi katika shughuli za kiuchumi za malazi, huduma ya chakula pamoja na sanaa na burudani ambazo zilikuwa na ukuaji hasi kwa mwaka 2020. Sekta zilizokua kwa viwango vya juu kwa mwaka 2020 ni pamoja na: Sekta ya Ujenzi (asilimia 9.1); Habari na Mawasiliano (asilimia 8.4); Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 8.4); Huduma zinazohusiana na Utawala (asilimia 7.8); Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi (asilimia 7.3); Madini na Mawe (asilimia 6.7); na Afya na Huduma za Jamii (asilimia 6.5).

15. **Mheshimiwa Spika**, Pato ghafi la Taifa lililozalishwa nchini lilikuwa shilingi trilioni 148.5 mwaka 2020, ikilinganishwa na shilingi trilioni 139.6 mwaka 2019. Aidha, mwaka 2020, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu milioni 55.9, ikilinganishwa na watu milioni 54.2 mwaka 2019. Hivyo, Wastani wa Pato kwa Mtu lilikadiriwa kufikia shilingi 2,653,790, sawa na dola za Marekani 1,151.0 mwaka 2020 ikilinganishwa na shilingi 2,573,324, sawa na dola za Marekani 1,118.9 mwaka 2019, ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.1.

## Mwenendo wa Bei

16. **Mheshimiwa Spika,**mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo ulipungua kutoka wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2019 hadi asilimia 3.3 mwaka 2020. Aidha, mfumuko wa bei umebaki katika wigo wa asilimia 3.3 Mei 2021. Mwenendo wa mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu kutokana na upatikanaji wa chakula

cha kutosha, kushuka kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani na usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti.

## Utekelezaji wa Sera ya Fedha 2020/21

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, malengo ya sera ya fedha yalikuwa ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 9.0;

(ii) Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 10.0;

(iii) Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 13.5; na

(iv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.0.

18. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Benki Kuu imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi ambayo imesaidia kupunguza baadhi ya viwango vya riba katika masoko ya fedha hususan riba za mikopo. Wastani wa riba za mikopo ya benki kwa ujumla katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021 ulipungua hadi asilimia 16.58, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.91 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, na riba za mikopo ya kipindi cha mwaka mmoja zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 16.05 kutoka asilimia 16.37. Aidha, wastani wa riba za amana kwa ujumla ulikuwa asilimia 6.95 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.69 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.77 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021 ikilinganishwa na asilimia 8.01 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

## Ujazi wa Fedha na Karadha

19. **Mheshimiwa Spika,** ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi inayoendana na mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Wastani wa ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia shilingi trilioni 31.0 Aprili 2021 ikilinganishwa na shilingi trilioni 28.76 Aprili 2020, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kufikia shilingi trilioni 23.59 Aprili 2021 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.03 Aprili 2020, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Ongezeko hili la ujazi wa fedha ni matokeo ya usimamizi thabiti wa sera ya fedha.

## Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

20. **Mheshimiwa Spika,** Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 4.8 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Ukuaji mdogo wa mikopo kwa sekta binafsi ulitokana na athari za UVIKO - 19 kwenye shughuli za kiuchumi nchini. Aidha, sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa katika shughuli binafsi ambazo zilipata asilimia 35.8 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 15.7, uzalishaji viwandani asilimia 10.1 na kilimo asilimia 8.0.

## Ukuzaji Rasilimali

21. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2020, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika ulifikia shilingi trilioni 59.2 kutoka shilingi trilioni 55.8 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Aidha, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 7.8 kutoka shilingi trilioni 59.4 mwaka 2019 hadi shilingi trilioni 64.0 mwaka 2020. Vilevile, thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za miaka husika ilipungua kwa shilingi trilioni 4.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na upungufu wa shilingi trilioni 3.7 mwaka 2019. Ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma uliongezeka kwa asilimia 7.8 kufikia shilingi trilioni 19.0 mwaka 2020 kwa bei za miaka husika wakati katika sekta

binafsi uliongezeka kwa asilimia 7.8 kufikia shilingi trilioni 45.0 mwaka 2020.

**Sekta ya Nje**

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje uliimarika kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 1,177.2, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,443.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa kulichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu na bidhaa za maua na mbogamboga sambamba na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta na vyombo vya usafiri.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma ilifikia dola za Marekani bilioni 8.5 kutoka dola za Marekani bilioni 9.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii, ikiwa ni matokeo ya hatua zilizochukuliwa na mataifa mengine duniani ili kupunguza kasi ya maambukizi ya UVIKO-19, hususan kuzuia safari za kimataifa. Aidha, katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilifikia dola za Marekani bilioni 9.3, ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 10.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta, vyombo vya usafiri na vifaa vya ujenzi.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021, thamani ya mauzo ya bidhaa iliongezeka kufikia dola za Marekani bilioni 6.35 kutoka dola za Marekani bilioni 5.67 kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 12.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia ikiwemo dhahabu, madini mengineyo, bidhaa za maua na mbogamboga pamoja na bidhaa za viwandani. Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 7.4 kutoka dola za Marekani bilioni 8.75 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2020 hadi dola za Marekani bilioni 8.11 katika kipindi

kama hicho mwaka 2021. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa baadhi ya bidhaa kufuatia kuimarika kwa uzalishaji katika viwanda vya ndani, hususan bidhaa za ujenzi kama vile marumaru, nondo na saruji.

25. **Mheshimiwa Spika,** mapato yatokanayo na huduma yalipungua kutoka dola za Marekani bilioni 3.89 katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2020, hadi dola za Marekani bilioni 2.20 Aprili 2021. Aidha, malipo ya huduma yalipungua na kufikia dola za Marekani bilioni 1.19 kutoka dola za Marekani bilioni 1.73 kutokana na kupungua kwa malipo yanayohusiana na usafiri wa nje.

### Akiba ya Fedha za Kigeni

26. **Mheshimiwa Spika,** akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi Aprili 2021, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 4.97 ambayo inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takribani miezi 5.8. Kiwango hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0 na ni zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

27. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani imeendelea kuwa tulivu ambapo dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,298.5 Aprili 2021, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,291.3 Aprili 2020. Utulivu wa shilingi umetokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika usimamizi wa Sera za Fedha na Bajeti, kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nje ya nchi pamoja na mwenendo chanya wa baadhi ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Vilevile, hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania katika kusimamia misingi ya uwazi katika ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni nchini zimechangia

thamani ya shilingi dhidi ya sarafu nyingine kubwa duniani kuwa tulivu.

## Deni la Serikali

28. **Mheshimiwa Spika,** hadi Aprili 2021, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 60.9, ikilinganishwa na shilingi trilioni 55.5 kipindi kama hicho mwaka 2020. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 43.7 na deni la ndani ni shilingi trilioni 17.3. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Taarifa ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2020 inaonesha kuwa deni la Serikali ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia ukomo wa viashiria vyote vinavyokubalika kimataifa.

## MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA KIPINDI CHA 2016/17 – 2020/21

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21, Serikali ilikuwa inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 kupitia Mipango ya Maendeleo ya mwaka mmoja mmoja. Dhima kuu ya Mpango wa Pili ilikuwa ni "*Ujenzi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Serikali ilijenga miundombinu ya msingi ili kuwezesha wananchi kujiletea maendeleo na kuchochea uwekezaji katika viwanda. Katika kipindi hicho, mafanikio mbalimbali yalipatikana hususan kuimarika kwa ustawi wa uchumi na maisha ya watu. Mafanikio hayo yanajumuisha:

(i) **Miundombinu ya Reli:** Kufikia asilimia 91 ya ujenzi wa Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa *(Standard Gauge Railway - SGR)* kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) na asilimia 61 kwa kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422); na kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) wenye thamani ya shilingi trilioni 3.07. Mafanikio mengine ni: kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam - Isaka (km 970); kukamilika kwa ukarabati na kuanza kutoa huduma za

reli ya Tanga hadi Arusha (km 439); na kukarabatiwa kwa mabehewa 347 ya mizigo.

(ii) **Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere – MW 2,115**: Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kuchepusha maji (*Diversion Tunnel*); kuendelea na ujenzi wa bwawa (main dam and spillways), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels), ujenzi wa kituo cha kuzalishia umeme (Power House) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard) ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 52.

(iii) **Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania:** Kununuliwa kwa ndege mpya 11 ambazo zinasafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya nchi; kuboreshwa kwa karakana ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro; ununuzi wa jozi ya injini za akiba kwa ndege aina ya *Dash* 8 Q400; na kulipa bima za ndege *Boeing 787-8 Dreamliner na Dash 8 Q400*.

(iv) **Miradi ya Umeme:** Kukamilika kwa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Makambako hadi Songea; kukamilika kwa ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme pamoja na njia za kusafirisha umeme katika **Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Bulyanhulu – Geita**; kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kV 400 Singida – Arusha – Namanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 91.6; kukamilika kwa asilimia 80 ya utekelezaji wa **mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo - MW 80**; kuendelea na utekelezaji wa **mradi wa Kinyerezi I ExtensionMW 185** ambapo utekelezaji umefikia asilimia 84; kukamilika kwa usanifu wa miradi ya **Kakono MW 87** na **Malagarasi MW 45**; kuendelea na kuhuisha upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya Kufua Umeme wa Maji ya **Ruhudji MW 358** na **Rumakali MW 222**; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha **mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi**; na kuunganishwa umeme kwa jumla ya vijiji 10,312 kati ya vijiji 12,317, sawa na asilimia 83.7 ya vijiji vyote nchini.

(v) **Ujenzi na Ukarabati wa Viwanja vya Ndege:** Kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Geita (asilimia 95), Songea (asilimia 95) na Mtwara (asilimia 55); kukamilika kwa maandalizi ya mradi wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato ambao utagharimu dola za Marekani milioni 330, sawa na shilingi bilioni 759; uzinduzi wa ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu Euro milioni 50 sawa na shilingi bilioni 136.85; kukamilika kwa upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; na kufungwa kwa mifumo ya kuongoza ndege katika viwanja vya ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza.

(vi) **Uendelezaji wa Bandari: Bandari ya Dar es Salaam**: Kuboreshwa kwa gati namba 1 – 5; kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari (RoRo); na kuendelea na uboreshaji wa gati namba 6 na 7. **Bandari ya Mtwara:** kukamilika kwa ujenzi wa gati jipya lenye urefu wa mita 300 na yadi ya kuhudumia makasha. **Bandari ya Tanga:** kukamilika kwa uongezaji wa kina cha lango la kuingia meli kutoka mita nne (4) hadi mita 13, kuweka vifaa vya kuongozea meli pamoja na ujenzi wa magati mawili (2) kwenye kina kirefu.

**Bandari za Maziwa Makuu:** Kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Nyamirembe, Magarine, Lushamba, Ntama na Mwigoberokatika **Ziwa Victoria;** kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Sibwesa na Kabwe pamoja na kuendelea na ujenzi wa Bandari za Karema, Ujiji, Kibirizi na Lagosa katika **Ziwa Tanganyika**;na kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari ya Kiwira na Itungi katika **Ziwa Nyasa**.

(vii) **Kuboresha Huduma za Usafiri na Usafirishaji wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu**

**Ziwa Victoria na Tanganyika**: Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambao umefikia asilimia 74; na

kukamilika kwa ujenzi wa chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza chenye uwezo wa kubeba meli au chombo chenye uzito kuanzia tani moja (1) hadi tani 4,000.

**Ziwa Nyasa:** Kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili (2) yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja; na kukamilika na kuanza kufanya kazi kwa meli moja mpya ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo.

(viii) **Barabara na Madaraja Makubwa:** Serikali imeendelea kujenga na kukarabati mtandao wa barabara nchini kwa lengo la kufungulia fursa za kiuchumi katika maeneo mbalimbali, kuongeza wigo wa utoaji huduma za msingi na ustawi wa maisha ya watu. Mafanikio yaliyopatikana yanajumuisha: ujenzi wa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilomita 3,537 (barabara kuu na za mikoa kilomita 2,209 na barabara za halmashauri kilomita 1,328) hivyo kufanya mtandao wabarabara kwa kiwango cha lami kufikia kilomita 13,044. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni: kukamilika na kuanza kutumika kwa daraja la juu la Kijazi *(KijaziInterchange)*; kukamilika kwa asilimia 87.38 ya upanuzi wa barabara sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 19.2); kuendelea na ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) lenye urefu wa kilomita 3.2 na upana wa mita 28.5 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 27; kuendelea na ujenzi wa DarajajipyalaTanzanite (Dar es Salaam) ambao umefikia asilimia 77.19; na Daraja Jipya la Wami (Pwani) asilimia 50.

(ix) **Huduma za Afya:** Ujenzi wa hospitali 99 za halmashauri ambapo hospitali 67 zimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje; kujengwa kwa hospitali 10 za rufaa za mikoa; kukamilika kwa ujenzi wa zahanati 1,198; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la wodi namba 18 ya Sewa Haji pamoja na ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa binafsi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la mionzi katika Hospitali ya Rufaa Dodoma; kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru – Dodoma ambayo imeanza kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje; kununuliwa kwa mashine za

kidigitali zamionzi na *ultrasound*, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea *BACTEC 960 (Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT) na Blood culture machine* katika Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto; ununuzi wa mashine ya *Positron Emmission Tomography(PET Scan*) kwa ajili ya Hospitali ya Ocean Road; ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Mwananyamala umefikia asilimia 98; ujenzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Rufaa Njombe umefikia asilimia 73; kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa moja la huduma za upasuaji, radiolojia na maabara na kufikia asilimia 51 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Simiyu; kufikia asilimia 98 ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Burigi (Chato); na ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo upatikanaji wa aina 30 za dawa zenye kukidhi magonjwa ya msingi (*30 tracer medicines*) ulifikia asilimia 86 na upatikanaji wa aina 312 za dawa muhimu umefikia asilimia 74.

(x) **Elimu:** Kuendelea kutekeleza Sera ya Serikali ya kuongeza fursa za elimu bora kwa kila mtoto nchini kwa kugharamia elimumsingi bila ada ambapo wastani wa shilingi bilioni 20.8 zinatolewa kila mwezi; kujengwa kwa miundombinu muhimu katika shule 3,904 (Msingi 3,021 na Sekondari 883), mabweni 547, nyumba 101 za walimu, majengo ya utawala 25 na maktaba 43; kukamilika kwa ujenzi wa maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133; kukarabatiwa kwa shule kongwe 84 kati ya 89; kuongezeka kwa wigo wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu; kuanzishwa kwa vituo vya umahiri vya mafunzo katika taasisi za elimu ya ufundi; kuimarishwa kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika taaluma za anga na Chuo cha Ufundi Arusha katika taaluma ya nishati; na kuendelea kugharamia chakula na malazi kwa wanachuo wote katika vyuo 35 vya mafunzo ya ualimu vya Serikali.

(xi) **Maji Mijini na Vijijini:** Kukamilika kwa miradi 1,845 ya maji mijini na vijijini hivyo kuwezesha huduma za maji kufikia asilimia 85 kwa wananchi waishio mijini na asilimia 72.3 vijijini hadi Machi 2021. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na hatua

zilizofikiwa ni: kukamilika kwa miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kigoma (asilimia 90), Mwanza (asilimia 76) na Arusha (asilimia 62); na kukamilika na kuzinduliwa kwa Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega. Aidha, katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani) utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90.

(xii) **Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

**Kilimo:** Kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji hivyo kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020; kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa skimu 17 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 8,536 kupitia ASDP II na skimu tano (5) za Kigugu – Mvomero (hekta 195), Msolwa Ujamaa (hekta 40), Njage – Kilombero (hekta 75), Mvumi – Kilosa (hekta 249) na Kilangali *Seed Farm* – Kilosa (hekta 400) kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji wa mpunga – *Expanded Rice Production Project (ERPP)*; kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 76,726 mwaka 2020; na kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika makao makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo – Morogoro.

**Mifugo:** Kuimarishwa kwa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji kilichopo *Usa River* Arusha kwa kununua kifaa (Chiller) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha naitrojeni; kujengwa kwa viwanda vipya vya kimkakati vya nyama vya *Tanchoice* (Pwani), *Elia Food Oversees Limited* (Arusha) na *Binjiang Company Limited* (Shinyanga); kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Foodand Beverage Company Limited* (Arusha); kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha chanjo cha *Hester Bioscience AfricaLimited* (Pwani) chenye uwezo wa kuzalisha chanjo aina 37; kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho; na kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa machinjio ya kisasa Vingunguti.

**Uvuvi:** Kuongezeka kwa uvunaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.48 mwaka 2015/16 hadi tani 497,567 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 2.34 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya Sangara kutoka tani 23,000.6 mwaka 2015/16 hadi tani 27,596.3 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/20, jumla ya tani 777.8 za mabondo zilisafirishwa; kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi bilioni 379.3 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 506.2 mwaka 2019/20; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na ununuzi wa meli nne (4) za uvuvi.

(xiii) **Madini:** Kupitia na kutunga Sheria, Sera na mikataba ya madini; kuanzishwa kwa kampuni mpya ya *Twiga Minerals Corporation* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Tanzania (hisa asilimia 16) na Kampuni ya Barrick (hisa asilimia 84) ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; kuanzishwa kwa kampuni ya *Tembo Nickel Corporation* ambayo ni ubia kati ya Serikali ya Tanzania (hisa asilimia 16) na kampuni ya *LZ Nickel Mining Limited* (hisa asilimia 84) kwa ajili ya uchimbaji wa madini wa Nickel Kabanga; kuanzishwa kwa kiwanda cha *Mwanza Precious Metals Refinery (MPMR)* kwa ajili ya kuchenjua dhahabu;kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 50 vya kuuzia madini; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; kuimarishwa kwa ulinzi wa rasilimali za madini kwa kujenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24 wa Mirerani Manyara pamoja na kujenga *one stop centre*, kufunga vifaa vya ulinzi ikiwa ni pamoja na taa na *CCTV Camera* kuzunguka ukuta na barabara ya kuzunguka ukuta wa ndani; na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Lwamgasa (Geita), Katente (Bukombe) na Itumbi (Chunya).

30. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi hicho umewezesha kuimarika kwa uchumi jumla, hivyo kuiwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za hadhi ya kipato cha kati cha chini Julai 2020. Katika kuhakikisha kuwa mafanikio ya Tanzania kuingia kipato cha kati yanakuwa endelevu, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuweza kustahimili changamoto zozote zitakazojitokeza ikijumuisha: kuimarisha viashiria vya uchumi mpana na kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi; kuhakikikisha kuwa ukuaji wa uchumi ni shirikishi ili kupunguza umaskini; na kujenga na kuimarisha tabaka la watu wa pato la kati kwa kuendeleza rasilimali watu na uboreshaji wa huduma muhimu za msingi.

31. **Mheshimiwa Spika,** Mafanikio yaliyopatikana yanajenga msingi wa kuendelea kutekeleza Mipango ya Maendeleo kwa kasi zaidi hususan kwa kuzingatia kaulimbiu ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya ***"Kazi Iendelee"***. Maono na miongozo yake inatoa dira na mwelekeo mpya wa Taifa katika kutumia vema fursa mbalimbali za kikanda na kimataifa. Natoa rai kwa watanzania wenzangu tuyaenzi mafanikio haya na tuendelee kufanya kazi kwa bidii ili kuliletea mafanikio zaidi Taifa letu.

## MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2021/22

### Malengo na Shabaha za Uchumi Jumla kwa Mwaka 2021/22

32.**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2021/22, shabaha za uchumi jumla zilizozingatiwa katika Mpango ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.6 mwaka 2021;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 hadi 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 na wastani wa asilimia 16.3 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2020/21;

(v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2021/22**

33. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*". Mpango huu utatekeleza miradi na programu ambazo utekelezaji wake haukukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Hivyo, miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2021/22 inaakisi maeneo matano (5) ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Aidha, maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ni: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

34. **Mheshimiwa Spika,** miradi ya kipaumbele inayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka 2021/22 ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Miradi hiyo inajumuisha miradi ya kielelezo ambayo ni: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha

Kimataifa (Standard Gauge Railway) kwa kuendelea na ujenzi wa kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422) na kipande cha Mwanza - Isaka (km 341); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; miradi ya Magadi Soda Engaruka, Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga; miradi ya Kufua Umeme wa Maji ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) - Njombe; ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na ununuzi wa meli za uvuvi; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi Bay *North*; Kanda Maalumu za Kiuchumi; na kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa maendeleo ya viwanda na ustawi wa jamii.

35. **Mheshimiwa Spika,** katika *kuchochea uchumi shindani na shirikishi,* msukumo utawekwa katika miradi inayolenga kuwa na utulivu wa uchumi na uendelezaji wa reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, nishati, bandari, viwanja vya ndege pamoja na utekelezaji wa Mpango Kazi wa kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji. Katika eneo hili, miradi ifuatayo itatekelezwa:

### Uendelezaji wa Miundombinu

**(i) Reli:** Katika mwaka 2021/22, shughuli zitakazopewa kipaumbele ni pamoja na: Ukarabati wa njia kuu ya reli katika maeneo ya Tabora - Kigoma (km 411), Tabora – Isaka - Mwanza (km 385) na matengenezo ya njia ya reli ya Tanga - Arusha (km 470); ukarabati wa karakana na majengo ya reli; ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa na ukarabati wa mabehewa; ukarabati wa mfumo wa ishara na mawasiliano wa reli; na uwekaji alama za mipaka katika maeneo ya reli.

**(ii) Barabara na madaraja:** Kipaumbele kitawekwa katika barabara za lami zinazofungua fursa za kiuchumi ambazo ni: barabara za Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499); Lukuyufusi – Mkenda (km 122.5); Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena (km 220); Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 365.36); barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235); Manyoni - Itigi – Tabora (km 259.75); Handeni– Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (Km 460); Dodoma – Mtera - Iringa (km 273.3); Dodoma – Babati (km 243.8); Mbeya – Chunya – Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (km 528); Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7); Barabara ya Mtwara – Newala - Masasi (km 210); Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.2); Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7); Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 234.8); Igawa – Songwe –Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (km 273.5); na Makambako – Songea na Mchepuo wa Songea (km 295).

36. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani zikiwemo: barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117); Isaka - Lusahunga (km 242.2); Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba na Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel – Murugarama (km 141); Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56); Nyanguge – Musoma na mchepuo wa Usagara (km 202.25); Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4); Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 121); Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25); Tarakea – Holili (km 53); Barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2); na barabara ya Geita - Bulyanhulu - Kahama (km 120).

Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara za kupunguza msongamano za Jijini Dar es Salaam (km 138.5) pamoja na barabara za mikoa, kuboresha miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kwa awamu zote nne, ujenzi wa barabara za juu (Flyover) Jijini Dar es Salaam, barabara za mzunguko katika Jiji la Dodoma pamoja na barabara za vijijini na mijini kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini

(TARURA). Vilevile, Serikali itaendelea na ujenzi wa madaraja makubwa yakiwemo madaraja ya New Wami (Pwani), Kitengule (Kagera), Kirumi (Mara) na Mkenda (Ruvuma).

(i) **Usafiri wa Majini;** Serikali itaendelea kuboresha usafiri wa majini kwa kujenga na kukarabati meli katika maziwa makuu ikijumuisha *MV Mwanza Hapa Kazi Tu, MV Liemba* na *MV Umoja*, ujenzi wa maegesho ya vivuko na ununuzi na ukarabati wa vivuko. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara pamoja na bandari za maziwa makuu zikijumuisha Bandari ya Ziwa Victoria na Nyasa.

(ii) **Usafiri wa Anga:** Miradi itakayotekelezwa ni: Ukarabati wa jengo la Pili la abiria (JNIA-TB II); kuboresha huduma katika viwanja vingine vya ndege na ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji – NIT. Aidha, Serikali itaendelea na uboreshaji wa viwanja vya ndege ikiwa ni pamoja na kiwanja cha kimataifa cha Songwe, Msalato, viwanja vya mikoa pamoja na kuanza ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Kigoma, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga.

(iii) **Nishati:** Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Kinyerezi I Extension - MW 185, Rusumo – MW 80, Malagarasi MW 45 na Kikonge – MW 330; Mradi wa njia za kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi; mradi wa kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 400 - North – West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi); mradi wa kusafirisha umeme wa kV 220 Geita – Nyakanazi na mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 400 Singida - Arusha – Namanga. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini pamoja na miradi ya gesi asilia na mafuta ikijumuisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia) na usambazaji wa gesi asilia kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi.

(iv) **Mapinduzi ya TEHAMA**: Serikali itaendelea kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuendelea na upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; ujenzi wa Mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi unaojumuisha mradi wa Tanzania ya Kidigitali; na kuimarisha matumizi ya Serikali mtandao katika utoaji huduma kwa umma.

37. **Mheshimiwa Spika,** katika *kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma,* miradi ifuatayo itatekelezwa:

(a)**Uzalishaji Viwandani:** Katika eneo hili miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC; kuboresha Shirika la Tanzania Automotive Technology Centre (TATC); kiwanda cha Kuunganisha Matrekta ya URSUS – TAMCO – Kibaha; eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO; na mradi wa mashamba na viwanda vya mazao ya mafuta. Aidha, Serikali itaendeleza Maeneo Maalumu ya Uwekezaji (SEZ/EPZ) ya Tanga, Kigoma, Kahama, Bunda, Songwe, Manyara, Arusha na Mtwara; kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda na kilimo zikiwemo CAMARTEC, TIRDO, SIDO na TEMDO; na kuimarisha uzalishaji viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

(b)**Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II**

(i) **Kilimo**: Maeneo yatakayopewa msukumo ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji; kuimarisha huduma za upimaji matabaka na ubora wa udongo; kuwezesha uanzishwaji wa mashamba makubwa ili kuwa kitovu cha teknolojia bora kwa wakulima wadogo; kuongeza matumizi ya teknolojia na mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi; kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao ili kuongeza uzalishaji na tija; na kuimarisha vituo vya utafiti wa mbegu bora, vyuo vya mafunzo na vituo vya mafunzo ya wakulima na huduma za ugani. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo zana za kilimo,

mbegu bora za mazao, mbolea na viuatilifu; kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo; uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo; na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi. Vilevile, Serikali itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mazao yakiwemo mazao ya kimkakati ya mkonge, chikichi, tumbaku, pareto, korosho, kahawa na pamba.

(ii) **Mifugo:** Serikali kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) itaendelea kuimarisha huduma za ugani, tafiti, tiba na udhibiti wa magonjwa ya mifugo; kuboresha huduma za uhimilishaji mifugo; kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa; kujenga machinjio ya kisasa na minada ya mifugo; kuboresha huduma za unyweshaji mifugo, malisho na vyakula vya mifugo; na kuimarisha vyuo vya mafunzo ya mifugo.

(iii) **Uvuvi:** Miradi itakayotekelezwa inajumuisha kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania – TAFICO; kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasilimali za uvuvi na mazingira; kujenga na kuimarisha miundombinu ya mazao ya uvuvi; kukarabati vituo vya ukuzaji viumbe maji; kuimarisha huduma za ugani, Taasisi ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

(iv) **Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia:** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo na kuanzisha mradi wa makaa ya mawe ya kupikia (coal briqquette) kupitia Shirika la Madini la Taifa – STAMICO; na kufanya tafiti za jiolojia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo na utafiti wa madini ya viwandani (gypsum, iron, graphite, limestone, coal, radioactive, helium gas) kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania – GST.

(c) **Huduma**

(i) **Maliasili na Utalii:** Miradi itakayopewa kipaumbele ni pamoja na mradi wa Kuendeleza Maliasili na Kukuza Utalii katika Maeneo ya Kipaumbele – REGROW; mradi wa

Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori Tanzania; mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; mradi wa Panda Miti Kibiashara; mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Nyuki – BEVAC; mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio – MICE; na Programu ya Misitu na Uendelezaji wa Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu – FORVAC.

(ii) **Huduma za Biashara:** Katika kuendeleza huduma za biashara, Serikali itaweka mkazo katika uendelezaji wa Kituo cha Biashara na Ugavi Kurasini ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji wa eneo hilo pamoja na kutafuta wawekezaji mahiri.

(iii) **Huduma za Fedha:** Katika kuendelea kuimarisha huduma za fedha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha ili kuongeza utoaji wa mikopo ikijumuisha mikopo kwa miradi ya uhifadhi wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; utoaji elimu ya fedha kwa umma; na kuendelea kusimamia masoko ya mitaji. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha na kuimarisha uendeshaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo – TADB, Soko la Mitaji na Dhamana, huduma za bima, huduma ndogo za fedha pamoja na huduma jumuishi za fedha.

(d) **Usimamizi wa Mashirika ya Umma:** Serikali itaimarisha usimamizi na uendeshaji wa Mashirika ya Umma ili kuhakikisha kuwa yanazalisha na kutoa huduma kwa tija. Lengo ni kuyawezesha kujiendesha kwa faida na kutoa mchango stahiki (gawio) Serikalini kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

(e) **Usimamizi wa Uchumi Jumla:** Serikali itaendelea kuimarisha usimamzi wa viashira vya uchumi jumla ikijumuisha: kudhibiti mfumuko wa bei; utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti ili kuchochea ukuaji wa uchumi, kuimarisha uzalishaji na mauzo nje, kuongeza ajira, mapato ya fedha za kigeni, kupunguza utegemezi wa kibajeti na hivyo kuimarisha ustawi wa maisha ya watu.

38. **Mheshimiwa Spika,** katika *kukuza uwekezaji na biashara*, Serikali itatekeleza miradi na programu mbalimbali zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa katika kukuza biashara. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Biashara na Uwekezaji (Blueprint) ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Miradi mahsusi itayotekelezwa ni pamoja na: mradi wa kuboresha mfumo wa kodi; mradi wa uendelezaji wa masoko ya bidhaa; kuendelea na udhibiti wa ubora wa bidhaa; na kukuza Soko la Bidhaa Tanzania – TMX kwa kujumuisha mazao ya chai, mkonge, kokoa, kahawa, mpunga, mahindi, mbao, pamba, mazao ya mifugo na nyanya kwenye soko la bidhaa.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika eneo la *kuchochea maendeleo ya watu*, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unaakisi maisha ya watu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha maisha ya watu kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu na mafunzo kwa ujumla, afya na ustawi wa jamii, kinga ya jamii, huduma za maji na usafi wa mazingira. Katika mwaka 2021/22, Serikali itatekeleza miradi ifuatayo:

(i) **Afya na Ustawi wa Jamii:** Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa za mikoa za Mount Meru (Arusha), Mbeya, Sekou Toure (Mwanza), Mwananyamala (Dar es Salaam), Tumbi (Pwani), Maweni (Kigoma), Manyara, Mawenzi (Kilimanjaro), Katavi, Njombe, Geita, Simiyu, Songwe, Kwangwa (Mara) na Shinyanga; kuboresha miundombinu katika hospitali za mikoa; kuimarisha upatikanaji wa damu salama kwa kununua vitendanishi vya maabara, vifaa vya kuhifadhi damu na kugharamia uendeshaji Mpango wa Damu Salama**;** kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; kuendelea na mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma na magonjwa ya kuambukiza; kuimarisha vyuo vya mafunzo ya afya; kuimarisha tafiti za afya, huduma za tiba asili na tiba mbadala; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya nchini; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati. Aidha, Serikali

itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya jamii pamoja na kuwezesha huduma za ustawi wa jamii.

(ii) **Elimu:** Kuendelea na utoaji wa elimumsingi bila ada na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, uboreshaji wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na ujenzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya ualimu vya Ndala, Kitangali, Shinyanga na Mpuguso. Aidha, Serikali itaendelea na ukarabati wa vyuo vikuu vya Dar es Salaam, Mzumbe, Sokoine (SUA), Ardhi, Ushirika Moshi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

(iii) **Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:** Katika kuendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi mijini na vijijini, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya uimarishaji wa mipaka kati ya Tanzania na nchi jirani, uimarishaji wa miundombinu ya upimaji na ramani na uboreshaji wa milki za ardhi na upangaji wa matumizi ya ardhi.

(iv) **Huduma ya Maji Safi na Maji Taka:** Serikali itaendelea kuboresha huduma za maji mijini na vijijini kwa kutekeleza miradi ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa; kujenga na kukarabati miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ya Masasi – Nachingwea, Same – Mwanga – Korogwe, Ziwa Victoria – Igunga, Nzega na Tabora, Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga; kuboresha huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam; na kuendelea na ufuatiliaji na uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji – WSDP II.

(v) **Hifadhi ya Jamii:** Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kuimarisha Programu ya Kusaidia Kaya Maskini na kuboresha huduma za hifadhi ya jamii kwa kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Jamii (2019/20 - 2022/23).

(vi) **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi:** Serikali itaendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kupitia utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali ikiwemo: kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu; kuwezesha taaasisi za fedha zinazogharamia maendeleo ambazo ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na Benki ya Maendeleo TIB. Kupitia uwezeshaji huu, shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, uzalishaji viwandani na biashara zinatarajiwa kukuzwa na kuendelezwa.

(vii) **Kuongeza Mapato katika halmashauri:** Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuwezesha halmashauri kujitegemea kimapato ikijumuisha miradi ya masoko ya kimkakati, stendi, maegesho ya malori, viwanda ili kuongeza wigo wa utoaji huduma, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na hatimaye halmashauri kujitegemea.

40. **Mheshimiwa Spika**, katika *kuendeleza rasilimali watu,* msukumo wa pekee utawekwa katika miradi na programu ambazo zinalenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasimali watu nchini. Miradi na programu hizo ni pamoja na: ukuzaji ujuzi wa nguvukazi na kuimarisha upatikanaji wa takwimu za soko la ajira; kukuza ubunifu na kuwezesha uhawilishaji wa teknolojia kwa vijana na watu wenye ulemavu; na kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu.

41. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha tasnia ya habari, burudani na michezo, Serikali itaendelea kuongeza wigo wa usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); kukusanya na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo nchini; kujenga vituo vya mazoezi na kupumzikia wananchi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Geita; kuimarisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa nchini; na upanuzi wa Chuo cha Michezo cha Malya.

42. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mchango na umuhimu wa Sekta Binafsi katika ugharamiaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi

katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Baadhi ya miradi itakayotekelezwa ni: ujenzi wa viwanda vya dawa muhimu na vifaa tiba; uendeshaji wa huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza; ujenzi wa hoteli ya nyota nne na kituo changamani cha biashara katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Aidha, Serikali itaendelea kuishirikisha sekta binafsi zikiwemo taasisi za fedha katika kugharamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.

43. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa ikijumuisha kukarabati na kujenga majengo ya ofisi za balozi katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Oman na Ethiopia. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia Kurasini Dar es Salaam.

44. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 utaendelea kuzingatia umuhimu wa kuimarisha Muungano wetu. Miradi itakayotekelezwa kwa pamoja Tanzania bara na Visiwani ni pamoja na:

(i) Kukarabati na kujenga Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Wete - Pemba na Kilimani – Dodoma na kukamilisha ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Tunguu – Zanzibar;

(ii) Kuongoa ardhi iliyoharibika na kuboresha kingo za mito katika maeneo ya Kaskazini A (Unguja) na Kishapu (Shinyanga) katika maeneo ya mradi kwa kutekeleza mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kupitia mifumo ya ikolojia; na

(iii) Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF III)* ambapo shughuli zilizopangwa ni kutambua na kutathmini hali za ustawi wa maisha ya kaya 886,724 za walengwa wa Mpango na

kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 1,146,723 katika maeneo 186 ya utekelezaji kwa mizunguko sita (6) ya malipo Tanzania bara na Visiwani.

45. **MheshimiwaSpika,** maelezo ya kina kuhusu miradi ya kipaumbele yanapatikana katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Nne.

**Vihatarishi vya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2021/22**

46. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mpango unaweza kuathiriwa na vihatarishi vya ndani na nje. Vihatarishi vya ndani ni pamoja na: rushwa; uharibifu wa mazingira; ushiriki mdogo wa sekta binafsi; na kutotabirika kwa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Vihatarishi vya nje ni pamoja na: mabadiliko ya tabianchi; mtikisiko wa uchumi wa kikanda na kimataifa; majanga asilia; na mlipuko wa magonjwa yanayoathiri dunia.

47. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango, Serikali itachukua hatua mbalimbali ikijumuisha: Kuendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wanaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa; kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya biashara ili kupunguza gharama za uwekezaji; kuimarisha maandalizi ya miradi; kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na urasimishaji wa sekta isiyo rasmi kwa lengo la kuongeza wigo wa kodi; kuimarisha taasisi za ndani za kugharamia maendeleo ili kuwezesha upatikanaji wa mitaji; na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo ya kieletroniki ya Serikali.

Mikakati mingine ni pamoja na: Kuhamasisha uwekezaji wa ndani katika kujenga viwanda vya kuzalisha pembejeo za kilimo, ikijumuisha kuimarisha kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi – *Climate Smart Agriculture*; kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa ndani ili kuongeza ushindani katika masoko ya nje; kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano ili kuzuia matukio yanayoweza

kuhatarisha amani nchini; na kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kibiashara na maendeleo ya kiuchumi ya kikanda na kimataifa.

**Ugharamiaji wa Mpango 2021/22**

48. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/22, shilingi bilioni 13,326.8 zinakadiriwa kutumika ili kugharamia miradi ya maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 37 ya Bajeti yote ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 6,180.0 ni matarajio ya mapato ya ndani, shilingi bilioni 4,190.9 ni mikopo ya ndani na nje yenye masharti ya kibiashara na shilingi bilioni 2,955.9 ni misaada na mikopo nafuu kutoka nje. Sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo itatumika kugharamia utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Aidha, miradi mingine ya maendeleo, itaendelea kugharamiwa kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) pamoja na utaratibu wa Kampuni Maalum *(Special Purpose Vehicles)*.

49. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kwa kufanya yafuatayo: kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kupanuka kwa wigo wa kodi; kuimarisha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari ikiwemo kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA na kutoa elimu kwa umma; kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi; kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kuoanisha na kuboresha tozo na ada mbalimbali. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki *(Tanzania Electronic Single Window System - TeSWS)* ili kurahisisha upitishaji wa mizigo katika vituo vya mipakani pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini; kuendelea kusimamia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato *(Government Electronic Payment Gateway - GePG);* kusimamia malipo ya tozo na ada mbalimbali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki inawasilishwa kwa wakati kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya

Serikali. Vilevile, Serikali itaimarisha usimamizi wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa uratibu wa fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwa watekelezaji wa miradi ya maendeleo *(D-fund Management Information System)* pamoja na kuimarisha maandalizi ya miradi ya maendeleo.

**Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji**

50. **Mheshimiwa Spika**, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa ni moja ya nyenzo muhimu inayowezesha utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Katika mwaka 2020/21, Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 248 katika sekta za Uchukuzi, Viwanda, Elimu, Afya, Ujenzi, Utawala Bora, Kilimo, Mifugo, Maji na Biashara inayotekelezwa Tanzania Bara na Visiwani. Serikali itaendelea kutumia mbinu na viashiria vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ili kupimautekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2021/22 na kuchukua hatua za kutatua changamoto zitakazobainika katika utekelezaji. Aidha, Serikali itaendelea kuzingatia miongozo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini ya Mpango ikiwemo Sheria ya Ununuzi wa Umma, SURA 410, Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348. Vile vile, Serikali itatoa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kuongoza uratibu wa ufuatiliaji na tathmini ili kupata matokeo tarajiwa.

51. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa wadau, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itashirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi katika kuratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango itapokea na kuchambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo – NPMIS.

Vilevile, Wizara itaandaa na kutoa taarifa ya mwaka ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

52. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inazielekeza Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafsiri malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 katika Mipango na Bajeti za kisekta kwa mwaka 2021/22. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa Mpango Kazi pamoja na kuimarisha mifumo ya ndani ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo na kuwajengea uwezo watumishi katika tasnia ya ufuatiliaji na tathmini.

53. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kuandaa na kutoa miongozo mbalimbali ya ukusanyaji, uchambuzi na uchakataji wa takwimu za viashiria vinavyosaidia katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango. Miongozo hiyo itapaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi wakati wa kuandaa taarifa za kitakwimu za mwenendo na matokeo ya utekelezaji wa Mpango. Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma zitaandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na programu na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Vilevile, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Wizara ya Fedha na Mipango.

## MAJUMUISHO

54. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali, Mpango huu ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango

wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".* Kama inavyofahamika, nchi yetu imefanikiwa kuingia katika kundi la nchi za hadhi ya uchumi wa kipato cha kati kupitia utekelezaji wa Mipango iliyotangulia. Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2021/22 unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa kuimarisha utulivu wa viashiria vya uchumi jumla na kasi ya ukuaji wa uchumi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na kuongeza uwekezaji wa viwanda vinavyotumia nguvukazi na malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini hususan mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, madini na gesi asilia, kuendeleza ujenzi wa miundombinu wezeshi na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

55. **Mheshimiwa Spika,**Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali ikijumuisha sekta ya viwanda na kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasilimali watu nchini hususan katika kuwajengea vijana stadi za kazi ili waweze kujiajiri na kuongeza tija katika uzalishaji; na kuchochea maendeleo ya watu kwa kuimarisha utoaji wa huduma za afya, elimu, maji na umeme vijijini.

## HITIMISHO

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Washirika wa Maendeleo na Wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ushirikiano wao umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ninawaomba waendelee kushirikiana na Serikali katika kutekeleza Mpango ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

57. **Mheshimiwa Spika,** kipekeenaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Hamad Yussuf Masauni (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara

Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba kwa kusimamia kikamilifu maandalizi ya hotuba hii.

58. **Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango *(www.mof.go.tz)*.

59. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22.

60. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa uwasilishaji mzuri sana wa hotuba yako, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kilichowasilishwa kwenu ni Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Wasilisho hili tutalijadili wakati tutakapokuwa tunajadili habari ya huu mpango na hali ya uchumi pamoja na bajeti itakayokuwa inapendekezwa. Na jioni ya leo kuanzia saa 10:00 alasiri, nakumbusha saa 10:00 sio saa 11:00 tuliyozoea, saa 10:00 tutapata wasilisho la Makadirio ya Mapato na Matumizi ya

Serikali ambayo jina rahisi tunaita bajeti. Kwa hiyo, tutapata Hotuba ya Bajeti kuanzia saa 10:00 alasiri jioni ya leo.

Nawaomba sana tusome vizuri huu Mpango wa Hali ya Uchumi wa Taifa na Maendeleo ya Taifa, ili itisaidie katika kuelewa bajeti inavyokuja na kuweza kujipanga vizuri kwa ajili ya uchangiaji wiki ijayo. Ni matarajio ya meza kwamba kila Mbunge wiki ijayo atapata nafasi ya kuchangia, kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutakuwa na nafasi ya kesho, Ijumaa, keshokutwa Jumamosi na Jumapili katika kujipanga vizuri. Kuanzia Jumatatu basi iwe ni moja kwa moja uchangiaji *non stop,* mpaka dakika ya mwisho tutakayoambiana ambayo tutakuwa tunapiga kura ile sasa ya kupitisha bajeti hii itakayokuwa inapendekezwa.

Matangazo sio mengi; tunao wageni 17 kutoka Arusha, wageni wa Mheshimiwa Zaytun Swai na Mheshimiwa Mrisho Gambo, kama mpo ahsante sana na karibuni sana, karibuni sana wageni kutoka Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Naomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho Ijumaa, tarehe 11 Juni tutakuwa na majadiliano kuhusu masuala ya uchumi na bajeti. Majadiliano haya yatahusisha wabobezi wa masuala ya uchumi na bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Vyuo Vikuu, Taasisi ya Sekta Binafsi *(TPSF),* Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Kijamii *(ESRF),* Taasisi ya Utafiti wa Kupunguza Umaskini *(REPOA)* na wengine.

Majadiliano haya yatafanywa katika Ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 04:00 asubuhi hivyo Waheshimiwa Wabunge wote tunaalikwa kushiriki majadiliano hayo. Majadiliano haya yatatusaidia vilevile katika kuelewa vizuri zaidi kuhusu kilichowasilishwa hap ana kutuandaa vizuri zaidi wakati wa mjadala ambao tutaufanya wiki ijayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge kesho kuanzia saa 04:00 asubuhi tukutane pale Ukumbi wa Msekwa ili tuweze kupata *presentantion* hizo na tuweze kushiriki katika majadiliano hayo. *(Makofi)*

Mwisho nimeambiwa kuna mechi inaandaliwa ya wachezaji Waheshimiwa wa Bunge wa Simba na Yanga. Kwa hiyo, wale wa Simba wanaombwa wajiorodheshe kwa Mheshimiwa Festo Sanga na wale wa Yanga wanaombwa wajiorodheshe kwa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. *(Makofi)*

Basi kwa hatua hii tunashukuru, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwisharudi tuko naye humu mjengoni, karibu sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiri tuwaruhusu sasa mjiandae kwa ajili ya kurudi mapema, *around* saa 09:30 alasiri kila mtu awe amekaa hapa. Hotuba ya Bajeti ni vizuri ukaisikiliza tangu mwanzo mpaka mwisho badala ya iko katikati wewe ndio unaingia, na kadhalika, ili tujiandae vizuri kwa ajili ya mjadala wa wiki inayokuja.

Ni ukweli usiopingika ninapata *message* za baadhi ya wapiga kura wakiniuliza hivi Mbunge wetu yumo humo Bungeni? Kweli, kabisa sio utani, kwa sababu, wengine hawasikiki wanafikiri, kama nilivyowaambieni *day one,* kukaa hapa kimya sio sifa, ni *massacre* kwa upande wako kama Mbunge. Sio usemeseme, lakini *at some point* lazima useme na katika mambo makubwa kama haya ya bajeti basi jiandae vizuri na uongee vizuri, wapiga kura wakusikie na wafurahi. Kwa hiyo, nawasisitiza sana katika kujiandaa na kuzungumza; ukiona wapiga kura wanamuuliza Spika kama Mbunge wao yupo ujue tatizo limeanza tena 2021 hata sio 2024 kwa hiyo, tujiandae Waheshimiwa Wabunge.

Basi kwa hatua hiyo sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10:00 jioni ya leo.

*(Saa 4:55 asubuhi, Bunge lilisitishwa hadi saa 10:00 Jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukakaa. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa *Engineer* Masauni. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha ya Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba tulisema asubuhi ilitakiwa tuwe na hii *Monetary Policy Statement for the Year* 2021/2022 ambayo ndio hii sasa tumeshaipata, kama tulivyoambiana asubuhi tutaendelea na hoja za Serikali sasa. Katibu!

**NDG. NENELWA MWIHAMBI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu tunakushukuru.

Sasa ni wakati wa Bunge kupokea Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kwa hatua hii sasa bila kupoteza muda nimuombe *Sergeant-At-Arms* atuletee Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

*(Hapa Waziri wa Fedha na Mipango aliingia ukumbini akiongozana na Wapambe wa Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango sasa Bunge lipo tayari kukusikiliza na vizuri ukajua Taifa zima linafuatilia hotuba yako ili Bunge hili liweze kupokea sasa mapendekezo yako ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha, karibu uendelee na hotuba yako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inawasilisha bajeti ya kwanza ya kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Bunge lako Tukufu yanawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura namba 439 pamoja na Kifungu cha 124(4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Bajeti ya Serikali; kitabu cha kwanza ni Makadirio ya Mapato, kitabu cha pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea pamoja na Wakala wa Serikali, kitabu cha tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kitabu cha nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2021 pamoja na Muswada

wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2021 nayo ni sehemu ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022. Aidha, namshukuru Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani, umoja na mshikamano na kutupatia kiongozi mwadilifu, thabiti na imara chini ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa kwanza wa Bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba, 2020 ambapo Chama cha Mapinduzi kilipata ridhaa ya wananchi kuendelea kuongoza nchi. Ushindi mkubwa wa kishindo uliopatikana kwa CCM umedhihirisha siyo tu imani kubwa ya wananchi kwa Chama cha Mapinduzi, bali pia ni matarajio na kiu kubwa waliyonayo ya maendeleo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 17 Machi, 2021 Taifa letu lilipata msiba mkubwa wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu, wanafamilia hususan Mama Janeth Magufuli na Watanzania wote kwa msiba huo mzito. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ataendelea kukumbukwa kwa uongozi wake shupavu wenye uthubutu na uzalendo wa hali ya juu uliotoa mabadiliko chanya ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu aipumzishe Roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Watanzania walioondokewa na viongozi wetu akiwepo Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mhandisi Balozi John William Kijazi,

aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa Kwanza Mwanamke katika historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hapa niweke na ufunguo, Katika Hotuba yangu popote nitakapo tumia neno "mama yetu" nitakuwa namaanisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika muda mfupi wa uongozi wake, mama yetu ameonesha dhahiri kuwa ni kiongozi makini, shupavu, mchapakazi, mwadilifu, msikivu na aliye na dira na nia thabiti ya kuendelea kuliletea Taifa letu maendeleo makubwa. Aidha, nimpongeze mama yetu kwa kupata kura zote za ndio za wajumbe 1,862 wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wana CCM na Watanzania wote kwa ujumla wana imani kubwa sana kwake katika kuliongoza Taifa pamoja na chama chetu kama misingi ya Katiba ya Chama inavyoelezea, naomba Watanzania wote kila mmoja wetu kwa imani yake tuendelee kumuombea Mheshimiwa Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ili Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu yake na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inawasilisha Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Sita na Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo mengi kupitia hotuba zilizokuwa zimetangulia, moja ikiwa ni ile ambayo imeelezea kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, na kuyaendeleza mema yaliyo tokea na kuleta mengine mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, makadirio ya bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022 yameandaliwa kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026 ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2020 hadi 2050 pamoja na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, pamoja na Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo pamoja na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kurejea baadhi ya maeneo ambayo yamebainishwa katika hotuba hii ambayo yanatokana na hotuba za Mheshimiwa Rais ikiwa ni pamoja na kudumisha Tunu za Taifa yaani amani, umoja na mshikamano ambavyo ni msingi mkuu wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo yamezingatiwa ni pamoja na kuongeza tija ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuboresha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za fedha, ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na benki nyingine, mengine ni pamoja na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, uongezaji wa thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko, mengine ni kukuza sekta ya viwanda hususan vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini na vyenye kuajiri watu wengi kwa kila sekta, mengine ni kuendelea kuziba mianya ya utoroshaji wa madini na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia rasilimali za hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali niombe taarifa yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021; katika kipindi cha Bajeti ya

mwaka 2020/2021 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 34.88 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje, hadi Aprili 2021, shilingi trilioni 24.53 zimekusanywa sawa na asilimia 86.1 ya lengo la kipindi hicho. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania yaani *TRA* yalifikia shilingi trilioni 14.54, sawa na asilimia 86.9;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trilioni 1.80, sawa na asilimia 78.5 ya lengo;

(iii) Mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 607.4 sawa na asilimia 88.5 ya lengo;

(iv) Misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa ilikuwa shilingi trilioni 1.89 sawa na asilimia 70.4 ya lengo;

(v) Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipa dhamana za Serikali iliyoiva ilifikia shilingi trilioni 3.99, sawa na asilimia 95.7 ya lengo; na

(vi) Mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara ilifikia shilingi trilioni 1.68 sawa na asilimia 88.1 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mlipuko wa UVIKO-19 umesababisha kutofikiwa kwa baadhi ya malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani hususan kwa sekta za utalii, usafiri wa anga na uingizaji wa bidhaa kutoka nje.

Aidha, baadhi ya mashirika na taasisi zimeathiriwa na UVIKO-19 na hivyo kupungua kwa michango na gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mathalani, mapato ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania yameathiriwa kufuatia kuporomoka kwa shughuli za utalii kulikosababishwa na kusambaa kwa UVIKO-19 katika nchi zinazoleta watalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha lengo la mapato ya ndani linafikiwa, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya kibiashara na uwekezaji kama ambavyo ilivyokuwa imeainishwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara hapa nchini iitwayo *blueprint*. Misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa hadi Aprili, 2021 ni shilingi trilioni 1.89 kama nilivyotangulia kusema ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.82 ya mwaka 2019/2020. Pamoja na athari za mlipuko wa UVIKO-19, misaada na mikopo nafuu iliongezeka kwa asilimia 3.84.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa matumizi; Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2020/2021 yalikuwa shilingi trilioni 34.88 ambapo shilingi trilioni 22.10 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 12.78 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya shilingi trilioni 24.74 zimetolewa sawa na asilimia 86.8 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 17.42 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi trilioni 6.09 kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 4.49 Matumizi Mengineyo na shilingi trilioni 6.84 kugharamia Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021 jumla ya shilingi trilioni 7.32 sawa na asilimia 74.1 ya lengo zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi trilioni 6.24 ni fedha za ndani sawa na asilimia 79.7 ya lengo na shilingi trilioni 1.08 ni fedha za nje ikiwa ni sawa na asilimia 52.8 ya lengo. Katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Serikali iliendelea kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia maeneo ya vipaumbele kama yaliyoainishwa katika bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Ulipaji wa Deni la Serikali kwa wakati likiwa shilingi trilioni 6.84.

(ii) Ulipaji wa mishahara ya watumishi kwa wakati ikiwa ni shilingi trilioni 6.09.

(iii) Miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Mwalimu Julius

Nyerere na Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini yaani *REA* jumla ya shilingi trilioni 1.02.

(iv) Lingine ni ujenzi na ukarabati wa reli ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa ambao ni shilingi trilioni 1.49.

(v) Ujenzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege ikiwa ni shilingi trilioni 1.15.

(vi) Ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, wazabuni na watoa huduma, wakandarasi na washauri elekezi ikiwa ni shilingi bilioni 965.1.

(vii) Lingine ni mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, elimu msingi bila ada, uimarishaji wa vyuo vya *VETA*, kukuza ujuzi kwa vijana na ujenzi wa miundombinu ya elimu ambayo imetumia shilingi bilioni 406.6.

(viii) Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ni ununuzi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya ambayo imetumia shilingi bilioni 265.8.

(ix) Na nyingine ni miradi ya maji mijini na vijijini ambayo tayari imeshatumia shilingi bilioni 207.5.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhimilivu wa Deni la Serikali; tathmini ya uhimilivu wa Deni la Serikali ilifanyika Novemba, 2020 kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura Namba 134. Tathmini hiyo ilionesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Katika tathmini hiyo, viashiria vilionesha kuwa uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 17.3 ikilinganishwa na ukomo ambao ni asilimia 55; na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo ambao ni asilimia 240.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viashiria vinavyopima uwezo wa nchi kulipa deni, matokeo yalibainisha kuwa uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23 na uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 14.0 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 21. Kwa kuzingatia viashiria hivyo, Tanzania ina uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ya nchi ili kugharamia miradi yake ya maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo hiyo punde itakapokuwa imeiva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari za UVIKO - 19; katika kuendeleza juhudi za kukabiliana na athari za ugonjwa wa virusi vya korona, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu aliunda Kamati Maalum ya Wataalamu kuchambua athari za ugonjwa huo na kushauri namna bora zaidi ya kukabiliana nao. Kamati ilikamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa tarehe 17 Mei, 2021 ambapo pamoja na mambo mengine Kamati ilibaini kuwa Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani imeathirika kiuchumi, kijamii kutokana na UVIKO-19 hasa katika sekta muhimu zikiwemo afya, utalii, biashara, usafirishaji, sanaa pamoja na burudani, ambazo zimesababisha kushuka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya huduma nje, akiba ya fedha za kigeni na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha shughuli za uchumi zilizoathirika zinarejea katika hali yake ya kawaida kama ilivyokuwa kabla ya mlipuko wa UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 3 Mei, 2021 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akizungumza na Bi. Kristalina Georgieva - Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* kwa nia ya kuimarisha mahusiano katika masuala ya kiuchumi na kijamii ikiwemo suala la mikakati ya kukabiliana na athari za UVIKO-19. Kufuatia mazungumzo hayo, Wizara ya Fedha na Mipango imeanza majadiliano na *IMF* ya mkopo wa dharura *(Rapid Credit Facility - RCF)* wa dola za Marekani milioni 571. Mkopo huu ni wa masharti nafuu kwa ajili ya kukabiliana na athari

za kiuchumi na kijamii zitakazotokana na UVIKO-19 kama ambavyo Wizara ya Afya itabainisha utaratibu wa kutumika punde mchakato wa upatikanaji ukiwa umekamilika.

Mheshimiwa Spika, Sera za Bajeti kwa mwaka 2021/2022; shabaha za uchumi jumla; Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 yameandaliwa kwa kuzingatia misingi pamoja na shabaha mahsusi za uchumi jumla. Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.6 mwaka 2021 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.2 ifikapo 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya wastani wa asilimia 3.0 – 5.0 kwa mwaka 2021/2022;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/2022;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2021/2022 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2020/2021;

(v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada haizidi asilimia 3.0 na kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4.0); na

(vii) Mwisho kuhakikisha kuwa viashiria vya ustawi wa jamii vinaimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera pamoja na mikakati ya kuongeza mapato; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali

itaendelea kuweka vipaumbele zaidi vya ukusanyaji wa mapato ya ndani. Masuala muhimu ya kuzingatia ni pamoja na kuimarisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuendelea kutekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuweka mazingira rafiki kwa mlipakodi kwa lengo la kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogo na za kati na kupanua wigo wa walipa kodi;

(ii) Kuendelea kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwianisha na kufuta au kupunguza wigo viwango vya kodi, tozo ambazo ni za kero; *(Makofi)*

(iii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA;

(iv) Kuendelea kuboresha Mifumo ya Serikali ya Kieletroniki inayotumika kukusanya mapato na kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinatumia mfumo huo;

(v) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika Taasisi, Mashirika ya Umma pamoja na kuhakikisha kuwa magawio Pamoja na michango stahiki inawasilishwa kwenye Mfuko Mkuu; na

(vi) Mwisho ni kuimarisha usimamizi wa fedha za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo za kuimarisha ukusanyaji wa mapato Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhamasisha ushiriki na uwekezaji kwenye soko la ndani la fedha na kuorodhesha hatifungani za Serikali katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Kwa upande wa matumizi sera za matumizi katika mwaka 2020/2021 zilijumuisha yafuatayo; ikiwa ni kuelekeza

fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya; kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kama vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vinavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa taasisi zinazotoza ada, Serikali inaweka utaratibu mpya na endelevu wa kusimamia mapato na matumizi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA),* Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* na Wakala wa Meli Tanzania *(TASAC).* Hivyo, kuanzia mwaka 2021/2022 mapato yanayoendelea kukusanywa katika taasisi hizo yatapitia mfumo wa *GePG* na kuingizwa kwenye akaunti ya makusanyo *(holding account)* zilizopo Benki Kuu. Aidha, taasisi hizi zitapatiwa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na fedha kutolewa kwenye akaunti ya makusanyo baada ya kupata ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Vilevile Serikali itafanya ufuatiliaji wa matumizi ya taasisi hizi kila robo mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuweka utaratibu wa utoaji fedha kwa Taasisi za Uhifadhi jambo hili ambalo lilisemwa kwa hisia kali na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wewe mwenyewe kwa *TANAPA, NCAA, TAWA* ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza azma hii Serikali itatoa fedha za matumizi mengineyo kwa miezi miwili mwaka wa fedha unapoanza na kuendelea kutoa mwezi mmoja mmoja. Huku ikiwa wanaakiba ya mwezi mmoja ili kuweza kutatua tatizo la wao kuendelea kuwa na fedha ambazo wanazihitaji kwa ajili ya shughuli zao za kila siku. Kwa hiyo, hakuna mwezi watakuwa hawana fedha punde watakapokuwa wanahitaji kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele; Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022 ni ya kwanza katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Bajeti hii itajielekeza katika utekelezaji

wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye maeneo yale matano katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022; maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuchochea uchumi shindani na shirikishi;

(ii) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo;

(iii) Kukuza uwekezaji na biashara;

(iv) Kuchochea maendeleo ya watu; na

(v) Kuendeleza rasilimali watu. Hata tutakapofika katika hatua za kikodi maeneo mengi utaona yatakuwa na neno kupunguza ili kuweza kuenzi dhima hiyo ya mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uchumi shindani na shirikishi, Serikali itajielekeza katika kugharamia miradi ambayo itajikita katika kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kusimamia utulivu wa viashiria vya uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara za kufungua fursa za kiuchumi na kuunganisha nchi jirani pamoja na kupunguza msongamano wa mijini pamoja na barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, vingine ni madaraja, usafiri wa majini na angani na mageuzi ya TEHAMA pamoja na kutekeleza miradi ya Tanzania ya kidijitali. Mengine ni nishati, bandari na viwanja vya ndege; eneo hili limetengewa jumla ya shilingi trilioni 7.44 ikijumuisha shilingi trilioni 3.13 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Undani wa miradi hii na miradi mingine upo katika kitabu kikubwa cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu niliyowasilisha leo ya Hali ya Uchumi wa Taifa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 imeainisha kwa

kina maeneo ya kipaumbele ambayo Serikali itajiekeleza kupitia Bajeti ya mwaka huu. Pamoja na miradi ya kielelezo, Serikali itatekeleza miradi mingineyo ikiwemo na ule wa uboreshaji wa miundombinu ambayo inagharamiwa na mikopo yenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Miradi hiyo ni Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili *(DMDP II)* na ule wa Awamu ya Tatu ambao unakaribia kufikia makubaliano ambayo yanalenga kushughulikia bonde la mto Msimbazi pamoja na maeneo mengine kama ambavyo umeainishwa ukiwa unatajiwa kugharimu dola za Marekani milioni 120.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine katika hatua nyingine Serikali imeanza mazungumzo na Benki ya Dunia kupitia dirisha la *International Development Association (IDA)* kwa ajili ya mradi wa uboreshaji miundombinu katika majiji na miji 45 *(TAKTIK)* mradi ambao nimemuona Mheshimiwa Chumi akiwa anafuatilia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine muhimu maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajiandaa kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351. Kama mojawapo ya maandalizi ya utekelezaji wa Sensa ya mwaka 2022 mojawapo ya maandalizi ambayo yanafanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar inafanywa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar imekamilisha kuandaa kitabu cha Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi kwa mwaka 2022. Kitabu hiki kinaainisha namna ya usimamizi na utekelezaji wa zoezi zima la sensa, gharama ya kufanya sensa pamoja na muundo wa Sensa utakavyokuwa katika ngazi zote za kiutawala.

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi bilioni 328.2 zinatarajiwa kutumika kugharamia sensa ya mwaka 2022 kwa mwaka wa kwanza katika historia ya Sensa hapa nchini, Sensa ya mwaka 2022 itatumia teknolojia ya vishikwambi

*(tablets)* katika utengaji wa maeneo ya kijiografia na ukusanyaji wa takwimu za uwandani. Matumizi ya teknolojia hii yana manufaa makubwa, hasa katika kupunguza gharama na muda wa kukusanya na kuchakata takwimu, hali hiyo itawezesha matokeo ya Sensa ndani ya nchi yetu kupatikana kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ni jukumu la kila mtu, natoa wito kwa Kamati zote za Sensa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kwa ujumla wetu kuhakikisha tunatoa ushirikiano wa kutosha katika maandalizi ya sensa na wajitokeze wote siku ya kuhesabu watu. Lengo ni kuhakikisha watu waliolala nchini usiku wa kuamkia siku ya sensa (usiku wa sensa) wanahesabiwa na kuchukuliwa taarifa zao za kiuchumi, kijamii, mazingira makazi wanayoishi na mengine mengi kwa ajili ya kupanga mipango endelevu ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya wafanyakazi; Serikali inatambua na kuthamini mchango wa watumishi wa umma na wa sekta binafsi katika kukuza Pato la Taifa. Kwa kutambua hilo, Serikali inachukua hatua mbalimbali za kuboresha maslahi ya wafanyakazi kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira *(PAYE)* kutoka asilimia tisa hadi asilimia nane. Hatua hii ni mwendelezo wa juhudi za kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi, ambapo kiwango hicho kimepunguzwa kutoka asilimia 11 mwaka 2015/2016 hadi sasa asilimia nane itakayoanza kutumika katika mwaka wa fedha huu unaoanza 2021/2022; *(Makofi)*

(ii) Kufuta tozo ya asilimia sita iliyokuwa ikitozwa kwa ajili ya kulinda thamani ya mkopo wa elimu ya juu *(Value Retention Fee)* kwa wanufaika; na

(iii) Kutenga jumla ya shilingi bilioni 449 kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi 92,619. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Madiwani, Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata; Madiwani wenzetu wanafanya kazi nzuri sana za kusimamia shughuli za maendeleo kwenye kata zetu. Hawa ni Wabunge wenzetu, ni Wabunge wakaazi kwenye maeneo ya kata zetu ambao kila siku wako na wananchi kwenye shughuli za kusimamia shughuli za maendeleo na hata hivyo katika baadhi ya Halmashauri Madiwani hao wamekuwa wakikopwa posho zao, na wengine hufikia hatua ya kupiga magoti kwa Wakurugenzi wao Watendaji ili waweze walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikipunguza ufanisi katika kusimamia Halmashauri zetu kwani Madiwani wengi wanafanya maamuzi yatakayopendekezwa na Wakurugenzi wao Watendaji hata kama hayana maslahi kwa Halmashauri zetu na kwa Taifa ili tu waweze kulipwa posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeongelewa kwa hisia kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, nipende kuwaeleze kuwa kilio chenu hicho mama yetu amekisikia na alinielekeza nikae pamoja na Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Ummy Mwalimu ili tuweze kutafuta ufumbuzi wa jambo hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali Kuu ianze kulipa posho za kila mwezi za Madiwani moja kwa moja...*(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waheshimiwa Madiwani nchi nzima hawajakusikia kabisa. Tunaomba urudie hapo. *(Makofi/Vigelegele)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, narudia tena.

Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, napenda niwaeleze kuwa mama yetu amesikia kilio chenu, alinielekeza mimi pamoja na Waziri wa TAMISEMI kufuatilia jambo hili na kulipatia ufumbuzi suala hili. Napendekeza

kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali Kuu ianze kulipa posho za kila mwezi za Waheshimiwa Madiwani moja kwa moja tena kwenye akaunti zao kwa Halmashauri zote zenye uwezo mdogo na Halmashauri 16 zenye uwezo mkubwa wa Daraja A zitaendelea kutumia mapato yao ya ndani, lakini kwa kulipa posho za Madiwani kwenye akaunti zao. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maafisa Tarafa hawa ni viunganishi muhimu sana wa ngazi za kata zetu pamoja na Wilaya ambapo wengi wao hufanya kazi nzuri sana za kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali katika maeneo yao. Kwa kutambua umuhimu wao, Serikali ya CCM iliwapatia pikipiki viongozi hawa ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Hata hivyo, wengi wao walishindwa kugharamia ununuzi wa mafuta pamoja na matengenezo ya vitendea kazi hivi na kulazimika kuwachangisha wananchi na hata wengine kuomba msaada kwa wadau mbalimbali. Hali hii inapunguza sana ufanisi katika Tarafa zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia hotuba hii, napenda niwajulishe Maafisa Tarafa kuwa mama yetu amesikia kilio chao, hivyo, napendekeza kuanzia mwaka wa fedha 2021/ 2022, Serikali Kuu ianze kulipa posho ya shilingi 100,000 kwa mwezi kwa kila Afisa Tarafa ili waweze kumudu gharama za mafuta pamoja na matengenezo.*(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Watendaji wa Kata ni wasimamizi wa kazi za sekta zote na ni Watendaji Wakuu kwenye Kata zetu. Wengi wao wanafanya kazi katika mazingira magumu ili kufanikisha shughuli za maendeleo katika kata zetu ikiwemo kusimamia ukusanyaji wa mapato, masuala ya usalama na idadi kubwa ya watendaji hawa hutumia mishahara yao kufanya kazi mbalimbali ikiwemo ufutiliaji wa mapato ya Serikali kwa kukodi pikipiki ili kufanikisha shughuli zilizopo. Kwa ujumla wanafanya kazi nzuri ya kusimamia shughuli za maendeleo kwenye kata zetu. Jambo hili limeongelewa kwa hisia kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Rose Busiga, Mbunge wa Viti

Maalum (Geita) ambaye ni Mtendaji wa Kata Mstaafu na ikaungwa mkono na wabunge wengi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mama yetu amesikia kilio hicho na kutuelekeza kulitafutia ufumbuzi suala hili. Hivyo, napendekeza kuanzia mwaka 2021/2022 Serikali kuanza kulipa posho ya madaraka ya shilingi 100,000 kwa mwezi kwa kila Mtendaji wa Kata kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri yaliyokuwa yakitumika sehemu kulipa Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhudu madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; wastaafu wetu walilitumikia Taifa hili kwa uzalendo mkubwa, uadilifu na bidii kubwa sana. Hatuwezi kuhesabu mafanikio ya nchi yetu bila kutaja mchango wa wazee hawa. Kumekuwepo na changamoto za muda mrefu za ulipaji wa mafao yao kutokana na ufanisi mdogo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuhudumia wastaafu wetu. Hali hiyo kwenye mifuko yetu imechangiwa pamoja na mambo mengine na uwepo wa madeni ambayo mifuko inaidai Serikali. Hata hivyo kusababisha wastaafu wetu kukosa au kusubiri kwa muda mrefu ili kulipwa mafao yao.

Mheshimiwa Spika, Jambo hili pia limejadiliwa kwa hisia kali sana na Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni, wazee wetu hawa hupata shida sana ambapo baadhi yao hufadhiliwa malazi kwa kulala misikitini na makanisani na wengine hutegemea wahisani kuhudumia familia zao kinyume na mchango walioutoa katika ujenzi wa nchi hii. Niwatangazie wazee wetu kuwa mama yetu amesikia kilio cha wazee na kutuelekeza Wizara ya Fedha na Mipango kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu tukiwa pamoja na mama yetu Mheshimiwa Jenista Mhagama kukamilisha zoezi la kitaalamu ili kujua hali halisi ya madeni na namna bora ya kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kulipa madeni yanayodaiwa na mifuko kwa kutenga fedha kwenye bajeti na kutumia utaratibu wa kutoa hatifungani maalum isiyo taslimu *(Non-cash Special Bond)* zitakazoiva kwa nyakati

tofauti kuanzia miaka miwili hadi 25. Utaratibu wa hatifungani una faida mbalimbali zikiwemo; kuipa Serikali nafasi ya kibajeti ya kuendelea kutekeleza miradi mingine ya maendeleo; kuiwezesha Serikali kuyatambua madeni hayo kwenye kanzidata ya madeni; na kuzuia madeni hayo kuendelea kuongezeka kulingana na tathmini ya thamani ya madai *(actuarial valuation).* Aidha, utaratibu huo utaboresha mizania ya hesabu na mtiririko wa mapato yanayotokana na riba ya hatifungani hizo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hatua hii inakwenda kumaliza kabisa tatizo hilo la wazee wetu kudai haki yao kwa damu na machozi ilhali wakiwa wameudumu nchi yetu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea malalamiko kuhusu kucheleweshwa kwa michango ya watumishi kupelekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, baadhi ya Ofisi za Serikali kutopeleka kabisa michango hiyo. Jambo hili limekuwa likisababisha usumbufu kwa watumishi punde wanapostaafu. Hivyo, napendekeza kulipa michango hiyo moja kwa moja kutokea Hazina kwa taasisi zote ambazo watumishi wake wanalipwa mishahara yao kupitia Hazina yaani mishahara ipelekwe bila makato ili haya makato yapelekwe Hazina moja kwa moja kwenye mifuko. Taasisi ambazo zinalipa watumishi kutokana na vyanzo vyao vya mapato zitaendelea kupeleka michango ya watumishi wao kwa ufuatiliaji wa karibu wa Serikali. Serikali itafanya uhakiki na kulipa madeni ya michango ambayo haijawasilishwa kwenye mifuko hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi; katika Jeshi la Polisi kwa askari wapiganaji wetu, kuna utaratibu wa wapiganaji kufanya kazi kwa mikataba ya muda mfupi kwa miaka 12 kabla hawajapata ajira za kudumu. Jambo hili huwasababishia wapatapo mkataba wa kudumu wawe wamechelewa kwa miaka 12 ikilinganishwa na mtumishi mwingine aliyeingia moja kwa moja kwenye ajira za kudumu. Jambo hili linamadhara hasi katika itifaki ya utumishi wao pamoja na mafao ya mpiganaji anapostaafu. Hiki kimekuwa kilio cha muda mrefu cha askari wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, mama yetu amesikia kilio chao, alitueleza mimi pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Simbachawene kukutana na kutafuta suluhisho la jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumelifanyia kazi jambo hilo, napendekeza kuanzia mwaka 2021/2022 askari wa Jeshi la Polisi wataingia mkataba wa kipindi cha miaka sita na kuingia katika ajira ya kudumu ili waweze kuingia katika maslahi yao ya kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kurahisisha kasi ya utekelezaji wa miradi na katika kuimarisha usimamizi na ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya mabadiliko katika Kanuni ya 21 ya Sheria ya Bajeti, SURA 439 ili kuondoa changamoto iliyopo ya fedha ambazo hazijatumika hadi tarehe 30 Juni kila mwaka kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Jambo hili iliongelewa kwa hisia kali sana na Wabunge na Mheshimiwa Spika hata wewe umelisisitiza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yatatoa fursa kwa Maafisa Masuuli kuwasilisha taarifa ya fedha ambazo zitavuka mwaka hadi tarehe 30 Juni kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali badala ya siku 15 kabla ya mwaka wa fedha kumalizika. Fedha hizo zitawekwa kwenye Akaunti ya Amana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli ambazo hazijakamilika wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, kuanzia sasa hakutakuwa na fedha zenye miradi inayotekelezwa kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka wa fedha isipokuwa pale ambapo Maafisa Masuuli wamekiuka masharti ya Sheria ya Bajeti, SURA Namba 439 na Sheria ya Fedha za Umma, SURA Namba 348 ikiwemo kutokutumia fedha hizo au kuchukua fedha huku hawana miradi au kuchukua fedha na kuanza kutumia kwenye miradi ambayo haijakusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa kodi ya majengo; kumekuwa na changamoto kubwa katika ukusanyaji wa kodi ya majengo, hali iliyosababisha Serikali kubadili njia za ukusanyaji mara kwa mara. Kabla ya mwaka 2017/2018 Serikali ilitumia Serikali za Mitaa kuwapa jukumu la kukusanya lakini hazikufanya vizuri sana. Kuanzia mwaka 2017/2018 Serikali ilitumia Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi hiyo ambapo pia haikufanya vizuri, tena haikufanya vizuri ukilinganisha na ile ya Serikali za Mitaa. Ukusanyaji wa kodi hii kwa kutumia Serikali za Mitaa au Mamlaka ya Mapato Tanzania umekuwa ukitumia njia za kizamani ambazo zinahusisha watu kusafiri, kupanga foleni na kukusanya fedha taslimu *(cash).* Utaratibu huu unatumia gharama kubwa, muda na pia ni hatarishi kwa mapato.

Katika kuhakikisha kodi hii inafikia malengo, Serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wajasiriamali; wafanyabiashara na watoa huduma wadogo nchini wameendelea kutambulika kupitia vitambulisho vya wajasiriamali. Tangu kuanza kwa zoezi la utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara na watoa huduma wadogo hawa jumla ya vitambulisho milioni 2.3 vimegawiwa ambavyo vimewezesha kukusanya jumla ya shilingi bilioni 46.71. Lengo ni kuendelea kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji zao za biashara. *(Makofi)*

Katika mwaka 2020/2021 Serikali imefanya maboresho ya vitambulisho hivyo kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti na kufungua fursa kwa wajasiriamali kuweza kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea na uratibu wa kugawa vitambulisho hivi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ambayo ndiyo yenye mfumo wa kusajili wafanyabiashara hao, kuchapisha vitambulisho na kuwapatia Halmashauri husika kwa ajili ya kugawa.

Mheshimiwa Spika, sasa maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali; napenda sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapendekezo ya kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi, ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa hapa nchini na sheria mbalimbali na kurekebisha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Baadhi ya kodi, tozo na ada ninazopenda kuzirekebisha nimeziorodhesha hapa moja baada ya nyingine na nitazirudia kuzitaja moja moja kadri tunavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwanza Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani SURA Namba 148; napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA Namba 148 kama ifuatavyo; kama nilivyosema kwa ajili ya kuboresha mazingira na kufufua uchumi tumetumia neno kupunguza katika maeneo mengi na tulipopandisha ni kwa namna ya kulinda viwanda vya ndani.

Moja kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyumba vya ubaridi *(cold rooms)* vinavyotambuliwa kwa *HS Code 9406.10.10* na 9406.9010. Lengo la msamaha huu ni kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mbogamboga na maua nchini ili kuchochea kilimo cha kisasa. *(Makofi)*

Pili, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini *(precious metals)* na makinikia yatakayoingizwa nchini kwa ajili ya kuchenjuliwa, kuongezewa thamani na kuuzwa kwenye masoko ya madini yanayotambulika nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la pendekezo hili ni kuviwezesha viwanda vyetu vya uchenjuaji vilivyoanzishwa nchini kupata malighafi ya kutosha kwa ajili ya uchakataji na hatimaye kuongeza ajira na mapato kwa vijana, na kwa kutumia hii niwatangazie pia kote duniani pale ambapo kuna madini walete kwenye viwanda hivi masuala mengine ya ukiritimba ya kiutawala yatarekebishwa na hapa tutatengeneza *hub* nzuri ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za bima ya mifugo. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea shughuli za ufugaji nchini. *(Makofi)*

Nne, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa na huduma zitakazoingizwa au kununuliwa hapa nchini kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Mafuta Ghafi *(EACOP).* Lengo la marekebisho haya ni kutoa unafuu wa kodi katika utekelezaji wa miradi tajwa.

Mheshimiwa Spika, tano, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ghafi yanayotambulika kwa *HS Code 2709.00.00* kwa lengo la kutoa unafuu kwa mlaji ikiwemo Kampuni ya Uendeshaji wa Bomba la Mafuta *(EACOP).*

Mheshimiwa Spika, viwanja vyetu vingi vya michezo hapa nchini ni vibovu sana labda ukiacha tu *Majaliwa Stadium* iliyoko kule Ruangwa, vingi ni vibovu na ubovu wa viwanja hivyo unasababisha timu bora kama Yanga inashindwa kupata matokeo inapokwenda mikoani kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo timu bora kama Yanga ikienda mikoani inashindwa kupata matokeo, napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyasi bandia zinazotambulika kwa *HS Code 5703.30.00* na *5703.20.00* kwa ajili ya viwanja vya mpira vilivyoko kwenye majiji kwa kuanzia kwenye majiji. Msamaha huo utahusisha ridhaa kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania na jambo hili Waziri wa sekta amelipigania sana ili kuweza kuendeleza sekta yake. Lengo la hatua hii ni kuendeleza michezo na kukuza vipaji nchini, tukifanikiwa kwenye majiji bajeti zinazofuata tutaenda manispaa na baadaye tutaenda kwenye viwanja mpaka kwenye timu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kadi za kutengeneza vitambulisho vya Taifa zinazotambulika kwa *HS Code 3921.11.90.00* na malighafi

nyingine za kutengeneza kadi hizo zinazotambulika kwa *HS Code 3921.11.90.00* zitakazoingizwa nchini na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA).* Lengo la pendekezo hili ni kupunguza gharama za kutengeneza Vitambulisho vya Taifa na kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekwepo na ukiritimba katika kupokea fedha za misaada kwenye miradi ya maendeleo katika hitaji la kisheria la kusubiri idhini ya Baraza la Mawaziri likae ili kuidhinisha misamaha hiyo. Katika kumaliza tatizo hilo napendekeza kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Taasisi zisizo za Kiserikali *(NGOs)* kwenye bidhaa na huduma zitakazotumika kwenye miradi inayotekelezwa na taasisi husika. Aidha, taasisi zitakazonufaika na msamaha huo ni zile ambazo zina mikataba na Serikali yenyewe katika kupeleka ama kuchochea kupitia bidhaa hizo ambazo zinasamehewa katika Kodi ya Ongezeko la Thamani, mfano kama huduma zinazotolewa na *AMREF* na pamoja na *Christian Social Services* ambazo zinaudumia maeneo ambayo Serikali ina maslahi nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya mawasiliano imekuwa ikikua vizuri na kuwa kiungo muhimu cha kuongeza wigo wa wananchi ambao wako kwenye ulimwengu wa kidijitali na kwenye sekta ya fedha *(Financial Inclusion).*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye simu janja za *mkononi (smart phones) HS Code 8517.12.00,* vishikwambi *(tablets) HS Code 8471.30.00* au *8517.12.00* na modemu *(modems) HS Code 8517.62.00* au *8517.69.00.* Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya huduma za mawasiliano ili kufikia lengo la asilimia 80 ya watumiaji wa intaneti ifikapo mwaka 2025 kutoka asilimia 46 iliyopo sasa kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchanguzi wa CCM. Jambo hili Mheshimiwa Ndugulile ambaye ni Waziri wa sekta amelisimamia na anapanga asilimia hiyo iweze kufikiwa kwa ajili ya kuipeleka Tanzania kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mikebe inayotumika kuhifadhia maziwa inayotambuliwa kwa *HS Code 7310.29.20* ambayo kwa sasa haitumiki kwa ajili ya kazi hiyo na badala yake napendekeza kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mikebe ya kubebea maziwa inayotambulika kwa *HS Code 7310.29.90, 7310.10.00* na *7612.90.90.* Lengo la pendekezo hili ni kuwapunguzia gharama wazalishaji na kuchochea ukuaji wa sekta ya maziwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taa zinazotumia umeme wa jua zinazotambulika kwa *H.S. Code 85.13* na *94.05.* Lengo la pendekezo hili ni kuwianisha msamaha huu sambamba na msamaha unaotolewa chini ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ambayo inasamehe kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha nishati ya umeme wa jua pekee na kurahisisha usimamizi wake. Aidha, pendekezo hili linalenga kuweka usawa katika ulipaji kodi kwa watumiaji wa taa zinazotumia nishati za aina zote;

Mheshimiwa Spika, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye huduma ya usafirishaji na huduma zinazohusiana na usafirishaji wa mafuta ghafi kupitia bomba linalojengwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Tanzania na Uganda; kuzitambua bidhaa za mtaji zilizomo kwenye Sura 84, 85 na 90 ya Kitabu cha Ushuru wa pamoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kuwa bidhaa za mtaji zitakazostahili kupata kivutio cha ahirisho la malipo ya *VAT.*

Mheshimiwa Spika, kubadilisha utaratibu wa kutoa msamaha kwenye miradi ya Serikali inayogharamiwa na fedha za Serikali na fedha za wafadhili ambapo mnufaika wa msamaha huo atawasilisha maombi kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania badala ya utaratibu wa kuwasilisha kwa Waziri wa Fedha kwa ajili ya kupata ridhaa na kutoa Tangazo la Serikali (*GN*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia *GN* umekuwa ukikwamisha utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo hasa miradi ya maji na jambo hili Waziri mwenye sekta amekuwa akililia na amekuwa akipiga kambi Wizara ya Fedha kila wakati kufuatilia *GN* ili miradi yake iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linahusishwa pia miradi ile ambayo Mheshimiwa Spika uliisemea hapa ikiwepo ya Mara, ya Zanzibar, mazingira hapa Dodoma pamoja na mengine. Utaratibu huu utarahisisha na kuharakisha utoaji wa misamaha badala ya utaratibu wa sasa kutokana na *TRA* kuwa na ofisi kwa kila mkoa nchini kote na zinaweza kupokea, kuchambua na kusimamia matumizi sahihi ya misamaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Zanzibar, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kurudisha utaratibu wa kurejesha *VAT* kwa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na kutumika Tanzania Zanzibar. Hii inatokana na mfumo wa kutoza *VAT* kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa bidhaa za viwandani pekee kutowanufaisha wafanyabiashara wa Zanzibar wanaonunua bidhaa na kutozwa *VAT* Tanzania Bara na kutozwa tena *VAT* bidhaa hizo zinapopelekwa Zanzibar. *(Makofi)*

Aidha, inapendekezwa marejesho ya *VAT* yatakayofanyika kwa bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar yafanyike pia kwa bidhaa zitakazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na ufanisi wa marejesho, maboresho ya mifumo yatafanyika ili isomane baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kutokana na utaratibu huu, kiwango cha asilimia sifuri ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kilichokuwa kikitumika kitakuwa kimesitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato SURA Namba 332; napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA Namba 332 kama

inavyoonyeshwa kwenye jedwali lililopo kwenye kitabu chetu. Upande wa juu ya jedwali hilo unaonyesha mapato ilivyokuwa mwanzo ambapo kwa mapato ya jumla yasiyozidi shilingi milioni 3.2 hakuna kodi; kwa mapato yanayozidi shilingi milioni 3.2 ni asilimia tisa ya kiasi kisichozidi shilingi milioni 3.2; mapato ya jumla yanayozidi shilingi milioni 6.2 kiwango cha kodi shilingi 270,000 ikijumuisha asilimia 20 ya kiasi kinachozidi shilingi milioni 6.2 kwa mapato ya jumla yanayozidi shilingi milioni 9.1, shilingi 846,000 ikijumuisha na asilimia 25 ya kiasi kinachozidi shilingi milioni 9.1.

Kwa jedwali ya sasa viwango vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mapato yasiyozidi shilingi 3,240,000 hakuna kodi, mapato ya jumla yanayozidi shilingi 3,240,000 lakini hayazidi shilingi 6,240,000 asilimia nane ya kiasi kisichozidi shilingi 3,240,000. Kwa mapato ya jumla ya shilingi 6,240,000 lakini hayazidi shilingi 9,120,000 shilingi 240,000 jumlisha asilimia 20 ya kiasi kinachozidi shilingi 6,240,000.

Mheshimiwa Spika, mapato ya jumla yanayozidi shilingi 9,120,000 lakini hayazidi shilingi milioni 12; shilingi 816,000 jumlisha asilimia 25 ya kiasi kinachozidi shilingi 9,120,000. Mapato ya jumla yanayozidi shilingi milioni 12, shilingi 1,536,000 jumlisha na asilimia 30 ya kiasi kinachozidi shilingi milioni 12.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itakayochukuliwa ikiwa ni dhamira ya Serikali ya muda mrefu kuwapunguzia mzigo wa kodi wafanyakazi. Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato kwa shilingi milioni 14,178.06;

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ni kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwenye hatifungani za Serikali. Sheria ya Kodi ya Mapato ilisamehe Kodi ya Mapato kwenye hatifungani kwa mwaka 2002/2003 pekee. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha soko la ndani la hatifungani linaendelea kusaidia kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ukiritimba katika kupokea fedha za kutoka kwa nchi wahisani zinazokwenda kutekeleza miradi ya maendeleo. Napendekeza kurejesha utaratibu wa Mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya fedha kutoa msamaha kwenye Tangazo la Serikali yaani *GN* bila kuhitaji ridhaa kutoka kwa Baraza la Mawaziri kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za wafadhili kupitia mikataba inayoingiwa baina ya nchi hizo na Serikali ya Tanzania yenye kifungu kinachoruhusu msamaha wa kodi ya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuharakisha utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na misamaha na mikopo yenye gharama nafuu ambayo utekelezaji wake umekuwa ukicheleweshwa kusubiri ridhaa ya Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hili tuliona kama fedha ziko kwenye bilioni mbili/bilioni tatu kusubiri Baraza na nchi zina mkataba kama ilivyo Japan na Tanzania ni kuchelewesha miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Pia kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia mbili kwenye malipo yanayohusisha mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye kampuni na mashirika yote yanayojihusisha na usindikaji wa ununuzi wa mazao. Kwa sasa Taasisi za Serikali pekee kama vile Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* ndizo zinazokata kodi hiyo kwa kiwango cha asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, aidha, pendekezo hili halitahusisha wakulima wadogo na wale wanaouza mazao yao kwenye masoko ya msingi yaani *AMCOS* na kwenye magulio. Lengo la pendekezo hili ni kuweka usawa katika utozaji wa kodi kwa Kampuni zote zinazojishughulisha na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kufanya maboresho ya Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuwezesha ukokotoaji wa gharama za

uchakavu kwa kiwango maalum cha asimilia tano kwenye gharama za mali za ujenzi wa bomba la mafuta.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ni kuweka utaratibu maalum wa utozaji wa kodi ya wachimbaji wasio rasmi *(artisanal miners)* wenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni 100 kwa mwaka kama ifuatavyo:-

(i) Kutoza kodi ya wachimbaji wasio rasmi wa madini kwa kiwango cha asilimia tatu kwenye thamani ya mauzo ya madini pindi yanapopatikana;

(ii) Kuweka muda wa ulipaji kodi kuwa ni wa kati wanapouza madini na kulipa mrabaha kwenye Tume ya Madini au maeneo maalum yaliyoanzishwa chini ya sheria ya madini;

(iii) Kuweka wajibu kwa wachimbaji wadogo wa madini kama mwajiri kukata kodi ya mapato ya ajira kutoka kwa wafanyakazi wake pale panapokuwepo na tu madini yatakapokuwa yamepatikana na kuuzwa katika masoko ya madini;

(iv) Kuweka utaratibu maalum wa kulipa kodi ya zuio la ajira kuwa ni wakati mchimbaji mdogo anapouza madini na kulipa mrabaha katika masoko ya madini au vituo vingine vya uuzaji na ununuzi wa madini vinayotambuliwa na Tume ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura Namba 147; kwa mujibu wa kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, marekebisho ya viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuvihuisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi wa jumla.

Mheshimiwa Spika hata hivyo kutokana na biashara za bidhaa hizi kuzorota kutokana na athari za UVIKO-19, napendekeza kutofanya mabadiliko ya viwango maalumu vya ushuru wa bidhaa katika bidhaa zote zisizo za petroli

isipokuwa vinywaji vikali na bia zitakazotengenezwa kwa kutumia shayiri zisizozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia kufanya marekebisho ya Ushuru wa bidhaa kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye bia zinazotengenezwa kwa kutumia shayiri iliyozalishwa hapa nchini kutoka shilingi 765 kwa lita za sasa hadi shilingi 620 kwa lita. Lengo la mapendekezo haya ni kuchochea kilimo cha shayiri hapa nchini; *(Makofi)*

(ii) Kuanza kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye nyuzi za kamba za plastiki zinazoingizwa kutoka nje ya nchi au kuzalishwa hapa nchini zinazotambuliwa kwa *HS Code 55.11* na *56.07* isipokuwa zile zinazotumika kwenye uvuvi. Lengo la marekebisho haya ni kulinda mazingira na kuchochea uzalishaji na matumizi ya bidhaa za katani. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 2,644; na

(iii) Kuanzisha tozo ya ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye pikipiki zilizotumika kwa zaidi ya miaka mitatu zinazoingizwa nchini zinazotambuliwa kwa *HS Code 8711.* Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti uingizaji wa pikipiki chakavu na kulinda mazingira. Hatua hii inatarajiwa kuongeza ya mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 263.7.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye viwango vya pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Mapendekezo ya hatua mpya za viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa *HS Codes 8702.10.99* na *8702.20.99* yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mwendokasi.

Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha usafiri kwa wananchi Dar es salaam pamoja na maeneo mengine.

(ii) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba yaani *cotton yarn* zinazotambulika kwa *Headings 52.05, 52.06* na *52.07.* Lengo la hatua ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo na kuongeza thamani ya zao la pamba hapa nchini;

(iii) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki yanayotambulika kwa *HS Code 4011.40.00.* Lengo la hatua ni kuongea mapato ya Serikali kwa kuwa matairi haya ni bidhaa zilizokamilika kwa ajili ya mtumiaji;

(iv) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye siagi ya karanga inayotambulika kwa *HS Code 2008.11.00.* Lengo la hatua ni kulinda wazalishaji wa bidhaa hiyo hapa nchini;

(v) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye nyaya zinazotambulika kwa *HS Codes 7229.20.00* na *7229.90.00.* Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji wanaotumia bidhaa hiyo kama malighafi;

(vi) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye *milk cans* zinazotambulika kwa *HS Codes 7310.10.00* na *7310.29.90.* Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye sekta ya maziwa hapa nchini; *(Makofi)*

(vii) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye *LABSA* inayotumika kwa *HS Code 3402.11.00* kwa utaratibu wa *duty remission* Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga na maji hapa nchini;

(viii) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa *HS Code* 3208.20.00 na *3210.00.10* kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa ngozi hapa nchini;

(ix) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa *HS Codes 2710.99.00, 2528.00.00* na *3505.20.00* kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea hapa nchini; *(Makofi)*

(x) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya tumbaku iliyochakatwa vinavyotambulika kwa *HS* Code 5310.10.00 kwa utaratibu wa *duty remission.* Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa tumbaku hapa nchini;

(xi) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa *HS Codes 4819.20.90, 5407.44.00* na *3923.29.00* kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa chai hapa nchini;

(xii) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi ya kutengeneza masufuria ya *aluminium* inayotambulika kwa *HS Code 7606.92.00* kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa masufuria hayo hapa nchini;

(xiii) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa wanaounganisha pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha *frame* kwa kuwa zinatengenezwa hapa nchini

(xiv) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au 10 hadi asilimia sifuri kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za zinazotengeneza mabomba ya plastiki kwa *HS Codes* zinazotambuliwa kwenye jedwali nililoliweka hapo kwa utaratibu wa *duty remission*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa mabomba hayo nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji; hapa nchini kuwa wa uhakika. *(Makofi)*

(xv) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri kwenye mabati ambayo tumeainisha urefu wake yanayotambuliwa kwa *HS Code 7225.30.00.* Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji wanaotumia bidhaa hiyo kama malighafi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2020/2021 ni kama haya ambayo nimeyabainisha katika hotuba hii inayoendelea na hotuba kubwa ya kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikubaliana kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Customs Management Act*, *2004)* kwa kuweka thamani ya chini ya bidhaa isiyopaswa kutozwa ushuru wa Forodha kuwa dola za Marekani 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuliachia jukumu la uthaminishaji wa vitenge vinavyoingizwa hapa nchini kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili uthaminishaji wa bidhaa hiyo uzingatie kanuni zinazotolewa kwenye sheria hiyo.

Hata hivyo Usimamizi wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004, sambamba na hatua hiyo, tunapendekeza utaratibu wa kuthaminisha vitenge uwe dola za Marekani kati ya 0.7 kwa mita ya kitenge cha *polyester* na dola za Kimarekani 0.8 kwa mita ya kitenge chenye

pamba inapotokea thamani hiyo imewasilishwa ya chini ili kuweza kulinda malighafi zinazopatikana kutoka kwa wakulima wetu zinazotengeneza vitenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuondoa sharti la kuweka dhamana ya asilimia 15 ya ziada ya ushuru wa forodha inayopaswa kurejeshwa yaani *refundable* kwenye sukari ya matumizi ya viwandani. Lengo la hatua hii ni kuwaongezea wazalishaji ukwasi kwa kutowazuilia mtaji wao *(working capital)*. Hata hivyo, wazalishaji watakaobainika kufanya udanganyifu watarejeshewa sharti la pamoja na kuchukuliwa hatua nyingine za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuanzia sasa tutaondoa sharti la kuweka dhamana ya asilimia 15 ya ziada ya ushuru wa forodha ambayo ilikuwa inapaswa kurejeshwa kwenye bidhaa za sukari ya matumizi ya viwandani hatua hizi kwa ujumla wake zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 32,626.38

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanyia Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi SURA Namba 438 kama ifuatavyo:-

(i) Kufuta kifungu cha 92A kwa lengo la kuziwezesha mahakama kukusanya mapato yanayotokana na adhabu na faini zinazolipwa mahakamani badala ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kama ilivyo kuwa faini na adhabu kwa makosa mengine ambayo mahakama huyatolea maamuzi na hivyo kurahisisha ukusanywaji wa mapato hayo;

(ii) Kufuta kifungu cha 70(2) ili kumpa Mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kutekeleza matakwa ya sheria husika ya kurahisisha upunguzaji au uondoaji wa riba na adhabu ya madeni iwapo kutakuwa na sababu za msingi za kufanya hivyo; na

(iii) Kufanya marekebisho ya Kanuni Namba 15 ya ukokotoaji wa kodi za kimataifa yaani *Transfer Pricing Regulations* kwa kufuta kifungu kinachoweka adhabu ya

asilimia 100 kwa kushindwa kutekeleza matakwa ya sheria. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea walipakodi adhabu kubwa ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kuvutia uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 napendekeza kufanya marekebisho ya sheria ya fedha za serikali za mitaa kama ifuatavyo:-

(i) Kubainisha mazingira ambayo Kampuni iliyolipa tozo ya huduma haitawajibika kulipa tozo ya uzalishaji. Marekebisho hayo yanalenga kutatua mgongano uliojitokeza kwenye kutafsiri kifungu husika; na

(ii) Kupunguza ada za matangazo kama ifuatavyo:-

(a) Mabango yanayowaka kutoka shilingi 18,000 hadi shilingi 13,000;

(b) Mabango yasiyowaka kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 10,000;

(c) Matangazo ya ukutani kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 10,000;

(d) Matangazo ya kielektroniki kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 10,000;

(e) Matangazo kwenye magari kutoka shilingi 15,000 hadi shillingi 10,000

(f) Matangazo ya muda mfupi kwa siku kutoka shilingi 55,000 hadi shilingi 50,000; na

(g) Kila mabango 100 ya promosheni ya kwanza au sehemu ya fungu la mabango 100 ya kwanza kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika**,** ada zote hizi zinatozwa kwa futi za mraba. Kushushwa kwa ada hizi kutapunguza gharama

za kutangaza biashara nchini na hatimaye kukuza ushindani kwenye biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Majengo, Sura 289 napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya kodi ya majengo, Sura 289 ili ukusanyaji wa kodi ya majengo ufanyike kwa kutumia mfumo wa ununuzi na utumiaji wa umeme kwa kutumia *TANESCO* Kila mita ya umeme ina uhusiano na mmiliki wa jengo au mtumiaji wa mita, na kwa kuwa Sheria ya Kodi ya Majengo inataka kodi hiyo ikusanywe kwa mmiliki au mtumiaji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tunapendekeza asilimia 15 ya fedha hizo ambazo zitakuwa zimepatikana iende kwenye Mfuko wa Serikali za Mitaa ili iweze kufanya kazi ya kurekebisha miundombinu ikiwepo madawati, lakini pia kutumika kama *equalization grant* yaani tuweze ku-*standardize* zile Halmashauri ambazo zina hali mbaya zaidi na zile ambazo hazina hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sheria ya Ardhi, Sura Namba 113 napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Kanuni zake za mwaka 2001 kwa kupunguza tozo ya mbele yaani *premium* inayotozwa wakati wa umilikishaji wa ardhi kama ifuatavyo:-

(i) Napunguza tozo kutoka asilimia 2.5 hadi asilimia 0.5 kwa umiliki mpya wa ardhi; na

(ii) Napunguza tozo kutoka asilimia moja hadi asilimia 0.5 kwa urasimishaji.

Mheshimiwa Spika, lengo la pendekezo hili ni kuhamasisha umiliki wa ardhi, kukamilisha taratibu za kupata hatimiliki na kufanikisha sehemu kubwa ya ardhi kuandikishwa na kupunguza migogoro. Hatua za kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 9,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ushuru wa Stempu napendekeza kufanya Marekebisho Sheria ya Ushuru wa Stempu kwa lengo la kuhuisha viwango vilivyopo sambamba na mfumuko wa bei kwa kuwa viwango hivyo ni vya muda mrefu tangu mwaka 2006. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ushuru wa Stempu kutoka shilingi 500 hadi shilingi 2,000;

(ii) Ushuru wa Stempu kwenye Katiba za Makampuni kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 10,000;

(iii) Ushuru wa Stempu kwenye nyaraka za ubia ambazo mtaji wake unazidi shilingi 100,000 lakini hauzidi shilingi 1,000,000 kutoka shilingi 2,000 hadi shilingi 5,000;

(iv) Ushuru wa Stempu kwenye nyaraka za ubia ambazo mtaji wake unazidi shilingi 1,000,000 kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 10,000; na

(v) Ushuru wa Stempu kwenye nyaraka za kumaliza ubia kutoka shilingi 1,000 hadi 10,000.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura Namba 82; napendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria hii kama ifuatavyo:-

(i) Kupandisha kiwango cha chini cha idadi ya waajiriwa wanaostahili kulipiwa kodi kutoka wanne wa sasa hadi kumi. Lengo la marekebisho haya ni kuwapunguzia mzigo wa kodi kwa waajiri wenye idadi ndogo ya waajiriwa na kuchochea ukuaji wa uwekezaji hapa nchini;

(ii) Kufuta tozo ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa hospitali zinazomilikiwa na taasisi za kidini kwa kuwa taasisi hizi zimekuwa zikiisaidia sana Serikali kufikisha huduma za afya hata kwenye maeneo ambayo Serikali haijaweza kupeleka huduma kutokana na ufinyu wa bajeti. Aidha, taasisi hizi zimekuwa na ushirikiano na Serikali kwa makubaliano

maalum kwa baadhi ya maeneo ya kutoa huduma za afya. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa utoaji huduma za afya kwa vituo vya afya; na

(iii) Kuanzisha utaratibu mahsusi wa ulipaji wa tozo kwa wachimbaji wadogo wa madini kuwa ni asilimia 0.4 ya thamani ya mauzo ya madini itakayolipwa na mchimbaji mdogo wa madini pindi atakapouza madini hayo kwenye masoko na vituo vya madini vinavyotambulika na Tume ya Taifa ya Madini.

Kwa upande wa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura Namba 41, napendekeza kufanya mabadiliko ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi *(Gaming Tax on Winnings)* kutoka asilimia 20 hadi asilimia 15 kwenye michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo *(sports betting).* Lengo lake ni kuongeza wachezaji kwenye mchezo huo na kuzuia wasicheze *online* katika Mataifa mengine ambayo hayatozi gharama hiyo;

(ii) Kuongeza kiwango cha kodi katika michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo *(sports betting)* kwa mapato ghafi kutoka asilimia 25 ya mauzo ghafi hadi asilimia 30 ya mauzo ghafi. Ongezeko la asilimia tano litapelekwa moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa ajili ya kuendeleza michezo nchini. Hatua nyingine ya kuendeleza michezo itafanyika pale patakapokuwa shughuli ya bahati nasibu imeshaanza kufanya kazi hapa nchini wakati sasa hivi ikiwa inaendelea kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

(iii) Kutoza kodi ya michezo ya kubahatisha kwa asilimia kumi ya mapato ghafi kwenye michezo ya kubahatisha inayoendeshwa kwa kompyuta; na

(iv) Kutoza kodi ya michezo ya kubahatisha kwa asilimia kumi ya mapato ghafi kwenye michezo ya kubahatisha iliyo chini ya majaribio.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itaongeza mapato ya Serikali kwa jumla ya shilingi milioni 14,925.38.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ukaguzi wa Umma; napendekeza kufanya Marekebisho kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura Namba 418 kama ifuatavyo:-

(i) Kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa na uwezo wa kisheria wa kukagua mashirika yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ambayo Serikali ina umiliki wa hisa ili kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kukagua mashirika/makampuni hayo. Kwa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakagua mashirika/ makampuni hayo bila kuwa na nguvu za kisheria, hali inayoweza kuleta mgogoro wa kisheria. *(Makofi)*

(ii) Kumwezesha Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuwasilisha Bungeni majibu kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye kikao kinachofuata cha Bunge baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa yake badala ya utaratibu wa sasa ambapo taarifa zote huwasilishwa kwa pamoja katika kikao kimoja cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura Namba 134; napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura Namba 134 ili kuruhusu Serikali kudhamini kampuni au taasisi yoyote kukopa kiasi kisichozidi thamani ya Hisa za Serikali ya Tanzania kwenye mradi husika baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, ilivyokuwa sasa sehemu ambayo Serikali haina asilimia 51 ya hisa isingeweza kuweka dhamana. Sasa tunaposhiriki kwenye mradi kama wa bomba la mafuta ambapo tuna asilimia 15, tunahitaji kurekebisha sheria ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usajili wa Magari, Sura Namba 124; napendekeza kufanya marekebisho kwenye

Sheria ya Usajili wa Magari Sura Namba 124, kwa kupunguza ada ya usajili wa magari kwa namba binafsi kutoka shilingi 10,000,000 hadi shilingi 5,000,000 kila baada ya miaka mitatu. Lengo la hatua hii ni kuwezesha wamiliki wengi wa magari kuchagua namba binafsi ya usajili wa gari kwa gharama nafuu na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa kuwa kiwango cha sasa hakina mwitikio mzuri, amebaki Musukuma tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Magari zinatarajiwa kutuongezea shilingi milioni 270. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani Sura Namba 168; vijana wengi wamejiajiri kwenye sekta ndogo ya kuendesha bajaji pamoja na pikipiki zinazojulikana kama bodaboda. Hata hivyo, vijana hawa hupata usumbufu mkubwa sana wa kulipa faini kutoka kwenye vipato vyao pale inapotokea kwamba wamevunja Sheria ya Usalama Barabarani hata kama uvunjwaji umefanywa na abiria wao. Hali hii imekuwa ikisababisha baadhi ya vijana hao kushindwa kulipa faini na hivyo kuzitelekeza pikipiki zao kwenye vituo vya polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alielekeza Jeshi la Polisi kujikita kwenye kutoa elimu kuhusu usalama barabarani badala ya kuwekeza kwenye makosa na kugeuza faini kama chanzo cha mapato. Hivyo basi, niwatangazie bodaboda wote kwamba mama yetu amesikia kilio chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kupunguza adhabu zinazotolewa chini ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura Namba 168 kwa makosa ya pikipiki na bajaji kutoka shilingi 30,000 za sasa hadi shilingi 10,000 kwa kosa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, bodaboda hawajakusikia, wangependa tafadhali urudie wakusikie nchi nzima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, vijana wengi wa bodaboda wamekuwa wakipata taabu katika kulipa faini hizo, niwatangazie bodaboda wote kwamba mama yetu amesikia kilio chao, alituagiza mimi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Jeshi la Polisi kulifanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa napendekeza kupunguza adhabu zinazotolewa chini ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura Namba 168, kwa makosa ya pikipiki na bajaji kutoka shilingi 30,000 za sasa hadi shilingi 10,000 kwa kosa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuweka adhabu kwa kuzingatia uwezo wa kulipa. Aidha, adhabu kwa makosa mengine ya vyombo vya moto zinazotolewa kwa mujibu wa sheria hiyo zitaendelea kubaki kama ilivyo sasa na ninaelekeza ofisi zinazohusika waweke katika kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa Sheria ya Raia wa Kigeni; napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Raia wa Kigeni (Uratibu wa Ajira), Namba 1 ya mwaka 2015 kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka adhabu ya kiasi cha shilingi 500,000 kwa kila mwezi kwa mwajiri aliyeajiri raia wa kigeni na kushindwa kuwasilisha ritani za kila mwezi zenye taarifa za raia wa kigeni aliowaajiri ikiwemo taarifa zao za mishahara kwa Kamishna wa Kazi. Lengo la pendekezo hili ni kuhimiza uwajibikaji wa hiari wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa, Wakala, Mamlaka za Udhibiti pamoja na Idara zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Kilimo; kuanzisha tozo za umwagiliaji kwa watumiaji wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha miradi hiyo kuwa endelevu na kuwezesha ujenzi wa miundombinu mipya. Viwango vinavyopendekezwa kama ifuatavyo: -

(a) Kutoza ada ya shillingi 60,000 kwenye usajili wa vyama vya umwagiliaji; na

(b) Kutoza ada ya huduma ya umwagiliaji ya asilimia tano ya mavuno ya msimu kwa eneo la vyama vya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Jumuiya ya Kijamii, Sura Namba 337 ili kuhuisha viwango vilivyokuwa vinatumika awali na kuanzisha tozo katika maeneo ambayo hayakuwa yanatozwa. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kutoza tozo ya shilingi 100,000 ya uharibifu wa cheti cha Jumuiya ya Kijamii unaolazimu kupewa cheti kipya;

(b) Kutoza tozo ya shilingi 50,000 ya kukosea kwa jina kulikosababishwa na mwombaji atakayepaswa kupewa cheti kipya;

(c) Kutoza tozo ya shilingi 50,000 ya kubadili taarifa za anuani ya posta au makao makuu ya Jumuiya;

(d) Kuongeza ada ya kuwasilisha maombi ya usajili wa Jumuiya ya Kijamii kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 50,000;

(e) Kuongeza ada ya mwaka kwa taasisi za kidini kutoka shilingi
20,000 hadi shilingi 100,000;

(f) Kuongeza ada ya mwaka kwa taasisi zisizo za kidini kutoka shilingi 40,000 hadi shilingi 50,000;

(g) Kuongeza ada ya mwaka kwa jumuiya za dini kutoka nje ya nchi kutoka dola za Marekani 30 hadi dola za Marekani 60;

(h) Kuongeza ada ya mwaka kwa jumuiya zisizo za kidini kutoka nje ya Nchi kutoka dola za Marekani 30 hadi dola za Marekani 60;

(i) Kuongeza tozo ya maombi ya kubadili jina la jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(j) Kuongeza tozo ya maombi ya marekebisho ya katiba ya jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(k) Kuongeza tozo ya maombi ya nakala kwa ajili ya ushahidi katika vyombo vya utoaji haki kwa jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(l) Kuongeza tozo ya maombi ya nyaraka kwa jumuiya yenyewe kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 50,000;

(m) Kuongeza tozo ya upotevu wa cheti cha jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(n) Kuongeza tozo ya upotevu wa cheti cha jumuiya kwa mara ya pili kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 200,000;

(o) Kuongeza ada ya upekuzi kwa jumuiya yenyewe kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000; na

(p) Kuongeza ada ya upekuzi kwa mwombaji mwingine kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 200,000.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS);* kuanzisha kanuni za ada na tozo za Shirika la Viwango ya mwaka 2021 ambazo zinaanzisha ada na tozo mpya pamoja na kupitia ada na tozo zilizokuwa zinatozwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania *(TFDA)* hapo awali. Mapendekezo hayo yameainishwa katika Kiambatisho Na. 5.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu; kufanya marekebisho kwenye kanuni za ada na tozo za Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu ya mwaka 2009 ili kupitia ada na tozo mbalimbali zilizoanzishwa kwa ajili ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu kama ilivyoambatishwa kwenye Kiambatisho Na. 6.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa janga la homa kali ya mapafu hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii; kupunguza ada ya leseni ya biashara ya utalii kwa Wakala za Safari kutoka dola za Marekani 2,000 hadi dola za Marekani 500 ili kuhamasisha biashara ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi; kutoza ada ya shilingi 40,000 kwenye kibali cha kupeleka nyama nje ya nchi kwa nyama zote bila kujali aina ya nyama badala ya ada ya shilingi 100 kwa kilo moja ya nyama ya ng'ombe na shilingi 50 kwa kilo moja ya nyama ya mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi; kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Sura Namba 263 kwa kupunguza kiwango cha mchango kwa sekta binafsi kutoka asilimia 1.0 inayotozwa sasa hadi asilimia 0.6 ya mapato ghafi ya wafanyakazi. Lengo

la hatua hii ni kutoa unafuu wa kutosha kwa biashara zilizopo na uwekezaji mpya utakaofanyika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya nguvu za mionzi Tanzania; kufuta ada ya utambuzi wa mionzi ambayo inatozwa kwa kiwango cha asilimia 0.2 ya Malipwani kwenye mizigo ya vyakula inayosafirishwa kwenye nchi ambazo hazina sharti la uhitaji wa cheti cha utambuzi wa mionzi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji:-

(a) Kuondoa ada ya kibali cha kuingia nchini *(visa/ pass fee)* kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka nchi ya Msumbiji kwa ajili ya Mpango wa kubadilishana Wanafunzi wa Elimu ya Juu baina ya Tanzania na Msumbiji. Lengo la pendekezo hili ni kutekeleza matakwa ya makubaliano kati ya nchi hiyo na Tanzania kuondoleana ada hizo ambapo Msumbiji wameshaanza kutekeleza makubaliano hayo; na

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa King, kwa upande wa Zanzibar, napendekeza kutekeleza utaratibu wa kuruhusu mapato yanayotokana na kodi na tozo za Muungano kwenye mapato yanayotokana na *visa* ili yaweze kutumika pale yalipokusanywa *(Derivation Principle)* kama ilivyo kwenye mapato mengine ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanafanya suala hili liondolewe kwenye orodha ya changamoto za Muuungano. Mapato yatokanayo na tozo za *Visa* upande wa Zanzibar yaonekane kwenye bajeti upande wa Zanzibar na kuidhinishwa na kutumika Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi ya Zimamoto na Uokoaji Sura Namba 427, kama ifuatavyo:-

(a) Kufuta tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye kilimo cha mbogamboga na maua;

(b) Kufuta tozo ya cheti cha umahiri cha kinga na tahadhari ya moto inayotozwa kwenye vituo vya mafuta nchini;

(c) Kufuta tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye mashamba makubwa na nyumba za makazi yaliyopo ndani ya mashamba hayo yaliyokuwa yakitozwa kati ya shilingi 100,000 hadi 1,000,000;

(d) Kuongeza ukubwa wa eneo lisilopaswa kutozwa tozo ya Ukaguzi wa Kinga na tahadhari ya moto linatumika kwa maonesho ya biashara kuanzia mita za mraba zisizopungua 2,000 hadi mita za mraba 10,000; na

(e) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa bweni kwa shule zisizopaswa kutozwa tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari za moto kutoka wanafunzi wasiozidi 100 hadi wanafunzi 200.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; kufanya marekebisho kwenye Kanuni ya Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2019 kama ifuatavyo: -

(a) Kupunguza ada ya kuharibu dawa zilizoisha muda wa matumizi yake kutoka shilingi 1,000,000 hadi shilingi 100,000; na

(b) Kupunguza ada ya kila mwaka ya mazingira kutoka shilingi 200,000 hadi shilingi 100,000.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Nyama Tanzania; kutoza ada ya shilingi 70,000 kwa cheti cha kukubaliwa kupeleka nyama nje ya nchi badala ya kiwango cha asilimia moja ya Malipwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA);* kupunguza tozo ya ukaguzi wa umeme kwa kipimo kimoja kutoka shilingi 590,000 hadi 150,000. Tozo hii inatozwa kabla ya kuanza biashara ya mafuta. Pendekezo hili linatarajia kuchochea mazingira

wezeshi ya biashara hapa nchini hususan katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, utoaji leseni za bima kwa makampuni; napendekeza kubadili utaratibu wa sasa wa makampuni ya bima kulazimika kuomba leseni upya kila mwaka na badala yake makampuni yanayofanya vizuri yaweze kupewa leseni ya kudumu na makampuni yalioko kwenye hali mbaya yawe kwenye uangalizi kwa kupewa leseni ya miaka mitatu huku yakiwa kwenye uangalizi na yakiimarika yaweze kupewa leseni za kudumu. Utaratibu huu utaondoa usumbufu wa ufuatiliaji wa kutafuta leseni kila mwaka na hivyo kuondoa *focus* kwenye kufanya kazi na kuanza kuhangaika na leseni.

Mheshimiwa Spika, taratibu zingine za ufuatiliaji na malipo ya kila mwaka yataendelea kama ilivyo sasa. Lengo la hili ni kupunguza ukiritimba na kuenzi kauli ya Mheshimiwa Rais ya kutengeneza mazingira bora ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara; sambamba na hatua za kikodi zilizolenga kupunguza gharama ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara, Serikali itakamilisha mfumo wa kimtandao wa kuwa na dirisha moja la upatikanaji wa vibali mbalimbali katika idara zote zinazohusika na usajili na vibali ili kuwapunguzia wawekezaji mizunguko ya kutembea ofisi zaidi ya moja kuhangaika nenda/rudi kutafuta vibali vinavyoweza kupatikana kwenye ofisi moja. Lengo la hatua hii ni kurahisisha mazingira ya kufanya biashara kama ilivyobainishwa kwenye *blueprint. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mahususi; barabara mijini na vijijini; hali ya barabara zetu mijini na vijijini hairidhishi ambapo bado vipo vijiji ambavyo havina barabara kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mtandao wa barabara zinazosimamiwa na *TARURA* una hali mbaya. Barabara zilizo

chini ya *TARURA* zina urefu usiopungua kilometa 108,946.2 ambazo zinaunganisha maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini. Hadi Desemba, 2020 mtandao wa barabara zilizo chini ya *TARURA* wenye kiwango cha lami ulishafika kilometa 2,250.69, sawa na asilimia 2.1 tu.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara hizi kuwa mbaya ina madhara makubwa sana katika jamii yetu kwani baadhi ya akina mama wajawazito wanapoteza maisha yao kwa kuchelewa kufika kwenye vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo wengine ambao wanajifungulia njiani kutokana na kuchelewa kufika kwenye vituo vya afya, wapo wanaopoteza maisha, wapo wanajifungulia njiani kwa sababu ya kuchelewa kufika kwenye vituo vya afya, wapo baadhi ya wanafunzi wanaosombwa na maji na kupoteza maisha kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara, hususan katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo bado wanaume wanapimana urefu ili wambebe mama mjamzito kwenye kitanda na mama anajifungulia mbele ya wanaume waliombeba kwenye kitanda kabla hajafika kwenye zahanati. Kadhalika bado kuna changamoto ya usafirishaji wa mazao na bidhaa kutoka sehemu za vijijini kwenda barabara kuu katika baadhi ya maeneo yetu na kuathiri mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeona ipo haja ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato, ili kuongeza mgawo katika Mfuko wa Barabara ili kuweza kufanikisha miundombinu ya barabara iweze kupitika. Kama tumeweza kwenye umeme kila kijiji, tunaweza pia kwenye barabara bora kila kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo mahususi la pili; upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini. Hali ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini bado hairidhishi. Maji hayana mbadala, maji ni uhai, maji ni maisha. Bado vipo vijiji

ambavyo havina kisima hata kimoja cha maji safi na salama, badala yake wananchi hutumia maji ya kwenye mapalio, maji ya kwenye madimbwi, maji ya kwenye mito na wanachangia na wanyama. Vipo vijiji vya aina hiyo licha ya kazi kubwa ambayo imeshafanyika. Tanzania ina vyanzo vingi vikubwa vya maji vya uhakika, pamoja na hivyo bado kuna shida hiyo kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna uwezekano wa kutumia mabwawa makubwa kama ya Kidunda, Ndembela pamoja na Farkwa kama yangekamilika, lakini utekelezaji wake haujaanza kwa sababu ya uhaba wa fedha. Ipo miradi mingi katika mikoa mingi ambayo haijatekelezwa kwa mfano, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora, Tanga na maeneo mengine. Mikoa ambayo sikuitaja hapa, ipo kwenye bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya ukosefu wa maji safi na salama ina madhara makubwa sana kwenye jamii yetu. Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa inampa nafuu mwanamke katika kufanya shughuli zake za kiuchumi, lengo likiwa ni kumtua mama ndoo kichwani, kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakumba akina mama pamoja na mabinti zetu katika harakati hizi za kutafuta maji. *(Makofi)*

Aidha, kuna baadhi ya wanafunzi wanakosa masomo na kuharibu maisha yao kutokana na uhaba wa maji katika maeneo yao. Hivyo basi, Serikali imeona ipo haja kuongeza fedha za kugharamia miradi ya maji kwa kubuni vyanzo mbadala vya mapato kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afya na Bima kwa Wote; sekta ya afya ni sekta muhimu sana katika ustawi wa jamii yetu na ni moja ya mahitaji muhimu sana katika maisha ya sasa ya mwanadamu. Serikali ya CCM imefanya kazi kubwa sana katika sekta hii, ingawa bado kuna kazi

kubwa ya kufanya kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na mabadiliko ya hali za kiafya kwa kizazi cha leo. Aidha, wananchi katika maeneo mbalimbali wametumia nguvu kubwa katika kutafuta ufumbuzi wa masuala ya upatikanaji wa huduma ya afya, kwa kujenga maboma takribani kila eneo. Yapo majengo yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yamekaa kwa muda mrefu sana, kati ya miaka mitano hadi 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2021 kuna jumla ya maboma 8,004 ya zahanati ambazo yapo katika mikoa mbalimbali hapa nchini, yapo katika hatua mbalimbali za kukamilishwa. Vilevile yapo maboma kwenye ngazi ya vituo vya afya zaidi ya 1,500 ambayo yametumia nguvu za wananchi na yanahitaji ukamilishwaji. Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma hayo na kuajiri wataalamu wa afya na kuimarisha upatikanaji wa dawa, vitendanishi, pamoja na vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mradi mkubwa wa bima ya afya kwa wote unaolenga kuwafikia Watanzania wote, Tanzania ina jumla ya kaya milioni 12.8 ambapo asilimia 20 ya kaya hizo, inakadiriwa kuwa ni kaya zisizokuwa na uwezo. Katika kufanikisha utekelezaji wa dhana ya bima ya afya kwa wananchi wote, Serikali itahitaji zaidi ya shilingi bilioni 149 kwa mwaka kwa ajili ya kuwezesha kaya zile zisizokuwa na uwezo. Serikali imeendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya na inaona kuna kila sababu ya kutafuta vyanzo mbadala vya kuwezesha mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu; jambo lingine mahususi; kuhusu sekta ya elimu kuna kazi kubwa bado iko mbele yetu, bado kuna shule ambazo zina wanafunzi wengi kuliko idadi ya madarasa, zipo shule ambazo bado wanapanga mikondo ya wanafunzi wengine wasome asubuhi wengine wasome mchana, pia zipo shule ambazo bado wanaweka ubao katikati ya darasa, mkondo mmoja usomee upande mwingine na mkondo mwingine usomee upande mwingine kwenye chumba kimoja. Zipo shule pia,

ambazo zinaweka ubao kutenganisha mikondo ya madarasa ambazo ziko madaraja tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo pia madarasa ambayo yameezekwa kwa nyasi na yana sakafu na ni ya vumbi. Kadhalika, mwaka ujao utakuwa mwaka wa kwanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza waliodahiliwa darasa la kwanza kwa mpango wa elimu bila malipo. Jambo hili lisipoangaliwa mapema litakuja kusababisha wanafunzi kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza na kukosa pa kwenda hadi miundombinu hiyo ijengwe kwa zimamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua ya maendeleo ya nchi yetu ilipofikia katika sekta mbalimbali, hali hii haipendezi na haitakiwi kuendelea. Kujenga miundombinu ya shule zetu kwa kusubiri irushwe kwenye mitandao ya kijamii ndio tuone inatutia aibu au kusubiri watoto wakose pa kwenda au wakose pa kukaa ndipo tukimbizane na kufukuzana, hii ni ishara kwamba hatupangi vizuri. Hili tusingependa kuliona linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kila mwaka wanafunzi kati ya asilimia 15 hadi 20 wanatoka kwenye mfumo wa elimu na kutokuendelea na kidato cha kwanza kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ujauzito, utoro, hali ngumu ya maisha na ukosefu wa mpango wa kugharamia mahitaji katika sekta ya elimu pamoja na matatizo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu ya juu, zaidi ya wanafunzi 11,000 wenye sifa za kujiunga na vyuo vikuu ambao tayari walishapata udahili katika vyuo mbalimbali walikosa mkopo. Hapa naongelea mkopo kwamba wanafunzi wa Kitanzania 11,000 wamekosa mkopo wakiwa wameshadahiliwa, wana chuo na wana sifa za kuingia katika chuo hicho. Sio fedha za bure, wamekosa mkopo ambao watаurejesha.

Katika jamii nyingi za Kitanzania, mtoto akikosa mkopo, akiwaona wenzake wanaendelea, inamfadhaisha sana. Ni mafadhaiko kwake na familia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hatua ya maendeleo ambayo nchi yetu imepata katika sekta zingine, Serikali inakusudia kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa inaongeza bajeti kwenye mikopo ya elimu ya juu, ili kuwanufaisha vijana wetu wote wenye sifa za kuweza kujiunga na masomo ya elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine mahususi; miradi ya kielelezo, Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere pamoja na Reli ya *SGR;* miradi ya Bwawa la Kufua Umeme ya Mwalimu Nyerere pamoja na *(SGR,)* sio tu ni miradi kielelezo bali ni miradi mama kwa kila Mtanzania, ni mradi mtoto wa kila Mtanzania, ni miradi inayoashiria uhuru wa nchi yetu, ni miradi inayoashiria kujitegemea kwa nchi yetu, ni miradi inayoashiria heshima kwa Mtanzania na itajengwa na Mtanzania. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais, kutokukamilika kwa miradi hii katika hotuba za mama yetu itakuwa ni laana kwa Taifa letu. Hatutajengewa miradi hii na mtu yeyote, tuwaenzi wabeba maono wa miradi hii kwa kujenga na kukamilisha miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alibeba maono ya miradi hii, Rais Magufuli alianzisha miradi hii, Mama Samia anakwenda kujenga na kukamilisha miradi hii. Niwahakikishie Watanzania, hautakuwepo mradi gofu hata mmoja na hatutamani kuona mradi hata mmoja unageuka gofu na wala hata mradi mmoja kusimama hata kwa mwezi mmoja kwa kukosa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na maeneo hayo mahsusi, barabara zilizo mbovu na vijiji visivyo na barabara mpaka sasa, ukosefu wa maji na vijiji visivyo na kisima hata kimoja hata sasa, wanafunzi zaidi ya 11,000 watoto wa Kitanzania kukosa mkopo sio fedha ya bure, kukosa mkopo fedha ya kurudisha, maboma yaliyokaa kwa zaidi ya miaka 15 ya nguvu ya wananchi waliojenga kwa nguvu zao, kukamilisha umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na kuhakikisha *SGR* inakamilika, napendekeza kwa Watanzania lazima tufunge mikanda. Lazima tuijenge nchi

yetu, lazima tukamilishe hii miradi, lazima tuondoe haya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, (a) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura Na. 220. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Ushuru wa Barabara na Mafuta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru wa barabara kwa shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli. *(Makofi)*

Kufanya marekebisho ya kifungu cha 4A(a) cha sheria inayoelekeza fedha zitakazokusanywa kutokana na ongezeko la ushuru wa barabara na mafuta ya shilingi 100, kwa aina zote za mafuta ziwe kwa ajili ya ujenzi wa barabara za vijijini - *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hatua hizi tutapata zaidi ya shilingi bilioni 300 tuzipeleke kwenye Mfuko wa Barabara *(TARURA)* na tutengeneze utaratibu wa barabara kila kijiji, ili tuokoe maisha ya mama zetu, tuokoe maisha ya wajawazito. *(Makofi)*

Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Petroli ili kuongeza tozo ya mafuta ya taa kutoka shillingi 150 hadi shillingi 250. Lengo la hatua hii ni kupunguza uchakachuaji wa mafuta kufuatia ongezeko la ushuru wa mafuta kwenye dizeli na petroli. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki kama ifuatavyo; kutoza tozo ya shillingi 10 hadi shilingi 10,000 katika kila muamala wa kutuma na kutoa pesa. Kiasi cha tozo kitatofautiana kulingana na thamani ya muamala wa fedha utakaotumwa au utakaotolewa. Pendekezo hili litaiongezea fedha za Serikali kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.2, lengo la fedha hizi ni twende tukaokoe maisha ya kina mama wanaojifungua wakiwa wamebebwa, wanaotozwa fedha hata wale ambao tulisema wanatakiwa wapate matibabu bure. Hata akina mama wanapojifungua yapo maeneo ambayo bado

wanatozwa fedha ili waweze kujifungua, yapo maeneo ambayo bado watu wanazuiliwa miili ya wapendwa wao ili walipe kwanza gharama, yapo maeneo ambayo kwenye afya maboma yamekaa kwa zaidi ya miaka 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kutoza kiasi cha shilingi 10 hadi shilingi 200 kwa siku, kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Pendekezo hili linapelekea kuongeza mapato ya shilingi milioni 396 na fedha hizo ziende kutatua tatizo la maji vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha nyingine itakayopatikana niliyoisema mwanzoni hapo iende kwenye elimu ya juu. Nawaonea huruma Watanzania naamini kwamba ni kweli ongezeko hili litatupa mzigo Watanzania. Nawaonea huruma na sipendi kuwapa mzigo, lakini nawaonea huruma sana Watanzania wanapofariki kwa kukosa barabara, nawaonea huruma zaidi wanafunzi zaidi ya 11,000 wanaotakiwa kupata mikopo ya elimu ya juu, nawaonea huruma sana watanzania wanapokosa kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zingine za kikodi zinaweza kunifanya niwe Waziri wa Fedha asiye maarufu yaani *unpopular Finance Minister,* lakini hata wakinipenda wapiga kura wangu, wakanipenda na mashabiki wa Yanga inatosha, lazima tuijenge nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, napendekeza kufanya marekebisho kwenye vinywaji vikali kuwa na kiwango kikubwa cha kilevi. Napendekeza kuongeza ushuru wa bidhaa wa asilimia 30 ili kuwa na uwiano wa viwango vya kodi ya vinywaji vikali pamoja na bia. Hatua hii inatarajia kutuongezea mapato Serikali ya kiasi cha shilingi milioni 60.7. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa hatua mpya; hatua hizi za kikodi zinalenga kuanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2021. Serikali inapanga kuja na njia mbadala pia za kutekeleza miradi mikubwa. Tunapendekeza njia mbadala za kutekeleza pia miradi

mikubwa; mosi, kwa mwaka 2020 nchi yetu ilifanikiwa kuingia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati cha chini yaani *lower middle income country*. Kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati maana yake kunatakiwa nchi kujiendesha bila kutegemea kiwango kikubwa cha misaada na mikopo yenye masharti nafuu ambayo hupewa nchi zenye kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ni lazima Serikali iboreshe mbinu inazozitumia na kubuni mbinu mpya za kupata mapato. Katika kutekeleza hatua hii, Serikali imeanza kufanya uchambuzi wa vyanzo mbadala vya rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama vile ufadhili mchanganyiko yaani *blended finance*. Wafadhili wanaotoa aina hii ya ufadhili hutoa fursa kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania kurekebisha au kujumuisha yaani *restructuring and consolidation* ya deni lake kwa makubaliano ya kutumia sehemu ya malipo ya deni, katika kuhifadhi mazingira au kuimarisha sekta za kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inadhamiria kukamilisha mchakato wa tathmini ya ukadiriaji wa kukopesheka kwa nchi yaani *sovereign credit rating*. Hatua hii inalenga kutuwezesha kujua nafasi yetu katika masoko ya fedha ya kimataifa na jinsi wakopeshaji wanavyotuona, hasa katika uwezo wa kusimamia uchumi na kulipa madeni yetu.

Katika jitihada hizo za kupanua wigo wa vyanzo vya rasilimali fedha, Serikali itaangalia uwezekano wa kutumia hatifungani zitakazotolewa na Halmashauri na Manispaa na Majiji kama njia mbadala ya kupata rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Baadhi ya njia zinazoweza kutumika ni pamoja na *infrastructure bond* pamoja na *euro bond* ambazo zinatumika ulimwenguni ili kuwa na njia nyingi zaidi za kuweza kufadhili miradi mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2021/2022; kwa kuzingatia shabaha, malengo pamoja na sera za bajeti kwa mwaka 2021/2022 Sura ya Bajeti inaonesha kuwa

jumla ya shilingi trilioni 36.33 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 26.03, sawa na asilimia 71 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 22.18, sawa na asilimia 13.5 ya Pato la Taifa. Aidha, Serikali inalenga kukusanya mapato yasiyo ya kodi ya shilingi trilioni 2.99 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 863.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia misaada na mikopo nafuu yenye jumla ya shilingi trilioni 2.96 sawa na asilimia 8.1 ya bajeti yote. Kiasi hicho kikijumuisha fedha za miradi ya maendeleo ya shilingi trilioni 2.67 na mifuko ya pamoja ya kisekta shilingi bilioni 282.3. Napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo kwa kuendelea kutoa fedha na misaada pamoja na mikopo nafuu, ili kufanikisha miradi pamoja na programu za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kipekee ningependa kuwatambua washirika wetu wa maendeleo kama ifuatavyo; Serikali za Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Korea ya Kusini, Japan, Ufaransa, Ujerumani, Norway, Poland, Ubelgiji, Uholanzi, Uswisi, Uingereza, Sweden na Marekani. *(Makofi)*

Vilevile kuna Mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano Dhidi ya Virusi vya UKIMWI, Kifua Kikuu, Malaria pamoja na Mfuko wa Umoja wa Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Umoja wa Mataifa na Mashirika yote yaliyopo chini yake, Mfuko wa *OPEC* kwa Maendeleo ya Kimataifa, Mfuko wa Mazingira pamoja na Shirikisho la GAVI. Ninapenda pia kuyatambua Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ndani na nje pamoja na mashirika ya ufadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 7.34 kutoka soko la ndani na nje kwa masharti ya kibiashara. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 4.99 ni mikopo ya

ndani ambayo inajumuisha shilingi trilioni 3.15 kwa ajili ya kulipa hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 1.84 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, shilingi trilioni 2.35 zinatarajiwa kukopwa kutoka soko la nje kwa ajili ya kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 36.33 kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo, kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 23.0 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 13.33 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi trilioni 10.66 kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Taifa la Serikali na shilingi trilioni 8.15 kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 4.19 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 200.0 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, wazabuni na watoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya shilingi trilioni 13.33 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti yote, kati ya kiasi hicho, fedha za ndani ni shilingi trilioni 10.37 na fedha za nje shilingi trilioni 2.96. Aidha, fedha za maendeleo zinajumuisha shilingi trilioni 1.19 kwa ajili ya miradi ya reli ikiwemo ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa; shilingi trilioni 2.08 kwa ajili ya miradi ya barabara, ujenzi wa madaraja pamoja na viwanja vya ndege; shilingi trilioni 2.34 kwa ajili ya miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; shilingi bilioni 589.4 kwa ajili ya miradi ya maji mijini na vijijini; na shilingi bilioni 233 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoelezea, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2021/2022 ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ninapoelekea mwisho wa hotuba hii, napenda kumshukuru kwa dhati "mama yetu"

kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba nitaibeba dhamana hii kwa uadilifu, weledi na uwezo wangu wote na ninamuomba Mungu anijalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu hayo. Naomba nielezee masuala machache muhimu kabla ya sijahitimisha kabisa hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa "mama yetu"; kwa matumaini makubwa aliyowapa Watanzania. "Mama yetu" ameonesha ni kiongozi makini, ni kiongozi shupavu, ni kiongozi mchapakazi, ni kiongozi mwadilifu, ni kiongozi msikivu, ni kiongozi aliye na dira thabiti na maono ya kuendelea kuliletea Taifa letu maendeleo. Ameweka wazi kuwa hataki kodi ya dhuluma, hataki kuendesha Serikali kwa mapato ya dhuluma, ameweka wazi kuwa atasimama imara kwenye masuala ya mapato na matumizi ya Serikali, ameweka wazi kuwa atakuwa imara kwenye vita dhidi ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hizo "mama yetu" ameonesha kuwa kukaa kwake katika nafasi mbalimbali katika awamu mbalimbali SMT na SMZ kumemfanya kuwa ni kiongozi aliye iva na aliye tayari kuiongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mbali na nafasi nyingi ambazo alishika katika kukaa kwake miaka zaidi ya ishirini Serikalini, "mama yetu" amekuwa Waziri katika Serikali ya Awamu ya Nne na amekuwa Makamu wa Rais katika Serikali ya Awamu ya Tano. Kuna *style* za uongozi amejifunza, hii ni *analysis* yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *style* za uongozi amejifunza, katika kupitia awamu hizo kwa nafasi alizopewa kuhudumu "mama yetu" alikuwa Waziri katika Serikali ya Awamu ya Nne iliyokuwa ikiongozwa na Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mheshimiwa Dkt. Kikwete alikuwa mzalendo wa kweli, alikuwa na maono *(visionary leader)*, alikuwa mwalimu, alikuwa mzazi, alikuwa mlezi, alikuwa kiongozi, alikuwa *rahim* sana, alikuwa

mvumilivu sana aliyeamini kwenye mfumo, taasisi na uendeshaji uongozi wa kitaasisi. Hii nikiifananisha kama refa kwenye mchezo wa mpira wa miguu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alikuwa anakwenda kuchezesha mechi zake akiwa na kadi ya njano tu. Kadi nyekundu alikuwa anaiacha nyumbani. Ukicheza rafu mara ya kwanza anakuonya kwa kukuelekeza, ukicheza rafu mara ya pili anakuonya kwa kukupa kadi ya njano, ukikosea tena anakupa kadi ya njano tena na alipotakiwa kutoa kadi nyekundu mara nyingi alikuonya kwa mdomo kwa kuwa kadi nyekundu alikuwa aliiacha nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuwa anaiacha nyumbani, Rais Kikwete aliamini sana kwenye mifumo na utendaji wa kitaasisi. Kwa mtazamo wangu, jinsi "mama yetu" alivyoanza ni dhahiri alipata funzo kwenye awamu hiyo, funzo la uzalendo, maono na kuamini kwenye mfumo, taasisi na uendeshaji wa kitaasisi, hapa naweza kusema aliichukua kadi ya njano, anayo na ameshaanza kutumia kama mnavyomuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, "mama yetu" alikuwa Makamu wa Rais katika Serikali ya Awamu ya Tano iliyokuwa ikiongozwa na Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Rais Magufuli alikuwa mzalendo wa kweli, alikuwa na maono na yeye *visionary leader*, alijitoa kwa nguvu zote yaani *dedicated*, alikuwa na uthubutu sana, mtu wa vitendo sana na muumini wa matokeo na kuchukua hatua za papo kwa papo. Kama refa wa michezo, mchezo wa mpira wa miguu, naweza kukwambia Rais Dkt. Magufuli alikuwa akienda kuchezesha anaibeba kadi nyekundu tu, kadi ya njano alikuwa anaiacha nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukicheza rafu mara ya kwanza anakupa kadi nyekundu, wakati mwingine hata asipoiona rafu yeye mwenye, hata mchezaji au shabiki akiiona rafu, akamwambia kuna rafu imechezwa, anakupa kadi nyekundu *(no nonsense)*, hata mimi niliwahi kutembelewa na kadi nyekundu nikakosa michezo kadhaa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Hayati Dkt. Magufuli aliamini kwenye nidhamu ya hali ya juu ya mchezo. "Mama yetu" akiwa *line one* na Mheshimiwa Majaliwa akiwa *line two;* wamepata mafunzo. "Mama yetu" wamepata mafunzo kwenye awamu hiyo mafunzo ya uzalendo, uthubutu, mtu wa vitendo na kuamini kwenye matokeo na nidhamu kazini na ameichukua kadi nyekundu na anayo na ameshaanza kuitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *style* za uongozi amejifunza "mama yetu" anazo kadi zote, kadi ya njano na kadi nyekundu. "Mama yetu" ni mzalendo, ni mwadilifu, ana uthubutu, ana maono, anaamini kwenye mifumo, taasisi na utendaji wa kitaasisi, hataki maneno anataka vitendo, ni mtu wa matokeo. Nitoe rai kwa watumishi wote wa umma na Watanzania kwa ujumla tuchape kazi kwa bidii, kwa uadilifu na kwa uzalendo mkubwa. Kwa watumishi wa umma tusimamie matumizi ya fedha za walipa kodi kwa uadilifu mkubwa na kwa Watanzania tulipe kodi bila shuruti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tabia moja ya refa asiyependa kuonea upande wowote, pia huwa hawezi kupendelea upande wowote. Tabia moja ya refa asiyependa kuonea upande wowote, pia huwa hawezi kupendelea upande wowote. Kwenye michezo ya mieleka huwa mnapewa tu *don't try this at home*, kwa "mama yetu" kwa maslahi ya nchi msimjaribu *don't try at all*. Tujiepushe tusije tukatembelewa na kadi nyekundu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tujenge utamaduni wa kuheshimu mali na rasilimali hapa nchini, mali za umma pamoja na mali binafsi. Kwa upande wa mali za umma, lazima tutangulize uzalendo na uadilifu tunapotekeleza majukumu yetu. Serikali inapoteza fedha nyingi kwenye kutekeleza Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa kutojali thamani ya fedha kwenye miradi. Watumishi wa Serikali wasio waaminifu wamekuwa wakishirikiana na wafanyabiashara wasio waaminifu kuongeza gharama za miradi ikilinganishwa na gharama halisi ingawa wanafuata taratibu zote za ununuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taratibu za ununuzi zinapokamilika, watumishi na wafanyabiashara huungana kugawana fedha na kiasi kidogo tu ndio kinakwenda kwenye miradi. Ukiwafuatilia kisheria huwapati walipokosea moja kwa moja kwa sababu walifuata taratibu, lakini thamani ya fedha haionekani. Kwa maana hiyo, wanakuwa wameiba kwa kwa mujibu wa sheria. Wanakuwa wameiba kwa kuzingatia Sheria. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawaelekeza wote wanaohusika na masuala ya ununuzi wa umma kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na kuzingatia thamani ya fedha kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mali binafsi, ni lazima tuheshimu biashara zetu na mali zinazotokana na shughuli zetu. Kuna hatua tunazozifanya katika sekta zote za umma pamoja na sekta binafsi zinadumaza uchumi wetu. Kwa mfano, kuna tabia imejitokeza kwenye mabenki inatokea mtu ana jambo ambalo linapunguza uwezo wa mabenki; tunakopa kwenye mabenki lakini hatulipi. Lakini inajitokeza sehemu nyingine tunatumia vibaya vyombo vyetu vya kisheria na kuna baadhi ya wakopeshaji pia hawaheshimu mali za wateja wao. Mfano, mteja anakuwa amelipa sehemu kubwa ya deni lake, ameshabakiza sehemu ndogo ya mkopo wake inatokea mkopeshaji na rafiki yake akiwa dalali wanapeana dhamana huku wakiwa wameshatamani dhamana iliyokuwa imewekwa na mteja, wanafanya mnada mali ya mteja inakwenda huku akiwa alishalipa sehemu kubwa ya deni lake.

Mheshimiwa Spika, nawaelekeza vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia kila eneo panapokuwa na mnada kwenye sekta binafsi na hata sekta ya umma ili panapotokea kuwepo kwa njama za kudhulumu wamiliki wa mali au kuchepusha sehemu ya mali hizo hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Vilevile na kwa wale ambao wanakopa wanaenda kupaki mikopo yao hawalipi wanatumia kichaka cha sheria

na yenyewe inasababisha kupoza uchumi wetu na kupunguza mzunguko wa fedha ambazo wangeweza kukopewshwa watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Kuna wanaodhani tutalegalega kwenye kukusanya. Tumeelekezwa kukusanya kwa weledi, sheria na kutenda haki. Tutakusanya mapato ya Serikali, tutakusanya mapato ya Serikali, tutakusanya mapato ya Serikali, tutakusanya mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa watumishi wote wa Serikali wanaohusika na kukusanya kodi, maduhuli pamoja na ushuru kuelewa vizuri maelekezo yaliyotolewa ya kuzingatia sheria, weledi na kutenda haki. Nimeanza kusikia visingizio kila kona, mara mfumo, mara mtandao, mara *EFD* haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusiwekeze kwenye visingizio, tusiwekeze kwenye kusaidiana kukwepa kodi, bali tuwekeze kwenye kufuata sheria. Akiwepo mtumishi akakusaidia kukwepa kodi nawe ukampa ahsante, utakuwa umetengeneza tatizo tu sio unafuu. Kwani kuna siku utakuja kukaguliwa huku aliyekusaidia kukwepa kodi akiwa amehamishwa au kuachishwa kazi. *(Makofi)*

Nitumie fursa hii kumwelekeza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kuweka watu mahususi na kufanya doria kila kona, Nchi nzima kuangalia mwenendo wa matumizi ya *EFD* watu wameanza kulegalega kwenye matumizi ya *EFD.* Lazima tukusanye kodi na lazima tuijenge nchi tutakayozingatia ni sheria, haki pamoja na taratibu za kukusanya kwa kutumia weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutasimamia nidhamu katika matumizi. Tutasimamia nidhamu katika matumizi. Tutasimamia nidhamu katika matumizi na mapambano dhidi ya rushwa. Lazima wananchi wetu wanapolipa kodi wawe na uhakika kwamba kodi yao itakwenda kutumika. Kazi inaendelea

Watanzania endeleeni kumwamini Mheshimiwa Rais wetu, yuko macho na wasaidizi wake wako macho, tutapambana na mchwa wote, kuna mengine mnayasikia, kuna mengine mnayaona na kuna mengine hata hamyaoni, lakini tunaendelea kuyafanyia kazi. Tuko na maelekezo thabiti kutoka kwa viongozi wetu wakuu na sisi Kinyiramba mnapoona tumekaa kimya ni vile na wewe Spika unajua hiyo mwinda kanga hapigi kelele**.** Tunaendelea na kazi mtakuwa mnaona vitendo vikiwa vinatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kwa kasi kutekeleza miradi kama nilivyokwisha kusema. Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya Jiji la Dodoma na kulifanya kuwa la kisasa. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kuendeleza wa ujenzi wa Wizara na Taasisi zake katika Mji wa Serikali Mtumba; kujenga barabara za mzunguko na kuboresha miundombinu ya maji. Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa Viwanja wa Ndege vya Kimataifa katika eneo la Msalato. Zoezi la nchi kuwa Dodoma halirudi nyuma linasonga mbele. Makao Makuu ya nchi kuwa Dodoma tunasonga mbele. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amenituma niwahakikishie Watanzania kupitia hotuba hii kuwa tunaendelea kuijenga nchi, tunaendelea kuijenga nchi, ije mvua, lije jua, tunaendelea kuijenga nchi. Uwe usiku au mchana, tunaendelea kuijenga nchi. Hakuna mradi hata mmoja utakaokwama, wala hakuna sekta hata moja itakayozorota. Mama mwenyewe amesema Kazi Iendelee, sijui ninyi Wabunge mnasemaje.

**WABUNGE FULANI:** Mheshiwa Spika, Kazi Iendelee.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda katika kumalizia, nikiwa naelekea mwisho kumpongeza Dkt. Philip Isdor Mpango aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na kuthibitishwa na Bunge lako kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumpongeza kwa dhati kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Usimamizi wa Uchumi kama Waziri wa Fedha wa Serikali ya Awamu ya Tano na kuiwezesha nchi kuingia katika kundi la nchi za hadhi ya uchumi wa kipato cha kati cha chini. Vilevile, nampongeza kwa kazi nzuri iliyotukuka katika kuisimamia Wizara ya Fedha na Mipango ambayo kwa hakika ameweka misingi mizuri wa utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mheshimiwa Rais Mwinyi, ameanza kazi vizuri sana na kuwapa matumaini mapya na makubwa wananchi wa Zanzibar katika kukuza uchumi na maendeleo na hasa kwa kuwekeza katika *blue economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuteuliwa na kuthibitishwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nampongeza kwa uongozi wake hodari ndani ya Serikali na hapa Bungeni na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zilizomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha Uchaguzi cha mwaka 2020 hadi 2025. Tuna kiranja mkuu mzuri na tunapata maelekezo mazuri ndio maana tunafanya kazi nzuri na mtu *rahim* sana hata wakati ule tulipoyumba wana Yanga alituchangia. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze wakuu wa mihimili mingine ya dola kwa usimamizi na uongozi shupavu, nikianza na wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakupongeza sana na utendaji wako mzuri unawatamanisha vijana wengi kuwa Wabunge,

unatengeneza somo zuri kwa vijana wetu. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa kuongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na busara kubwa, ndio maana wananchi wa Mbeya Mjini walikupa ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa uongozi makini wa mhimili wa Mahakama unaozingatia, miiko, dira na dhima ya mhimili pamoja na majukumu hayo. Hakika uongozi wake umefanikisha upatikanaji wa haki kwa wanyonge na kujenga misingi imara ya utawala wa sheria hapa nchini. Amewezesha kuifanya nchi yetu iendelee kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Hussein Athman Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Mawaziri na Mkuu wa Utumishi wa Umma. Nampongeza kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Vilevile nawapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na usalama. Wameijengea heshima nchi yetu kwa namna wanavyofanya kazi katika nafasi zao. Kipekee, naomba niwatambue wakuu wa vyombo hivyo nikianza na Mkuu wa Majeshi - Jenerali Venance Salvatory Mabeyo, Inspekta Jenerali wa Polisi - Simon Nyakoro Sirro, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa - Diwani Athuman Msuya, Kamishna Jenerali wa Magereza - Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji - Dkt. Anna Peter Makakala,

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - *CP* Salum Hamdun, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya - Gerald Kusaya Musabila na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji - John William Masunga. Utumishi wao uliotukuka na uzalendo wa hali ya juu umetuwezesha kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwa amani. Tunaomba waendelee kutimiza wajibu weo na kulinda amani na usalama wa nchi yetu kwa moyo wa kizalendo kama wanavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati yako ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kwa umakini wao katika kuchambua na kutoa maoni na ushauri ambao umesaidia kuboresha mapendekezo ya bajeti hii. *(Makofi)*

Aidha, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa michango waliyotoa kupitia vikao vya Kamati za Kisekta iliyotuwezesha kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru viongozi na watumishi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu, nikianza na Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni mchango wake ni muhimu sana na ndiyo maana wananchi wa Jimbo la Kikwajuni wameendelea kumuamini. *(Makofi)*

Ninamshukuru sana Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel Tutuba, pamoja na Naibu Makatibu Wakuu, Amina Shaaban, Adolf Ndunguru pamoja na Dkt. Khatibu Kazungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nimshukuru Profesa Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kusimamia sekta ya fedha kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Ndugu Alphayo J. Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kuendelea na ukusanyaji wa mapato unaofanikisha kutekeleza miradi. Kadhalika, namshukuru *CPA* Charles Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anazofanya za kukagua na kutoa taarifa nzuri ya matumizi wakati wakiishauri Serikali. *(Makofi)*

Namshukuru *CPA* Athumani Mbuttuka, Msajili wa Hazina kwa kuendelea kusimamia Mashirika ya Umma na kuhakikisha Serikali inapata mchango na gawio stahiki. Pia namshukuru Dkt. Albina Chuwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kusimamia Ofisi ya Taifa ya Takwimu na kuendelea na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote na Naibu Mawaziri wote mlioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia Suluhu Hassan. Aidha, niwapongeze pia Wabunge wenzangu wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na wananchi na kuaminiwa na vyama vyao na kuchaguliwa kuwa Wabunge. *(Makofi)*

Kwa moyo wa dhati napenda kuishukuru sana familia yangu hususan mke wangu Bi. Neema Nchemba na watoto wangu kwa kunitia moyo na kuniombea wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Vilevile nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi walioniamini na kunichagua tena kwa kishindo kuwa Mbunge wao. Ninawaahidi kuwa sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wafanyabiashara na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari. Rai yangu kwao ni kuwa tukitumia rasilimali za nchi yetu vizuri kufanya kazi kwa umoja na bidii, tutaifanya Tanzania kuwa kitovu cha uchumi na biashara sio tu kwa kanda wa Afrika Mashariki bali kwa Afrika nzima. *(Makofi)*

Vilevile navishukuru vyombo vyote vya habari kwa kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua zao zilizowezesha kukamilisha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa amani na utulivu.

Aidha, nawashukuru kwa kuliombea Taifa letu katika kipindi kigumu tulichopitia cha kuondokewa na viongozi wetu wa kitaifa pamoja na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya korona. Sala na dua zao zimetuwezesha kupita kwa amani katika kipindi cha mabadiliko ya uongozi wa Kitaifa na hatimaye kumpata Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Ninawasihi waendelee kuliombea Taifa letu bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa mara nyingine, mwisho kabisa japo si kwa umuhimu nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha hoja hii na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno yote haya, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/22 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## I. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/22. Hotuba hii inawasilisha bajeti ya kwanza ya Kipindi cha Kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Bunge lako Tukufu yanawasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 137 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 23 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kifungu cha 124 (4) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020.

**2. Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii ninawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Bajeti ya Serikali. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato; Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali; Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa mwaka 2021 nayo ni sehemu ya bajeti hii.

**3. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuijalia nchi yetu amani, umoja na mshikamano na kutupatia kiongozi mwadilifu, thabiti na imara chini ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

**4. Mheshimiwa Spika,** huu ni Mkutano wa kwanza wa Bunge la Bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba 2020, ambapo Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilipata ridhaa ya wananchi kuendelea kuongoza nchi yetu. Ushindi mkubwa na wa kishindo uliopatikana kwa CCM umedhihirisha siyo tu imani kubwa ya wananchi kwa Chama Cha Mapinduzi, bali pia ni matarajio na kiu kubwa waliyonayo ya maendeleo kwa Taifa letu.

**5. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa tarehe 17 Machi, 2021 Taifa letu lilipata msiba mkubwa wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Naomba kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Bunge lako Tukufu, Wanafamilia hususan Mama Janeth Magufuli na Watanzania wote kwa msiba huo mzito. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ataendelea kukumbukwa kwa uongozi wake shupavu wenye uthubutu na uzalendo wa hali ya juu ulioleta mabadiliko chanya ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu. Mwenyezi Mungu aipumzishe Roho yake mahali pema peponi. Amina! Aidha, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Watanzania kwa kuondokewa na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mhandisi Balozi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina!

**6. Mheshimiwa Spika,** kipekee nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa kwanza mwanamke katika historia ya nchi yetu. **Mheshimiwa Spika** naomba **Niweke Ufunguo**, Katika Hotuba yangu popote nitakapo tumia neno **"MAMA YETU"** Nitakuwa namaanisha Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Katika muda mfupi wa uongozi wake, MAMA YETU ameonesha dhahiri kuwa ni kiongozi makini, shupavu, mchapa kazi, mwadilifu, msikivu na aliye na dira thabiti ya kuendelea kuiletea nchi yetu maendeleo makubwa. Aidha, ninampongeza "MAMA YETU" kwa kupata kura zote za ndio za wajumbe 1,862 wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Wana CCM na watanzania kwa ujumla wana imani kubwa sana kwake katika kukiongoza Chama kwa kuzingatia misingi ya Katiba ya Chama Cha Mapinduzi hasa ukizingatia uzoefu wake wa miaka 20 ya uongozi ndani ya chama. Hongera sana Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Ninawaomba watanzania wote kila mmoja kwa imani yake tuendelee kumuombea Mheshimiwa Rais ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ili Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu yake na **"KAZI IENDELEE"**.

**7. Mheshimiwa Spika,** hotuba hii inawasilisha Bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yenye Dira na Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita ya "**Kudumisha mazuri ya Awamu zilizopita, Kuyaendeleza mema yaliyopo na Kuleta mengine mapya**. Hivyo, makadirio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 yameandaliwa kwa kuzingatia nyaraka na miongozo mbalimbali ikiwemo: Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025; Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeyaridhia. Aidha, Bajeti imezingatia kikamilifu maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia Bunge hili tarehe 22 Aprili 2021.

**8.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kurejea baadhi ya maeneo yaliyobainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo yamezingatiwa katika bajeti hii kama ifuatavyo: Kudumisha Tunu za Taifa yaani Amani, Umoja na Mshikamano ambavyo ni msingi mkuu wa maendeleo wa Taifa letu; kuendelea kutekeleza kikamilifu Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini kwa kufanya marekebisho ya Sera, Sheria na kanuni mbalimbali ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuongeza fursa za ajira; kufanya maboresho ya mfumo wa utozaji na ukusanyaji wa kodi ili kurahisisha ulipaji wa kodi na kuongeza wigo wa walipa kodi; na kuendelea kuimarisha uendeshaji wa mashirika ya umma ili yaweze kujiendesha kwa faida na kutoa gawio na mchango stahiki kwa
Serikali.

**9.** **Mheshimiwa Spika,** maeneo mengine ni kuongeza tija ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuboresha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji kwa kushirikisha taasisi za fedha, ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo pamoja na benki nyingine; kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, uongezaji wa thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko; kukuza sekta ya viwanda hususan vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini na vyenye kuajiri watu wengi; kuendelea kuziba mianya ya utoroshaji wa madini na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji na uchakataji wa madini nchini ili kuongeza mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa; kuimarisha miundombinu ya usafiri, usafirishaji na nishati ikiwemo ujenzi wa barabara na madaraja, reli, usafiri wa majini na angani, upanuzi wa bandari pamoja na uzalishaji na usafirishaji wa umeme; kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma za jamii, hususan afya, elimu na maji; na kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa.

## II. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2020/21

### Mwenendo wa Mapato

**10. Mheshimiwa Spika,** katika bajeti ya mwaka 2020/21,
Serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 34.88 kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje. Hadi Aprili, 2021 shilingi trilioni 24.53 zimekusanywa sawa na asilimia 86.1 ya lengo la kipindi hicho. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:

(i) Mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalifikia shilingi trilioni 14.54, sawa na asilimia 86.9;

(ii) Mapato yasiyo ya Kodi yalifikia shilingi trilioni 1.80, sawa na asilimia 78.5 ya lengo;

(iii) Mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 607.4 sawa na asilimia
88.5 ya lengo;

(iv) Misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa ilikuwa shilingi trilioni 1.89 sawa na asilimia 70.4 ya lengo;

(v) Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipa dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia shilingi trilioni 3.99, sawa na asilimia 95.7 ya lengo; na

(vi) Mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara ilifikia shilingi trilioni 1.68 sawa na asilimia 88.1 ya lengo.

**11. Mheshimiwa Spika,** mlipuko wa UVIKO-19 umesababisha kutofikiwa kwa baadhi ya malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani hususan kwa sekta za utalii, usafiri wa anga na uingizaji wa bidhaa kutoka nje. Aidha, baadhi ya mashirika na taasisi zimeathiriwa na UVIKO-19 na hivyo kupungua kwa michango na gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Mathalani, mapato ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania yameathiriwa kufuatia kuporomoka kwa shughuli za utalii kulikosababishwa na kusambaa kwa UVIKO-19 katika nchi zinazoleta watalii wengi nchini.

**12. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha lengo la mapato ya ndani linafikiwa, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kama ilivyoainishwa ndani ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kufanya Biashara Nchini (Blueprint) kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, Serikali imeendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji sahihi wa sheria, kanuni na taratibu za kodi; kuboresha mifumo ya TEHAMA ikiwemo Electronic Fiscal Device Management System (EFDMS). Vilevile, Serikali imeendelea kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za Serikali pamoja na kuendelea kuhamasisha utalii wa ndani.

**13. Mheshimiwa Spika**, misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa hadi Aprili 2021 ni shilingi trilion 1.89 ikilinganishwa na shilingi trilion 1.82 mwaka 2019/20. Pamoja na athari za mlipuko wa UVIKO -19, misaada na mikopo nafuu iliongezeka kwa asilimia 3.84 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo ili kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu katika kuchangia bajeti ya Serikali.

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara, Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na baadhi ya Taasisi za Fedha za Kimataifa ili kuhakikisha kiasi kilichopangwa kukopwa kinapatikana. Vilevile, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wawekezaji kwenye soko la ndani la fedha ili kuhakikisha kiasi kilichopangwa kukopwa kinapatikana kwa wakati.

**Mwenendo wa Matumizi**

**15. Mheshimiwa Spika,** makadirio ya matumizi kwa mwaka 2020/21 yalikuwa shilingi trilioni 34.88 ambapo shilingi trilioni 22.10 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 12.78 ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, jumla ya shilingi trilioni 24.74 zimetolewa sawa na asilimia 86.8 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 17.42 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi trilioni 6.09 kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 4.49 Matumizi Mengineyo na shilingi trilioni 6.84 kugharamia deni la Serikali.

**16. Mheshimiwa Spika,** hadi Aprili 2021, jumla ya shilingi trilioni 7.32 sawa na asilimia 74.1 ya lengo zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi trilioni 6.24 ni fedha za ndani sawa na asilimia 79.7 ya lengo na shilingi trilioni 1.08 ni fedha za nje sawa na asilimia 52.8 ya lengo.

**17. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Serikali iliendelea kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia maeneo ya vipaumbele yaliyoainishwa kwenye bajeti kama ifuatavyo:

(i) Ulipaji wa deni la Serikali kwa wakati shilingi trilioni 6.84;

(ii) Ulipaji wa mishahara ya watumishi kwa wakati shilingi trilioni 6.09;

(iii) Miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ikiwemo mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere; na mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) shilingi trilioni 1.02;

(iv) Ujenzi na ukarabati wa Reli ikiwemo ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa shilingi trilioni 1.49;

(v) Ujenzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege shilingi trilioni 1.15;

(vi) Ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa ya Watumishi, Wazabuni na Watoa Huduma, Wakandarasi na Washauri Elekezi shilingi bilioni 965.1;

(vii) Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, elimumsingi bila ada, uimarishaji wa vyuo vya VETA, kukuza ujuzi kwa vijana na ujenzi wa miundombinu ya elimu shilingi bilioni 406.6;

(viii) Ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya shilingi bilioni 265.8; na

(ix) Miradi ya maji mijini na vijijini shilingi bilioni 207.5.

**Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali**

**18. Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya Uhimilivu wa Deni la Serikali ilifanyika Novemba, 2020 kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134. Tathmini hiyo ilionesha kuwa viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika Tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa: uwiano wa thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 27.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 70; uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 17.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; na uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240.

**19. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa viashiria vinavyopima uwezo wa nchi kulipa deni, matokeo yalibainisha kuwa, uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 23 na uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 14.0 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 21. Kwa kuzingatia viashiria hivyo, Tanzania ina uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ya nchi ili kugharamia miradi ya maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo inayoiva kwa wakati.

**Mwenendo wa Sekta ya Fedha**

**20. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka unaoishia Aprili 2021, viwango vya riba za mikopo ya benki kwa ujumla vilipungua na kufikia asilimia 16.58 kutoka wastani wa asilimia 16.91 Aprili 2020. Riba za mikopo za kipindi cha mwaka mmoja zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 16.05 kutoka asilimia 16.37 Aprili 2020. Aidha, riba za amana ziliongezeka na kufikia asilimia 6.95 kutoka asilimia 6.69 Aprili 2020. Riba za amana za mwaka mmoja ziliongezeka na kufikia asilimia 8.77 ikilinganishwa na asilimia 8.01 Aprili 2020. Hali hii inafanya tofauti kati ya riba za mkopo na amana kwa mwaka mmoja (interest rate spread) kupungua na kufikia asilimia 7.28 kutoka asilimia 8.36 Aprili 2020. Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa sekta ya benki ili kuongeza kasi ya kushuka kwa viwango vya riba za mikopo.

**21. Mheshimiwa Spika,** sekta ya benki imeendelea kuimarika ambapo uwiano wa mali inayoweza kubadilishwa kwa muda mfupi kuwa fedha taslimu (Liquid Assets to Demand Liabilities) ulikuwa ni asilimia 29.63 Machi 2021, ikiwa ni zaidi ya uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 20. Uwiano wa mikopo chechefu umepungua na kufikia asilimia 9.36 Machi 2021 ikilinganishwa na asilimia 10.50 Machi 2020. Aidha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 4.8 Aprili 2021. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unaenda sanjari na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi na utekelezaji wa mpango wa Serikali wa kuboresha mazingira ya biashara nchini.

**Athari za UVIKO - 19**

**22. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza juhudi za kukabiliana na athari za ugonjwa wa virusi vya korona (UVIKO-19), Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliunda Kamati Maalum ya Wataalamu kuchambua athari za ugonjwa huo na kushauri namna bora zaidi ya kukabiliana nao. Kamati ilikamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa tarehe 17 Mei 2021 ambapo, pamoja na mambo mengine, Kamati ilibaini kuwa Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani imeathirika kiuchumi na kijamii kutokana na UVIKO-19 hasa katika sekta muhimu zikiwemo afya, utalii, biashara, usafirishaji, sanaa na burudani, ambazo zimesababisha kushuka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya huduma nje, akiba ya fedha za kigeni na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha shughuli za uchumi zilizoathirika zinarejea katika hali ya kawaida kama ilivyokuwa kabla ya mlipuko wa UVIKO-19.

**23. Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 3 Mei 2021, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizungumza na Bi. Kristalina Georgieva - Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa nia ya kuimarisha mahusiano katika masuala ya kiuchumi na kijamii likiwemo suala la mikakati ya kukabiliana na athari za UVIKO-19. Kufuatia mazungumzo hayo, Wizara ya Fedha na Mipango imeanza majadiliano na IMF ya mkopo wa dharura (Rapid Credit Facility - RCF) wa dola za Marekani milioni 571. Mkopo huu ni wa masharti nafuu kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na UVIKO-19.

## III. SERA ZA BAJETI KWA MWAKA 2021/22

### Shabaha za Uchumi Jumla

**24. Mheshimiwa Spika**, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/22, yameandaliwa kwa kuzingatia misingi (assumptions) pamoja na shabaha mahsusi za uchumi jumla.
Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.6 mwaka 2021 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 6.2 ifikapo mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja kati ya wastani wa asilimia 3.0 – 5.0 kwa mwaka 2021/22;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2020/21;

(v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4.0); na

(vii) Kuhakikisha kuwa viashiria vya ustawi wa jamii vinaimarika.

**Sera na Mikakati ya Kuongeza Mapato**

**25. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Serikali itaendelea kuweka vipaumbele zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Masuala muhimu ya kuzingatia ni pamoja na kuimarisha na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuendelea kutekeleza hatua zifuatazo:

(i) Kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kuweka mazingira rafiki kwa mlipakodi kwa lengo la kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogo na za kati ili kupanua wigo wa kodi;

(ii) Kuendelea kutekeleza mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwianisha na kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada kero;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA;

(iv) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Serikali wa Kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG) na kuhakikisha taasisi zote za Serikali zinatumia mfumo huo;

(v) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi na Mashirika ya Umma ili kuhakikisha kuwa gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati;

(vi) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato;

(vii) Kuhamisha jukumu la uwekaji vinasaba kwenye mafuta ya petroli kutoka kwa mkandarasi binafsi kwenda Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kuhakiki ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini na kudhibiti ukwepaji kodi kutokana na uchakachuaji unaofanywa kwenye mafuta yanayopita hapa nchini; na

(viii) Kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa mikakati na miradi ya kuongeza mapato.

**26. Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua hizo za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma ili kuhamasisha ushiriki wa wawekezaji kwenye soko la ndani la fedha na kuorodhesha Hatifungani za Serikali katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza masuala yaliyoainishwa katika Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework - DCF) ili kuwezesha upatikanaji wa misaada na mikopo ya masharti nafuu na kukopa kwa utaratibu wa udhamini kutoka taasisi za udhamini wa mikopo (Export Credit Agencies - ECA), ambayo masharti yake yana unafuu.

**Sera za Matumizi**

**27. Mheshimiwa Spika,** Sera za Matumizi katika mwaka 2020/21 zitajumuisha yafuatayo:

(i) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;

(ii) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kuendana na vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(iii) Kudhibiti uzalishaji na ulimbikizaji wa madeni;

(iv) Kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma; na

(v) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali ili kuongeza ufanisi ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalamu wa ndani kwenye eneo la usalama wa mifumo (systems security).

**28. Mheshimiwa Spika,** ili kuendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa taasisi zinazotoza ada, Serikali inaweka utaratibu mpya na endelevu wa kusimamia mapato na matumizi ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Wakala wa Meli Tanzania (TASAC). Hivyo, kuanzia mwaka 2021/22, mapato yataendelea kukusanywa na taasisi hizo kupitia mfumo wa GePG na kuingizwa kwenye akaunti za makusanyo (holding account) zilizopo Benki Kuu. Aidha, taasisi hizi zitapatiwa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na fedha kutolewa kwenye akaunti ya makusanyo baada ya kupata ridhaa ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Vilevile, Serikali itafanya ufuatiliaji wa matumizi ya taasisi hizi kila robo mwaka.

**29. Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia utaratibu wa utoaji fedha kwa Taasisi za Uhifadhi (TANAPA, NCAA, TAWA) ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika kutekeleza azma hii Serikali itatoa fedha za matumizi mengineyo kwa miezi miwili unapoanza mwaka wa fedha na kuendelea kutoa kwa mwezi mmoja mmoja kila mwezi. Hatua hii itaziwezesha taasisi hizi kuwa na akiba ya fedha za kukidhi mahitaji ya mwezi unaofuata kwa kipindi chote cha mwaka.

**Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2021/22**

**30. Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 ni ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya **"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"**. Bajeti hii itajielekeza katika utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika maeneo matano (5) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Maeneo hayo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

**31. Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na uchumi shindani na shirikishi, Serikali itajielekeza katika kugharamia miradi ambayo itajikita katika: Kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kusimamia utulivu wa viashiria vya uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara za kufungua fursa za kiuchumi, kuunganisha nchi jirani, kupunguza msongamano mijini na barabara za vijijini, madaraja, usafiri wa majini na angani, mageuzi ya TEHAMA pamoja na kutekeleza mradi wa Tanzania ya Kidijitali, nishati, bandari na viwanja vya ndege. Eneo hili limetengewa jumla ya shilingi trilioni 7.44 ikijumuisha shilingi trilioni 3.13 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo.

**32. Mheshimiwa Spika**, miradi mingine ya kielelezo itakayotekelezwa ni: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli ya kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway) kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Ruhudji MW 358; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Rumakali MW 222; Uchimbaji wa madini ya Nickel; Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na Ununuzi wa Meli za Uvuvi; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi Bay North; Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi

wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Ustawi wa Jamii; na kuendeleza Kanda Maalumu za Kiuchumi.

**33. Mheshimiwa Spika**, katika eneo la kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, msukumo utawekwa kwenye miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Katika eneo hili, kipaumbele ni pamoja na: Kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi wa mazao ya kilimo; kuimarisha vituo vya utafiti na huduma za ugani; kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi; kuboresha huduma za uhimilishaji mifugo; na kujenga machinjio ya kisasa na minada ya mifugo.

**34. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaweka mkazo kwenye ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani ya madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini. Aidha, Bajeti hii itajielekeza katika kugharamia miradi na programu inayolenga kuboresha huduma za utalii, fedha na bima pamoja na kuendeleza viwanda vya uzalishaji wa dawa muhimu na vifaa tiba. Jumla ya shilingi trilioni 1.38 zimetengwa kugharamia utekelezaji wa miradi katika eneo hili.

**35. Mheshimiwa Spika**, katika eneo la kukuza uwekezaji na biashara, Serikali itagharamia programu zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa katika kukuza biashara. Masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, ikiwemo bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu. Vilevile, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ikiwemo kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Biashara na Uwekezaji (Blueprint). Eneo hili limetengewa jumla ya shilingi bilioni 31.6.

**36. Mheshimiwa Spika**, ili kuchochea maendeleo ya watu, miradi itakayotekelezwa italenga kuboresha maisha ya watu kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu na mafunzo kwa ujumla, afya na ustawi wa jamii, huduma za maji na usafi wa mazingira na kinga ya jamii ikijumuisha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kupitia TASAF. Aidha, Serikali itaendelea kupanga, kupima na kumilikisha ardhi mijini na vijijini, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji; na kuendelea na utekelezaji wa programu za kulinda mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya shilingi trilioni 4.43 zimetengwa.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuendeleza rasilimali watu, Serikali itagharamia programu inayolenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasimali watu katika ngazi zote za elimu ikiwemo kuweka mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Jumla ya shilingi bilioni 50.5 zimetengwa.

**38. Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu niliyowasilisha leo asubuhi ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 imeainisha kwa kina maeneo ya kipaumbele ambayo Serikali itayatekeleza kupitia Bajeti ya mwaka 2021/22.

**39. Mheshimiwa Spika,** pamoja na miradi ya kielelezo, Serikali itatekeleza miradi mingine ya uboreshaji wa miundombinu ambayo itagharamiwa na mikopo yenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Miradi hiyo ni Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili (DMDP II) wa kukabiliana na mafuriko kwenye Bonde la Mto Msimbazi utakaogharimu dola za Marekani milioni 120. Mradi huu utahusisha ujenzi wa daraja katika eneo la Jangwani, na upanuzi na ujenzi wa kingo za mto Msimbazi. Mradi wa pili unahusisha uboreshaji wa barabara za kukuza fursa shirikishi za kijamii na kiuchumi ambapo Benki ya Dunia itatoa dola za Marekani milioni 300 na mchango wa Serikali ni dola za Marekani milioni 50. Mradi huu unalenga kuboresha barabara za vijijini katika maeneo yenye tija kubwa ya uzalishaji wa mazao ya kilimo.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Serikali imeanza mazungumzo na Benki ya Dunia kupitia dirisha la International Development Association (IDA) kwa ajili ya mradi wa uboreshaji miundombinu katika Majiji na Miji 45. Utekelezaji wa mradi huu utaanza katika mzunguko wa 20 (IDA 20) unaotegemewa kuanza Julai 2022 na utagharimu kiasi cha dola za Marekani milioni 500. Mradi utahusisha ujenzi wa miundombinu ya msingi ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kukuza uchumi wa miji husika.

**Maeneo Mengine Muhimu**

**Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi Mwaka 2022**

**41. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajiandaa kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu SURA 351. Kama mojawapo ya maandalizi ya utekelezaji wa Sensa ya Mwaka 2022 Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa upande wa Tanzania Bara na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar imekamilisha kuandaa Kitabu cha Mkakati wa Usimamizi na Utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka, 2022. Kitabu hiki kinaainisha namna ya usimamizi na utekelezaji wa zoezi zima la Sensa, gharama ya kufanya Sensa pamoja na muundo wa Sensa utakavyokuwa katika ngazi zote za kiutawala.

**42. Mheshimiwa Spika,** jumla ya shilingi bilioni 328.2 zinatarajiwa kutumika kugharamia sensa ya mwaka 2022. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Sensa nchini, Sensa ya Mwaka 2022 itatumia teknolojia ya vishikwambi (tablets) katika utengaji wa maeneo ya kijiografia na ukusanyaji wa takwimu uwandani. Matumizi ya teknolojia hii yana manufaa makubwa, hasa katika kupunguza gharama na muda wa kukusanya na kuchakata takwimu, hali inayowezesha kutoa matokeo ya Sensa ndani ya muda mfupi.

**43. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ni jukumu la kila mtu, natoa wito kwa kamati zote za Sensa, Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote, Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote kwa ujumla kuhakikisha wanatoa ushirikiano wa kutosha katika maandalizi ya Sensa na wajitokeze wote siku ya kuhesabu watu. Lengo ni kuhakikisha Watu waliolala nchini usiku wa kuamkia siku ya Sensa (usiku wa sensa) wanahesabiwa na kuchukuliwa taarifa zao za kiuchumi, kijamii, mazingira na makazi wanayoishi na mengine mengi kwa ajili ya kupanga mipango endelevu ya maendeleo ya wananchi.

**Maslahi ya Wafanyakazi**

**44. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatambua na kuthamini mchango wa watumishi wa umma na wa sekta binafsi katika kukuza Pato la Taifa. Kwa kutambua hilo, Serikali itachukua hatua mbalimbali za kuboresha maslahi ya wafanyakazi kama ifuatavyo:

(i) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira (PAYE) kutoka asilimia 9 hadi asilimia 8. Hatua hii ni mwendelezo wa juhudi za Serikali za kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi, ambapo kiwango hicho kimepunguzwa kutoka asilimia 11 mwaka 2015/16 hadi asilimia 8 itakayoanza kutekezwa mwaka 2021/22;

(ii) Kufuta tozo ya asilimia 6 iliyokuwa ikitozwa kwa ajili ya kulinda thamani ya mkopo wa elimu ya juu (Value Retention Fee) kwa wanufaika; na

(iii) Kutenga jumla ya shilingi bilioni 449 kwa ajili ya kuwapandisha vyeo watumishi 92,619.

**Maslahi ya Madiwani, Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata**

**45. Mheshimiwa Spika**, Madiwani wenzetu wanafanya kazi nzuri sana za kusimamia shughuli za maendeleo kwenye kata zetu. Hawa ni wabunge wakaazi wa kwenye kata zetu ambao kila siku wako na wananchi wetu kwenye kusimamia shughuli za maendeleo. Hata hivyo, katika baadhi ya halmashauri madiwani wamekuwa wakikopwa posho zao, na wengine hufikia hatua ya kupiga magoti kwa wakurugenzi watendaji ili walipwe. Hali hii imekuwa ikipunguza ufanisi katika halmashauri zetu kwa madiwani wengi kufanya maamuzi yanayopendekezwa na wakurugenzi watendaji hata kama hayana maslahi kwa Taifa ili waweze kulipwa posho zao. Jambo hili limeongelewa kwa hisia kali sana na Waheshimiwa Wabunge hapa bungeni. Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani, napenda niwaeleze kuwa MAMA YETU amesikia kilio chenu na alinielekeza mimi pamoja na Waziri wa TAMISEMI kulitafutia ufumbuzi suala hili.

**46. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kuanzia mwaka 2021/22, Serikali Kuu ianze kulipa posho za kila mwezi za Waheshimiwa Madiwani moja kwa moja tena

kwenye akaunti zao kwa Halmashauri zote zenye uwezo mdogo kimapato. Halmashauri 16 zenye uwezo mkubwa wa kimapato (Daraja A) zitaendelea kutumia mapato yake ya ndani kulipa posho za Madiwani kupitia kwenye akaunti zao.

**47. Mheshimiwa Spika,** Maafisa Tarafa ni viunganishi muhimu wa ngazi za kata na Wilaya zetu ambapo wengi wao hufanya kazi nzuri sana ya kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali katika maeneo yao. Kwa kutambua umuhimu wao, Serikali ya CCM iliwapatia pikipiki viongozi hawa ili waweze kufanya kazi zao vizuri.
Hata hivyo, wengi wao wanashindwa kugharamia ununuzi wa mafuta na matengenezo ya vitendea kazi hivi na kulazimika kuwachangisha wananchi na hata wengine kuomba msaada kwa wadau mbalimbali. Hali hii inapunguza sana ufanisi katika Tarafa zetu. Kupitia hotuba hii, napenda niwajulishe Maafisa Tarafa wote nchini kuwa MAMA YETU amesikia kilio chenu. Hivyo, napendekeza kuanzia mwaka 2021/22, Serikali Kuu ianze kulipa posho ya shilingi 100,000/= kwa mwezi kwa kila Afisa Tarafa ili waweze kumudu gharama za mafuta na matengenezo ya pikipiki.

**48. Mheshimiwa Spika,** Watendaji Kata ndio wasimamizi wa kazi za sekta zote na ni watendaji wakuu kwenye kata. Wengi wao wanafanya kazi katika mazingira magumu ili kufanikisha shughuli za maendeleo katika kata zetu ikiwemo kusimamia ukusanyaji wa mapato na masuala ya usalama. Idadi kubwa ya watendaji hawa hutumia mishahara yao kufanya kazi mbalimbali ikiwemo ufutiliaji wa mapato ya Serikali kwa kukodi pikipiki ili kufanikisha shughuli zilizopo. Kwa ujumla wanafanya kazi nzuri sana ya kusimamia shughuli za maendeleo kwenye kata zetu. Jambo hili limeongelewa kwa hisia kali sana na Mheshimiwa Rose Busiga, Mbunge wa Viti Maalum (Geita), ambaye ni mtendaji wa kata mstaafu na kuungwa mkono na wabunge wengi hapa bungeni. Waheshimiwa wabunge, MAMA YETU amesikia kilio hiki na kutuelekeza kulitafutia ufumbuzi suala hili. Hivyo, napendekeza kuanzia mwaka 2021/22, Serikali kuanza kulipa posho ya shilingi 100,000/= kwa mwezi kwa kila Mtendaji Kata kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri yaliyokuwa yakitumika kulipa madiwani.

### Madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**49. Mheshimiwa Spika,** wastaafu wetu walilitumikia Taifa hili kwa uzalendo, uadilifu na bidii kubwa sana. Hatuwezi kuhesabu mafanikio ya nchi yetu bila kutaja mchango wa wazee hawa. Kumekuwepo na changamoto za muda mrefu za ulipaji wa mafao yao kutokana na ufanisi mdogo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kuhudumia wastaafu wetu. Hali hiyo kwenye mifuko yetu imechangiwa, pamoja na mambo mengine, na uwepo wa madeni ambayo mifuko inaidai Serikali na hivyo kusababisha wastaafu wetu kukosa au kusubiri kwa muda mrefu ili kulipwa mafao yao. Jambo hili pia limejadiliwa kwa hisia kali na Waheshimiwa Wabunge hapa bungeni. Wazee wetu hawa hupata shida sana, ambapo baadhi yao hufadhiliwa malazi kwa kulala misikitini na makanisani na wengine hutegemea wahisani kuhudumia familia zao kinyume na mchango

walioutoa katika ujenzi wa nchi hii. MAMA YETU amesikia kilio cha wazee hawa na kutuelekeza Wizara ya Fedha na Mipango kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu kukamilisha zoezi la kitaalamu ili kujua hali halisi ya madeni na namna bora ya kulipa madeni hayo.

**50. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kulipa madeni yanayodaiwa na mifuko kwa kutenga fedha kwenye bajeti na kutumia utaratibu wa kutoa hatifungani maalum isiyo taslimu (Non-cash Special Bond) zitakazoiva kwa nyakati tofauti kuanzia miaka miwili hadi 25. Utaratibu wa hatifungani una faida mbalimbali zikiwemo: kuipa Serikali nafasi ya kibajeti ya kuendelea kutekeleza miradi mingine ya maendeleo; kuiwezesha Serikali kuyatambua madeni hayo kwenye kanzidata ya madeni; na kuzuia madeni hayo kuendelea kuongezeka kulingana na tathmini ya thamani ya madai (actuarial valuation). Aidha, utaratibu huo utaboresha mizania ya hesabu na mtiririko wa mapato yanayotokana na riba ya hatifungani hizo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hatua hii inakwenda kumaliza kabisa tatizo hilo la wazee wetu kudai haki yao kwa damu na machozi yaliyodumu kwa muda mrefu.

**51. Mheshimiwa Spika**, Serikali imepokea malalamiko kuhusu kucheleweshwa kwa michango ya watumishi kupelekwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na baadhi ya ofisi za Serikali kutopeleka kabisa michango hiyo. Jambo hili limekuwa likisababisha usumbufu kwa watumishi punde wanapostaafu. Hivyo, napendekeza kulipa michango hiyo moja kwa moja kutokea Hazina kwa taasisi zote ambazo watumishi wanalipwa na Hazina. Taasisi ambazo zinalipa watumishi kutokana na vyanzo vyao vya mapato zitaendelea kupeleka michango ya watumishi wao kwa ufuatiliaji wa karibu wa Serikali. Serikali itafanya uhakiki na kulipa madeni ya michango ambayo haijawasilishwa kwenye mifuko hadi sasa.

**Jeshi la Polisi**

**52. Mheshimiwa Spika,** katika jeshi la polisi kwa askari wapiganaji, kuna utaratibu wa wapiganaji kufanya kazi kwa mikataba ya muda mfupi kwa miaka 12 kabla hawajapata ajira za kudumu. Jambo hili huwasababishia wapatapo mkataba wa kudumu wawe wamechelewa kwa miaka 12 ikilinganishwa na mtumishi mwingine aliyeingia pamoja kazini katika idara nyingine. Jambo hili linamadhara hasi katika itifaki ya utumishi na mafao ya mpiganaji anapostaafu. Hiki kimekuwa kilio cha muda mrefu cha askari wa Jeshi la Polisi. Kutokana na changamoto hiyo, MAMA YETU amesikia kilio cha askari hao na alituelekeza tukae na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kutafuta suluhisho la jambo hili. Napendekeza kuanzia mwaka 2021/22 askari wa Jeshi la Polisi wataingia mkataba wa kipindi cha miaka 6 na kuingia katika ajira ya kudumu.

**Kurahisisha Kasi ya Utekelezaji wa Miradi**

**53. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usimamizi na ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya mabadiliko katika Kanuni ya 21 ya Sheria ya Bajeti, SURA 439 ili kuondoa changamoto iliyopo ya

fedha ambazo hazijatumika hadi tarehe 30 Juni kila mwaka kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Mabadiliko hayo yatatoa fursa kwa Maafisa Masuuli kuwasilisha taarifa ya fedha kuvuka mwaka hadi tarehe 30 Juni kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali badala ya siku 15 kabla ya mwaka wa fedha kumalizika. Fedha hizo zitawekwa kwenye Akaunti ya Amana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli ambazo hazijakamilika wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha husika. Kwa msingi huo, kuanzia sasa hakutakuwa na fedha zenye miadi zitakazorejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka wa fedha isipokuwa pale ambapo Maafisa Masuuli wamekiuka masharti ya Sheria ya Bajeti, SURA 439 na Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348.

**Kodi ya Majengo**

**54. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na changamoto kubwa katika ukusanyaji wa kodi ya majengo, hali iliyosababisha Serikali kubadili njia za ukusanyaji mara kwa mara. Kabla ya mwaka 2017/18, Serikali za Mitaa zilikuwa na jukumu la kukusanya mapato hayo lakini hazikufanya vizuri. Kuanzia mwaka 2017/18, Serikali ilitumia Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi hiyo, ambapo pia haikufanya vizuri. Ukusanyaji wa kodi hii kwa kutumia Serikali za Mitaa au TRA umekuwa ukitumia njia za kizamani ambazo zinahusisha watu kusafiri, kupanga foleni na kukusanya fedha taslimu (cash). Utaratibu huu unatumia gharama kubwa, muda na ni hatarishi kwa mapato. Katika kuhakikisha kodi hii inafikia malengo, Serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi ya majengo.

**Kodi ya Wajasiliamali**

**55. Mheshimiwa Spika,** wafanyabiashara na watoa huduma wadogo nchini wameendelea kutambulika kupitia vitambulisho vya wajasiriamali. Tangu kuanza kwa zoezi la utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara na watoa huduma wadogo nchini, jumla ya vitambulisho 2,335,711 vimegawiwa ambavyo vimewezesha kukusanya jumla ya shilingi bilioni 46.71. Lengo ni kuendelea kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji biashara. Katika mwaka 2020/21, Serikali imefanya maboresho ya vitambulisho hivyo kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti na kufungua fursa kwa wajasiriamali kuweza kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya. Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea na uratibu wa kugawa vitambulisho hivi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ambayo ndiyo yenye mfumo wa kusajili wafanyabiashara hao, kuchapisha vitambulisho na kuwapatia Halmashauri husika kwa ajili ya kugawa.

**IV. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA NA TOZO MBALIMBALI**

**56. Mheshimiwa Spika,** napenda sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapendekezo ya kufanya **marekebisho ya mfumo wa kodi**, ikiwemo baadhi ya **viwango vya kodi**, **tozo na ada zinazotozwa chini ya Sheria mbalimbali na kurekebisha taratibu za ukusanyaji na usimamiaji wa mapato ya**

**Serikali.** Marekebisho haya yamezingatia dhamira ya Serikali ya kurejesha ukuaji wa uchumi katika hali ya kawaida baada ya athari zilizotokana na UVIKO-19 sambamba na kuendelea kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika ili kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje. Vile vile, marekebisho yanalenga **kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi** hususan katika **sekta ya kilimo na viwanda**, **kuongeza kipato kwa waajiriwa** na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (BluePrint) kwa kuwianisha tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Wizara na Mamlaka za Udhibiti kwa lengo la kupunguza na kurahisisha ulipaji wake au kuzifuta baadhi ya tozo na ada hizi. Marekebisho yanayopendekezwa yanahusu Sheria zifuatazo:

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148;

(b) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;

(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;

(d) Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;

(e) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;

(f) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;

(g) Sheria ya Kodi ya Majengo, SURA 289;

(h) Sheria ya Ardhi, SURA 113;

(i) Sheria ya Ushuru wa Stempu, SURA 189;

(j) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82;

(k) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41;

(l) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, SURA 418;

(m) Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134

(n) Sheria ya Usajili wa Magari, SURA 124;

(o) Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168;

(p) Sheria ya Raia wa Kigeni (Uratibu wa Ajira) Na. 1 ya mwaka 2015;

(q) Marekebisho ya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa Wakala, Mamlaka za Udhibiti na Idara zinazojitegemea;

(r) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali;

(s) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara (Blueprint) kwa kurekebisha Ada na Tozo mbalimbali;

(t) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220;

(u) Sheria ya Petroli, SURA 392; na

(v) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306.

**A. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148**

**57. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 kama ifuatavyo:

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyumba vya ubaridi (cold rooms) vinavyotambuliwa kwa H.S Code 9406.10.10 na 9406.9010. Lengo la msamaha huu ni kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mbogamboga na maua nchini ili kuchochea kilimo cha kisasa;

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini (precious metals) na makinikia yatakayoingizwa nchini kwa ajili ya kuchenjuliwa, kuongezewa thamani na kuuzwa kwenye masoko ya madini yanayotambulika nchini. Lengo la pendekezo hili ni kuviwezesha viwanda vya uchenjuaji vilivyoanzishwa nchini kupata malighafi ya kutosha kwa ajili ya uchakataji na hatimaye kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za bima ya mifugo. Lengo la marekebisho haya ni kuchochea shughuli za ufugaji nchini;

(iv) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa na huduma zitakazoingizwa au kununuliwa hapa nchini kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mafuta ghafi (EACOP). Lengo la marekebisho haya ni kutoa unafuu wa kodi katika utekelezaji wa miradi tajwa;

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ghafi yanayotambulika kwa H.S Code 2709.00.00 kwa lengo la kutoa unafuu kwa mlaji ikiwemo Kampuni ya uendeshaji wa bomba la mafuta (EACOP);

(vi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Nyasi Bandia zinazotambulika kwa HS Code 5703.30.00 na 5703.20.00 kwa ajili ya Viwanja vya Mpira vilivyoko kwenye Majiji. Msamaha huo utahusisha ridhaa kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuendeleza michezo na kukuza vipaji nchini;

(vii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kadi za kutengeneza vitambulisho vya taifa zinazotambulika kwa H.S Code 3921.11.90.00 na malighafi nyingine za kutengeneza kadi hizo zinazotambulika kwa H.S Code 3921.11.90.00 zitakazoingizwa nchini na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Lengo la pendekezo hili ni kupunguza gharama za kutengeneza Vitambulisho vya Taifa na kuharakisha upatikanaji wake;

(viii) Kumekwepo na ukiritimba katika kupokea fedha za misaada kwenye miradi ya maendeleo kwa hitaji la kisheria la kusubiri idhini ya Baraza la Mawaziri likae ili kuidhinisha misamaha. Napendekeza Kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Taasisi zisizo za kiserikali (NGO's), kwenye bidhaa na huduma zitakazotumika kwenye miradi inayotekelezwa na taasisi husika. Aidha, taasisi zitakazonufaika na msamaha huo ni zile ambazo zina mikataba na Serikali yenye kipengele kinachotoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani;

(ix) Sekta ya mawasiliano imekuwa ikikua vizuri na kuwa kiungo muhimu cha kuongeza wigo wa wananchi ambao wako kwenye ulimwengu wa kidijitali na kwenye sekta ya fedha (Financial Inclusion). Napendekeza kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye simu janja za mkononi (smart phones) HS Code 8517.12.00, vishikwambi (Tablets) HS Code 8471.30.00 au 8517.12.00 na modemu (modems) HS Code 8517.62.00 au 8517.69.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya huduma za mawasiliano ili kufikia lengo la asilimia 80 ya watumiaji wa intaneti ifikapo mwaka 2025 kutoka asilimia 46 iliyopo sasa;

(x) Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mikebe inayotumika kuhifadhia maziwa inayotambuliwa kwa H.S Code 7310.29.20 ambayo kwa sasa haitumiki kwa ajili ya kazi hiyo na badala yake napendekeza kutoa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mikebe ya kubebea maziwa inayotambulika kwa H.S Code 7310.29.90, 7310.10.00 na 7612.90.90. Lengo la Pendekezo hili ni kuwapunguzia gharama wazalishaji na kuchochea ukuaji wa sekta ya maziwa nchini;

(xi) Kufuta msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taa zinazotumia umeme wa jua zinazotambulika kwa H.S. Code 85.13 na 94.05. Lengo la pendekezo hili ni kuwianisha msamaha huu sambamba na msamaha unaotolewa chini ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ambayo inasamehe Kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha nishati ya umeme wa jua pekee na kurahisisha usimamizi wake. Aidha, pendekezo hili linalenga kuweka usawa katika ulipaji kodi kwa watumiaji wa taa zinazotumia nishati za aina zote;

(xii) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye huduma ya usafirishaji na huduma zinazohusiana na usafirishaji wa mafuta ghafi kupitia bomba linalojengwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Tanzania na Uganda (EACOP). Lengo la pendekezo hili ni kuwezesha huduma tajwa kutekelezwa bila kodi sanjari na uzoefu wa kimataifa kwa bidhaa zilizopita hapa kwenda nchi jirani au ng'ambo;

(xiii) Kuzitambua bidhaa za mtaji zilizomo kwenye Sura ya 84, 85 na 90 ya Kitabu cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha wa Afrika Mashariki kuwa bidhaa za mtaji zitakazostahili kupata kivutio cha ahirisho la malipo ya VAT. Lengo la pendekezo hili ni kuwianisha maana ya bidhaa za mtaji kwenye Sheria za kodi na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali kwenye kifungu tajwa;

(xiv) Kubadilisha utaratibu wa kutoa msamaha kwenye miradi ya Serikali inayogharamiwa na fedha za serikali na fedha za wafadhili ambapo mnufaika wa msamaha huo atawasilisha maombi kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania badala ya utaratibu wa kuwasilisha kwa Waziri wa Fedha kwa ajili ya kupata ridhaa na kutoa Tangazo la Serikali (GN) kwa kila mradi. Utaratibu huu utarahisisha na kuharakisha utoaji wa misamaha badala ya utaratibu wa sasa kutokana na TRA kuwa na ofisi kwa kila mkoa nchini kote ambazo zinaweza kupokea, kuchambua na kusimamia matumizi sahihi ya misamaha; na

(xv) Kuhusu Zanzibar, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kurudisha utaratibu wa kurejesha VAT kwa bidhaa zinazonunuliwa Tanzania Bara na kutumika Tanzania Zanzibar. Hii inatokana na mfumo wa kutoza VAT kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa bidhaa za viwandani pekee kutowanufaisha wafanyabiashara wa Zanzibar wanaonunua bidhaa na kutozwa VAT Tanzania Bara na kutozwa tena VAT bidhaa hizo zinapopelekwa Zanzibar. Aidha, inapendekezwa marejesho ya VAT yatakayofanyika kwa bidhaa zinazotoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar yafanyike pia kwa bidhaa zitakazotoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara sambamba na marekebisho ya vifungu husika vya Sheria za VAT kwa pande zote mbili za muungano. Ili kuwa na ufanisi wa marejesho, maboresho ya mifumo yatafanyika ili isomane baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Kutokana na utaratibu huu, kiwango cha asilimia sifuri ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kilichokuwa kinatozwa bidhaa hizo kitasitishwa.

Hatua zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla zinatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 55,499.97.**

**B. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332**

**58. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 kama ifuatavyo:

(i) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza Kodi ya Mapato yanayohusiana na ajira kutoka asilimia 9 hadi asilimia 8 kama ilivyobainishwa katika **Jedwali Na. 1A na 1B.**

| **Jedwali Na. 1A: Viwango vya sasa** | |
|---|---|
| **Jumla ya Mapato** | **Kiwango cha Kodi** |
| Mapato ya jumla yasiyozidi shilingi 3,240,000/= | Hakuna kodi |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 3,240,000/= lakini hayazidi shilingi.6,240,000/= | 9% ya kiasi kinachozidi shilingi 3,240,000/= |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 6,240,000/= lakini hayazidi shilingi 9,120,000/= | Shilingi 270,000/= jumlisha 20% ya kiasi kinachozidi shilingi 6,240,000/= |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 9,120,000/= lakini hayazidi shilingi 12,000,000/= | Shilingi 846,000/= jumlisha 25% ya kiasi kinachozidi shilingi 9,120,000/= |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 12,000,000/= | Shilingi 1,566,000/= jumlisha 30% ya kiasi kinachozidi shilingi 12,000,000/= |
| **Jedwali Na. 1B Viwango vinavyopendezwa** | |
| Mapato ya jumla yasiyozidi shilingi 3,240,000/= | Hakuna kodi |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 3,240,000/= lakini hayazidi shilingi 6,240,000/= | 8% ya kiasi kinachozidi shilingi 3,240,000/= |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 6,240,000/= lakini hayazidi shilingi 9,120,000/= | Shilingi 240,000/= jumlisha 20% ya kiasi kinachozidi shilingi 6,240,000/= |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 9,120,000/= lakini hayazidi shilingi 12,000,000/= | Shilingi 816,000/= plus 25% ya kiasi kinachozidi shilingi 9,120,000/= |
| Mapato ya Jumla yanayozidi shilingi 12,000,000/= | Shilingi.1,536,000/= plus 30% ya kiasi kinachozidi shilingi 12,000,000/= |

Hatua hii inachukuliwa ikiwa ni dhamira ya Serikali ya muda mrefu kuwapunguzia mzigo wa Kodi wafanyakazi. Hatua hii inatarajiwa **kupunguza** mapato kwa shilingi **milioni 14,178.06;**

(ii) Kutoa msamaha wa Kodi ya Mapato kwenye hatifungani za Serikali. Sheria ya Kodi ya Mapato ilisamehe Kodi ya Mapato kwenye hatifungani kwa mwaka 2002/03 pekee. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha soko la ndani la hatifungani linaendelea kusaidia kugharamia miradi ya Serikali;

(iii) Kumekuwepo na ukiritimba katika kupokea fedha za kutoka kwa nchi wahisani zinazokwenda kutekeleza Miradi ya maendeleo. Napendekeza Kurejesha utaratibu wa Mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutoa msamaha kwa kutoa tangazo la Serikali (GN) bila sharti la kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za wafadhili kupitia mikataba iliyoingiwa baina ya nchi hizo na Serikali yenye kifungu kinachoruhusu msamaha wa kodi ya mapato. Lengo la marekebisho haya ni kuharakisha utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa kwa misaada na mikopo yenye gharama nafuu ambayo utekelezaji wake umekuwa ukichelewa kusubiri ridhaa ya Baraza la Mawaziri;

(iv) Kutoza Kodi ya Zuio kwa kiwango cha asilimia mbili (2) kwenye malipo yanayohusisha mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye kampuni na mashirika yote yanayojihusisha na usindikaji na ununuzi wa mazao. Kwa sasa, Taasisi za Serikali pekee kama vile (Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ndizo zinakata kodi hiyo kwa kiwango cha asilimia mbili (2). Aidha, pendekezo hili halitahusisha wakulima wadogo na wale wanaouza mazao yao kwenye masoko ya msingi (AMCOS) na kwenye magulio. Lengo la pendekezo hili ni kuweka usawa katika utozaji wa kodi kwa Kampuni zote zinazojishughulisha na mazao ya Kilimo, mifugo na uvuvi.
Pendekezo hili linatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 43,954.2**;

(v) Kufanya maboresho ya Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuwezesha ukokotoaji wa gharama za uchakavu kwa kiwango maalum cha asimilia tano (5) kwenye gharama za mali za ujenzi wa bomba la mafuta (EACOP). Lengo la pendekezo hili ni kuwianisha gharama za uchakavu na muda wa matumizi wa bomba husika kwa kuzingatia masharti ya mkataba uliosainiwa baina ya Serikali za Uganda na Tanzania;

(vi) Kuweka utaratibu maalum wa utozaji kodi kwa wachimbaji wadogo wa madini wenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni 100 kwa mwaka kama ifuatavyo: -

(a) Kutoza kodi wachimbaji wadogo wa madini kwa kiwango mfuto cha asilimia 3 kwenye thamani ya mauzo ya madini pindi yanapopatikana;

(b) Kuweka muda wa ulipaji kodi kuwa ni wakati wanapouza madini na kulipa mrabaha kwenye Tume ya Madini au maeneo maalum yaliyoanzishwa chini ya sheria ya madini;

(c) Kuweka wajibu kwa mchimbaji mdogo wa madini kama mwajiri wa kukata kodi ya mapato ya ajira kutoka kwa wafanyakazi wake pale tu madini yatakapokuwa yamepatikana na kuuzwa katika masoko ya madini;

(d) Kuweka muda maalum wa kulipa kodi ya zuio ya ajira kuwa ni wakati mchimbaji mdogo anapouza madini na kulipa mrabaha katika masoko ya madini au vituo vingine vya uuzaji na ununuzi wa madini vinayotambuliwa na Tume ya Madini; na

(e) Kuweka kiwango cha kodi cha mapato ya ajira (PAYE) cha asilimia 0.6 ya thamani ya mauzo ya madini ambayo italipwa na mwajiri (mchimbaji mdogo wa madini) kwa niaba ya wafanyakazi wake.

Lengo la mapendekezo haya ni kurahisisha utozaji na ulipaji wa kodi kutoka kwa wachimbaji wadogo wa sekta ya madini ili kuongeza mchango wa kodi ya mapato kutoka kwenye sekta hiyo. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajia **kuongeza** mapato ya Serikali shillingi **milioni 29,776.14**

**C. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

**59. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, marekebisho ya viwango maalumu vya ushuru wa bidhaa (specific duty rates) kwa bidhaa zote zisizo za petroli yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuvihuisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Hata hivyo, kutokana na biashara za bidhaa hizi kuzorota kutokana na athari za kiuchumi zilizosababishwa na ugonjwa wa UVIKO-19, **napendekeza kutofanya mabadiliko ya viwango maalumu vya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zote zisizo za petroli isipokuwa vinywaji vikali na bia zitakazotengenezwa kwa kutumia shayiri iliyozalishwa hapa nchini**.

**60. Mheshimiwa Spika,** napendekeza pia kufanya **marekebisho ya Ushuru wa bidhaa** kwenye bidhaa zifuatazo:

(i) Kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye bia zinazotengenezwa kwa kutumia shayiri iliyozalishwa hapa nchini kutoka shilingi 765 kwa lita za sasa hadi shilingi 620 kwa lita. Lengo la mapendekezo haya ni kuchochea kilimo cha shayiri hapa nchini;

(ii) Kuanza kutoza Ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye nyuzi na kamba za plastiki (synthetic fibres) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi au kuzalishwa hapa nchini zinazotambuliwa kwa heading 55.11 na 56.07 isipokuwa zile zinazotumika kwenye Uvuvi (HS Code 5607.50.00). Lengo la marekebisho haya ni kulinda

mazingira na kuchochea uzalishaji na matumizi ya bidhaa za katani. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** mapato ya
Serikali kwa shilingi **milioni 2,644;** na

(iii) Kuanzisha tozo ya ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye pikipiki zilizotumika kwa zaidi ya miaka 3 zinazoingizwa nchini zinazotambuliwa kwa HS Code 8711. Lengo la marekebisho haya ni kudhibiti uingizaji wa pikipiki chakavu na kulinda mazingira. Hatua hii inatarajiwa **kuongeza** ya mapato ya Serikali kwa shilingi **milioni 263.7.**

Hatua za kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,907.7.**

**D. Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

**61. Mheshimiwa Spika,** Kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha Maandalizi ya Bajeti (EAC PreBudget Consultative Meeting of Ministers of Finance) kilichofanyika tarehe 7 Mei 2021 mjini Arusha, kilipendekeza kufanya marekebisho ya Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha (EAC-Common External Tariff) na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Customs Management Act, 2004) kwa mwaka wa fedha 2021/22. Mapendekezo hayo yanalenga katika Kuboresha Maisha ya Watu Kupitia Maendeleo ya Viwanda na Kutengeneza Ajira kwa ajili ya Ustawi wa Pamoja wa Watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**62. Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Mawaziri wa Fedha ya kufanya marekebisho kwenye Viwango vya Pamoja vya Ushuru wa Forodha yanahusisha hatua mpya na zinazoendelea ambazo zimekuwa zikitekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2020/21. Hatua hizo ni kama zifuatazo:

(i) Mapendekezo ya hatua mpya za Viwango vya Ushuru wa Forodha ni kama ifuatavyo: -

(a) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye mabasi ya abiria yanayotambulika kwa HS Codes 8702.10.99 na 8702.20.99 yanayoingizwa nchini kwa ajili ya mradi wa mwendokasi. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za uingizaji wa mabasi hayo ili kurahisisha usafiri kwa wananchi;

(b) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyuzi za pamba (cotton yarn) zinazotambulika kwa Headings 52.05, 52.06 na 52.07. Lengo la hatua ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo na kuongeza thamani ya zao la pamba (value addition) nchini;

(c) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye matairi mapya ya pikipiki (new pneumatic tyres of rubber) yanayotambulika kwa HS Code 4011.40.00. Lengo la hatua ni kuongea mapato ya Serikali kwa kuwa matairi haya ni bidhaa zilizokamilika kwa ajili ya mtumiaji;

(d) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye siagi ya karanga (peanut butter) inayotambulika kwa HS Code 2008.11.00. Lengo la hatua ni kulinda wazalishaji wa bidhaa hiyo nchini;

(e) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye nyaya (wire of other alloy steel) zinazotambulika kwa HS Codes 7229.20.00 na 7229.90.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji wanaotumia bidhaa hiyo kama malighafi;

(f) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye milk cans zinazotambulika kwa HS Codes 7310.10.00 na 7310.29.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwenye sekta ya maziwa nchini;

(g) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye LABSA (Organic surface-active agents – Anionic) inayotambulika kwa HS Code 3402.11.00 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa sabuni za unga na maji nchini;

(h) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kuchakata ngozi zinazotambulika kwa HS Code 3208.20.00 na 3210.00.10 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa ngozi nchini;

(i) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mbolea zinazotambulika kwa HS Codes 2710.99.00, 2528.00.00 na 3505.20.00 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea nchini;

(j) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya tumbaku iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Code 5310.10.00 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa tumbaku nchini;

(k) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya chai iliyochakatwa vinavyotambulika kwa HS Codes 4819.20.90, 5407.44.00 na 3923.29.00 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wachakataji wa chai (tea blenders) nchini;

(l) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi ya kutengeneza masufuria ya aluminium

inayotambulika kwa HS Code 7606.92.00 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa masufuria hayo nchini;

(m) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa waunganishaji wa pikipiki za matairi matatu bila kujumuisha fremu kwa kuwa zinatengenezwa hapa nchini (CKD for three-wheel motorcycles excluding chassis and its components) zinazotambulika kwa HS Code 8704.21.90 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa waunganishaji wa pikipiki hizo nchini ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo;

(n) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 au 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi za kutengeneza mabomba ya plastiki (glass reinforced plastic pipes) zinazotambulika kwa HS Codes 3920.61.10, 7019.39.00, 7019.31.00, 6006.90.00, 7019.12.00, 3920.10.10, 4016.93.00, na 3907.91.00 kwa utaratibu wa duty remission. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa watengenezaji wa mabomba hayo nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya maji; na

(o) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwenye mabati (Flat-rolled products of other alloy steel, of a width of 600mm or more, not further worked than hot-rolled, in coils) yanayotambulika kwa HS Code 7225.30.00. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa wazalishaji wanaotumia bidhaa hiyo kama malighafi.

(ii) Mapendekezo ya kuendelea na utekelezaji wa Viwango vya Ushuru wa Forodha vya mwaka 2020/21 ni kama ifuatavyo:

(a) Kupunguza Ushuru wa Forodha hadi asilimia 0 kutoka viwango vya awali vya asilimia 10 na asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye malighafi zinazotumika katika uzalishaji wa vifaa maalum vinavyotumika katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu (UVIKO-19) vikiwemo Barakoa (Masks), kipukusi (sanitizer), mashine za kusaidia kupumua (ventilators), na mavazi maalum ya kujikinga yanayotumiwa na madaktari na wahudumu wa afya (PPE). Msamaha huu utatolewa kwa utaratibu wa "duty remission". Hatua hii inalenga kutoa unafuu wa uzalishaji wa vifaa hivyo hapa nchini ili kuongeza kasi katika kupambana na ugonjwa huo;

(b) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye mashine za kielektroniki zinazotumika kukusanya mapato ya Serikali (Cash registers, Electronic Fiscal Device (EFD) Machines and Point of Sale (POS) machines zinazotambulika katika HS Code 8470.50.00 na 8470.90.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha matumizi ya vifaa hivi katika kuhasibu mapato ya Serikali;

(c) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vinavyotumiwa na wazalishaji wa maziwa

kwa joto la juu yanayodumu kwa muda mrefu (UHT Milk) vinavyotambulika kwa HS codes 4819.50.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa maziwa hapa nchini. Utaratibu wa Duty Remission utakaotumika kutoa unafuu huo;

(d) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka kiwango cha asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifuniko vya chupa za mvinyo (corks and stoppers) vinavyotambulika kwa HS Codes 4503.10.00 kwa kuzingatia kuwa havizalishwi hapa nchini. Hatua hii inalenga kuwapunguzia gharama wazalishaji wa mvinyo ili kuhamasisha na kuendeleza kilimo cha zao la zabibu nchini pamoja na ajira. Utaratibu wa Duty Remission utakaotumika kutoa unafuu huo;

(e) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za marumaru zinazotambulika kwa HS Code 6907.21.00; 6907.22.00; na 6907.23.00 zinazoingizwa kutoka nje. Lengo la hatua hii ni kulinda na kukuza viwanda vya ndani vinavyozalisha marumaru pamoja na kuongeza ajira;

(f) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye chai inayotambulika kwa HS Code 09.02 inayoagizwa kutoka
nje. Lengo la pendekezo hili ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha kilimo cha chai hapa nchini pamoja na kuongeza ajira katika sekta ya kilimo;

(g) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye magunia ya kitani (sacks and bags of jute or other textile bast fibers of heading 53.03) yanayotambulika kwa HS Code 6305.10.00 yanayoagizwa kutoka nje. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani vinavyotengeneza magunia ya katani, kukuza na kuendeleza kilimo cha zao la mkonge hapa nchini pamoja na kuongeza ajira na mapato ya Serikali;

(h) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 0 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye unga wa kakao unaoingizwa kutoka nje unaotambulika kwa HS Code 1805.00.00. Lengo ni kuchochea na kuhamasisha kilimo cha zao la kakao nchini pamoja na kuongeza mapato ya Serikali;

(i) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia kahawa vinavyotumiwa na viwanda vya kusaga kahawa nchini. Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS codes 7310.21.00; 6305.10.00; 3923.50.10; 3923.50.90 na 3920.30.90. Hatua hii inalenga kuongeza thamani kwenye zao la kahawa na kuvipa unafuu wa gharama viwanda vinavyosaga kahawa hapa nchini. Utaratibu wa "Duty Remission" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo;

(j) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia korosho. Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS code 3923.21.00. Hatua hii

inalenga kuongeza thamani kwenye zao la korosho na kuvipa unafuu wa gharama viwanda vinavyochakata korosho hapa nchini. Aidha utaratibu wa "Duty Remission" utatumika katika kuagiza vifungashio hivyo;

(k) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye vifungashio vya kuhifadhia pamba. Vifungashio vitakavyohusika ni vile vinavyotambulika katika HS codes 3920.30.90; 6305.39.00 na 7217.90.00. Hatua hii inalenga kuvutia uwekezaji ili kuongeza thamani ya zao la pamba nchini;

(l) Kupunguza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwenye malighafi za kutengeneza taulo za watoto (Baby Diapers) zinazotumbulika kwa HS code 3506.91.00 Hot Melt Adhesive; PE film HS Code 3920.10.90, Empty bag for Baby Diapers HS Code 6305.33.00, Plastic cask HS Code 3926.90.90; na kiwango cha awali cha asilimia 10 kwenye Super Absorbent Polymer HS Code 3906.90.00, Wet strength paper HS Code 4803.00.00, Non-woven HS Code 5603.11.00, Polyethylene laminated Nonwovens HS Code 5903.90.00, Spandex HS Code 5402.44.00 na Dust free paper HS Code 4803.00.00. Aidha, msamaha huu utatolewa kwa utaratibu wa "Duty Remission". Hatua hii inatarajiwa kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji na kuongeza ajira;

(m) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwenye vifaa vinavyotumika katika kukata, kung'arisha na kuongeza thamani ya madini ya vito vinavyotambulika kwa HS Codes 6804.10.00; 7018.90.00; 7020.00.99; na kiwango cha awali cha asilimia 10 kwenye HS Codes 3606.90.00; 6813.20.00; 8202.20.00; 8202.99.00; 8203.20.00; 8205.10.00; 8423.89.90; 8513.10.90; na 9002.19.00. Hatua hii inalenga kuchochea uongezaji wa thamani kwenye madini. Utaratibu wa "Duty Remission" utatumika katika kuagiza vifaa hivyo;

(n) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwenye makaratasi (HS Code 4805.24.00 na 4805.25.00) yanayotumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio aina ya maboksi (corrugated boxes). Utaratibu wa "Duty Remission" utatumika. Lengo la hatua hii ni kuwapa unafuu wazalishaji wa vifungashio hivyo hapa nchini ili wananchi waweze kuvipata kwa bei nafuu;

(o) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwenye vifungashio vya mbegu vinavyotambulika katika HS codes 3923.29.00; 6305.10.00; 4819.40.00; 7310.29.90; 6305.33.00; 6305.20.00; 6304.91.90 na 7607.19.90. Utaratibu utakaotumika kutoa unafuu huo ni wa "duty remission". Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbegu hapa nchini;

(p) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye kahawa inayotambulika kwa Heading 09.01 inayoagizwa

kutoka nje ya nchi. Lengo la pendekezo hili ni kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha kilimo cha kahawa hapa nchini pamoja na kuongeza ajira katika sekta ya kilimo;

(q) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za kimarekani 125 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa. Bidhaa hizo ni "Flat -rolled products of iron or Non-alloy steel na Flat –rolled products of other alloy steel." Bidhaa hizi hutambulika katika HS Codes 7209.16.00; 7209.17.00; 7209.18.00; 7209.26.00; 7209.27.00; 7209.28.00; 7209.90.00; 7211.23.00; 7211.90.00; 7225.50.0 na 7226.92.00. Lengo la kuendelea kutoza viwango hivyo ni kulinda viwanda vya hapa nchini, kukuza ajira pamoja na kudhibiti udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo kutoka nje;

(r) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika kwa HS codes 7210.41.00; 7210.49.00; 7210.61.00; 7210.69.00; 7210.70.00 na 7210.90.00 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya ushuru wa asilimia 25 au dola za kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton), kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuwalinda wazalishaji wa bidhaa hizo hapa nchini kutokana na ushindani wa nje;

(s) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au dola za kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za mabati zinazotambulika katika HS Code 7212.60.00 badala ya ushuru wa asilimia 10 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (under-invoicing and under valuation), na kulinda ajira na mapato ya Serikali;

(t) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za kimarekani 250 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kwenye bidhaa za mabati kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa. Ushuru huo unahusu bidhaa zinazotambulika katika HS Code 7212.30.00; 7212.40.00 na 7212.50,00. Hatua hii ina lengo la kulinda viwanda vya ndani kutokana na udanganyifu wa thamani halisi ya bidhaa hizo zinapoingizwa kutoka nje (under-invoicing and under valuation), na kulinda ajira na mapato ya Serikali;

(u) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za kimarekani 250 badala ya kiwango cha asilimia 25 au dola za kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo (metric ton) kwenye bidhaa za chuma kwa mwaka mmoja kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye nondo kwa mwaka mmoja. (Reinforment bars and hallow profile). Hatua hii inahusu bidhaa zinazotambulika katika HS codes 7213.10.00; 7213.20.00; 7213.99.00; 7214.10.00; 7214.20.00; 7214.30.00; 7214.90.00; 7214.99.00; 7215.10.00; 7215.50.00; 7215.90.00; 7225.90.00;

7225.92.00; 7225.99.00; 7306.30.00; 7306.50.00; 7306.61.00; 7306.69.00; na 7306.90.00. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha nondo hapa nchini na kuongeza ajira;

(v) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za mboga mboga (horticultural products) zinazotambulika kwa HS codes 0603.11.00; 0603.12.00; 0603.13.00; 0603.14.00; 0603.15.00; 0603.19.00; 0604.20.00; 0604.90.00; 0701.90.00; 0702.00.00; 0703.10.00; 0703.20.00; 0703.90.00; 0706.10.00; 0706.90.00; 0710.10.00; 0710.21.00; 0710.22.00; 0710.30.00; 0714.10.00; 0714.20.00; 0804.30.00; 0804.40.00; 0804.50.00; 0805.10.00; 0805.40.00; 0805.50.00; 0806.10.00; 0807.11.00; 0807.20.00; 0808.10.00; 0808.30.00; 0910.11.00 na 0910.12.00. Lengo la hatua hii ni kulinda wakulima wa ndani ili kuendeleza kilimo cha matunda, mbogamboga na maua hapa nchini;

(w) Kutoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwenye bidhaa za fito za plastiki zijulikanazo kama PVC Profiles HS Code 3916.10.00; 3916.20.00; 3916.90.00 ambazo hutumika kwa ajili ya kutengenezea fremu za milango, madirisha n.k. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali;

(x) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwenye karatasi zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini ambazo zinazotambulika kwa HS codes 4804.11.00; 4804.21.00; 4804.29.00; 4804.31.00 na 4804.41.00. Lengo la hatua hii ni kuendelea kulinda viwanda vinavyozalisha karatasi hizo hapa nchini;

(y) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 35 kwenye ngano inayotambulika kwa HS Code 1001.99.10 na HS Code 1001.99.90 kwa utaratibu wa "Duty Remission" ambapo wanaonufaika na unafuu huu ni wenye viwanda vya kusaga ngano. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama kwa Viwanda vinavyozalisha unga wa ngano;

(z) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 kwa utaratibu wa duty remission kwenye bidhaa ijulikanayo kama "Printed Alluminium Barrier Laminates" (ABL) HS Code 3920.10.90 ambayo hutumika kama malighafi ya kutengeneza vifungashio vya dawa ya meno kwenye viwanda vya ndani. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa gharama kwa viwanda vinavyozalisha dawa ya meno nchini;

(aa) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 10 kwa utaratibu wa "Duty Remission" kwenye malighafi ya kutengeneza sabuni ijulikanayo kama RBD Palm Stearin (HS Code 1511.90.40) kwa viwanda vinavyotengeneza sabuni nchini. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vya kuzalisha sabuni nchini;

(bb) Kutoza kwa mwaka mmoja Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za kimarekani 1.35 kwa kilo moja ya viberiti (safety match boxes) vinavyotambuliwa kwenye HS code 3605.00.00 kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa badala ya asilimia 25 pekee. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha viberiti nchini dhidi ya bidhaa zenye ruzuku kutoka nje na hivyo kuwa na ushindani sawa katika soko;

(cc) Kutoza kwa mwaka mmoja Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za kimarekani 350 kwa kila tani moja ya ujazo (Metric ton) kutegemea kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye bidhaa za chuma za misumari zinazotambulika kwa HS code 7317.00.00 (nails, tacks, drawing pins, corrugated nails, and staples other than those of heading 83.05) badala ya asilimia 25 pekee. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo nchini.

(dd) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye soseji (sausages) na bidhaa za aina hiyo zinazotambulika kwa HS code 1601.00.00. Lengo ni kuendelea kulinda wajasiriamali wa ndani wanaozalisha bidhaa hizo;

(ee) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye chingamu (chewing gum HS Code 1704.10.00), biskuti (Heading 19.05) na peremende (HS code 1704.90.00) zinazoagizwa kutoka nje. Lengo ni kuendelea kulinda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa hizo na kukuza ajira;

(ff) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye chokoleti (chocolates) Heading 18.06 kwa mwaka mmoja. Lengo ni kulinda viwanda vya ndani na kukuza ajira;

(gg) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye nyanya zilizosindikwa (tomato sauces) zinazotambulika katika HS code 2103.20.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavyosindika nyanya nchini;

(hh) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 60 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye maji ya kunywa (mineral water) yanayotambulika katika HS code 2201.10.00. Hatua hii inalenga kulinda viwanda vinavozalisha maji ya kunywa nchini;

(ii) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 25 kwenye nyama zilizoainishwa katika SURA ya 2 katika Viwango vya pamoja vya ushuru wa forodha (meat and edible meat offal of Chapter 2) kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuendelea kulinda na kuchochea sekta ya ufugaji nchini;

(jj) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 25 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha awali cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula yanayotambulika kwa HS codes 1507.10.00, 1580.10.00, 1511.10.00, 1512.11.00,

1513.11.00, 1514.11.00, 1514.91.00, 1515.11.00, 1515.21.00 na 1515.30.00. Hatua hii inalenga kulinda na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira mashambani, viwandani pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

(kk) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 badala ya asilimia 10 au 25 kwa mwaka mmoja kwenye mafuta ya kula yaliyochakatwa kwa kiwango cha kati na mwisho (semi-refined and refined) yanayotambulika kwa HS codes 1507.90.00, 1508.90.00, 1509.90.00, 1510.00.00, 1511.90.10, 1511.90.30, 1511.90.90, 1512.19.00, 1512.29.00, 1513.19.00, 1513.29.00, 1514.19.00, 1514.99.00, 1515.19.00, 1515.20.00, 1515.50.00 na 1515.90.00. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta ya kula nchini, kuongeza ajira viwandani na mashambani pamoja na kulinda fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta hayo nje ya nchi;

(ll) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 0 kwenye Gypsum Powder HS code 2520.20.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda wazalishaji wa Gypsum Powder nchini;

(mm) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 35 kwa mwaka mmoja kutoka kiwango cha asilimia 100 kwenye sukari ya matumizi ya kawaida (consumption sugar) inayoagizwa kutoka nje ya nchi kwa vibali maalum kwa lengo la kuziba pengo (gap) la uzalishaji hapa nchini;

(nn) Kutoza kwa mwaka mmoja Ushuru wa Forodha wa asilimia 35 kwenye mitumba inayoingia kutoka nje badala ya asilimia 35 au dola za marekani 0.40 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi kikubwa kwa lengo la kutoa unafuu kwa watumiaji nchini;

(oo) Kutoa unafuu wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi, vipuri na mashine vinavyotumika katika kutengeneza viatu vya ngozi na nguo. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ukuaji wa sekta ya nguo na viatu vya ngozi nchini; na

(pp) Kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 0 kwa utaratibu wa "Duty Remission" kwenye malighafi ya kutengeneza leaf springs za magari inayotambulika kwa HS Code 7228.20.00. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vya kuzalisha bidhaa hiyo nchini.

(iii) Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikubaliana kufanya **marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Customs Management Act, 2004)** kwa kuweka thamani ya chini ya bidhaa isiyopaswa kutozwa ushuru wa Forodha kuwa Dola za Marekani 50.

(iv) Serikali inapendekeza kuliachia jukumu la uthaminishaji wa vitenge vinavyoingizwa nchini kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili uthaminishaji wa bidhaa hiyo uzingatie Kanuni zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria

ya Usimamizi wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2004). Sambamba na hatua hiyo, napendekeza utaratibu wa kuthaminisha vitenge kuwa dola za Marekani kati ya 0.55 hadi dola za Marekani 1 kwa mita ya kitenge cha Polyester na dola za Marekani kati ya 0.60 hadi dola za Marekani 1 kwa mita ya kitenge chenye pamba inapotokea thamani iliyowasilishwa (declared) kuwa chini ya kiwango hicho maalumu kwa kuzingatia taratibu za uthaminishaji wa bidhaa hizo.

(v) Kuondoa sharti la kuweka dhamana ya asilimia 15 ya ziada ya Ushuru wa Forodha inayopaswa kurejeshwa (refundable) kwenye sukari ya matumizi ya viwandani. Lengo la hatua hii ni kuwaongezea wazalishaji ukwasi (liquidity) kwa kutowazuilia mtaji wa uzalishaji (working capital). Hata hivyo, wazalishaji watakaobainika kufanya udanganyifu watarejeshewa sharti hili pamoja na kuchukuliwa hatua nyingine zilizopo kisheria.

Hatua hizi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kupunguza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 32,626.38.**

**E. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**

**63. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanyia Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi SURA 438 kama ifuatavyo:

(i) Kufuta kifungu cha 92A kwa lengo la kuziwezesha mahakama kukusanya mapato yanayotokana na adhabu na faini zinazolipwa mahakamani badala ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kama ilivyo kwa faini na adhabu kwa makosa mengine ambayo mahakama huyatolea maamuzi na hivyo kurahisisha ukusanywaji wa mapato hayo;

(ii) Kufuta kifungu cha 70(2) ili kumpa Mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kutekeleza matakwa ya Sheria husika na kurahisisha upunguzaji au uondoaji wa riba na adhabu ya madeni iwapo kutakuwa na sababu za msingi za kufanya hivyo; na

(iii) Kufanya marekebisho ya Kanuni Na. 15 ya ukokotoaji wa kodi za kimataifa (Transfer Pricing Regulations) kwa kufuta kifungu kinachoweka adhabu ya asilimia 100 kwa kushindwa kutekeleza matakwa ya Sheria. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea walipakodi adhabu kubwa ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kuvutia uwekezaji nchini.

**F. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290**

**64. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya Marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:

(i) Kubainisha mazingira ambayo Kampuni iliyolipa tozo ya huduma haitawajibika kulipa tozo ya uzalishaji. Marekebisho hayo yanalenga kutatua mgongano uliojitokeza kwenye kutafsiri kifungu husika; na

(ii) Kupunguza ada za matangazo kama ifuatavyo:

(a) Mabango yanayowaka kutoka shilingi 18,000 hadi shilingi 13,000;

(b) Mabango yasiyowaka kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 10,000;

(c) Matangazo ya ukutani kutoka shilingi 15,000 hadi shilingi 10,000;

(d) Matangazo ya kielectroniki kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 10,000;

(e) Matangazo kwenye magari kutoka shilingi 15,000 hadi shillingi 10,000 kwa watangazaji wanaotangaza bidhaa za watu wengine;

(f) Matangazo ya muda mfupi/promosheni kwa siku kutoka shilingi 55,000 hadi shilingi 50,000; na

(g) Kila mabango 100 ya promosheni ya kwanza au sehemu ya fungu la mabango 100 ya kwanza kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 50,000.

Ada zote hizi zinatozwa kwa futi za mraba. Kushushwa kwa ada hizi kutapunguza gharama za kutangaza biashara nchini na hatimaye kukuza ushindani kwenye biashara.

**G. Sheria ya Kodi ya Majengo, SURA 289**

**65. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya kodi ya majengo, SURA 289 ili ukusanyaji wa kodi ya majengo ufanyike kwa kutumia mfumo wa ununuzi na utumiaji wa umeme kupitia mashine za LUKU. Kila mita ya umeme ina uhusiano na mmiliki wa jengo au mtumiaji wa mita, na kwa kuwa Sheria ya Kodi ya Majengo inataka kodi hiyo ikusanywe kwa mmiliki au mtumiaji wa jengo, hivyo, napendekeza kodi ya majengo ya kiwango cha shilingi 1,000/= kwa mwezi kwenye nyumba za kawaida zenye mita moja na itakatwa kwenye ununuzi wa umeme (LUKU). Aidha, napendekeza kiwango cha shilingi 5,000/= kwa mwezi kwa kila ghorofa au apartment zenye mita moja na itakatwa kwenye ununuzi wa umeme (LUKU). Serikali itaweka utaratibu kwenye nyumba za kawaida na za ghorofa zinazochangia mita moja na zinazotumia mita zaidi ya moja.

**H. Sheria ya Ardhi, SURA 113**

**66. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi, SURA ya 113 na Kanuni zake za mwaka 2001 kwa kupunguza tozo ya mbele (premium) inayotozwa wakati wa umilikishaji wa ardhi kama ifuatavyo:

(i) Kupunguza tozo kutoka asilimia 2.5 hadi asilimia 0.5 kwa umiliki mpya wa ardhi; na

(ii) Kupunguza tozo kutoka asilimia 1 hadi asilimia 0.5 kwa urasimishaji.

Lengo la pendekezo hili ni kuhamasisha wamiliki wa ardhi kukamilisha taratibu za kupata hatimiliki na kufanikisha sehemu kubwa ya ardhi kuandikishwa na kupunguza migogoro. Hatua za kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 9,000.**

**I. Sheria ya Ushuru wa Stempu, SURA 189**

**67. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kuifanyia Marekebisho Sheria ya Ushuru wa Stempu kwa lengo la kuhuisha viwango vilivyopo sambamba na mfumuko wa bei kwa kuwa viwango hivyo ni vya muda mrefu tangu mwaka 2006. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Ushuru wa Stempu kutoka shilingi 500 hadi shilingi 2,000;

(ii) Ushuru wa Stempu kwenye Katiba za Makampuni kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 10,000;

(iii) Ushuru wa Stempu kwenye nyaraka za Ubia ambazo mtaji wake unazidi shilingi 100,000 lakini hauzidi shilingi 1,000,000 kutoka shilingi 2,000 hadi shilingi 5,000;

(iv) Ushuru wa Stempu kwenye nyaraka za Ubia ambazo mtaji wake unazidi shilingi 1,000,000 kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 10,000; na

(v) Ushuru wa Stempu kwenye nyaraka za kumaliza ubia kutoka shilingi 1,000 hadi 10,000.

Hatua za kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Stempu kwa ujumla wake zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,500.89.**

**J. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82**

**68. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi stadi kama ifuatavyo:

(i) Kupandisha kiwango cha chini cha idadi ya waajiriwa wanaostahili kulipiwa kodi kutoka 4 wa sasa hadi 10. Lengo la marekebisho haya ni kuwapunguzia mzigo wa kodi waajiri wenye idadi ndogo ya waajiriwa na kuchochea ukuaji wa uwekezaji nchini;

(ii) Kufuta tozo ya Elimu na mafunzo ya Ufundi Stadi kwa hospitali zinazomilikiwa na taasisi za kidini kwa kuwa taasisi hizi zimekuwa zikiisaidia sana Serikali kufikisha huduma za afya hata kwenye maeneo ambayo Serikali haijaweza kupeleka huduma kutokana na ufinyu wa Bajeti. Aidha, taasisi hizi zimekuwa na ushirikiano na Serikali kwa makubaliano maalum kwa baadhi ya maeneo ya kutoa huduma za afya. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa utoaji huduma za afya kwa vituo vya Afya; na

(iii) Kuanzisha utaratibu mahsusi wa ulipaji wa tozo kwa wachimbaji wadogo wa madini kuwa ni asilimia 0.4 ya thamani ya mauzo ya madini itakayolipwa na mchimbaji mdogo wa madini pindi atakapouza madini hayo kwenye masoko na vituo vya madini vinavyotambulika na Tume ya Taifa ya Madini.

**K. Sheria ya Michezo ya Kubatisha, SURA 41**

**69. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya mabadiliko ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kama ifuatavyo:

(i) Kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi (Gaming tax on Winnings) kutoka asilimia 20 hadi asilimia 15 kwenye Michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (Sports betting);

(ii) Kuongeza kiwango cha Kodi katika michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (sports betting) kwa mapato ghafi (Gross Gaming Revenue - GGR) kutoka asilimia 25 ya mauzo ghafi hadi asilimia 30 ya mauzo ghafi. Ongezeko la asilimia 5 litapelekwa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa ajili ya kuendeleza michezo nchini;

(iii) Kutoza kodi ya michezo ya kubahatisha kwa asilimia 10 ya mapato ghafi kwenye michezo ya kubahatisha inayoendeshwa kwa kompyuta (Virtual Games); na

(iv) Kutoza Kodi ya michezo ya kubahatisha kwa asilimia 10 ya mapato ghafi kwenye michezo ya kubahatisha iliyo chini ya majaribio.

Lengo la hatua hizi ni kuleta usawa wa utozaji kodi katika michezo ya kubahatisha. Hatua hizi za marekebisho ya michezo ya kubahatisha zinatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 14,925.38.**

**L. Sheria ya Ukaguzi wa Umma, SURA 418**

**70. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya Marekebisho kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma, SURA 418 kama ifuatavyo;

(i) Kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa na uwezo wa kisheria wa kukagua mashirika yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Makampuni ambayo Serikali ina umiliki wa hisa ili kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kukagua mashirika/makampuni hayo. Kwa sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakagua mashirika/makampuni hayo bila kuwa na nguvu za kisheria, hali inayoweza kuleta mgogoro wa kisheria; na

(ii) Kumwezesha Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuwasilisha Bungeni majibu kuhusu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye kikao kinachofuata cha Bunge baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa yake badala ya utaratibu wa sasa ambapo taarifa zote huwasilishwa kwa pamoja katika kikao kimoja cha Bunge.

**M. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134**

**71. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134 ili kuruhusu Serikali kudhamini kampuni au taasisi yoyote kukopa kiasi kisichozidi thamani ya Hisa za Serikali ya Tanzania kwenye mradi husika baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

**N. Sheria ya Usajili wa Magari, SURA 124**

**72. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili wa Magari SURA 124, kwa kupunguza ada ya usajili wa magari kwa namba binafsi kutoka shillingi 10,000,000 hadi shillingi 5,000,000 kila baada ya miaka mitatu. Lengo la hatua hii ni kuwezesha wamiliki wa magari kuchagua namba binafsi ya usajili wa gari kwa gharama nafuu na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa kuwa kiwango cha sasa hakina mwitikio mzuri.

Hatua hizi za marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Magari inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 270.**

O. Sheria ya Usalama Barabarani, SURA 168

**73. Mheshimiwa Spika,** vijana wengi wamejiajiri kwenye sekta ndogo ya kuendesha bajaji na pikipiki zikijulikana kama bodaboda. Hata hivyo, Vijana hawa hupata usumbufu mkubwa wa kulipa faini kutoka kwenye vipato vyao pale panapotokea uvunjaji wa Sheria ya Usalama Barabarani umefanywa na abiria wao. Hali hii imekuwa ikisababisha baadhi yao kushindwa kulipa faini na hivyo kuzitelekeza pikipiki zao kwenye vituo vya polisi. Mheshimiwa Rais alielekeza jeshi la Polisi kujikita kwenye kutoa elimu kuhusu usalama barabarani badala ya kuwekeza kwenye makosa na kugeuza faini kuwa chanzo cha mapato. Hivyo

basi, napendekeza kupunguza adhabu zinazotolewa chini ya Sheria ya Usalama Barabarani SURA 168 kwa makosa ya Pikipiki na Bajaji kutoka shilingi 30,000 za sasa hadi shilingi 10,000 kwa kosa moja. Lengo la hatua hii ni kuweka adhabu kwa kuzingatia uwezo wa kulipa. Aidha, adhabu kwa makosa mengine ya vyombo vya moto zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria zinaendelea kubaki kama ilivyo sasa.

**P. Sheria ya Raia wa Kigeni (Uratibu wa Ajira), Na. 1 ya mwaka 2015**

**74. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Raia wa Kigeni (Uratibu wa Ajira), Na. 1 ya 2015 kama ifuatavyo:

(i) Kuweka adhabu ya kiasi cha shilingi 500,000/= kwa kila mwezi kwa mwajiri aliyeajiri raia wa kigeni na kushindwa kuwasilisha ritani za kila mwezi zenye taarifa za raia wa kigeni aliowaajiri ikiwemo taarifa zao za mishahara kwa Kamishna wa Kazi.
Lengo la pendekezo hili ni kuhimiza uwajibikaji wa hiari;

(ii) Kuweka adhabu ya kifungo cha miezi 12 au faini ya shilingi millioni kumi (10) au vyote kwa mwajiri aliyeajiri raia wa kigeni na kushindwa kuwasilisha ritani za mwezi zenye taarifa za raia wa kigeni aliowaajiri ikiwemo taarifa zao za mishahara kwa Kamisha wa kazi. Lengo la pendekezo hili ni kuhimiza uwajibikaji wa hiari.

**Q. Marekebisho ya Ada na Tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa, Wakala, Mamlaka za Udhibiti na Idara zinazojitegemea**

**75. Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa, Wakala, Mamlaka za Udhibiti na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Aidha, marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021 na Matangazo ya Serikali (Government Notices). Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

**i. Wizara ya Kilimo**

Kuanzisha Tozo za Umwagiliaji kwa watumiaji wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha miradi hiyo kuwa endelevu na kuwezesha ujenzi wa miundombinu mipya. Viwango vinavyopendekezwa kama ifuatavyo:

(a) Kutoza ada ya shillingi 60,000 kwenye usajili wa vyama vya umwagiliaji; na

(b) Kutoza ada ya Huduma ya umwagiliaji ya asilimia 5 ya mavuno ya msimu kwa eneo la vyama vya umwagiliaji.

**ii. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kufanya marekebisho kwenye Kanuni za Jumuiya ya Kijamii, SURA 337 ili kuhuisha viwango vilivyokuwa vinatumika awali na kuanzisha tozo katika maeneo ambayo hayakuwa yanatozwa. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

(a) Kutoza tozo ya shilingi 100,000 ya uharibifu wa cheti cha Jumuiya ya Kijamii unaolazimu kupewa cheti kipya;

(b) Kutoza tozo ya shilingi 50,000 ya kukosea kwa jina kulikosababishwa na mwombaji atakayepaswa kupewa cheti kipya;

(c) Kutoza tozo ya shilingi 50,000 ya kubadili taarifa za anuani ya Posta au makao makuu ya Jumuiya;

(d) Kuongeza ada ya kuwasilisha maombi ya usajili wa Jumuiya ya Kijamii kutoka shilingi 10,000 hadi shilingi 50,000;

(e) Kuongeza ada ya mwaka kwa taasisi za kidini kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 100,000;

(f) Kuongeza ada ya mwaka kwa taasisi zisizo za kidini kutoka shilingi 40,000 hadi shilingi 50,000;

(g) Kuongeza ada ya mwaka kwa jumuiya za dini kutoka nje ya Nchi kutoka Dola za Marekani 30 hadi Dola za Marekani 60;

(h) Kuongeza ada ya mwaka kwa jumuiya zisizo za kidini kutoka nje ya Nchi kutoka Dola za Marekani 30 hadi Dola za Marekani 60;

(i) Kuongeza tozo ya maombi ya kubadili jina la jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(j) Kuongeza tozo ya maombi ya marekebisho ya katiba ya jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(k) Kuongeza tozo ya maombi ya nakala kwa ajili ya ushahidi katika vyombo vya utoaji haki kwa jumuiya kutoka shilingi 50,000/= hadi shilingi 100,000;

(l) Kuongeza tozo ya maombi ya nyaraka kwa jumuiya yenyewe kutoka shilingi 20,000 hadi shilingi 50,000;

(m) Kuongeza tozo ya upotevu wa cheti cha jumuiya kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(n) Kuongeza tozo ya upotevu wa cheti cha jumuiya kwa mara ya pili kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 200,000;

(o) Kuongeza ada ya upekuzi kwa jumuiya yenyewe kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000; na

(p) Kuongeza ada ya upekuzi kwa mwombaji mwingine kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 200,000.

**iii. Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

Kuanzisha kanuni za ada na tozo za Shirika la Viwango ya mwaka 2021 ambazo zinaanzisha ada na tozo mpya pamoja na kupitia ada na tozo zilizokuwa zinatozwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) hapo awali. Mapendekezo hayo yameainishwa katika **Kiambatisho Na. 5.**

**iv. Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

Kufanya marekebisho kwenye kanuni za ada na tozo za Hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu ya mwaka 2009 ili kupitia ada na tozo mbalimbali zilizoanzishwa kwa ajili ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu kama ilivyoambatishwa kwenye **Kiambatisho Na. 6.**

**R. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali.**

**76. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2021** na Matangazo ya Serikali (Government Notices).

**S. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya kufanya Biashara (Blueprint) kwa kurekebisha Ada na Tozo mbalimbali**

**77. Mheshimiwa Spika,** napendekeza kufuta au kupunguza ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea ili Kuondoa kero na urasimu kwa wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hasa katika kipindi hiki cha mlipuko wa janga la homa kali ya mapafu duniani. Hatua hizi ni sehemu ya mwendelezo wa utekelezaji wa **Mpango wa kuboresha Mfumo wa udhibiti wa Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment)**. Marekebisho hayo yatajumuisha:

**i. Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kupunguza ada ya leseni ya Biashara ya Utalii (TTBL) kwa Wakala za Safari kutoka Dola za Marekani 2000 hadi Dola za Marekani 500 ili kuhamasisha biashara ya utalii.

**ii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kutoza ada ya shilingi 40,000 kwenye kibali cha kupeleka nyama nje ya nchi kwa nyama zote bila kujali aina ya nyama badala ya ada ya shilingi 100 kwa kilo moja ya nyama ya ng'ombe na shilingi 50 kwa kilo moja ya nyama ya mbuzi na kondoo.

**iii. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi**

Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, SURA 263 kwa kupunguza kiwango cha mchango kwa Sekta Binafsi kutoka asilimia 1.0 inayotozwa sasa hadi asilimia 0.6 ya mapato ghafi ya wafanyakazi. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa kutosha kwa biashara zilizopo na uwekezaji mpya utakaofanyika nchini.

**iv. Tume ya nguvu za mionzi Tanzania**

Kufuta ada ya Utambuzi wa Mionzi ambayo inatozwa kwa kiwango cha asilimia 0.2 ya Malipwani kwenye mizigo ya vyakula inayosafirishwa kwenye nchi ambazo hazina sharti la uhitaji wa cheti cha utambuzi wa mionzi. Lengo la hatua hii ni kupunguza tozo kero na gharama za biashara na hivyo kuchochea mauzo ya bidhaa nje ya nchi sambamba na kupunguza utoroshaji wa mazao hayo kwenda nchi jirani kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi.

**v. Idara ya Uhamiaji**

(a) Kuondoa ada ya kibali cha kuingia nchini (VISA/PASS FEE) kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka nchi ya Msumbiji kwa ajili ya Mpango wa kubadilishana Wanafunzi wa Elimu ya Juu baina ya Tanzania na Msumbiji (TAMOSE). Lengo la pendekezo hili ni kutekeleza matakwa ya makubaliano kati ya nchi hiyo na Tanzania kuondoleana ada hizo ambapo Msumbiji imeshaanza kutekeleza makubaliano hayo; na

(b) Kuhusu Zanzibar, napendekeza kutekeleza utaratibu wa kuruhusu mapato yanayotokana na Kodi na tozo za Muungano kwenye mapato yanayotokana na tozo za VISA ili yaweze kutumika pale yalipokusanywa (Derivation Principle) kama ilivyo kwenye mapato mengine ya Muungano. Mapendekezo haya yanafanya suala hili liondolewe kwenye orodha ya changamoto za Muuungano. Mapato yatokanayo na tozo za VISA upande wa Zanzibar yaonekane kwenye bajeti upande wa Zanzibar, kuidhinishwa na kutumika Zanzibar.

**vi. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi ya Zimamoto na Uokoaji SURA 427 kwa kufuta na kupunguza ada na tozo zifuatazo:

(a) Kufuta tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye kilimo cha mbogamboga na maua;

(b) Kufuta tozo ya Cheti cha Umahiri (Certificate of Competence) cha Kinga na tahadhari ya moto inayotozwa kwenye Vituo vya Mafuta nchini;

(c) Kufuta tozo ya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto kwenye mashamba makubwa na nyumba za makazi yaliyopo ndani ya mashamba hayo yaliyokuwa yakitozwa kati ya shillingi 100,000 hadi 1,000,000;

(d) Kuongeza ukubwa wa eneo lisilopaswa kutozwa tozo ya Ukaguzi wa Kinga na tahadhari ya moto linatumika kwa maonyesho ya biashara kuanzia mita za mraba zisizopungua 2000 hadi mita za mraba 10,000; na

(e) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa bweni kwa shule zisizopaswa kutozwa tozo ya Ukaguzi wa Kinga na tahadhari za moto kutoka wanafunzi wasiozidi 100 hadi wanafunzi 200.

**vii. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

Kufanya marekebisho kwenye kanuni ya ada na tozo Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2019 kama ifuatavyo:

(a) Kupunguza ada ya kuharibu dawa zilizoisha muda wa matumizi yake kutoka shilingi 1,000,000 hadi shilingi 100,000; na

(b) Kupunguza ada ya kila mwaka ya mazingira kutoka shilingi 200,000 hadi shilingi 100,000.

**viii. Bodi ya Nyama Tanzania**

Kutoza ada ya shilingi 70,000 kwa Cheti cha Kukubaliwa kupeleka nyama nje ya Nchi badala ya kiwango cha asilimia 1 ya malipwani.

**ix. Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**

Kupunguza tozo ya ukaguzi wa Umeme kwa kipimo kimoja (electrical inspection, electrical insulation test and general inspection) kutoka shilingi 590,000 hadi 150,000. Tozo hii inatozwa kabla ya kuanza biashara ya mafuta. Pendekezo hili linatarajia kuchochea mazingira wezeshi ya biashara nchini hususan katika maeneo ya vijijini.

**x. Utoaji Leseni za Bima kwa Makampuni**

Napendekeza kubadili utaratibu wa sasa wa makampuni ya bima kulazimika kuomba leseni upya kila mwaka na badala yake makampuni yanayofanya vizuri yawe na leseni ya kudumu, na makampuni yalioko kwenye hali ya uangalizi yapewe leseni na miaka mitatu huku yakiwa kwenye uangalizi na yakiimarika na kufanya vizuri yaingie kwenye leseni za kudumu. Taratibu za ufuatiliaji na malipo ya kila mwaka yaendelee kama ilivyo sasa. Lengo ni kupunguza ukiritimba.

**xi. Uboreshaji wa Mazingira ya Ufanyaji Biashara**

Sambamba na hatua za kikodi zilizolenga kupunguza gharama ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara, Serikali itakamilisha mfumo wa kimtandao wa kuwa na dirisha moja la upatikanaji wa vibali mbalimbali katika Idara zote zinazohusika na usajili na vibali ili kuwapunguzia wawekezaji mizunguko ya kutembea ofisi zaidi ya moja kuhangaika nenda rudi kutafuta vibali vinavyotolewana ofisi zaidi ya moja. Lengo la hatua hii nikurahisisha mazingira ya kufanya biashara kama ilivyobainishwa kwenye Blueprint.

**T. Maeneo Mahususi**

**i. Barabara za Mijini na Vijijini**

**78. Mheshimiwa Spika,** hali ya barabara vijijini hairidhishi ambapo bado vipo vijiji ambavyo havina barabara kabisa. Barabara nyingi zinazosimamiwa na TARURA zina hali mbaya. Kwa sasa mtandao wa barabara zilizo chini ya TARURA una urefu usiopungua kilomita 108,946.2 ambazo zinaunganisha maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini. Hadi Desemba 2020, mtandao wa barabara zilizo chini ya TARURA wenye kiwango cha lami ulifikia kilometa 2,250.69, sawa na asilimia 2.1 tu, changarawe kilometa 27,809.26 (asilimia 25.6) na udongo kilometa 78,886.25 (asilimia 72.4).

**79. Mheshimiwa Spika,** hali hii ya barabara ina madhara makubwa sana kwa jamii yetu kwani baadhi ya akina mama wajawazito wanapoteza maisha kwa kuchelewa kufika kwenye vituo vya afya. Aidha, wapo wengine ambao wanajifungulia njiani kutokana na kuchelewa kufika kwenye vituo vya afya. Vilevile, wapo baadhi ya wanafunzi wanaosombwa na maji na kufariki kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara, hususan katika maeneo ya vijijini. Kadhalika, bado kuna changamoto ya usafirishaji wa mazao na bidhaa kutoka au kwenda barabara kuu katika baadhi ya maeneo. Serikali imeona ipo haja ya kutafuta vyanzo vipya vya mapato kuongezea katika mgawo wa sasa kupitia Mfuko wa Barabara ili kufanikisha ugharamiaji wa mtandao wa barabara hizo.

**ii. Upatikanaji wa Maji Safi na Salama Mijini na Vijijini**

**80. Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini bado hairidhishi. Maji hayana mbadala, maji ni uhai, maji ni maisha kwa viumbe hai vyote. Bado vipo vijiji ambavyo havina kisima hata kimoja cha maji safi na salama na badala yake hutumia maji ya mapalio, maji ya madimbwi, maji ya mito wanayochangia na wanyama. Tanzania ina vyanzo vikubwa na vya uhakika vya maji ikiwa ni pamoja na Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Ziwa Chala, Mto Kiwira, Ruvu, Rufiji na Ruvuma pamoja na mingine. Aidha, kuna uwezekano wa kutumia mabwawa makubwa kama ya Kidunda, Ndembela na Farkwa kama yangekamilika lakini utekelezaji wake haujaanza pamoja na fidia kutolewa na Serikali kutokana na uhaba wa fedha. Ipo miradi mingi katika mikoa ya Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora, Tanga na Simiyu inayotakiwa kutekelezwa katika mwaka 2021/22, lakini haikuwa katika bajeti. Mikoa mingine ambayo sikuitaja hapa iko kwenye bajeti ya Wizara husika.

**81. Mheshimiwa Spika,** hali ya ukosefu wa maji safi na salama ina madhara makubwa sana kwa jamii yetu. Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa inampa nafuu mwanamke katika kufanya shughuli zake za kiuchumi, lengo likiwa ni kumtua mama ndoo kichwani na kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakumba akina mama na mabinti katika harakati za kutafuta maji. Aidha, kuna baadhi ya wanafunzi wanakosa masomo na kuharibu maisha yao kutokana na uhaba wa maji katika maeneo yao. Hivyo, Serikali imeona ipo haja ya kuongeza fedha za kugharamia miradi ya maji kwa kubuni vyanzo mbadala vya mapato kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji hususan katika maeneo ambayo yana uhaba mkubwa wa maji.

**iii. Afya na Bima ya Afya kwa Wote**

**82. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Afya ni sekta muhimu katika ustawi wa jamii yetu na ni moja ya mahitaji muhimu sana katika maisha ya sasa ya mwanadamu. Serikali ya CCM imefanya kazi kubwa sana katika sekta hii, ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na mabadiliko ya hali za kiafya kwenye kizazi cha leo. Aidha, wananchi katika maeneo mbalimbali wametumia nguvu kubwa katika kutafuta ufumbuzi wa masuala ya upatikanaji wa huduma za afya kwa kujenga maboma karibu na maeneo yao. Majengo yaliojengwa kwa nguvu za wananchi yamekaa kwa muda mrefu, kati ya miaka mitano (5) hadi 15. Hadi kufikia Juni 2021, kuna jumla ya maboma 8,004 ya zahanati ambayo yapo katika mikoa mbalimbali nchini na yapo katika hatua mbalimbali za kukamilishwa. Vilevile, yapo maboma kwenye ngazi ya vituo vya afya zaidi ya 1,500 ambayo yametumia nguvu ya wananchi na yanahitaji kukamilishwa. Serikali itaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma hayo pamoja na kuajiri wataalamu wa afya na kuimarisha upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba.

**83. Mheshimiwa Spika,** kuna mradi mkubwa wa bima kwa wote (Universal Health Care) unaolenga kuwafikia watanzania wote. Tanzania ina jumla ya kaya

milioni 12.827, ambapo asilimia 20 ya kaya hizo inakadiriwa kuwa ni kaya zisizokuwa na uwezo. Katika kufanikisha utekelezaji wa dhana ya bima ya afya kwa wananchi wote, Serikali itahitaji zaidi ya shilingi bilioni 149 katika mwaka wa kwanza kwa ajili ya kaya zisizo na uwezo. Kiasi hicho cha fedha kitaendelea kuongezwa kila mwaka ili ifikapo mwaka 2034/35, wananchi wote wawe wamefikiwa na bima ya afya. Serikali imeendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ambapo vituo vya kutolea huduma za afya kwa ngazi mbalimbali vimeendelea kujengwa ili bima ya Afya iweze kutumika na kuwanufaisha wananchi wote.

**iv. Elimu**

**84. Mheshimiwa Spika,** kuhusu sekta ya elimu kuna kazi kubwa bado iko mbele yetu. Bado kuna shule ambazo zina wanafunzi wengi kuliko idadi ya madarasa na zipo zinazogawa mikondo ili wanafunzi wengine wasome asubuhi na wengine wasome mchana. Hali hii inapunguza muda wa wanafunzi kusoma. Zipo shule ambazo kwenye darasa moja wanaweka uzio wa ubao kutenganisha ili chumba kimoja wasome wanafunzi wa madaraja mawili. Aidha, zipo shule ambazo miundombinu yake imechakaa sana kiasi cha kutishia usalama wa watoto na walimu wetu. Yapo pia madarasa yaliyoezekwa kwa nyasi na yana sakafu ya vumbi. Kadhalika, mwaka ujao utakuwa wa kwanza wa kupokea wanafunzi kidato cha kwanza waliodahiliwa darasa la kwanza kwa mpango wa elimumsingi bila ada. Jambo hili lisipoangaliwa mapema litakuja kusababisha wanafunzi kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza na kukosa pa kwenda hadi miundombinu ijengwe kwa zimamoto. Kwa hatua ya maendeleo nchi yetu iliyofikia katika sekta mbalimbali, hali hii haipendezi na haitakiwi kuendelea. Kujenga miundombinu ya shule zetu kwa kusubiri irushwe kwenye mitandao ya kijamii ndio tuone inatutia aibu, au kusubiri watoto wakose pa kwenda au wakose pa kukaa ndipo tukimbizane na kufukuzana, ni ishara ya kutopanga vizuri. Hili tusingependa liendelee kuwepo.

**85. Mheshimiwa Spika,** kila mwaka kuna wanafunzi kati ya asilimia 15 - 20 wanatoka kwenye mfumo wa elimu kwa kutoendelea na kidato cha kwanza kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupata ujauzito, utoro na hali ngumu ya maisha. Ukosefu wa mpango wa kugharamia mahitaji ya sekta ya elimu ndiyo chanzo cha tatizo hili.

**86. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa elimu ya juu, zaidi ya wanafunzi 11,000 wenye sifa za kujiunga na vyuo vikuu ambao tayari walishapata udahili katika vyuo mbalimbali walikosa mikopo. Naongelea mkopo, sio fedha ya bure, bali ni mkopo ambao ataurejesha. Katika jamii nyingi za kitanzania, mtoto akikosa mkopo huku akiwaona wenzake wanaendelea, inamfadhaisha sana. Ni mfadhaiko kwake na familia nzima. Kwa hatua ya maendeleo ambayo nchi yetu imepata katika sekta mbalimbali hali hii haipendezi na haitakiwi kuendelea. Serikali inakusudia kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa inaongeza bajeti ya mikopo ya elimu ya juu ili kuwanufaisha vijana wote wenye sifa za kupata mkopo.

**v. Miradi ya Kielelezo ya Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Mwalimu Nyerere na Reli ya Kisasa (SGR)**

**87. Mheshimiwa Spika,** Miradi ya bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere na Reli ya Kisasa (SGR) sio tu ni miradi ya kielelezo bali ni miradi "mama" kwa kila mtanzania. Ni miradi inayoashiria uhuru wa nchi yetu, ni miradi inayoashiria kujitegemea kwa nchi yetu, ni miradi inayoashiria heshima ya mtanzania na inajengwa na mtanzania. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais, kutokamilika kwa miradi hii itakuwa laana kwa Taifa letu. Hatutajengewa miradi hii na mtu yeyote, tutawaenzi wabeba maono wa miradi hii kwa kujenga na kuikamilisha. Mwalimu Nyerere alibeba maono ya miradi hii, Rais Magufuli alianzisha miradi hii, Rais Samia anakwenda kuijenga miradi hii. Niwahakikishie watanzania hapatakuwepo GOFU hata la Mradi mmoja wala kusimama kwa mradi unaotekelezwa hata kwa mwezi mmoja.

**88. Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na maeneo mahsusi hayo niliyotangulia kuyasema, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria zifuatazo:

**a. Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220**

Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza Ushuru wa barabara kwa shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli;

(ii) Kufanya marekebisho ya kifungu cha 4 A(a) cha sheria ili kuelekeza fedha zitakazokusanywa kutokana na ongezeko la ushuru wa barabara na mafuta la shilingi 100 kwa aina zote za mafuta ziwe kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini kupitia TARURA.

Hatua hii ya marekebisho ya Sheria inatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 322,158.20.**

**b. Sheria ya Petroli, SURA 392**

Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Petroli ili kuongeza tozo ya Mafuta ya Taa kutoka shillingi 150 hadi shillingi 250. Lengo la hatua hii ni kupunguza uchakachuaji wa mafuta kufuatia ongezeko la ushuru wa mafuta kwenye dizeli na petroli.

**c. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306**

Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki kama ifuatavyo:

(i) Kutoza tozo ya shillingi 10 hadi shilingi 10,000 katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa. Kiasi cha tozo kinatofautiana kulingana na thamani ya muamala wa fedha unaotumwa au kutolewa. Pendekezo hili litaongeza mapato ya Serikali kiasi cha shillingi **milioni 1,254,406.14**; na

(ii) Kutoza kiasi cha shilingi 10 hadi shilingi 200 kwa siku kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio kwa watumiaji. Pendekezo hili litapelekea kuongeza mapato ya Serikali kiasi cha shillingi **milioni 396,306.0.**

**d. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147**

Kutokana na vinywaji vikali kuwa na kiwango kikubwa cha kilevi, napendekeza kuongeza ushuru wa bidhaa kwa asilimia 30 ili kuwa na uwiano wa viwango vya kodi kati ya Vinywaji kali na Bia. Hatua hii inatarajia **kuiongezea** mapato Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 60,769.35**.

Utekelezaji wa hatua hizi nne kwa pamoja unatarajiwa **kuongeza** mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 2,033,639.66.**

**U. Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi**

**89. Mheshimiwa Spika,** hatua hizi za kikodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe **1 Julai, 2021,** isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo. Aidha, Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa **Sheria ya Fedha ya mwaka 2021** na
Matangazo ya Serikali (Government Notices).

**V. Njia Mbadala za Kutekeleza Miradi Mikubwa**

**90. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2020 nchi yetu ilifanikiwa kuingia katika kundi la nchi zenye kipato cha kati cha chini (Lower MiddleIncome Country). Kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kati kunaifanya nchi yetu kutakiwa kujiendesha kiuchumi bila kutegemea kwa kiwango kikubwa misaada na mikopo yenye masharti nafuu ambayo, hupewa nchi zenye kipato cha chini. Hivyo, ni lazima Serikali iboreshe mbinu inazotumia na kubuni mbinu mpya za kupata mapato. Katika kutekeleza hatua hii, Serikali imeanza kufanya uchambuzi wa vyanzo mbadala vya rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama vile **ufadhili mchanganyiko (Blended Finance)**. Wafadhili wanaotoa aina hii ya ufadhili hutoa fursa kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania, kurekebisha au kujumuisha (restructuring or consolidation) deni lake kwa makubaliano ya kutumia sehemu ya malipo ya deni katika uhifadhi wa mazingira au kuimarisha sekta za kiuchumi na kijamii.

**91. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2021/22, Serikali inadhamiria kukamilisha mchakato wa Tathmini na Ukadiriaji wa Kukopesheka kwa Nchi (Sovereign Credit

Rating). Hatua hii inalenga kutuwezesha kujua nafasi yetu katika masoko ya fedha ya kimataifa na jinsi wakopeshaji wanavyotuona hasa katika uwezo wa kusimamia uchumi na kulipa madeni yetu. Hatua hiyo itatuwezesha pia kuongeza wigo wa wakopeshaji ambao wako tayari kutukopesha, hususan katika Masoko ya Mitaji ya Kimataifa (International Capital Markets). Serikali itaanza mara moja mchakato wa wazi wa kutekeleza na kukamilisha kazi ya Sovereign Credit Rating ndani ya mwaka 2021/22.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kupanua wigo wa vyanzo vya rasilimali fedha, Serikali itaangalia uwezekano wa kutumia Hati Fungani zitakazotolewa na Halmashauri za Manispaa na Majiji kama njia mbadala ya kupata rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya kimkakati. Hatua hii itapunguza mzigo kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hasa kwa Halmashauri zenye miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu na kuwa na uhakika wa uwezo wa miradi hii kujiendesha kwa faida (bankable projects). Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (United National Capital Development Fund - UNCDF) na Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji (Capital Markets and Securities Authority - CMSA) imeanza mchakato wa kuhakikisha kwamba Halmashauri, Manispaa na Majiji yatakayokidhi vigezo na masharti ya matumizi ya Hati Fungani hizi yanaanza kutumia utaratibu huu.

**93. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaona umuhimu wa kutumia Masoko ya Hati Fungani za Kimataifa maarufu kama "Eurobonds" ikiwa ni chanzo cha kuaminika na thabiti cha kugharamia miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Mkakati wa Deni la Muda wa Kati (Medium Term Debt Strategy - MTDS). Hatua hii inakwenda sambamba na hatua nyingine inayopendekezwa katika hotuba hii ya kufungua soko la dhamana za Serikali ili kuruhusu wawekezaji wa nje ya Tanzania na Afrika Mashariki kununua hati fungani zetu ili kuongeza ukwasi katika soko la ndani.

**94. Mheshimiwa Spika,** Soko la Eurobond ulimwenguni linakadiriwa kuwa na zaidi ya dola za Marekani trilioni 30 zilizotolewa kwa nchi zinazotafuta rasilimali fedha kwa njia ya mikopo kutoka kwenye masoko ya kimataifa yenye ukwasi mkubwa ili kugharamia miradi ya maendeleo. Njia hii pia hutumiwa na mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika wanapotafuta fedha kwa ajili ya kufadhili miradi yao kote duniani. Aidha, nchi mbalimbali za kusini mwa Jangwa la Sahara zinazofanya vizuri kiuchumi zimekuwa zikitumia Soko la eurobond kama chanzo thabiti na chenye masharti rafiki katika kugharamia utekelezaji wa miradi yao ya maendeleo. Tanzania itahitaji kufanyiwa tathmini ya kukopesheka ili kufikia masoko ya mitaji ya kimataifa kupitia eurobonds. Hivyo, zoezi la kukadiria au kutathmini kukopesheka kwa Tanzania ni hatua isiyoepukika.

**95. Mheshimiwa Spika,** tangu mwaka 2010 tulipopitisha Sheria ya PPP hatujapata mafanikio ya kujivunia katika eneo hili pamoja na faida kubwa na nyingi ambazo Taifa linaweza kupata kupitia mfumo wa PPP hasa katika miradi mikubwa inayohitaji fedha nyingi na utaalamu kutoka sekta binafsi. Utekelezaji wa miradi ya PPP hupunguza mzigo kwenye deni la Serikali na hata katika Mfuko

Mkuu wa Hazina ya Serikali na hutoa nafuu ya kibajeti (Fiscal Space) kwa kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu mengine ambayo hayawezi kugharamiwa na sekta binafsi. Hivyo, ni muhimu kutumia PPP kwenye miradi mbalimbali inayokidhi Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103.

**96. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia manufaa ya PPP, Serikali itaongeza kasi ya kushughulikia miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi ikiwa ni pamoja na: Ujenzi wa viwanda vya dawa muhimu na vifaa tiba; ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Kituo Changamani cha Biashara katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Aidha, wananchi na wawekezaji wengine wanaalikwa kubainisha maeneo ambayo wanaweza kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya PPP kulingana na uwezo wao wa mitaji na utaalamu.

**V. SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2021/22**

**97. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia shabaha, malengo pamoja na sera za bajeti kwa mwaka 2021/22, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 36.33 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika. Mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 26.03, sawa na asilimia 71.7 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 22.18, sawa na asilimia 13.5 ya Pato la Taifa. Aidha, Serikali inalenga kukusanya mapato yasiyo ya kodi ya shilingi trilioni 2.99 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 863.9.

**98. Mheshimiwa Spika**, Washirika wa Maendeleo wanatarajia kuchangia misaada na mikopo nafuu yenye jumla ya shilingi trilioni 2.96, sawa na asilimia 8.1 ya bajeti yote. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za miradi ya maendeleo shilingi trilioni 2.67 na Mifuko ya Pamoja ya Kisekta shilingi bilioni 282.3. Napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa kuendelea kutoa fedha za misaada na mikopo nafuu ili kufanikisha miradi na programu mbalimbali za maendeleo zitakazotekelezwa katika bajeti ya mwaka 2021/22.

**99. Mheshimiwa Spika,** kipekee ningependa kuwatambua Washirika wetu wa Maendeleo kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Italia, Korea ya Kusini, Japan,Ufaransa, Ujerumani, Norway, Poland, Ubelgiji, Uholanzi, Uswisi, Uingereza, Sweden na Marekani. Vilevile, kuna Mashirika ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi katika Afrika, Mfuko wa Abu Dhabi, Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa kimataifa wa kusaidia mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi, kifua kikuu na malaria, Umoja wa Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Umoja wa mataifa na mashirika yote yaliyopo chini yake, Mfuko wa OPEC kwa Maendeleo ya Kimataifa, Mfuko wa Mazingira, pamoja na Shirikisho la GAVI. Ninapenda pia kuyatambua Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya ndani na nje

pamoja na mashirika ya ufadhili - philanthropies kwa misaada yao kwenye sekta mbalimbali.

**100. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 7.34 kutoka soko la ndani na nje kwa masharti ya kibiashara. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 4.99 ni mikopo ya ndani ambayo inajumuisha shilingi trilioni 3.15 kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 1.84 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, shilingi trilioni 2.35 zinatarajiwa kukopwa kutoka soko la nje kwa lengo la kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**101. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2021/22, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 36.33 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 23.0 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 13.33 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi trilioni 10.66 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali, shilingi trilioni 8.15 kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 4.19 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 200.0 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya watumishi, wazabuni na watoa huduma.

**102. Mheshimiwa Spika**, jumla ya shilingi trilioni 13.33 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 37 ya bajeti yote. Kati ya kiasi hicho, fedha za ndani ni shilingi trilioni 10.37 na fedha za nje shilingi trilioni 2.96. Aidha, fedha za maendeleo zinajumuisha, shilingi trilioni 1.19 kwa ajili ya miradi ya reli ikiwemo ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa; shilingi trilioni 2.08 kwa ajili ya miradi ya barabara, ujenzi wa madaraja, na viwanja vya ndege; shilingi trilioni 2.34 kwa ajili ya miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ikiwemo mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere; shilingi bilioni 589.4 kwa ajili ya miradi ya maji mijini na vijijini; shilingi bilioni 233.3 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi; shilingi bilioni 500 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; shilingi bilioni 215.6 kwa ajili ya maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022; na shilingi bilioni 312.1 kwa ajili ya elimumsingi bila ada. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 400.0 kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya miradi ya maendeleo.

**103. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza, sura ya bajeti kwa mwaka 2021/22 ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2:** Mfumo wa Bajeti ya Mwaka 2021/22

| | | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|---|
| | Mapato | | 2021/22 |
| A. | Mapato ya Ndani-Serikali Kuu | | 25,168,718 |
| | (i) Mapato ya Kodi (TRA) | 22,178,721 | |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | 2,989,998 | |
| B. | Mapato ya Halmashauri | | 863,858 |
| C. | Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo | | 2,955,923 |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | 0 | |
| | (ii)Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | 2,673,617 | |
| | (iii)Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | 282,306 | |
| D. | Mikopo ya Ndani na Nje | | 7,341,240 |
| | (i) Mikopo ya Nje | 2,352,107 | |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | 1,838,796 | |
| | (iii)Mikopo ya Ndani- Rollover | 3,150,337 | |
| | JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D) | | 36,329,740 |
| | | | |
| | Matumizi | | |
| E. | Matumizi ya Kawaida | | 23,002,951 |
| | | | |
| | o/w (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | | 10,663,278 |
| | -Malipo ya Riba Ndani | 1,561,637 | |
| | -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | 3,150,337 | |
| | -Malipo ya Mtaji Nje | 3,015,070 | |
| | - Malipo ya Riba Nje | 1,151,376 | |
| | - Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | 1,247,149 | |
| | -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | 537,710 | |
| | (ii) Mishahara | | 8,150,509 |
| | (iii)Matumizi Mengineyo (OC) | | 4,189,164 |
| | - Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | 200,000 | |
| | - Matumizi ya Halmashauri (own source) | 532,768 | |
| | - Matumizi mengineyo | 3,456,396 | |
| F. | Matumizi ya Maendeleo | | 13,326,788 |
| | (i) Fedha za Ndani | | 10,370,865 |
| | o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | 400,000 | |
| | o/w Ugharamiaji wa SGR | 898,005 | |
| | o/w Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere | 1,440,000 | |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri | 331,090 | |
| | o/w Miradi mingine | 7,301,770 | |
| | (ii) Fedha za Nje | | 2,955,923 |
| | JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F) | | 36,329,740 |
| | NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA) | | 1.8% |

## VI. HITIMISHO

**104. Mheshimiwa Spika,** ninapoelekea mwisho wa hotuba hii, napenda kumshukuru kwa dhati "MAMA YETU" kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa wabunge na Watanzania wote kwamba, nitaibeba dhamana hii kwa uadilifu, weledi na uwezo wangu wote na ninamuomba Mwenyezi Mungu anijalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza majukumu hayo. Naomba nielezee masuala machache muhimu kabla ya kuhitimisha hotuba hii.

**105. Mheshimiwa Spika,** kwanza natoa pongezi kwa "MAMA YETU" kwa matumaini makubwa aliyowapa watanzania. "MAMA YETU" ameonesha ni Kiongozi Makini, ni Kiongozi Shupavu, ni Kiongozi Mchapa Kazi, ni Kiongozi Mwadilifu, ni Kiongozi Msikivu, ni Kiongozi aliye na dira thabiti na maono ya kuendelea kuiletea nchi yetu maendeleo makubwa. **Ameweka wazi kuwa hataki kodi ya dhuluma, hataki kuendesha Serikali kwa mapato ya dhuluma, ameweka wazi kusimama imara kwenye masuala ya mapato na matumizi ya Serikali, ameweka wazi kuwa atakuwa imara kwenye vita dhidi ya rushwa.**

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa kauli hizo "MAMA YETU" ameonesha kuwa, kukaa kwake katika nafasi mbalimbali katika Serikali za awamu mbalimbali SMT na SMZ kumemfanya awe kiongozi aliyeandaliwa na KUIVA na aliye tayari kuiongoza nchi kwa ufanisi mkubwa. Itakumbukwa mbali na nafasi zingine nyingi alizoshika katika miaka yake takribani ishirini Serikalini, MAMA YETU amekuwa Waziri katika Awamu ya Nne na amekuwa Makamu wa Rais katika Awamu ya Tano. "Kuna style za uongozi amejifunza".

**107. Mheshimiwa Spika** "kuna style za uongozi amejifunza" kupitia Awamu hizo alikopewa nafasi kuhudumu katika nafasi mbalimbali. "MAMA YETU" alikuwa Waziri katika awamu ya nne iliyokuwa ikiongozwa na Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mheshimiwa Kikwete alikuwa Mzalendo wa kweli, alikuwa na maono (Visionary Leader), alikuwa mwalimu, alikuwa mzazi, alikuwa mlezi na kiongozi, alikuwa rahim sana, alikuwa mvumilivu sana aliyeamini kwenye **Mifumo, Taasisi na Utendaji wa Kitaasisi**. Hii naweza kuifananisha kama **"Refa kwenye mchezo"** wa mpira wa miguu, ambaye anachezesha mechi zake akiwa na **"kadi ya njano tu", kadi nyekundu** anaiacha nyumbani. Ukicheza rafu mara ya kwanza anakuonya kwa kukuelekeza, ukicheza rafu mara ya pili anakupa kadi ya njano, ukikosea anakupa kadi ya njano tena na alipotakiwa kutoa kadi nyekundu mara nyingi alionya kwa mdomo, kwa kuwa kadi nyekundu alikuwa anaiacha nyumbani. Rais Kikwete aliamini sana kwenye **Mifumo na Utendaji wa Kitaasisi**. Kwa mtazamo wangu, jinsi "MAMA YETU" alivyoanza ni dhahiri amepata funzo kwenye awamu hiyo ikiwemo **funzo la Uzalendo, maono na kuamini kwenye** "**Mifumo, Taasisi na Utendaji wa Kitaasisi"**, na hapa naweza kusema ameichukua "**kadi ya njano"**, anayo na ameanza kutumia kama mnavyoona.

**108. Mheshimiwa Spika,** "MAMA YETU" alikuwa Makamu wa Rais katika awamu ya tano iliyokuwa ikiongozwa na Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Rais Magufuli alikuwa mzalendo wa kweli, alikuwa na Maono (Visionary Leader), alijitoa kwa nguvu zote (Dedicated), alikuwa na uthubutu sana, mtu wa vitendo sana na muumini wa **matokeo** na kuchukua hatua za papo kwa papo. Kama **refa wa mchezo** wa mpira wa miguu, alikuwa akienda kuchezesha Mechi zake akiwa na **"kadi nyekundu tu", kadi ya njano** alikuwa anaiacha nyumbani. Ukicheza rafu mara ya kwanza tu anakupa **kadi nyekundu**, wakati mwingine hata asipoiona rafu yeye, mchezaji au shabiki akisema ameona rafu anakupa kadi Nyekundu **(no nonsense)**, hata mimi mwenyewe niliwahi kutembelewa na **kadi nyekundu** nikakosa michezo kadhaa. Hayati Dkt. Magufuli aliamini kwenye

nidhamu ya hali ya juu ya mchezo. "MAMA YETU" alikuwa **Line one** na Mheshimiwa Majaliwa akiwa **Line two**. Hivyo, "MAMA YETU" amepata mafunzo kwenye awamu hiyo ya **Uzalendo**, **Uthubutu**, **mtu wa vitendo** kuamini **kwenye matokeo na nidhamu kazini na ameichukua "kadi nyekundu"**.

**109. Mheshimiwa Spika** "kuna style za uongozi amejifunza". "MAMA YETU" anazo kadi zote**, "kadi ya njano" na "kadi nyekundu".** MAMA YETU" **ni Mzalendo wa kweli**, **ni Mwadilifu sana**, **ana Uthubutu, ana Maono**, **anaamini kwenye** "**Mifumo, Taasisi na Utendaji wa Kitaasisi"**, **hataki maneno anataka vitendo**. Nitoe rai kwa watumishi wote wa umma na watanzania kwa ujumla tuchape kazi kwa bidii, kwa uadilifu na uzalendo mkubwa. Kwa watumishi wa umma tusimamie matumizi ya fedha za walipa kodi kwa uadilifu mkubwa na kwa watanzania tulipe kodi bila shuruti. Tabia moja ya refa asiyependa kuonea upande wowote, huwa hawezi kupendelea upande wowote. Kwenye michezo ya mieleka huwa mnapewa tahadhari ya don't try this at home, kwenye maslahi ya nchi wanaotaka kumjaribu MAMA YETU nawaonya **"Don't try at all". Tujiepushe na kadi Nyekundu**.

**110. Mheshimiwa Spika,** lazima tujenge utamaduni wa kuheshimu mali na rasilimali hapa nchini (mali za umma na mali binafsi). Kwa upande wa mali za umma, lazima tutangulize uzalendo na uadilifu tunapotekeleza majukumu yetu. Serikali inapoteza fedha nyingi kwenye kutekeleza Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kutojali thamani ya fedha kwenye miradi. Watumishi wa Serikali wasio waaminifu wamekuwa wakishirikiana na wafanyabiashara wasio waaminifu kuongeza gharama za miradi ikilinganishwa na gharama halisi ingawa wanafuata taratibu zote za ununuzi. Taratibu za ununuzi zinapokamilika, watumishi na wafanyabiashara hawa hugawana fedha na kiasi kidogo tu kilichosalia ndicho kinaelekezwa kwenye mradi husika na hatimaye kupata mradi ulio chini ya kiwango. Ukiwafuatilia kisheria hupati moja kwa moja pa kuwashika, hivyo wanakuwa wameiba kwa mujibu wa sheria, wameiba kwa kuzingatia sheria. Nawaelekeza wote wanaohusika na masuala ya ununuzi wa umma kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na kutanguliza mbele uzalendo na uadilifu.

**111. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mali binafsi, ni lazima tuheshimu biashara zetu na mali zinazotokana na biashara hizo. Kuna hatua tunazozifanya sekta zote za umma na binafsi zinadumaza uchumi wetu. Kwa mfano, kuna tabia ya kutolipa madeni kwenye benki zetu, jambo ambalo linapunguza uwezo wa benki kutoa mikopo kwa watu wengine. Aidha, wapo watu wengine ambao wakidaiwa kwa makusudi ya kuchelewesha malipo wanakimbilia mahakamani. Tusitumie vibaya vyombo vyetu vya sheria. Vilevile, kuna baadhi ya wakopeshaji ambao hawaheshimu mali za wateja wao. Mfano, mteja anakuwa amelipa sehemu kubwa ya mkopo wake lakini ikitokea mkopeshaji, rafiki au dalali akaipenda dhamana iliyowekwa, hufanya njama ya kupiga mnada dhamana hiyo kwa bei isiyolingana na thamani ya dhamana au sehemu ya deni iliyobaki sio hata robo ya dhamana hiyo. **Nawaelekeza vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia kila eneo panapokuwa na minada kwenye sekta binafsi na hata sekta ya umma na pale patakapoonekana kuwepo kwa njama za kudhulumu wamiliki**

**wa mali au kuchepusha sehemu ya mali zinazouzwa kwa mnada hatua kali za kisheria ziweze kuchukuliwa.**

**112. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Kuna wanaodhani tunapoongelea kukusanya kwa weledi, sheria na haki wanachukulia tutaacha kukusanya kodi. Nataka nisisitize kuwa, **tutakusanya Mapato ya Serikali. Tutakusanya Mapato ya Serikali. Tutakusanya Mapato ya Serikali**. Nitoe rai kwa watumishi wote wa Serikali wanaohusika na kukusanya kodi, maduhuli na ushuru kuelewa vizuri maelekezo haya kwa kuzingatia sheria, weledi na kutenda haki kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza. Nimeanza kusikia visingizio kila kona, **mara mfumo, mara mtandao mara EFD haifanyi kazi.** Kwa watoza kodi na walipakodi wote visingizio hivi vitaturudisha kwenye ukaguzi. Tusiwekeze kwenye kusaidiwa kukwepa kodi bali tusaidiwe kwenye kufuata sheria. Akiwepo mtumishi akakusaidia kukwepa kodi nawe ukampa asante unatengeneza tatizo tu sio unafuu kwani kuna siku utakuja kukaguliwa huku aliyekusaidia akiwa amehamishwa au kuachishwa kazi. Nitumie fursa hii kumwelekeza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kuweka watu mahususi wa kufanya doria kila kona, nchi nzima kuangalia mwenendo wa matumizi sahihi ya EFD na mifumo mingine ya malipo kuwa muda wote inafanya kazi.

**113. Mheshimiwa Spika,** tutasimamia nidhamu katika matumizi. Tutasimamia nidhamu katika matumizi. Tutasimamia nidhamu katika matumizi na tutaendeleza mapambano dhidi ya **Rushwa na Ufisadi**. Nazijua mbinu zote za udanganyifu, nazijua njia zote za majizi na watakaoendelea na tabia za kudokoadokoa fedha za walipa kodi, nitawashukia kama mwewe. Kazi inaendelea, watanzania endeleeni kumwamini Mheshimiwa Rais wetu, yuko macho na wasaidizi wake tuko macho, tutapambana na MCHWA wote, kuna mengine mnayasikia, kuna mengine mnayaona na mengine hata hamyaoni, yote tunaendelea kuyafanyia kazi kwa maelekezo thabiti na ya kizalendo ya Mheshimiwa Rais wetu. Kinyiramba kuna msemo usemao "**MWINDA KANGA HAPIGI YOWE."**

**114. Mheshimiwa Spika,** tuendeleze kwa kasi na kukamilisha miradi ya kimkakati ambayo inalenga kukuza uchumi, kuimarisha huduma za jamii na kuongeza fursa za ajira, hususan ajira kwa vijana. Tutakamilisha ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, tutaendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) mpaka itakamilika, tutamalizia ujenzi wa barabara zinazounganisha mikoa zilizosalia, tutakamilisha ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi na madaraja mengine kuwaunganisha wananchi wetu, tutaendelea na usambazaji wa umeme kutoka kila kijiji kwenda kila kitongoji na hatimaye kila nyumba.

**115. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya Jiji la Dodoma na kulifanya kuwa la kisasa. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa ofisi za wizara na taasisi zake katika mji wa Serikali Mtumba; kujenga barabara za mzunguko; na kuboresha miundombinu ya maji.

Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa katika eneo la Msalato.

**116. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amenituma niwahakikishie watanzania kupitia hotuba hii kuwa, tunaendelea kuijenga nchi, tunaendelea kuijenga nchi, ije mvua, lije jua, tunaendelea kuijenga nchi, uwe usiku au mchana, tunaendelea kuijenga nchi.** Hakuna mradi hata mmoja utakaokwama, wala hakuna Sekta ya maendeleo itakayozorota.
**"KAZI INAENDELEA."**

**117. Mheshimiwa Spika,** nampongeza Dkt. Philip Isdor Mpango aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, napenda kumpongeza kwa dhati kwa kazi nzuri aliyoifanya katika usimamizi wa uchumi kama Waziri wa Fedha wa Serikali ya Awamu ya Tano ulioiwezesha nchi yetu kuingia katika kundi la nchi za hadhi ya uchumi wa kipato cha kati cha chini. Vilevile, nampongeza kwa kazi nzuri iliyotukuka katika kuisimamia Wizara ya Fedha na Mipango ambayo kwa hakika imeweka msingi mzuri wa utekelezaji wa majukumu yangu.

**118. Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe Rais Mwinyi, ameanza kazi vizuri sana na kuwapa matumaini mapya wananchi wa Zanzibar katika kukuza uchumi na maendeleo hasa kwa kuwekeza kwenye "Blue Economy".

**119. Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza kwa uongozi wake hodari ndani ya Serikali na hapa Bungeni pamoja na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025.

**120. Mheshimiwa Spika,** naomba niwapongeze wakuu wa mihimili mingine ya Dola kwa usimamizi na uongozi shupavu, nikianza na wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Kongwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa kuongoza Bunge hili kwa umahiri na busara. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania kwa uongozi makini wa Mhimili wa Mahakama unaozingatia, miiko,dira na dhima ya mhimili huo. Hakika uongozi wake umefanikisha upatikanaji wa HAKI kwa wanyonge na kujenga misingi imara ya utawala wa sheria hapa nchini.

**121. Mheshimiwa Spika,** niruhusu pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Hussein Athman Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Mawaziri na Mkuu wa Utumishi wa Umma. Nampongeza kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa weledi mkubwa. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**122. Mheshimiwa Spika,** napenda niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati wakuu wote wa vyombo vya ulinzi na Usalama. Kipekee, naomba niwatambue Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Salvatory Mabeyo; Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Nyakoro Sirro; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Diwani Athuman Msuya; Kamishna Jenerali wa Magereza, Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Peter Makakala; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, CP Salum Hamdun; Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya, Gerald Kusaya Musabila; na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, John William Masunga. Utumishi wao uliotukuka na uzalendo wa hali ya juu umetuwezesha kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwa amani Tunawaomba muendelee kutimiza wajibu wenu wa kulinda amani na usalama wa nchi yetu kwa moyo wa uzalendo.

**123. Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Omar Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kwa umakini wao katika kuchambua na kutoa maoni na ushauri ambao umesaidia kuboresha mapendekezo ya Bajeti hii. Aidha, ninawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa michango waliyotoa kupitia vikao vya Kamati za Kisekta iliyowezesha kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2021/22.

**124. Mheshimiwa Spika,** ninawashukuru viongozi na watumishi wenzangu wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku hususan maandalizi ya bajeti hii. Kipekee ninamshukuru Mheshimiwa Hamad Y. Masauni, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni. Ninamshukuru sana Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Emmanuel M. Tutuba, pamoja na Naibu Makatibu Wakuu, Amina Kh. Shaaban, Adolf H. Ndunguru na Dkt. Khatibu M. Kazungu pamoja na watumishi wa kada zote wa Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, ninamshukuru Profesa Florens D. Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kusimamia sekta ya fedha kwa weledi mkubwa.

**125. Mheshimiwa Spika**, namshukuru Ndugu Alphayo J. Kidata, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi mkubwa. Kadhalika, namshukuru CPA Charles E.

Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya ya kukagua na kutoa taarifa za matumizi ya fedha za umma kwa wakati pamoja na kuishauri Serikali. Ninamshukuru CPA Athumani S. Mbuttuka, Msajili wa Hazina kwa kuendelea kusimamia Mashirika ya Umma na kuhakikisha Serikali inapata mchango na gawio stahiki. Ninamshukuru pia Dkt. Albina Chuwa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa kusimamia vizuri Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na kuendelea na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

**126. Mheshimiwa Spika**, nawapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye nyadhifa hizo. Aidha, niwapongeze pia wabunge wenzangu wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuaminiwa na vyama vyao na kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha bungeni. Kwa moyo wa dhati napenda kuishukuru sana familia yangu hususan mke wangu mpenzi Bi Neema Nchemba, na watoto wangu kwa kunitia moyo na kuniombea wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Vile vile, nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Iramba Magharibi walioniamini na kunichagua tena kwa kishindo kuwa Mbunge wao. Ninawaahidi kuwa sitawaangusha.

**127. Mheshimiwa Spika**, niwashukuru wafanyabiashara na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari. Rai yangu kwao ni kuwa, tukitumia rasilimali za nchi yetu vizuri na kufanya kazi kwa umoja na bidii, tutaifanya Tanzania kuwa kitovu cha uchumi na biashara sio tu kwa ukanda wa Afrika Mashariki bali kwa Afrika nzima. Vile vile, navishukuru vyombo vyote vya habari kwa kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari kwa maendeleo ya Taifa letu.

**128. Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua zao zilizotuwezesha kukamilisha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa amani na utulivu. Aidha, nawashukuru kwa kuliombea Taifa katika kipindi kigumu tulichopitia cha kuondokewa na viongozi wa kitaifa pamoja na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya korona. Sala na dua zao zimetuwezesha kupita kwa amani katika kipindi cha mabadiliko ya uongozi wa kitaifa na hatimaye kumpata Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.
Ninawasihi waendelee kuliombea Taifa letu bila kuchoka.

**129. Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**130. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

| Jedwali Na 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Serikali: 2015/16 - 2021/22 | | | | | | | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2015/16** | **2016/17** | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2020/21** | **2021/22** |
| | **Halisi** | **Halisi** | **Halisi** | **Halisi** | **Halisi** | **Bajeti** | **Matarajio** | **Bajeti** |
| | | | | | | | | |
| **Jumla ya Mapato (Yakijumuisha Halmashauri)** | **14,139,230** | **16,639,933** | **17,944,887** | **18,527,293** | **21,069,957** | **24,065,543** | **21,441,795** | **25,298,660** |
| | | | | | | | | |
| **A. Mapato yanayotokana na Kodi** | **12,525,378** | **14,126,590** | **15,191,421** | **15,511,330** | **17,622,822** | **20,325,780** | **18,416,133** | **22,178,721** |
| 1. Ushuru wa Forodha | 880,296 | 998,164 | 1,109,205 | 1,201,045 | 1,253,272 | 1,473,805 | 1,387,078 | 1,605,305 |
| 2. Ushuru wa Bidhaa | 2,144,395 | 2,106,442 | 2,199,900 | 2,370,414 | 2,512,423 | 3,002,765 | 2,808,699 | 3,282,441 |
| 3. Kodi ya Ongezeko la Thamani | 2,992,835 | 3,912,674 | 4,425,968 | 4,736,876 | 4,987,319 | 6,029,967 | 5,226,689 | 6,593,344 |
| 4. Kodi ya Mapato | 4,594,971 | 5,117,862 | 5,157,106 | 5,072,402 | 6,490,240 | 7,029,831 | 6,678,667 | 7,840,532 |
| 5. Kodi Nyingine | 1,912,880 | 1,991,449 | 2,299,242 | 2,130,594 | 2,379,569 | 2,789,413 | 2,315,000 | 2,857,098 |
| | | | | | | | | |
| **B. Mapato yasiyotokana na Kodi** | **1,613,852** | **2,513,343** | **2,753,466** | **3,015,963** | **3,447,135** | **3,739,763** | **3,025,662** | **3,119,939** |
| 1. Michango na Gawio la Mashirika | 388,551 | 893,935 | 803,502 | 682,331 | 738,810 | 1,055,638 | 729,945 | 977,618 |
| 2. Wizara Nyingine na Mikoa | 799,449 | 1,107,690 | 1,408,464 | 1,674,534 | 1,991,076 | 1,869,164 | 1,551,114 | 2,093,424 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. Mapato ya Halmasahuri | 425,852 | 511,718 | 541,499 | 659,098 | 717,249 | 814,961 | 744,603 | 48,897 |
| **Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

| Jedwali 2a: Mfumo wa Bajeti 2015/16 - 2021/22 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | Shilingi Milioni |
| | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Bajeti | Matarajio | Bajeti |
| | | | | | | | | |
| I. Mapato Yote | 22,543,664 | 25,417,791 | 26,439,542 | 28,962,515 | 29,515,050 | 34,879,793 | 30,059,331 | 36,329,740 |
| Mapato ya Ndani | 13,622,182 | 16,128,215 | 17,403,388 | 17,868,195 | 20,352,708 | 23,250,582 | 20,697,193 | 25,168,718 |
| Mapato ya Halmashauri | 425,852 | 511,718 | 541,499 | 659,098 | 717,249 | 814,961 | 744,603 | 863,858 |
| Misaada na Mikopo ya Bajeti | 291,381 | 342,785 | 246,688 | 125,396 | 391,433 | 138,323 | 258,205 | 0 |
| Misaada na Mikopo ya Miradi | 1,186,982 | 1,857,399 | 1,856,185 | 1,822,839 | 2,821,650 | 2,460,506 | 1,744,783 | 2,673,617 |
| Mikopo ya Kisekta (Basket Loans) | 161,842 | 104,991 | 74,681 | 44,281 | 166,027 | 79,005 | 77,622 | 59,736 |
| Misaada ya Kisekta (Basket Grants) | 86,199 | 168,984 | 117,166 | 181,378 | 181,091 | 196,538 | 68,618 | 222,570 |
| Mikopo ya Ndani (Rollover) | 3,005,789 | 4,615,670 | 4,835,199 | 3,718,008 | 3,976,811 | 3,316,078 | 3,316,078 | 3,150,337 |
| Mikopo ya Ndani (Financing) | 2,299,151 | 1,300,000 | 869,200 | 3,037,177 | 376,924 | 1,588,169 | 1,588,169 | 1,838,796 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Marekebisho | 1,010,781 | -838,731 | -978,745 | 361,320 | -1,290,936 | 0 | -712,663 | 0 |
| Mikopo ya kibiashara | 453,504 | 1,226,760 | 1,474,282 | 1,144,822 | 1,822,093 | 3,035,630 | 2,276,723 | 2,352,107 |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| II. Matumizi Yote | 22,543,664 | 25,417,791 | 26,610,843 | 27,270,435 | 29,515,050 | 34,879,793 | 30,059,331 | 36,329,740 |
| | | | | | | | | |
| Matumizi ya Kawaida | 18,204,111 | 18,144,967 | 18,995,074 | 18,776,596 | 20,206,266 | 22,100,538 | 21,113,852 | 23,002,951 |
| | | | | | | | | |
| CFS | 6,480,906 | 8,643,560 | 9,532,987 | 9,113,538 | 9,919,609 | 10,476,832 | 9,976,294 | 10,663,278 |
| Kulipa Madeni | 5,047,764 | 7,234,530 | 8,133,063 | 7,701,842 | 8,304,618 | 8,649,941 | 8,536,619 | 8,878,420 |
| Malipo Mengine | 1,433,142 | 1,409,030 | 1,399,924 | 1,411,696 | 1,614,991 | 1,826,891 | 1,439,675 | 1,784,858 |
| | | | | | | | | |
| Matumizi ya Kawaida (Bila CFS) | 11,723,205 | 9,501,407 | 9,462,087 | 9,663,058 | 10,286,658 | 11,623,706 | 11,137,558 | 12,339,673 |
| o/w Malipo ya Mishahara | 5,627,497 | 5,599,246 | 5,544,384 | 5,699,188 | 5,939,616 | 6,583,033 | 6,542,126 | 6,912,184 |
| Mishahara ya Mashirika | 925,760 | 767,901 | 783,292 | 960,385 | 1,066,695 | 1,179,357 | 1,167,563 | 1,238,325 |
| Fedha ya Halmashauri | 170,340 | 251,484 | 216,600 | 349,322 | 419,428 | 481,870 | 457,401 | 532,768 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Matumizi Mengine | 4,999,607 | 2,882,775 | 2,917,811 | 2,654,163 | 2,860,918 | 3,379,447 | 2,970,469 | 3,656,396 |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| Matumizi ya Maendeleo | 4,339,553 | 7,272,824 | 7,615,768 | 8,493,838 | 9,308,784 | 12,779,255 | 8,945,479 | 13,326,788 |
| Fedha za Ndani | 2,904,530 | 5,141,451 | 5,397,034 | 6,535,879 | 6,840,104 | 10,043,206 | 7,030,244 | 10,370,865 |
| Fedha za Nje | 1,435,023 | 2,131,374 | 2,218,735 | 1,957,959 | 2,468,680 | 2,736,049 | 1,915,234 | 2,955,923 |
| | | | | | | | | |
| Pato la Taifa | 101,355,820 | 113,553,411 | 122,835,229 | 132,049,549 | 143,297,783 | 157,767,884 | 155,005,471 | 167,286,243 |
| | | | | | | | | |
| Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango | | | | | | | | |

## Jedwali 2b: Mfumo wa Bajeti 2015/16 - 2021/22

**Asilimia ya Pato la Taifa**

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

| | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Bajeti | Matarajio | Bajeti |
| | | | | | | | | |
| Mapato Yote | 22.2% | 22.4% | 21.7% | 21.9% | 20.6% | 22.1% | 19.4% | 21.7% |
| Mapato ya Ndani | 13.4% | 14.2% | 14.2% | 13.5% | 14.2% | 14.7% | 13.4% | 15.0% |
| Mapato ya Halmashauri | 0.4% | 0.5% | 0.4% | 0.5% | 0.5% | 0.5% | 0.5% | 0.5% |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Bajeti | 0.3% | 0.3% | 0.2% | 0.1% | 0.3% | 0.1% | 0.2% | 0.0% |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 1.2% | 1.6% | 1.5% | 1.4% | 2.0% | 1.6% | 1.1% | 1.6% |
| Mikopo ya Kisekta (Basket Loans) | 0.2% | 0.1% | 0.1% | 0.0% | 0.1% | 0.1% | 0.1% | 0.0% |
| Misaada ya Kisekta (Basket Grants) | 0.1% | 0.1% | 0.1% | 0.1% | 0.1% | 0.1% | 0.0% | 0.1% |
| Mikopo ya Ndani (Rollover) | 3.0% | 4.1% | 3.9% | 2.8% | 2.8% | 2.1% | 2.1% | 1.9% |
| Mikopo ya Ndani (Financing) | 2.3% | 1.1% | 0.7% | 2.3% | 0.3% | 1.0% | 1.0% | 1.1% |
| Marekebisho | 1.0% | -0.7% | -0.8% | 0.3% | -0.9% | 0.0% | -0.5% | 0.0% |
| Mikopo yenye masharti ya kibiashara | 0.4% | 1.1% | 1.2% | 0.9% | 1.3% | 1.9% | 1.5% | 1.4% |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| II. Matumizi Yote | 22.2% | 22.4% | 21.7% | 21.9% | 20.6% | 22.1% | 19.4% | 21.7% |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |
| Matumizi ya Kawaida | 18.0% | 16.0% | 15.5% | 15.5% | 14.1% | 14.0% | 13.6% | 13.8% |
| | | | | | | | | |
| CFS | 6.4% | 7.6% | 7.8% | 6.9% | 6.9% | 6.6% | 6.4% | 6.4% |
| Kulipa Madeni | 5.0% | 6.4% | 6.6% | 5.8% | 5.8% | 5.5% | 5.5% | 5.3% |
| Malipo Mengine | 1.4% | 1.2% | 1.1% | 1.1% | 1.1% | 1.2% | 0.9% | 1.1% |
| | | | | | | | | |
| Matumizi ya Kawaida (Bila CFS) | 11.6% | 8.4% | 7.7% | 7.3% | 7.2% | 7.4% | 7.2% | 7.4% |
| o/w Malipo ya Mishahara | 5.6% | 4.9% | 4.5% | 4.3% | 4.1% | 4.2% | 4.2% | 4.1% |
| Mishahara ya Mashirika | 0.9% | 0.7% | 0.6% | 0.7% | 0.7% | 0.7% | 0.8% | 0.7% |
| Fedha za Halmashauri | 0.2% | 0.2% | 0.2% | 0.3% | 0.3% | 0.3% | 0.3% | 0.3% |
| Matumizi Mengine | 4.9% | 2.5% | 2.4% | 2.0% | 2.0% | 2.1% | 1.9% | 2.2% |
| | | | | | | | | |
| Matumizi ya Maendeleo | 4.3% | 6.4% | 6.2% | 6.4% | 6.5% | 8.1% | 5.8% | 8.0% |
| Fedha za Ndani | 2.9% | 4.5% | 4.4% | 4.9% | 4.8% | 6.4% | 4.5% | 6.2% |
| Fedha za Nje | 1.4% | 1.9% | 1.8% | 1.5% | 1.7% | 1.7% | 1.2% | 1.8% |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango | | | | | | | | |

**Jedwali Na. 3 Misaada na Mikopo Nafuu kutoka Nje 2016/17 - 2021/22**

Shilingi Milioni


| | | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Bajeti | Matarajio | Bajeti |
| | | | | | | | | |
| **Misaada ya Kibajeti** | Misaada | 190,303 | 246,688 | 0 | 265,338 | 138,323 | 47,670 | 0 |
| | Mikopo yenye Masharti Nafuu | 152,482 | 0 | 125,396 | 126,094 | 0 | 210,535 | 0 |
| | **Jumla** | **342,785** | **246,688** | **125,396** | **391,433** | **138,323** | **258,205** | **0** |
| | | | | | | | | |
| **Mifuko ya Kisekta** | Misaada | 168,984 | 117,166 | 181,378 | 181,091 | 196,538 | 68,618 | 222,570 |
| | Mikopo yenye Masharti Nafuu | 104,991 | 74,681 | 44,281 | 166,027 | 79,005 | 77,622 | 59,736 |
| | **Jumla** | **273,975** | **191,847** | **225,659** | **347,118** | **275,543** | **146,240** | **282,306** |
| | | | | | | | | |
| **Miradi ya** | Misaada | | | | | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Maendeleo** | | 674,938 | 635,704 | 707,797 | 481,419 | 614,461 | 450,891 | 915,506 |
| | Mikopo yenye Masharti Nafuu | 1,182,461 | 1,220,481 | 1,115,041 | 2,340,232 | 1,846,045 | 1,293,892 | 1,758,111 |
| | | **1,857,399** | **1,856,185** | **1,822,839** | **2,821,650** | **2,460,506** | **1,744,783** | **2,673,617** |
| | **Jumla** | | | | | | | |
| | **Jumla Kuu** | **2,474,159** | **2,294,720** | **2,173,893** | **3,560,201** | **2,874,372** | **2,149,228** | **2,955,923** |
| Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango | | | | | | | | |


**Jedwali 4: Mwenendo wa Mikopo ya Serikali**


| | | | |
|---|---|---|---|
| **MAKADIRIO YA MIKOPO MIPYA YA NDANI NA NJE INAYOTEGEMEWA KUKOPWA (MILIONI SHILINGI)** | | | |
| | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** |
| **1. Jumla ya Mikopo mipya ya Ndani na nje (a+b)** | **8,851,548.5** | **9,864,927.3** | **9,159,086.9** |
| **(a) Mikopo Mipya ya Ndani** | **4,959,992.2** | **4,904,247.6** | **4,989,132.9** |
| (i) Mikopo mipya ya Ndani (Kulipia dhamana za Serikali zilizoiva) | 3,460,218.0 | 3,316,078.4 | 3,150,336.7 |
| (ii) Mikopo mipya ya Ndani (Kuziba nakisi ya Bajeti) | 1,499,774.2 | 1,588,169.2 | 1,838,796.2 |
| | | | |
| **(b) Mikopo Mipya ya Nje** | **3,891,556.4** | **4,960,679.7** | **4,169,954.0** |
| (i) Mikopo yenye Masharti nafuu (Miradi ya Maendeleo) | 1,449,162.3 | 1,925,049.7 | 1,817,847.0 |
| (ii) Mikopo yenye Masharti nafuu (Bajeti) | 125,990.5 | - | - |
| (iii) Mikopo yenye masharti ya Kibiashara | 2,316,403.6 | 3,035,630.0 | 2,352,106.9 |
| | | | |
| **(c ) Malipo ya Madeni ya Ndani** | **4,899,168.0** | **4,946,747.0** | **4,711,974.1** |
| (i) Mtaji -Kulipia Dhamana za Serikali zilizoiva (Rollover) | 3,460,218.0 | 3,316,078.4 | 3,150,336.7 |
| (ii) Riba | 1,438,950.0 | 1,630,668.6 | 1,561,637.4 |
| | | | |
| **(d) Malipo ya Madeni ya Nje** | **2,963,410.0** | **3,703,194.5** | **4,166,445.8** |
| (i) Riba | 987,312.00 | 1,239,913.84 | 1,151,376.3 |
| (ii) Mtaji | 1,976,098.00 | 2,463,280.62 | 3,015,069.5 |
| | | | |


| | | | |
|---|---|---|---|
| **(e) Ongezeko Halisi la Mikopo ya Ndani (a-c(i)** | **1,499,774.2** | **1,588,169.2** | **1,838,796.2** |
| | | | |
| **(f) Ongezeko Halisi la Mikopo ya nje (b-d(ii) /1** | **1,915,458.4** | **2,497,399.1** | **1,154,884.5** |
| | | | |
| **2. Ongezeko Halisi la Mikopo ya Ndani na Nje (e+f)** | **3,415,232.5** | **4,085,568.3** | **2,993,680.7** |
| /1Ongezeko hili halijuishi fedha zinazoendelea kupokelewa kwenye Mikopo ya zamani | | | |






.



Kiambatanisho Na 2:
VYANZO VYA MAPATO YA NDANI
2020/21 - 2021/22
Shilingi Milioni
9000000
8000000
7000000
6000000
5000000
4000000
3000000
2000000
1000000
0
Ushuru Wa Forodha
Ushuru wa Bidhaa za Nje
Ushuru wa Bidhaa za Ndani
VAT - Bidhaa za Nje
VAT-Bidhaa za Ndani
Kodi ya Mapato
Kodi Nyingine
Mapato Yasiyo ya Kodi
Mapato ya Halmashauri
2020/21
2021/22


Kiambatanisho Na. 3a: Vyanzo vya Fedha za Bajeti, 2021/22
Jumla Shs. 36,329,740
Mikopo ya ndani na Nje (Ikijumuisha Rollover)
20%
Misaada na Mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa maendeleo
8%
Mapato ya ndani (yakijumuisha ya Halmashauri)
72%


Kiambatisho Na. 3b: Vyanzo vya Fedha za Bajeti, 2020/21
Jumla Shs. 34,879,793
ya ndani na Nje (Ikijumuisha Rollover) 23%
Misaada na Mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa maendeleo 8%
Mapato ya ndani (yakijumuisha ya Halmashauri) 69%


Kiambatisho Na. 4a: Matumizi ya Serikali, 2021/22
Jumla Shs. 36,329,740
Malipo ya Deni la Serikali 24%
Matumizi ya Maendeleo 37%
Michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na malipo mengine 5%
Matumizi mengine 12%
Mishahara 22%


Kiambatisho Na. 4b Matumizi ya Serikali, 2020/21
Jumla Shs. 34,879,793
Malipo ya Deni la Serikali
25%
Matumizi ya Maendeleo
37%
Michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na malipo mengine
5%
Matumizi mengine
11%
Mishahara
22%


Kiambatisho Na. 4C: Maeneo ya Kipaumbele ya FYDP III
Kuendeleza rasilimali watu 0.34%
Kuchochea uchumi shindani na shirikishi 55.83%
Kuchochea maendeleo ya watu 33.24%
Kukuza uwekezaji na biashara 0.24%
Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma 10.36%

**KIAMBATISHO NA. 5 MABORESHO YA TOZO ZA SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA**

**USAJILI WA CHAKULA NA BIDHAA ZA CHAKULA**

| S/N | AINA YA HUDUMA | TOZO YA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA |
|---|---|---|---|
| 1 | Usajili wa maziwa na bidhaa za maziwa | 450 | 600,000 |
| 2 | Usajili wa nafaka na bidhaa za nafaka | 400 | 600,000 |
| 3 | Usajili wa kunde | 350 | 500,000 |
| 4 | Usajili wa Karanga | 350 | 500,000 |
| 5 | Usajili wa bidhaa za mashina na mizizi | 360 | 500,000 |
| 6 | Usajili wa vinywaji visivyo vya kileo | 350 | 500,000 |
| 7 | Usajili wa vileo | 300 | 500,000 |
| 8 | Usajili wa sukari na asali | 360 | 500,000 |
| 9 | Usajili wa chumvi iliyowekewa iodini | 280 | 500,000 |
| 10 | Usajili wa mafuta ya kula | 280 | 500,000 |
| 11 | Usajili wa mahani ya chai na kahawa | 450 | 600,000 |
| 12 | Usajili wa kakao na bidhaa za kakao | 400 | 600,000 |
| 13 | Usajili wa viungo mbalimabali vya chakula, chai n.k na mimea | 400 | 600,000 |
| 14 | Usajili wa siki (vinega) | 230 | 500,000 |
| 15 | Usajili wa samaki na bidhaa za samaki | 370 | 600,000 |
| 16 | Usajili wa nyama na bidhaa za nyama | 400 | 600,000 |
| 17 | Usajili wa matunda na bidhaa za matunda | 330 | 500,000 |
| 18 | Usajili wa maji ya kunywa | 410 | 600,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 19 | Usajili wa mboga za majani na bidhaa zake | 330 | 500,000 |
| 20 | Usajili wa chakula cha Watoto wachanga na formula za ukuzaji | 900 | 1,000,000 |
| 21 | Usajili wa virutubisho vya chakula | 800 | 800,000 |
| 22 | Usajili wa vyakula vya nafaka vilivyosindikwa kwa ajili ya watoto | 850 | 1,000,000 |
| 23 | Usajili wa viongezeo vya chakula | 250 | 500,000 |
| 24 | Usajili wa bidhaa tamutamu kama chocolate, pipi, biskuti, n.k | 380 | 550,000 |

**MAELEZO**

Tozo zinazopendekezwa zinajumuisha gharama za kutathmini bidhaa, upimaji wa maabara na ukaguzi sokoni kwa muda wa miaka

1. mitano. Tozo hizi zinapendekezwa kupunguzwa ili kuendana na dhamira na muongozo wa serikali wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara

Tozo hizi zinapendekezwa kupungua kwa sababu sehemu ya gharama za ukaguzi na ufuatiliaji wa muenendo wa bidhaa sokoni

2. zimeshughulikiwa katika mifumo mingine jumuishi ndani ya TBS

3. Tozo zilizopunguzwa zinatarajiwa kuongeza idadi ya wasajiliwa na bidhaa zitakazosajiliwa, hivyo mapato ya Shirika hayataathiriwa.

## TOZO BORESHWA ZA UPIMAJI KATIKA MAABARA

| Na. | VIPIMO | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO ZA VIPIMO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA |
|---|---|---|---|
| | **MAABARA YA KEMIA** | | |
| 1 | Hydroquinone kwenye vipodozi | 435 | 150,000/= |
| 2 | Kojiki asidi kwenye vipodozi | 435 | 150,000/= |
| | **MAABARA YA CHAKULA** | | |
| 3 | Kiasi cha unyevu | 30 | 30,000/= |
| 4 | Crude fibre | 55 | 30,000/= |
| 5 | Acid insoluble ash | 55 | 30,000/= |
| 6 | Protini | 55 | 60,000/= |
| 7 | Asidi ya foliki | 65 | 50,000/= |
| 8 | Madini joto | 60 | 30,000/= |
| 9 | Total ash | 45 | 30,000/= |
| 10 | Volatile oils | 55 | 30,000/= |
| 11 | Sumukuvu | 120 | 150,000/= |
| 12 | Aflatoxins | 225 | 150,000/= |
| 13 | Kiasi cha chumvi | 35 | 30,000/= |
| 14 | Chromate test | 25 | 30,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | physical tests (kila moja) | 5 | 10,000/= |
| 16 | Slip point (Melting point) | 25 | 30,000/= |
| 17 | Acid value | 50 | 30,000/= |
| 18 | Unsaponifiable matter | 50 | 30,000/= |
| 19 | Peroxide value | 50 | 30,000/= |
| 20 | Insoluble impurities | 25 | 30,000/= |
| 21 | Soap content | 20 | 30,000/= |
| 22 | Relative density | 10 | 20,000/= |
| 23 | Refractive index | 10 | 20,000/= |
| 24 | Saponification value | 50 | 30,000/= |
| 25 | Rangi ( ICUMSA) | 30 | 20,000/= |
| 26 | Ethyl alcohol (Ethanol) content | 25 | 30,000/= |
| 27 | pH | 10 | 15,000/= |
| 28 | Carbon dioxide | 20 | 20,000/= |
| 29 | Polarisation | 25 | 30,000/= |
| 30 | Water insoluble matter | 25 | 30,000/= |
| 31 | Sulphated ash | 50 | 30,000/= |
| 32 | Acidity | 25 | 30,000/= |
| 33 | Brix (Total soluble solids) | 15 | 20,000/= |
| 34 | Specific gravity | 10 | 20,000/= |
| 35 | Total carbohydrates | 30 | 20,000/= |
| 36 | Fat content | 60 | 45,000/= |
| 37 | Ascorbic acid | 65 | 30,000/= |
| 38 | Water soluble ash | 50 | 30,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 39 | Alkalinity | 25 | 30,000/= |
| 40 | Kiasi cha sukari | 50 | 30,000/= |
| 41 | Kafeini | 65 | 50,000/= |
| 42 | Alkalinity of water-soluble ash | 40 | 30,000/= |
| 43 | Density | 10 | 20,000/= |
| 44 | Sorbic acid | 55 | 20,000/= |
| 45 | Total solids | 30 | 20,000/= |
| 46 | Volatile acidity | 25 | 30,000/= |
| 47 | Aldehydes | 25 | 50,000/= |
| 48 | Methanol (for Alcoholic Beverages and Spirits) | 50 | 50,000/= |
| 49 | Total acidity | 25 | 20,000/= |
| 50 | Chloride (as NaCl) | 35 | 30,000/= |
| 51 | Free Fatty acids (FFA) | 25 | 30,000/= |
| 52 | Higher alcohols (for Alcoholic beverages and Spirits) | 45 | 50,000/= |
| 53 | Hydroxymethyl furfural (HMF) | 50 | 50,000/= |
| 54 | Dry matter | 30 | 30,000/= |
| 55 | Kiasi cha nyama | 55 | 20,000/= |
| 56 | Sulphur dioxide | 50 | 30,000/= |
| 57 | Total cocoa solids | 15 | 20,000/= |
| 58 | Fat free cocoa solids | 15 | 20,000/= |
| 59 | Cocoa butter | 35 | 35,000/= |
| 60 | Purity | 50 | 30,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 61 | Vitamini (kila moja) | 65 | 50,000/= |
| 62 | Madini tembo (kila moja) | 55 | 35,000/= |
| 63 | Mabaki ya viuatilifu | 120 | 300,000/= |
| 64 | Mabaki ya dawa (pesticide residues) | 135 | 150,000/= |
| 65 | Vikolezo vya utamu | 65 | 50,000/= |
| 66 | Kihifadhi (kila kimoja) | 65 | 50,000/= |
| 67 | Rangi za chakula | 65 | 50,000/= |
| 68 | Total plate count | 130 | 30,000/= |
| 69 | Yeast and Moulds | 160 | 30,000/= |
| 70 | *Salmonella spp* (kila moja) | 155 | 40,000/= |
| 71 | *Escherichia coli* | 130 | 40,000/= |
| 72 | Coliforms | 125 | 30,000/= |
| 73 | *Staphylococcus aureus* | 150 | 40,000/= |
| 74 | *Listeria spp* | 150 | 40,000/= |
| 75 | *Bacillus spp* (kila moja) | 165 | 40,000/= |
| 76 | *Pseudomonas aeruginosa* | 125 | 40,000/= |
| 77 | *Shigella* | 155 | 40,000/= |
| 78 | Enterobacteriaceae | 130 | 30,000/= |
| 79 | *Clostridium spp* (kila moja) | 165 | 40,000/= |
| 80 | *Sulfite reducing anaerobes* | 125 | 40,000/= |
| 81 | *Streptococcus spp* (kila moja) | 125 | 40,000/= |

**MAELEZO**

Gharama za vipimo vya kimaabara zinapendekezwa kupunguzwa ili kukidhi matakwa ya "Government Blueprint For Regulatory Reform" yanayolenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini.

**USAJILI WA VIPODOZI**

| S/N | AINA YA HUDUMA | TOZO YA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA |
|---|---|---|---|
| 1. | Usajili wa vipodozi | 100 | 440,000 |

**MAELEZO**

---

Tozo hii inapendekezwa kuongezwa ili kukidhi gharama za upimaji

**TOZO ZA MAABARA YA METROLOGY**

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TUNGAMO | Mzani mdogo | (0-200) g | 120,000 | 155 | 135,000.00 | 195 |
| | | Mzani wa uchambuzi | Up to 200 g | 80,000 | 103 | 90,000.00 | 129 |
| | | Mzani wa uchambuzi | (201-2000) g | 75,000.00 | 97 | 90,000.00 | 129 |
| | | Mzani wa dijitali | (2100-6000) g | 70,000.00 | 91 | 90,000.00 | 129 |
| | | Mzani usio wa digitali | (0-20) kg | 70,000.00 | 91 | 90,000.00 | 129 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mzani wa uzito | (10-50) kg | 80,000.00 | 103 | 90,000.00 | 129 |
| | | | (51-150) kg | 110,000.00 | 142 | 135,000.00 | 194 |
| | | | (151-250) kg | 150,000.00 | 194 | 220,000.00 | 285 |
| | | | (251-500) kg | 250,000.00 | 323 | 350,000.00 | 453 |
| | | Daraja la kupimia Uzito | (500-5000) kg | 1,000,000.00 | 1294 | 1,400,000.00 | 1,811 |
| | | | Above 5 Tone to 40 Tone | 1,200,000.00 | 1552 | 1,600,000.00 | 2,070 |
| | | | Above 50 Tone | 1,700,000.00 | 2199 | 2,200,000.00 | 2,846 |
| | | Mzani mkubwa wa kuchanganyia | (500-2000) kg | 950,000.00 | 1229 | 1,300,000.00 | 1,682 |
| | | Mzani wa kuninginiza | - | 90,000.00 | 116 | 100,000.00 | 129 |
| | | Mobile Weighing Crane | (0-20) Tone | 1,500,000.00 | 1940 | 2,200,000.00 | 2,846 |
| | | Mzani wa Kupimia ndege | 3781kg (Red pad) | 200,000.00 | 259 | 350,000.00 | 453 |
| | | | 4143kg (Yellow pad) | 200,000.00 | 259 | 350,000.00 | 453 |
| | | | 2039kg | 200,000.00 | 259 | 350,000.00 | 453 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (Green pad) | | | | |
| | | Seti ya Mawe ya Tungamo | 1mg to 1000 g | 25,000.00 | 32 | 25,000.00 | 32 |
| | | | (2000-5000) g | 20,000.00 | 26 | 20,000.00 | 26 |
| | | | From 10 kg and above | 30,000.00 | 39 | 30,000.00 | 39 |
| 2 | KANI | Mashine ya kukandamizia | | 700,000.00 | 906 | 1,200,000.00 | 1,552 |
| | | CBR (proving) ring | | 400,000.00 | 517 | 600,000.00 | 776 |
| | | Torque Wrench | | 110,000.00 | 142 | 160,000.00 | 207 |
| | | Load Cell | | 780,000.00 | 1009 | 1,200,000.00 | 1,552 |
| | | Rebound Hammer | | | 259 | 250,000.00 | 323 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 200,000.00 | | | |
| | | Tensile Machine | | 260,000.00 | 336 | 350,000.00 | 453 |
| | | Marshall machine | | 400,000.00 | 517 | 600,000.00 | 776 |
| | | Torque meter | | 150,000.00 | 194 | 180,000.00 | 233 |
| | | Tension meter | | 90,000.00 | 116 | 100,000.00 | 129 |
| 3 | JOTO RIDI | Vipima joto:<br>i).Vipima joto vyenye vimiminika | (0-200)'C | 85,000.00 | 110 | 90,000.00 | 129 |
| | | | (201-600) t | 95,000.00 | 123 | 99,000.00 | 142 |
| | | | (-30-200)'C | 85,000.00 | 110 | 90,000.00 | 129 |
| | | ii). Vipima joto vya dijtali<br>a). Mfumo wa kipima joto na kichwa cha | (-30-200)'C | 85,000.00 | 110 | 90,000.00 | 129 |
| | | | (200-600)'C | 95,000.00 | 123 | 99,000.00 | 142 |
| | | | More than | | 142 | 108,000.00 | 155 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kusomea ( Pt.100 probes/RTDs) | three points | 110,000.00 | | | |
| | | | (-30-1200)'C | 110,000.00 | 142 | 117,000.00 | 168 |
| | | b) Thermocouple probes | (-30-200)'C | 85,000.00 | 110 | 90,000.00 | 129 |
| | | | (200-600)'C | 85,000.00 | 110 | 90,000.00 | 129 |
| | | c) Kipima joto aina ya kalamu<br>iii). Dial Temp. Gauges | (-30-600)'C | 110,000.00 | 142 | 108,000.00 | 155 |
| | | iv). Kipima joto na unyevunyevu | (-30-200)'C | 110,000.00 | 142 | 108,000.00 | 155 |
| | | Dry block | | 260,000.00 | 336 | 315,000.00 | 453 |
| | | Water bath | | 120,000.00 | 155 | 135,000.00 | 194 |
| | | Ugezi wa nukta moja | | 95,000.00 | 123 | 135,000.00 | 194 |
| | | Ugezi wa nukta zisizo zidi tatu | | 160,000.00 | 207 | 180,000.00 | 259 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ugezi wa nukta zaidi ya tatu | | 175,000.00 | 226 | 225,000.00 | 323 |
| | | Autoclave (Ugezi wa nukta moja) | | 215,000.00 | 226 | 180,000.00 | 259 |
| | | Autoclave (Ugezi wa nukta zisizo zidi tatu) | | 215,000.00 | 278 | 225,000.00 | 323 |
| | | Autoclave (Ugezi wa nukta Zaidi ya tatu) | | 110,000.00 | 278 | 270,000.00 | 388 |
| | | Friji/Friji la kugandisha | | 120,000.00 | 142 | 117,000.00 | 168 |
| | | Ovens (Ugezi wa nukta moja) | | 120,000.00 | 155 | 135,000.00 | 194 |
| | | Tanuri (Ugezi wa nukta zisizozidi tatu) | | 120,000.00 | 155 | 180,000.00 | 259 |
| | | Ovens (Ugezi wa nukta zisizo zidi tatu) | | 150,000.00 | 155 | 225,000.00 | 323 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MUFFLE FURNANCES | | 130,000.00 | 194 | 180,000.00 | 259 |
| | | Incubators (Ugezi wa nukta moja) | | 130,000.00 | 168 | 162,000.00 | 194 |
| | | Incubators(Ugezi wa nukta zisizo zidi tatu) | | 130,000.00 | 168 | 145,800.00 | 259 |
| | | Incubators(Ugezi wa nukta Zaidi ya tatu) | | 100,000.00 | 168 | 225,000.00 | 323 |
| | | HOT PLATES(Ugezi wa nukta moja)) | | 100,000.00 | 129 | 135,000.00 | 194 |
| | | HOT PLATES(Ugezi wa nukta zisizo zidi tatu) | | 100,000.00 | 129 | 180,000.00 | 259 |
| | | HOTPLATES(Ugezi wa nukta Zaidi ya tatu) | | 165,000.00 | 129 | 180,000.00 | 259 |
| | | Vyumba vya kupima Unyevynyevu | | 165,000.00 | 213 | 180,000.00 | 259 |
| | | Vyumba vya Baridi | | 165,000.00 | 213 | 180,000.00 | 259 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Sahani za Kugandishia | | 165,000.00 | 213 | 180,000.00 | 259 |
| | | Blast freezers | | 165,000.00 | 213 | 180,000.00 | 259 |
| | | Vyumba vya baridi /Chill rooms | | 165,000.00 | 213 | 180,000.00 | 259 |
| | | VIDHIBITI JOTO | | 165,000.00 | 213 | 180,000.00 | 259 |
| | | Thermographs | | 85,000.00 | 110 | 90,000.00 | 129 |
| | UGEZI PAMOJA NA UCHORAJI (Incubators, Oven, Liquid bath, Refregirators) | | | | | | |
| | | Ugezi wa nukta moja | | - | - | 540,000.00 | 776 |
| | | Ugezi wa nukta tatu | | - | - | 720,000.00 | 1,035 |
| | | Ugezi wa nukta Zaidi | | - | - | 900,000.00 | 1,294 |

| **S/N** | **AINA YA HUDUMA** | **AINA YA KIFAA** | **UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA** | **TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA** | **TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI** | **TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA** | **TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ya tatu | | | | | |
| | UGEZI PAMOJA NA UCHORAJI (Autoclave) | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ugezi wa nukta moja | | - | - | 720,000.00 | 1,035 |
| | | Ugezi wa nukta tatu | | - | - | 900,000.00 | 1,294 |
| | | Ugezi wa nukta Zaidi ya tatu | | - | - | 1,080,000.00 | 1,552 |
| | | | | - | | | |
| 4 | KEMIA NA VINGINE | Refractometer | | 90,000.00 | 116 | 108,000.00 | 155 |
| | | Mita ya pH | | 90,000.00 | 116 | 108,000.00 | 155 |
| | | Mashine ya kuchambua Unyevunyevu | | 90,000.00 | 116 | 108,000.00 | 155 |
| | | Hydrometer | | 90,000.00 | 116 | 108,000.00 | 155 |
| | | Mita ya Wiani | | 100,000.00 | 129 | 108,000.00 | 155 |
| 5 | UJAZO | Upimaji wa uwezo wa ujazo | (0-1000)ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |
| | | | (1001 to 2000) ml | 50,000.00 | 65 | 45,000.00 | 65 |
| | | | Above 2000 ml | 60,000.00 | 78 | 54,000.00 | 78 |
| | | Pycnometer | (50-100)ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |
| | | TOT | | 30,000.00 | 39 | 27,000.00 | 39 |
| | | Flaski ya ujazo | (0-50)ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |
| | | | (51-1000) ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |
| | | | (1001-2000)ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |
| | | Burettes | (11-100)ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Measuring Cylinder | (0-2000)ml | 40,000.00 | 52 | 36,000.00 | 52 |
| 6 | UJAZO MDOGO | Bomba ndogo za | (0-1000) µl | 40,000.00 | 52 | 45,000.00 | 65 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kupimia ujazo mdogo | Above 1000 µl | 60,000.00 | 78 | 54,000.00 | 78 |
| | | Bomba ndogo za kupimia ujazo mdogo zenye Njia Zaidi ya moja | (0 -1000) | 120,000.00 | 155 | 117,000.00 | 168 |
| | | Chupa ya Mzunguko | (0-1000) ml | 30,000.00 | 39 | 27,000.00 | 39 |
| | | Bika | (0-1000) ml | 30,000.00 | 39 | 27,000.00 | 39 |
| | | Sindano | (1-10) ml | 30,000.00 | 39 | 27,000.00 | 39 |
| | | | (0-5) $M^3$ | 500,000.00 | 647 | 500,000.00 | 647 |
| | | | (0-10) M3 | 750,000.00 | 970 | 750,000.00 | 970 |
| | | SYRUP TANKS | (0-15) M3 | 800,000.00 | 1035 | 800,000.00 | 1,035 |
| | | | (0-20) M3 | 1,000,000.00 | 1294 | 1,000,000.00 | 1,294 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (0-1000)1 | 160,000.00 | 207 | 160,000.00 | 207 |
| | | SIMTANK | (0-2000)1 | 250,000.00 | 323 | 250,000.00 | 323 |
| | | Matenki ya ujazo mkubwa | (0-5000) M | 2,000,000.00 | 2587 | 2,000,000.00 | 2,587 |
| | | | (6000-45000) L | 12,000,000.00 | 15524 | 12,000,000.00 | 15,524 |
| | | ROAD TANKERS | (Each at a cost) | 450,000.00 | 582 | 450,000.00 | 582 |
| 7 | MUDA NA MASAFA | 5 points measurements | (1-60)s | 90,000.00 | 116 | 81,000.00 | 116 |
| | | 5 points measurements | (1 to60)min | 100,000.00 | 129 | 90,000.00 | 129 |
| | | 5 points measurements | (61-180)min | 120,000.00 | 155 | 108,000.00 | 155 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 5 points measurements | (180min-24Hrs) | 130,000.00 | 168 | 117,000.00 | 168 |
| | | 5 points measurements | Above 1 day | 190,000.00 | 246 | 171,000.00 | 246 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Stomacher | Time/ RPM | 110,000.00 | 142 | 99,000.00 | 142 |
| | | Centrifuge | Time /RPM | 110,000.00 | 142 | 99,000.00 | 142 |
| | | Vortex/ Mixer | Time / RPM | 110,000.00 | 142 | 99,000.00 | 142 |
| | | Rotator | Time / RPM | 110,000.00 | 142 | 99,000.00 | 142 |
| | | Los Angeles | Time /RPM | 110,000.00 | 142 | 110,000.00 | 142 |
| | | Shaker | Time / RPM | 110,000.00 | 142 | 99,000.00 | 128 |
| | | Tachometer | Time /RPM | 120,000.00 | 155 | 108,000.00 | 140 |
| 8 | DIMENSIONAL(UREFU) | Measuring Tape | (0-30)m | 110,000.00 | 142 | 110,000.00 | 142 |
| | | | Above 30 m | 160,000.00 | 207 | 200,000.00 | 259 |
| | | Dip tape | | 110,000.00 | 142 | 200,000.00 | 259 |
| | | Height gauge | | 100,000.00 | 129 | 100,000.00 | 129 |
| | | Depth /thickness gauge | | 100,000.00 | 129 | 100,000.00 | 129 |
| | | Ruler | | 100,000.00 | 129 | 100,000.00 | 129 |
| | | Dipstick Marking | | | 233 | 180,000.00 | 233 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 180,000.00 | | | |
| | | Tank Marking | (0-2000) mm | 150,000.00 | 194 | 150,000.00 | 194 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (0-4000)mm | 230,000.00 | 298 | 230,000.00 | 298 |
| | | | (0-6000) mm | 300,000.00 | 388 | 300,000.00 | 388 |
| | | Micrometer Screw | (0-50) mm | 85,000.00 | 110 | 100,000.00 | 129 |
| | | Gauge | | | | | 155 |
| | | Vernier Calipers | (0-150) mm | 95,000.00 | 123 | 100,000.00 | 129 |
| | | | (0-500) mm | 100,000.00 | 129 | 120,000.00 | 155 |
| | | Dial Indicators/gauges | | 85,000.00 | 110 | 100,000.00 | 129 |
| | | Height gauges | | 85,000.00 | 110 | 100,000.00 | 129 |
| | | Set of Gauge Blocks | (0-10) mm | 40,000.00 | 52 | 40,000.00 | 52 |
| | | | Above 10 mm | 45,000.00 | 58 | 45,000.00 | 58 |
| | | Penetrometer | | 85,000.00 | 110 | 100,000.00 | 129 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | GO-NO-GO gauge | | 85,000.00 | 110 | 100,000.00 | 129 |
| 9 | SHINIKIZO | Pressure Gauge | (0-4) bar | 70,000.00 | 91 | 72,000.00 | 103 |
| | | Sphygmomanometer | (0-40) bar | 80,000.00 | 103 | 90,000.00 | 129 |
| | | Differential pressure | (41-100) bar | 100,000.00 | 129 | 117,000.00 | 168 |
| | | Pressure transmitter & switch | (101-400) bar | 115,000.00 | 149 | 117,000.00 | 168 |
| | | | (401-1000) bar | 125,000.00 | 162 | 135,000.00 | 194 |
| | | | (1001-4000) bar | 135,000.00 | 175 | 135,000.00 | 194 |
| | | Dead Weight Tester/Pressure balance | | 200,000.00 | 259 | 250,000.00 | 323 |

| S/N | AINA YA HUDUMA | AINA YA KIFAA | UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA | TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI | TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA | TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Pressure Safety Valves | (0-20) bar | 115,000.00 | 149 | 200,000.00 | 259 |
| | | (PSV) | (21-100) bar | 165,000.00 | 213 | 200,000.00 | 259 |
| | | | (Above 100) bar | 215,000.00 | 278 | 250,000.00 | 323 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | UMEME AC/DC | Potentiometer | | 180,000.00 | 233 | 220,000.00 | 285 |
| | | Ohmmeter | | 150,000.00 | 194 | 170,000.00 | 220 |
| | | Resistor | | 100,000.00 | 129 | 150,000.00 | 194 |
| | | Ammeter | | 150,000.00 | 194 | 200,000.00 | 259 |
| | | Resistance meter | | 100,000.00 | 129 | 150,000.00 | 194 |
| | | Voltmeter | | 100,000.00 | 129 | 150,000.00 | 194 |
| | | Standard cell | | 100,000.00 | 129 | 150,000.00 | 194 |
| | | Decade resistance Box | | 180,000.00 | 233 | 230,000.00 | 298 |
| | | Megger | | 150,000.00 | 194 | 180,000.00 | 233 |
| | | Levelling staff | | 80,000.00 | 103 | 100,000.00 | 129 |
| | | DMM Voltage and Resistance Measurements | Range 61/2Digit | 200,000.00 | 259 | 250,000.00 | 323 |
| | | | Range 5 1/2 Digit | 250,000.00 | 323 | 300,000.00 | 388 |
| | | | Range 4 1/2 | 150,000.00 | 194 | 200,000.00 | 259 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Digit | | | | |
| | | | Range 3 1/2 Digit | 100,000.00 | 129 | 150,000.00 | 194 |
| **S/N** | **AINA YA HUDUMA** | **AINA YA KIFAA** | **UWEZO AU KIWANGO CHA KUPIMA** | **TOZO ZA SASA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA** | **TOZO ZA SASA KWA DOLA ZA KIMAREKANI** | **TOZO PENDEKEZWA KWA SHILINGI ZA KITANZANIA** | **TOZO PENDEKEZWA KWA DOLA ZA KIMAREKANI** |
| | | DMM Current Measurements | Range 6 1/2 Digit | 150,000.00 | 194 | 200,000.00 | 259 |
| | | | Range 5 1/2 Digit | 150,000.00 | 194 | 200,000.00 | 259 |
| | | | Range 4 1/2 Digit | 150,000.00 | 194 | 200,000.00 | 259 |
| | | Energy meter | Single phase | 150,000.00 | 194 | 200,000.00 | 259 |
| | | | Three phase | 250,000.00 | 323 | 300,000.00 | 388 |

**MAELEZO**
Tozo hizi zinajumuisha gharama za uendeshaji kama vile utunzaji wa vifaa na manunuzi wa mahitaji ya ugezi.

**TOZO ZA VIPIMO VIPYA VYA MAABARA**

| Na. | VIPIMO VIPYA | TOZO ZA VIPIMO ZINAZOPENDEKEZWA (SHILINGI ZA KITANZANIA) |
|---|---|---|
| | **MAABARA YA UHANDISI UJENZI** | |
| 1 | Upimaji wa wiani (density) na kiwango cha unyevu kwenye lami (pavement) | 30,000/= |
| | **MAABARA YA UHANDISI WA MITAMBO** | |
| 1 | Upimaji wa utofauti wa mgandamizo kwenye chujio la mafuta na upepo | 50,000/= |
| 2 | Upimaji wa joto la juu kwenye chujio la mafuta na upepo) | 45,000/= |
| 3 | Upimaji wa ufanisi kamili wa maisha ya chujio la mafuta na upepo | 165,000/= |
| 4 | Upimaji wa uwezo na ufanisi wa chujio la mafuta na upepo kuhimili vumbi | 250,000/= |
| | **MAABARA YA KEMIA** | |
| 1 | Upimaji wa Spot kwenye rangi (thinner) | 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| **MAABARA YA VIFUNGASHIO** | | |
| 1 | Upimaji wa kiwango cha mvuke kinachopitishwa kwenye vifungashio vya vyakula (WVTR) | 50,000/= |
| 2 | Upimaji wa kiwango cha hewa ya oksijeni kinachopitishwa kwenye vifungashio vya vyakula (OTR) | 50,000/ = |
| **MAABARA YA NGUO NA NGOZI** | | |
| 1 | Upimaji wa ugumu wa soli za viatu | 30,000/= |
| 2 | Upimaji wa chromium kama chromic oxide ($Cr_2O_3$) kwenye bidhaa za ngozi | 50,000/= |
| 3 | Upimaji wa uimara wa mshono kwenye mshono wa nguo | 50,000/= |
| 4 | Upimaji wa uimara wa kifungo/kishikizo kwenye nguo | 40,000/= |
| 5 | Upimaji wa uimara wa Poly Vinyl Chloride (PVC coated fabric) dhidi ya kuchomwa | 50,000/= |
| 6 | Upimaji wa mgandamizo kwenye mpira wa michezo | 20,000/= |
| 7 | Upimaji wa kiasi cha unyevu kwenye bidhaa za nguo na ngozi | 30,000/= |
| 8 | Upimaji wa rangi za bendera ya taifa (Pantone Matching System) | 20,000/= |
| **MAABARA YA CHAKULA** | | |
| 1 | Upimaji wa bakteria waaozalisha Hydrogen sulphide | 40,000/= |
| 2 | Upimaji wa Leuconostoc mesenteroides | 40,000/= |

**MAELEZO**

1. Hizi ni tozo za vipimo vipya ambavyo Shirika limejenga uwezo wa upimaji kutokana na uwepo wa bidhaa mpya sokoni, viwango vipya na ukuaji wa teknolojia.
2. Hizi tozo zinajumuisha gharama za kununua, kemikali na mahitaji mengine ya upimaji
3. pamoja na gharama za uendeshaji wa mashine.

**TOZO YA UKAGUZI WA BIDHAA ZINAZOINGIA KUTOKA NJE YA NCHI**

| S/N | HUDUMA | TOZO | TOZO YA SASA | TOZO PENDEKEZWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ukaguzi wa bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi isipokuwa magari yaliyotumika | Tozo ya kuthibitisha ubora wa shehena | 0.2% ya Gharama na Usafirishaji (C&F) kulingana na thamani ya mzigo iliyotathminiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 6 Tsh/Kg |

**MAELEZO**

1. Tozo ya kuthibitisha ubora wa shehena inakusudiwa kulipia gharama za ukaguzi na ufuatiliaji wa bidhaa sokoni. Tozo ya zamani ilikokotolewa kwa kujumuisha gharama ya kusafirisha shehena nzima bila kuonyesha kiwango
2. kilichotumika kwa kila bidhaa iliyopo kwenye orodha ya bidhaa zilizosafirishwa ili kutenganisha kati ya bidhaa zinazodhibitiwa na TBS na zile zinazodhibitiwa na taasisi nyingine.
3. Tozo inayopendekezwa itatozwa kulingana na uzito wa shehena badala ya thamani yake.

***KIMABATISHO NA. 6***

**MABORESHO YA TOZO ZA HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU, 2009. MAREKEBISHO YANAYOPENDEKEZWA**

| S/N | TOZO ZA SASA | MAPENDEKEZO |
|---|---|---|
| A | ADA YA KIINGILIO KWA MTU MMOJA KWA SIKU KATIKA HIFADHI ZA BAHARI | |

| | | |
|---|---|---|
| 1. | (i) Wenye umri zaidi ya miaka 15- • **Mtanzania-** Tshs. 2,000.00<br>• **Asiye Mtanzania)** - US$ 20<br><br>(ii) Umri kati ya miaka 5 hadi 15-<br><br>**Mtanzania** **-** Tshs. 1,000.00<br>**Asiye Mtanzania)** - US$ 10<br><br>(iii) Watoto wenye umri chini ya miaka 5- • Watanzania - Bure<br>• Wasio Watanzania - Bure | Kwa mtu Mwenye umri wa miaka 16 au zaidi-<br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) - Tshs. 10,000.00<br>• Wageni ambao sio raia wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - US$ 20 • Wageni wasio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - US$ 10<br><br>) Umri wa kati ya miaka 5 hadi 15-<br><br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) - Tshs. 2,000.00<br>• Wageni ambao sio raia wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - US$ 10 • Wageni wasio raia wa nchi Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - US$ 5<br><br>Kuongeza kipengele kipya<br>- **(iii)** Wanafunzi-<br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki- Tshs. 5,000.00<br>• Ambao sio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - US$ 10<br>• Wanafunzi wasio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - US$ 5<br><br>(iv) Watoto wenye umri chini ya miaka 5<br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki- Bure<br>• Ambao sio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - Bure<br>• Wanafunzi wasio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania – Bure |

| B. | ADA YA KIINGILIO KWA MTU MMOJA KWA SIKU KATIKA MAENEO TENGEFU | |
|---|---|---|
| | (i) Wenye umri zaidi ya miaka 15- • **Mtanzania-** Tshs. 2,000.00<br>• **Asiye Mtanzania)** - US$ 20 | (ii) Kwa mtu Mwenye umri wa miaka 16 au zaidi-<br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) - Tshs. 10,000.00<br>• Wageni ambao sio raia wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - US$ 15 • Wageni wasio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - US$ 10 |
| | (ii) Umri kati ya miaka 5 hadi 15-<br>**Mtanzania** **-** Tshs. 1,000.00<br>**Asiye Mtanzania)** - US$ 5 | (ii) Umri wa kati ya miaka 5 hadi 15-<br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) - Tshs. 2,000.00<br>• Wageni ambao sio raia wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - US$ 10 • Wageni wasio raia wa nchi Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - US$ 5<br><br>Kuongeza kipengele kipya<br>- **(iii)** Wanafunzi-<br><br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki- Tshs. 5,000.00<br>• Ambao sio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - US$ 10<br>• Wanafunzi wasio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - US$ 5 |
| | (iii) Watoto wenye umri chini ya miaka 5- • Watanzania - Bure<br>• Wasio Watanzania - Bure | (iv) Watoto wenye umri chini ya miaka 5<br>• Raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki- Bure<br>• Ambao sio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki - Bure<br>• Wanafunzi wasio raia wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wenye vibali vya makazi Tanzania - Bure |

| | | |
|---|---|---|
| | | • |
| **C.** | **MALIPO YA BOTI NA ADA ZA UVUVI WA MICHEZO KATIKA HIFADHI ZA BAHARI** | |
| | Boti binafsi za burudani zisizo za kibiashara zinazoingia na kukaa **kwa muda usiozidi siku**<br>**5 (tano)** - **US$ 100** | (i) Boti binafsi za burudani zisizo za biashara zinazoingia na kukaa **kwa muda usiozidi siku** 7 (saba) - **US$ 100**<br><br>(ii) Boti za burudani za kibiashara zikiwemo za kukodi zinazoingia na |

| | | |
|---|---|---|
| | ) Boti za burudani za kibiashara zikiwemo za kukodi zinazoingia na kukaa kwa muda usiozidi siku **5 (tano)** - **US$ 200** | kukaa kwa muda usiozidi siku **7 (saba)** - **US$ 200.** |

| | | |
|---|---|---|
| | (iii) Boti za uvuvi wa michezo zinazoingia na kukaa kwa muda usiozidi siku 5 (tano) - **US$ 200**<br><br>(iv) Meli/Boti za abiria za utalii zinazoingia na kukaa kwa muda usiozidi siku 5 (tano) - **US$ 1,000**<br><br>(v) Ada ya uvuvi wa michezo kwa watalii wanaotumia Boti zinazomilikiwa na wawekezaji waliosajiliwa kwenye Hifadhi za Bahari au boti za michezo zilizoingia kihalali kwenye maeneo ya Hifadhi kwa muda usiozidi **siku 5 (tano)- US$ 50**<br><br>(vi) Ada kwa wavuvi waliopo kwenye boti za uvuvi wa michezo kwa muda | (iii) Boti za uvuvi wa michezo zinazoingia na kukaa kwa muda usiozidi siku 7 (saba) - **US$ 200**<br><br>(iv) Meli/Boti za abiria za utalii zinazoingia na kukaa kwa muda usiozidi siku 7 (saba) - **US$ 1,000**<br><br>(v) Ada ya uvuvi wa michezo kwa watalii wanaotumia Boti zinazomilikiwa na wawekezaji waliosajiliwa kwenye Hifadhi za Bahari au boti za michezo zilizoingia kihalali kwenye maeneo ya Hifadhi kwa muda usiozidi **siku 7 (saba)** - **US$ 50**<br><br>(vi) Ada kwa wavuvi waliopo kwenye boti za uvuvi wa michezo kwa muda usiozidi **siku 7 - US$ 50**<br><br>**Kipengele kipya-**<br><br>(viii) Kibali cha Boti za kasi kwa mwezi - **US$ 100**<br><br>(x) Kibali cha Boti za kioo za ndani kwa mwezi **-US$ 100** |

| | | |
|---|---|---|
| | usiozidi **siku 5 - US$ 50** | |
| **D.** | **BOTI ZILIZOSAJILIWA ZINAZOFANYA KAZI KWENYE MAENEO TENGEFU** | |
| | (i) Ada ya Boti za abiria kwa mwezi zenye uwezo wa kubeba watu 7 (saba) - **US$ 300** | (i) Ada ya Boti za abiria kwa mwezi zenye uwezo wa kubeba watu 7 (saba) hadi ishirini (20)- **US$ 100**<br><br>(ii) Ada kwa mwezi kwa Boti yenye uwezo wa kubeba abiria ishirini na moja (21) na kuendelea **- US$ 150**<br><br>**Kipengele kipya**<br>(iii) Meli kubwa za watalii kwa siku 7 (saba) - US$ 1000 (iv) Kibali cha Boti za kasi kwa mwezi - **US$ 100.**<br>(iv) Kibali cha Boti za kioo za ndani kwa mwezi **-US$ 100** |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| **E.** | **TOZO ZA UWEKEZAJI (CONCESSION)** | |
| | (i) Kibali cha kuendesha shughuli za kijamii (mf. migahawa, na kambi za usiku) katika maeneo Tengefu - **USS 1,200 kwa mwezi.** | (i) Kibali cha kuendesha shughuli za kijamii (mf. Migahawa, kambi za usiku) kulingana na aina tofauti za uwekezaji; |

| | | |
|---|---|---|
| | | **AINA ZA UWEKEZAJI**<br><br>Maeneo Tengefu (US$)<br><br>**A** **B** **C** **D**<br>40,000 20,000 10,000 2,500<br><br>) Hifadhi za Bahari (US$)<br><br>**A** **B** **C** **D**<br>25,000 10,000 3, 000 1,000<br><br>**AINA YA UWEKEZAJI**<br>A = Hoteli za Nyota Nne na kuendelea<br>B = Nyota Tatu |

| | | |
|---|---|---|
| | (ii)<br>Kibali cha kuendesha shughuli za kijamii (Mf. Hoteli za kitalii na kambi za usiku) katika Hifadhi za Baharu tozo ni **- US$ 1,500 kwa mwezi.** | C = Hoteli za Nyota Mbili, Huduma za Kuzamia na huduma nyingine za michezo ya kwenye maji<br>D =<br>Nyumba za kulala wageni, Nyumba za mapumziko,<br>Hosteli, Malazi ya nyumbani ya watalii (Home stay),maduka ya zawadi na Migahawa<br><br>***Zingatia: Kiasi pendekezwa ni kadirio la chini kwa kila aina.***<br><br>(ii) Tozo za uwekezaji maeneo yenye rasilimali za upekee (prime area) - **US$ 50,000 kwa mwaka.**<br>**Kipengele kipya**<br><br>(iii) Kodi za kutua ndege za baharini na helikopta - **US$ 100 kwa kila mtuo**.<br><br>(iv) Waongoza watalii watatakiwa kulipa kodi ya kuongoza watalii - **US$ 50 kwa mwaka**. |
| **F.** | **TOZO ZA KUPIGA PICHA KIBIASHARA** | |
| | Upigaji picha wa aina tofauti mf. picha mnato,filamu kwa ajili ya biashara ndani ya maeneo Tengefu au Hifadhi za Bahari atalipa US$ 1,000 kwa siku saba (7). | Upigaji picha wa aina tofauti mf. picha mnato,filamu kwa ajili ya biashara ndani ya maeneo Tengefu au Hifadhi za Bahari atalipa **US$ 200.00 kwa siku.** |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| G. | **MGAWANYO WA MAPATO KATI YA MPR NA WADAU WAKUU** | |
| | Kiasi cha mapato baada ya makato (net revenue) kitagawanywa kati ya MPRU na jamii ambazo ziko katika maeneo ya hifadhi kwendana na sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kitagawanywa kama ifuatavyo;<br><br>Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)-70%<br><br>Halmashauri ya Wilaya<br><br>) Jamii zilizoko katika maeneo ya Hifadhi-20% | Kiasi cha mapato baada ya gharama za uhifadhi kitagawanywa kati ya hifadhi na jamii inayozunguka hifadhi husika kuendana na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kitagawanywa kama ifuatavyo;<br><br>(i)Kugharamia Uhifadhi - 70%<br><br>Mamlaka ya Serikali za mitaa hifadhi inakopatikana - 5%<br><br>) Jamii zilizoko katika maeneo ya Hifadhi- 10%<br><br>)Gawio la Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund) 15% |

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hoja imetolewa na imeungwa mkono sana. Ahsante sana kwa hotuba yako ambayo imechukua takriban masaa mawili na dakika kama 20 hivi. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tumpigie makofi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kweli Hotuba ya Bajeti ya safari hii ni ya kiwango na ni ya kipekee kabisa. Na kwa niaba yenu, tuseme kwamba tumepokea salamu za mama yetu zote zilizo ndani ya hotuba hii kwa mikono miwili kabisa, nashukuru sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kesho hatutakuwa na shughuli hapa ili kuwapa nafasi ya kuweza kusoma, kuchambua na kuelewa hotuba iliyosomwa hapa pamoja na vitabu vilivyoambatana nayo ambavyo vingi vyake tayari vimo katika vishkwambi vyetu, halafu Jumamosi na Jumapili pia. Kwa hiyo Jumatatu baada ya maswali tutaanza sasa kujadili hotuba hii na utekelezaji wake. Niwaambie tu Waheshimiwa Madiwani sio kwamba lile pendekezo limeshapita, haya ni mapendekezo ameleta Mheshimiwa Waziri. Mkae vizuri na Wabunge huko, muwapigie simu, mkileta jeuri lile pendekezo halipiti hapa. *(Kicheko)*

Lakini kwa vile ninyi ni wenzetu, naamini Waheshimiwa watazingatia pendekezo zuri lililokuja. *(Makofi)*

Tunao wageni wengi, haitakuwa rahisi kuwatambulisha wote, lakini basi tujaribu kwa wale ambao tunao.

Nianze na Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Mheshimiwa Phillip Mangula, ahsante sana, amefuatana na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar Dkt. Abdulla Sadala. *(Makofi/ Vigelegele)*

Lakini pia amefuatana na Katibu Mwenezi Taifa Ndugu Shaka, ahsante sana, ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

Kipekee naomba nimtambulishe Spika Mstaafu Mama Anne Semamba Makinda, karibu sana Mama Makinda. Karibu sana Bungeni kwenye Jengo lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mama Makinda alikaa humu Bungeni takribani miaka 45 nadhani, ni rekodi ambayo sio rahisi, hata ninyi Wabunge mnaosema vijana na yeye alikuja kama Mbunge kijana, miaka 40 kukaa humu ni shughuli kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Nilipoingia hapa Bungeni nilipangwa kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wangu akawa ni Mama Anne Makinda. Awamu ya miaka mitano iliyofuata yeye akawa Mwenyekiti wa Bunge, mimi nikawa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili, akaniachia kijiti. Baadaye akawa Naibu Spika, mimi nikawa Mwenyekiti wa Bunge. Akawa Spika, nikawa Naibu Spika. Ameenda kustaafu, nimekuwa Spika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi huwa nafuata mguu wake, anapotoa, naweka! Sasa kwa kuwa alishaenda kustaafu na mimi nafuatia fuatia, nitakuja kuwaambia huko mbele. Wakati wake bado, lakini kazi yangu kufuata nyayo zake. Namshukuru sana mama kwa malezi, mkiona naharibu kwa kweli alaumiwe yeye maana yeye ndiyo mwalimu wangu kila hatua. Tumefurahi kuja kwako Mama Makinda. *(Makofi/Vigelegele)*

Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi, tunae Mnadhimu Mkuu wa Jeshi akimwakilisha Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi *(CDF) Lieutenant General* Yakub Mohamed, ahsante. *(Makofi)*

Mwakilishi wa *IGP,* Kamishna wa Polisi Liberatus Sabas, ahsante. *(Makofi)*

Naibu Kamishna Jenerali wa Magereza Ndugu Yeremia Katungu, ahsante. *(Makofi)*

Mwakilishi Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, James Mwanjotile. *(Makofi)*

Mwakilishi wa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jesward Ikonko. *(Makofi)*

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya, Gerald Mwasabila. *(Makofi)*

Naibu Kamishna wa Polisi akimwakilisha Mratibu wa Baraza la Usalama, Geofrey Kamwela. *(Makofi)*

Mkuu wa JKT Brigedia Jenerali Rajabu Mabele. *(Makofi)*

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Neema Mwakalyelye na Neema ni mara ya kwanza anakuja hapa, alikuja wakati fulani, lakini leo pia amekuja. Tunakukaribisha sana Neema kwa nafasi hii kubwa sana uliyoipata katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Viongozi waandamizi kutoka katika Mkoa wa Dodoma, yupo Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa yupo hapo, yuko Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma Profesa Davis Mwamfupe, ahsante sana, mwalimu wangu huyu. *(Makofi)*

Yuko Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, *RPC* Anania Amo, ahsante. *(Makofi)*

Mkuu wa Usalama - *RSO,* Methuselah Ntonda. *(Makofi)*

Na yuko *RAS* wa Mkoa wa Dodoma... *(Makofi/ Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, sina uhakika...

**MBUNGE FULANI:** Hatujamuona. Hatujamuona.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sina hakika kama tumemuona *RAS* wa Dodoma, hebu asimame tena. Asimame hatujamuona. Eeeeh! Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna familia ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, mke wa Mheshimiwa Waziri Mwigulu, Neema Nchemba, karibu sana, karibu mama. Wako watoto wetu, Gracious, Isaack, Dennis, Nazareth, Emirand na Ukende, karibu sana wanafamilia pia. *(Makofi)*

Watendaji Waandamizi wa Taasisi za Serikali, tuna Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali *(CAG)* Ndugu Charles Kichere, ahsante, yuko pale *CAG. (Makofi)*

Tuna Gavana wa Benki Kuu, Profesa Florens Luoga, ahsante sana. *(Makofi)*

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania - *TRA,* Alphayo Kidata. *(Makofi)*

Tunae mgeni maalum kabisa wa Mheshimiwa Spika, naye si mwingine nae si mwingine bali ni Msajili wa Vyama vya Siasa - Jaji Francis Mutungi, ahsante sana Msajili. *(Makofi)*

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Dkt. Wilson Mahera, ahsante. *(Makofi)*

Mwakilishi wa Kamishna ya Sekretarieti ya Maadili Ndugu John Kaole na Mtendaji Mkuu wa Mahakama Mathias Kabunduguru, ahsante sana. *(Makofi)*

Nina viongozi wa Benki ya *CRDB,* Mwenyekiti wa Bodi Ndugu Ally Lai, karibu sana, yuko *DG* wa *CRDB* - Abdulmajid Nsekela, yuko Mkurugenzi - Tully Mwambapa, yuko Mkurugenzi - Fred Shekinabo, yuko Meneja wa Kanda - Chabu Mishwaro, yuko Mkurugenzi - Boma Labara, lakini wote hawa wameongozwa na Meneja wetu wa Tawi la Bunge Grace Adam. *(Makofi)*

Wewe wa kamera, muoneshe Grace yuko wapi? Inaelekea bado yuko kibaruani. Mtampelekea salamu zake, tumem-*miss* meneja wetu. *(Makofi)*

Mabalozi na Wakuu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa; *Ambassador Democratic People's Republic of Korea,* ahsante; *Ambassador Zimbabwe* - Lieutenant *General (Rtd) Anselim Sanyatwe; High Commissioner United Kingdom - David Concar; Ambassador Switzerland - Didier Chassat; Ambassador Norway - Elizabeth Jacobsen; Ambassador Denmark - Mette Norgaard dissing Spandet; High Commissioner Namibia - Labbius Thobias; High Commissioner Zambia - David Shinfyembe; Economic Policy Officer British High Commission - Francis Sampa; Senior Political Officer British Embassy - Sylvester Ernest; Country Economist Norway Embassy - Trond Augdal; Public Finance Management Development Partners Group Coordinator Norway Embassy - Simon Moshy; Head of Chancery Malawi - Andre Malombera; Political Counsellor China Embassy - Yang Zhiyu; Counsellor Zimbabwe Embassy - Masocha; First Secretary China Embassy* - Wang Qiang; *Senior Policy Officer Netherlands Embassy* - Neema Matafu; *Third Secretary Uganda Embassy - Comfort Amviko; Liaison Officer Germany Embassy - Richard Shaba; Team Leader Trade and EAC Affairs Germany - Oscar Mkude; First Secretary Political Administration Zambia Embassy - Derrick Kondowe; Political Attaché Switzerland Embassy - Victoria Zelger; Financial Attaché Uganda Embassy - Victoria Emily Asea. (Makofi)*

Pia tunao Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Adam Kimbisa. Ahsante sana Wabunge wenzetu wa Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Kimbisa kama Mwenyekiti na wenzako waliokuja na wasiokuja karibuni sana, lakini pia amefuatana na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Makame, yuko pia Mheshimiwa Happiness Lugiko, yuko Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Mnyaa, yuko Mheshimiwa Dkt. Ngwalu Maghembe. *(Makofi/ Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Hatujamuona vizuri.

**SPIKA:** Chanda chema huvikwa pete eeh?

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ngwalu inaelekea umepita bila kupingwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Asimame.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma pale mlipo msimame wote, wakuu wa Wilaya, karibuni sana Wakuu wa Wilaya. *(Makofi)*

Wakurugenzi wa Halmashauri wa Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wenyeviti wa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma popote pale mlipo, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa kwa makundi naomba niwasimamishe Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote pale mlipo, naomba msimame kwa pamoja. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Watendaji wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake, Watendaji Waandamizi wa CCM na Viongozi na Jumuiya zake, Wakuu wa Wilaya nimeshawataja na Wakurugenzi, Wawakilishi wa Vyama vya Siasa, karibuni; Viongozi wa Dini karibuni, Wakuu wa Mashirika ya Umma, karibuni na Wadau wa Vyombo vya Habari, karibuni. *(Makofi)*

Viongozi wa CCM Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti Godwin Mkanwa na Katibu wa CCM wa Mkoa - Pili Augustino, naomba msimame pale mlipo, karibuni sana, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia wale wa kutoka Kongwa, Mwenyekiti wa Halmashauri - White Zuberi, Katibu wa CCM wa Kongwa -

Ndugu Mbanga, ahsante. Katibu wa Wazazi Kongwa, karibu; Katibu UWT Kongwa, karibu; Katibu wa Vijana Kongwa, karibu na karibuni sana. *(Makofi)*

Sio kwa umuhimu, kipekee kabisa nimtambulishe Mheshimiwa aliyekuwa Mbunge Mstaafu wa Mbarali, Mheshimiwa Haroon Mulla. Mheshimiwa Haroon, karibu sana. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, pia tunao Maofisa kutoka Benki ya *NMB* wakiongozwa na Mtendaji Mkuu - Ruth Zaipuna, karibu sana Ruth, karibu sana; amefuatana na Afisa Mkuu Fedha, Juma Kimori, karibu sana, lakini yuko Vicky Bushubo, yuko Nsolo Mlozi, Meneja wa Kanda na kama kawaida wameongozwa na Meneja wetu wa *NMB* Grace, ahsante Grace. *(Makofi)*

Sasa matangazo Waheshimiwa Wabunge kama tulivyotangaza jana hapa Mezani, tunawakumbusha kwamba keshokutwa Jumamosi kutakuwa na bonanza kubwa kabisa la aina yake lililoandaliwa na Benki ya *CRDB* katika Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma, Mgeni Rasmi atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye bonanza hilo. Ni bonanza la kipekee sana mnaombwa Waheshimiwa Wabunge kuhudhuria. *(Makofi)*

Bonanza hili litaanza saa 12:00 asubuhi hapa hapa kwa matembezi kuanzia Ofisi ya Bunge kuelekea Uwanja wa Jamhuri ambapo michezo mbalimbali itafanyika pale Uwanja wa Jamhuri. Kutwa nzima ya siku hiyo itakuwa ni shughuli za michezo ya aina kwa aina katika Uwanja wa Jamhuri. Kwa hiyo, nawaomba sana tuwahi asubuhi na mapema, ili tuungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi mwenyewe nitakuweko pale na kwa kweli imeandaliwa vizuri sana. Kama mnavyowajua *CRDB* wanavyopenda kuandaa vitu vyao kwa viwango. Wananiambia maandalizi haya yatazidi ile futari ya wakati wa mwezi wa Ramadhani. *(Makofi/Kicheko)*

*NMB* tumewa-*miss* safari hii, mmezidi uchoyo, kwenye futari hatujawaona, kwenye *activity* yoyote hatujawaona na

hii imeanza toka huyu Mkurugenzi Mkuu Ruth ameingia. *(Kicheko)*

Mkurugenzi Ruth unawaangusha wanawake, jamani hilo natania tu msije mkamhukumu Ruth. Nia yangu akajipange kivingine atakapokuja *CRDB* mjipange. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, Jumamosi Waheshimiwa tuwahi mapema asubuhi hapa katika *track suits* zetu tuungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba kuna wakati yalitolewa Maelezo Binafsi hapa Bungeni tarehe 4 Mei, 2021 na Mheshimiwa Francis Mtega, Mbunge wa sasa wa Mbarali ambaye alilalamikia masuala yanayohusiana na mahusiano ya wananchi wake na Hifadhi ya Ruaha.

Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama imekaa na imenishauri na mimi naagiza ifuatavyo; kwamba Serikali iendelee kuboresha mahusiano kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na wananchi wa maeneo ya jirani na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii basi iendelee kufuatilia katika utaratibu wa kawaida, taarifa ile ya tathmini iliyofanywa na Mawaziri wanane kuhusu vijiji 920 na uamuzi kuhusu vijiji 55 vinavyopakana na Hifadhi ya Ruaha kadri Serikali itakavyoelekeza, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuliwahi pia kutangaza hapa kwamba kuna baadhi ya mashirika na taasisi ambazo hazikuwa zimewasilisha hesabu kwa *CAG* na kwa hiyo, taarifa zao hazikuwepo katika Taarifa ya *CAG* iliyowekwa hapa mezani.

Kamati ya *PAC* imeshafanyia kazi jambo hilo na ningependa kulimaliza kwa kutoa maelekezo yafuatayo; hoja kuhusu Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili *(MOI),* Kampuni ya Mbolea *(TFC)* na Shirika la Magazeti *(TSN)* tunashauri Serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya taasisi hizo ili kutilia nguvu masharti ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418.

Kuhusu Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC)* na Shirika la Magazeti Serikalini *(TSN)* kushindwa kufunga hesabu zake, tumeshauri Serikali ifanye tathmini ya kina ili kubaini iwapo mashirika hayo mawili yanatakiwa kuendelea kufanya kazi katika mfumo wa sasa au kuyafanyia marekebisho makubwa yaani *restructuring* ya mashirika hayo.

Kuhusu Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* kutofunga hesabu kwa sababu ya kutokuwepo kwa makubaliano ya maandishi *(Written Loan Agreement)* kati ya Mfuko na Serikali ya ulipaji wa mkopo wa shilingi bilioni 231; sisi tunashauri Serikali na *NHIF* wakamilishe makubaliano ya kimaandishi ikiwemo ratiba maalum ya ulipaji *(date repayment schedule)* na kuanza kulipa madeni husika kwa ratiba ambayo watakuwa wamekubaliana.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu Taasisi ya Mifupa Muhimbili *(MOI)* kutokukamilisha hesabu kutokana na changamoto za mfumo wa kitabibu *(medi-pro)* kutowasiliana ipasavyo na mfumo wa hesabu; tunaishauri Serikali ifanye uchunguzi wa mchakato mzima wa ununuzi na usimikaji wa mfumo wa shughuli za kitabibu uliopo *MOI,* hiyo *medi-pro* ili kubaini iwapo taratibu zilifuatwa na kama mfumo huo una manufaa kwa Taifa. Aidha, Serikali ipeleke wataalam wenye sifa kule *MOI* ili kutekeleza shughuli za ukaguzi na uhasibu. Pana shida ya wahasibu pale *MOI, qualifications* zao. Kwa hiyo, tupate ambao ni *more qualified.*

Waheshimiwa Wabunge, ipo pia ya kutokukamika kwa wakati ukaguzi wa hesabu za taasisi tatu; Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO),* Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* na Shirika Posta *(TPC);* kutokana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuhusiana na mashirika hayo matatu, ushauri; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iboreshe mipango ya ukaguzi *(audit plans)* na kuzingatia ipasavyo wakati wote wa ukaguzi kuzingatia huo mpango kazi.

Kuhusu kuongezwa kwa muda wa ukaguzi wa hesabu za taasisi tatu zikiwemo Shirika la Reli Tanzania, Soko la Bidhaa *(TMX)* na Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja *(UTT),* ushauri; Ofisi

ya Taifa ya Ukaguzi izingatie kwa ukamilifu masharti ya kifungu cha 32(4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 kinachotoa mamlaka ya kuongeza muda wa ukaguzi kwa Bunge pekee kupitia Azimio la Bunge. Kwa hiyo, ni lazima wawe wanafunga hesabu kwa wakati na ikibidi basi lazima kibali kiombwe Bungeni na kwa Azimio la Bunge ambalo si rahisi kulipata. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maelekeo yetu ni kwamba kila taasisi ifunge mahesabu kwa wakati na Taarifa ya Mkaguzi Mkuu inapokuja hapa ijumuishe taasisi zote, maana zingine zinajua kwamba tutapata hati chafu, kwa hiyo, wanakwepa wakati wa ukaguzi, wanapeleka hesabu zao baada ya tarehe zile, kwa hiyo, kitabu kinachowekwa hapa mezani na *CAG* kinakuwa hakina hesabu zao. Sasa mbinu hiyo tumeigundua, tumeshastuka. Nilitaka kuwajulisha tu kwamba tumestuka na basi kwa neno ambalo limekuwa katika wiki hii kama wana busara wajirekebishe, maana ndiyo neno la wiki hili. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine ni kwamba kwa mujibu wa ratiba yetu kesho, Ijumaa, hatutakuwa na Kikao cha Bunge na badala yake Wabunge tutatumia siku hiyo kusoma na kutafakari kuhusu Hotuba ya Bajeti na viambatanisho vyake vyote. Hata hivyo, kwa mwaka huu tumepanga kuitumia siku ya kesho kwa ajili ya kupata mada na mjadala wa masuala ya kiuchumi *(Parliamentary Economic Dialogue).* Shughuli itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4:00 asubuhi na masuala yote ya utaratibu yamezingatiwa, yaani maandalizi ya semina, yaani makabrasha na mambo mengine tumeandaa. *(Kicheko/ Makofi)*

Orodha ya watoa mada ni Profesa Prosper Ngowi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe atakuwa *Moderator;* Profesa Samwel Wangwe kutoka Taasisi ya Utafiti ya Kupunguza Umasikini – *REPOA;* Dkt. Suleiman Misango - Mkurugenzi wa Sera na Utafiti na Uchumi kutoka Benki Kuu ya Tanzania; atakuwepo pia Dkt. Tausi Kida - Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Utafiti Masuala ya Uchumi na Kijamii – *ESRF;* Dkt. Albina Chuwa - Mtakwimu Mkuu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu –

*NBS;* Ndugu Francis Majige Nanai -Mtendaji Mkuu kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi – *TPSF* na Ndugu William Mhoja - Kamishna wa Sera kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Nawaombeni saa 04:00 asubuhi kesho tuwepo pale Msekwa kwa ajili ya semina hiyo muhimu sana, ni vizuri kuwahi. *(Makofi)*

Mwisho Waheshimiwa, naomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho asubuhi mapema iko shughuli pale kwenye Hoteli ya Morena kwa wale ambao mmepewa kadi, aah ni kesho kutwa Jumamosi, samahani.

Kesho ni semina, kesho kutwa siku ya Jumamosi kutakuwa na kitu ambacho kimeandaliwa na wenzetu wanaitwa *Kingdom Leaders Network Tanzania* ambayo ni *National Prayer Breakfast* pale Hoteli ya Morena na watu mmepewa kadi, wale ambao mnatakiwa kushughulika.

Wale wenye kadi ndio waende kwenye hii *Prayer Breakfast,* wengine wote tunaenda kwenye shughuli ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu atatuongoza ambayo imeandaliwa na wenzetu wa *CRDB.* Shughuli hiyo itaanza saa 12:45 asubuhi yaani saa moja kasoro robo asubuhi na maandalizi yake ni mazuri na makubwa. Kwa hiyo, kama nilivyosema wale ambao hamtakuwa katika *Prayer Breakfast* lazima tujiunge kwenye shughuli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 14 Juni, 2021, saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 12:55 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 14 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*